Kikao cha Ishirini na Nne - Tarehe 18 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika, (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 11

Ndege ya Serikali

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Serikali inatumia fedha nyingi sana kwa kukodi ndege ili kufanikisha safari za Viongozi Wakuu wa Serikali.

(a) Je, ndege ya aina ya *JET* ya serikali imepotea katika mazingira gani.

(b) Kama iliuzwa, aliuziwa nani na kwa bei gani.

(c) Serikali ina mpango gani wa kununua ndege nyengine ili kujiepusha na gharama za kukodi ndege za watu binafsi.

Mhe. Waziri wa Fedha - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa na kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi namba 11 lenye sehemu tatu (a),(b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kama yafuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, mnamo mwezi Juni, 1982 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilinunua ndege aina ya *HS 125-700* "*Executive Jet*" kutoka Kampuni ya *British Aerospace(BAE*) ya Uingereza. Kwa taarifa ndege hiyo ilinunuliwa kwa thamani ya Dola za Kimarekani milioni 5.

Aidha, mnamo mwezi Februari, 1992 ndege hiyo ilisita kutumika baada ya kupata matatizo ya kiufundi na ZMZ kuamua kuiuza kwa Kampuni ya *British Aerospace,* kwa thamani ya Dola milioni 2,500,000 kutokana na kwamba ndege hiyo kutumika kwa muda mrefu na matengenezo yake kuonekana kuwa makubwa.

Mhe. Naibu Spika, mnamo mwezi Novemba, 1992 SMZ iliingia mkataba Canadian *Imperial Commerce Bank* kwa ajili ya ununuzi wa ndege ya aina ya HS 125-1000 *Executive Jet* kwa njia ya ukodishwaji, yaani *lease purchase,* kwa thamani ya dola za Kimarekani 13.7 milioni. Makubaliano hayo yaliitaka SMZ kulipa deni hilo katika kipindi cha miaka 10, kwa utaratibu wa kulipa malipo sawa kila baada ya miezi sita, yaani *equal instalment.*

Mhe. Naibu Spika, ndege ya aina ya HS 125-1000 ilitumika kwa muda mfupi baada ya kujitokeza hitilafu na kurejeshwa Uingereza kwa matengenezo. Aidha, kwa mujibu wa mkataba SMZ ilitakiwa kulipa sehemu ya kwanza, yaani *first instalment* ya malipo, lakini kutokana na hali mbaya ya uchumi, SMZ ilishindwa kulipa na ilipofikia malipo ya awamu ya pili SMZ pia ilishindwa kulipa na hivyo kuonekana taratibu za kimkataba kutokufuatwa na kwa kuwa ndege hiyo ilikuwa inunuliwe kwa njia ya ukodishwaji, yaani *lease purchase* iliendelea kuwepo Uingereza kwa sababu SMZ kushindwa kutekeleza mkataba kwa ukamilifu. Hadi hapo tulipoandikiwa rasmi kuwa SMZ imevunja mkataba wa kuilipia ndege hiyo, hivyo ndege hiyo kurejeshwa kwa wamiliki.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwa heshima kubwa sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, ndege ya SMZ aina ya HS 125 - 700 haikupotea iliuzwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, na ndege ya aina ya HS 125 - 1000 ambayo ilikuwa inunuliwe na SMZ kwa

njia ya ukodishwaji, yaani *lease purchase* imebaki kwa mmiliki baada ya SMZ kushindwa kuilipia kwa mujibu wa mkataba.

b) Mhe. Naibu Spika, ndege ya aina HS 125-700 iliuzwa kwa *British Aerospace* (*BAE*) ya Uingereza kwa thamani ya dola za Kimarekani 2.5 millioni.

c) Mhe. Naibu Spika, kwa wakati huu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina mpango wa kununua ndege kwa ajili ya viongozi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kupata jibu kama lilivyoelezwa, kuwa ndege hii haikupotea iliuzwa na ndege nyengine haikuwezekana kwa sababu ya serikali kushindwa kulipia fedha.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu serikali inatumia fedha nyingi sana kwa kukodi ndege kwa safari za viongozi na kwa sababu nchi hii awali ilikuwa na ndege yake wenyewe rasilimali yake na iliuzwa, na kwa sababu kila kikija kipindi cha bajeti kama hiki hakuna hata mwaka mmoja tunapoambiwa kuwa uchumi haukuwi, na kila mtu anajua umuhimu wa Zanzibar kuwa na ndege yake kama nchi.

Je, ni sababu gani muda wote huo mrefu ikawa serikali haijaona umuhimu wa kuwa na ndege hiyo na wakati ilikuwa nayo ikauzwa ikaongeza fedha, na kwa vyovyote itakavyokuwa, lakini ikawa na ndege nyengine kwa kujinusuru kwa kutumia pesa nyingi sana za kukodi ndege za watu binafsi.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, sababu kubwa kwa serikali kutokununua ndege kwa ajili ya viongozi, ni kutokana na hali yetu ya kifedha. Hali ya kifedha itakapokuwa nzuri, nasema tena na serikali ikikubali kununua ndege na Baraza letu la Wawakilishi likiridhia, basi serikali itanunua ndege kwa ajili ya viongozi. Kama hali yetu ya kiuchumi itakuwa nzuri, na hali yetu ya kifedha itakuwa nzuri.

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, kununua ndege ni suala moja na kuiendesha ndege ni suala jengine. Hapa zaidi tunazungumzia kuiendesha ndege ndio inaleta gharama kubwa sana. Unaweza kuinunua mara moja, lakini uendeshaji wake uko kila siku. Kwa hivyo, tuvute subira hali itakapokuwa nzuri ya uchumi, mapato yetu yatakapokuwa mazuri na viongozi wakishakukubali kwamba sasa ni wakati mzuri wa kununua ndege kwa ajili ya viongozi, basi ni sisi wananchi tukikubaliana, hali ikiwa nzuri, fedha zikiwepo hakuna tatizo.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri, ningependa kujua tu, je huu mkataba ambao ikiwa ni wa kukodi hii ndege umemalizika muda wake. Katika kukubaliana mkataba huu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuuvunja, imeingia hasara kiasi gani.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa mkataba ilielezwa, kila baada ya miezi sita kwa kipindi cha miaka 10 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatakiwa kulipa instalment moja baada ya moja, mpaka ifike miaka 10 ile *amount* ya dola 13.7 milioni itakuwa imemalizika. Kama serikali itashindwa na mkataba wenyewe ndio unavyosema, maana yake atakuwa mwenyewe mkataba umeuvunja. Bahati nzuri serikali ilishindwa kulipa *first instalment*, ikashindwa kulipa *second instalment* tukaandikiwa barua kwamba kwa mujibu wa mkataba mmeshavunja mkataba.

Mhe. Naibu Spika, ndege ile ya pili kama nilivyosema ilinunuliwa kwa utaratibu wa *lease purchase*. Kwa hivyo, inavyoelekea ni kwamba hakukuwa na athari yoyote, isipokuwa kwamba wale wenye ndege yao wakachukua ndege yao na kwa sababu ilikuwa haikutumika kwa muda mrefu, ilionekana ina athari na wao wakazuwia ndege yao basi wakaendelea na shughuli nyengine.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ya kiufasaha na kuielewa *subject matter very well*, kwa hivyo nampongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, hapa tunazungumzia ndege ya kiongozi na mara nyingi ndege ya kiongozi inakuwa na gharama kubwa, kwa sababu haizalishi, haina tija ya kuzalisha fedha ila kumuhudumia kiongozi katika utendaji wake wa kiserikali.

a) Je, Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri haoni kuna umuhimu wa kuzungumza na wafanyabiashara ama wawekezaji. Mfano kama ndugu Said Salim Bakharesa, kuanzisha *AZAM Airline* ambayo itaweza kuingia ubia na serikali.

b) Thamani ya ndege ni *route* yake *commercial value* na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ina kasma katika *route* za ndege za Anga za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa Mhe. Waziri haoni kuna umuhimu wa kufanya mazungumzo na wawekezaji binafsi ili waanzishe Shirika la Ndege la Zanzibar ambalo litawahudumia wananchi wa Zanzibar, ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimepokea shukrani zake na pongezi zake. Lakini la pili nataka niseme Mhe. Naibu Spika, ni kwamba wazo ambalo amelitoa Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo ni wazo zuri sana, la kuzungumza na wawekezaji wa ndani na nje ili kuja kuanzisha Shirika la Ndege la Zanzibar kwa kushirikiana na serikali, kwa maana ya *Private Public Partnership*. Naliafiki na nadhani sio jukumu la Waziri wa Fedha peke yake, ni jukumu la Wazanzibari sote, kama tutaweza kuwapata wafanyabiashara ambao watakaokuwa tayari kuanzisha Shirika la Ndege la Zanzibar, basi tutaweza kukaa nao sisi serikali pamoja na wafanyabiashara hao, ili tuweze kuona tutakwendaje katika kuanzisha shirika hili.

Kwa hivyo, hilo ni wazo zuri, nimelipokea na nitalifanyia kazi. Namuomba Mhe. Mahamoud Thabiti Kombo na Waheshimiwa Wawakilishi wengine, tushirikiane katika wazo zuri kama hili, ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 40

Mpango wa Kuwezeshwa Wavuvi wa Vijiji vya Muyuni, Bwejuu na Jambiani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Wananchi wengi wa vijiji vya Muyuni, Bwejuu na Jambiani, mmoja mmoja au kwa vikundi, wamejiajiri katika sekta ya uvuvi na kuisaidia serikali yao mzigo wa kuajiri. Licha ya hatua hiyo ya kimaendeleo, wavuvi wa vijiji hivyo weamekuwa wakikabiliwa na tatizo la kutowezeshwa kwa kukosa rasilimali vifaa vya kisasa vya uvuvi na fedha.

Je, serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wavuvi wa vijiji hivyo kupata rasilimali hizo ili waendelee kujiajiri na kuipinguzia serikali mzigo wa kuajiri.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uwezo wa kusimama kwenye Baraza lako tukufu. Pili nikushukuru kwa kunipa nafasi ya pili ya siku hii ya leo.

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 40 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2014 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia wizara yangu, iliwapatia wananchi wa vijiji vya Muyuni, Bwejuu na Jambiani vitendea kazi kama ifuatavyo:-

Kijiji cha Muyuni - Walipatiwa boti mbili za kisasa za uvuvi wa kienyeji pamoja na mashine zake.
Kijiji cha Bwejuu - Walipatiwa boti mbili za kisasa na mashine zake.
Kijiji cha Jambiani - Walipatiwa mradi wa uhifadhi wa utalii kwa ajili ya kufanya kazi mbadala ya kihistori ambapo wamejengewa ofisi ya makumbusho na kuboreshewa eneo la pango lililomo katika kijiji chao.

Aidha, wamepatiwa boti ya uvuvi na mashine yake pamoja na miradi miwili ya ufugaji wa kuku yenye thamani ya milioni 18 kama kazi mbadala. Hatua hizi zote zililenga kuwaendeleza wavuvi ikiwa ni pamoja na kupunguza nguvu kazi za uvuvi wa vijiji hivyo na kupatiwa kazi mbadala.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kujibu kitu sijui tuseme kama kiini macho au kisichokuwepo. Jimbo la Muyuni walipokea boti au ngarawa nilikuwa nataka kujua hicho. Lakini ninavyojua mimi walipewa ngarawa na gharawa hizo zilikuwa mbovu na zimechukuliwa. Nataka kujua ngarawa hizo ziko wapi hadi leo na kwa nini hajapelekewa, sikumbuki kupewa boti na boti zilizoletwa zimeletwa na *TASSAF* pamoja na nguvu za wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, boti moja ambayo imepelekwa katika kijiji cha Muyuni ilikuwa na matatizo madogo na makundi makubwa ndio yaliyosababisha hivyo. Boti ile ilipelekwa katika kijiji cha Kizimkazi kwa kuhifadhiwa na sasa imerejeshwa Muyuni.

Hata hivyo, Mhe. Naibu Spika, palikuwa na manung'uniko mawili matatu, ya kundi moja kuweza kuchukua boti ile, lakini boti ile ilikabidhiwa lile kundi jengine. Katika bajeti ya mwaka jana tulimuahidi Mhe. Jaku Hashim kama hali itaruhusu tutaweza kumpa bodi nyengine ili na wale watu wengine wasiwe na malalamiko ya kudumu.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba wizara kwa kupitia mradi wa *MACEMP* ilitoa vifaa mbali mbali vya uvuvi, vikiwemo boti, mashine na nyavu. Je, wizara imefanya tathmini gani kuona vifaa hivyo kwanza vipo na kwa sababu kuna misemo inasema kama kuna baadhi ya vijana vifaa hivyo wengine wameuza. Je, hilo ni kweli, naomba majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba arudie swali la mwanzo sikulisikia vizuri.

Mhe. Naibu Spika: Anaomba Mhe. Naibu Waziri, swali la mwanzo ulirudie na ukaribie kipaza sauti ili apate kusikia vizuri, kwa sababu wewe mrefu kidogo.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Naibu Spika, swali la mwanzo nililomuuliza Mhe. Naibu Waziri ni kwamba wizara kwa kupitia mradi wa *MACEMP* ilitoa vifaa mbali mbali vya uvuvi, vikiwemo, boti, mashine na nyavu. Je, wizara imefanya tathmini ili kuona kwamba vifaa hivyo vimewasaidia vipi vijana hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, kwanza wizara yangu imefanya tathmini juu ya mambo yote au juu ya mradi wa *MACEMP* uliyopelekewa. Lakini tathmini hiyo inaelekea na kuwa na uhakika kuwa wengi waliopewa hawakufanya vizuri katika miradi hiyo na ime-*fail* kabisa, na ni kutokana na kukosekana kupewa elimu mwanzo.

Suala la pili, ni kweli vijana baadhi yao na sio vijana tu, hata viongozi waliopewa miradi hii pamoja na wanavijiji mbali mbali waliuza boti hizo. Hatua zinaendelea na tunaendelea kuwafuatilia kwa karibu zaidi.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi hii kutupa afya njema. Namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa kuna kikundi kimoja cha Paje cha ushirika, walichukua mikopo wakawa wanashughulika na mambo ya uvuvi na mkopo ule walinunua nyavu, lakini serikali iliwaambia wazirejeshe zile nyavu ni uvuvi haramu. Vijana wale walijisalimisha wakazirejesha, serikali iliniahidi kwamba watawapelekea nyavu zile. Lakini hadi leo hii nyavu zile hawajapelekewa. Mhe. Waziri ataniambia nini kuhusu suala hili.

Mhe. Naibu Spika: Swali lilikuwa linahusu boti, lakini Mhe. Waziri kama unalojibu mjibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwa sasa kupitia bajeti hii na wizara hii haitakuwa na uwezo wowote wa kuwapatia vijana wale nyavu na vitu vyengine vinavyohusiana na hayo. Lakini hali itakaporuhusu tutaendelea kuwasaidia na katika zile sehemu zao za hifadhi tunaweza kuwapatia vifa hivi kama ilivyo.

Nam. 54

Udhibiti wa Maradhi ya Muhogo

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Tatizo la ugonjwa wa muhogo wa kufanya jasi katika majani (*cassava mill bugs*) ni tatizo la zamani na sugu katika eneo lote la Jimbo la Wawi. Kwa kuwa ugonjwa huu husababisha muhogo kuwa na majani yaliyojikunja na hatimaye mazao kuwa machungu au muhogo kuwa na *'brown drops'* na hatimaye muhogo huo kuwa hauliki.

(a) Je, serikali imeshindwa kupata dawa ya ugonjwa huu.
(b) Ni lini serikali itatoa mbegu ya muhogo inayohimili ugonjwa huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima kuweza kuja hapa na kuendelea na majuku yetu. Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 54 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali bado haijashindwa kutafuta dawa ya maradhi haya kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali za kitaifa na kimataifa. Hivyo, serikali inaendelea na utafiti wa kudhibiti maradhi haya. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli maradhi haya si janga na Zanzibar tu, isipokuwa ni janga na ukanda mzima wa Kusini mwa Afrika na jitihada mbali mbali zinafanywa kuweza kupata suluhisho la kudumu la maradhi haya. Kwa upande wetu wa hapa Zanzibar sisi ni afadhaliya kuwa na mbegu zinazostahamili maradhi haya.

(b) Kuhusu mbegu mpya ya zao la muhogo. Wizara yangu kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo inapendekeza mbegu nne ambazo zinastahamili wadudu na maradhi ya muhogo ikiwemo maradhi ya michirizi na wadudu wengineo. Mbegu zenyewe ni hizi zifuatazo:-
   (i) Kizimbani;
   (ii) Kama;
   (iii) Machui; na
   (iv) Mahonda.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa maradhi haya ya muhogo ya aina ya *cassava mill bugs* ni ya kipindi kirefu sana na kwa kuwa Wazanzibari wengi wakiwemo wa huku Kusini Unguja ikiwemo Makunduchi, Jambiani na sehemu nyengine pamoja na ukanda wa Mashariki ya Pemba wanategemea sana mihogo kama chakula chao cha kawaida.

(a) Kutokana na maradhi hayo zao la muhogo limekuwa halipatikani sana. Je, ni tafiti ngapi ambazo zimefanywa na serikali kwa ajili ya kuweza kutubadilishia mbegu. Kwa mfano, muhogo pira ule ukauchanganya na mbegu hizi za kawaida zinakuwa zinastahamili sana na maradhi haya. Hivi serikali imeshawahi kuchanganya baina ya muhogo pira na yule wa kawaida kwa ajili ya kuangalia ni kwa kiasi gani unaweza kuhimili maradhi haya.

(b) Kwa kuwa upande wa Mashariki ya Pemba kule hawana uzoefu sana wa kulima viazi vikuu, ili kuwa mbadala wa chakula cha muhogo. Je, ni lini seriklai itakwenda kutoa taaluma kule sehemu za Wawi, Vitongoji, Mwambe, kwa sababu mazao ya muhogo hawayapati na badala yake wakapanda viazi vikuu, ili kuwa mbadala wa muhogo kwa vile muhogo maradhi haya hayajapata tiba.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, tafiti zilizofanyika kwa kuchanganya muhogo wa aina ya pira na yule wa kawaida kwa ajili ya kuzalisha mbegu nyengine, swali hili nitamjibu kwa maandishi Mhe. Mjumbe.

Pili kuhusu kutoa taaluma sehemu za Wawi katika kilimo hichi cha muhogo. Mhe. Mwenyekiti, taaluma inatolewa kila siku kutokana na haya maradhi ambayo tunayo ni maradhi ya kudumu, kwa sababu maradhi haya tunaweza kusema ni sawa na maradhi ya janga la UKWIMWI. Kwa hivyo, taaluma inatolewa na bado kama nilivyosema tunaendelea kufanya tafiti, kwa ajili ya kupambana na maradhi haya.

Kwa maana hiyo, bado watu wa Wawi kupitia maafisa wetu wanapewa taaluma, ili kujua na kuliondosha hili tatizo na ambapo tumesema wamepata mbegu nyengine na hivyo hivyo, ili mbadala wake baada ya kwamba watu wasiache, kwa sababu muhogo ni chakula chetu kizuri kuona kwamba mbegu hizi zina matatizo, ili kupanda mbegu nyengine.

Tatizo lililopo ni kwamba hizi mbegu ambazo tumezitoa wakulima wengi wanaona kwamba zinachukua muda mrefu kwa mwaka mzima na hili ndilo tatizo ambalo lipo. Hata hivyo, wakulima wanaendelea kupewa taaluma mbali mbali na *Inshallah* watafahamu juu ya hili.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Waziri katika tafiti zilizofanywa, watafiti wamegundua maradhi haya yanatokana na nini na tafiti ngapi ambazo zimefanyika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, sikulifahamu vizuri naomba areje tena Mhe. Mjumbe swali lake.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, rejea kidogo kidogo swali hakulifahamu Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Mhe. Naibu Spika, ni tafiti ngapi ambazo zimefanyika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, tafiti zilizofanywa kuhusu maradhi haya ni tafiti tano na katika tafiti hizi imeonekana kwamba maradhi haya yanasababishwa na virusi vya muhogo na hasa hutokana na nzi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru na mimi kuniona, ili nipate nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa suala hili la ugonjwa wa mihogo limezidi hasa katika maeneo ya Mashariki ambao ni ukanda wenye jua kali zaidi. Vile vile wizara hii inao wataalamu wengi pamoja na mabibi shamba na mabwana shamba hatuwaoni katika kanda zile za mashariki ambazo ni sehemu za ukawe wa jua kali kuwaelekeza watu katika kilimo hicho.

Hivi ni nili Wizara ya Kilimo na Maliasili itawapeleka mabibi shamba na mabwana shamba kama vile Mwambe, Vitongoji na Micheweni, kwa ajili ya kuwaelekeza wananchi kilimo kinachostahamili ukame pamoja na huo ugonjwa wa muhogo, kwa sababu kule ndio kilimo kikubuwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, sehemu ambazo amezitaja ni kweli tulikuwa na matatizo ya mabibi shamba na mabwana shamba. Kwa mfano, shehia 6 anaweza akapewa bwana shamba mmoja ahudumie sehemu hizo zote na hilo alilolisema Mhe. Mjumbe inawezekana kwamba hizo sehemu hazifiki mabibi shamba au mabwana shamba. Lakini tatizo hili hivi karibuni litaondoka ambapo tunaajiri mabibi shamba hao na hususan kwa hiyo sehemu aliyoitaja tunawapeleka mabibi shamba na kwenda kutoa hiyo taaluma.

Mhe. Naibu Spika, nanayo imani kwamba tatizo hilo litaondoka, kwa ajili ya kwenda kuwapa taaluma. Vile vile kuna tatizo jengine ambalo lipo wakati nilipokuwa kwenye ziara nililikuta, kwamba mabibi shamba wanakwenda, lakini kutokana na hali hata wale wakulima hawawezi kufananisha bibi shamba yupi na afisa yupi na hili ndilo tatizo lililotokea.

Kwa mfano, anakwenda bibi shamba lakini akifika pale anasema bibi shamba au bwana shamba hajenda na tumelikuta tatizo hili lipo na tunakuta saini za bibi shamba ambaye ametia saini zake na tunauliza huyu ni nani, kumbe hawajui kutofautisha baina ya bibi shamba au bwana shamba na afisa, na hili ni tatizo ambalo lipo. *(Makofi)*

Nam. 66

Mapato Yanayotokana na Shughuli za Bandari

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa kuwa njia mojawapo ya mapato ya serikali inatokana na makusanyo ya kodi mbali mbali za bandari ni kwa wasafari wa vyombo vya baharini.

(a) Je, serikali inakusanya wastani wa shilingi ngapi kwa siku kwa kila chombo kinachoondoka kwenye Bandari ya Zanzibar kwenda Dar-es-Salaam.
(b) Je, serikali inatumia utaratibu gani wa kuhakikisha kuwa mapato yote yanayokusanywa bandarini yanawasilishwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 66 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo. Shirika la Bandari linakusanya ada za kuegesha meli na ada za ardhia kwa mizigo. Makusanyo ya kodi mbali mbali zilizobakia zinahusiana na masuala ya wasafiri (*Port Services Charge*) yanakusanywa na Serikali Kuu kwa kupitia *agent* wao *ZRB.*

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

(a) Makusanyo yote yanayokusanywa na *ZRB* kwa madhumuni ya mapato ya serikali yanatokana na utaratibu maalum wa kuweka mapato hayo kutokana na mtu anayesafiri kulingana na idadi ya abiria. Hivyo, hakuna takwimu maalum kusema kwamba kwa kila siku tunapata kiasi gani, isipokuwa kwa kila chombo kwa mujibu wa idadi yake kulingana na rate iliyopangwa ya shilingi 2,000/= kwa kila abiria.

(b) Suala la mapato haya yote ya serikali kwa namna moja au nyengine yanarudi serikalini, kwa sababu ndio serikali ilifanya maamuzi ya kuwa na *agent* mmoja tu mkusanyaji, ili kuweza kudhibiti mapato hayo yasiwe na wakusanyaji wengi kwa ajili ya kudhibiti matumizi ambayo sio halali na pia udhibiti wa fedha zenyewe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, swali hili linajieleza kwamba je, serikali inakusanya wastani wa shilingi ngapi kwa siku wakati chombo kinapoondoka bandarini Zanzibar kuelekea Dar-es-Salaam na hizi takwimu zipo, nafikiri ndugu yangu alikuwa hajawa tayari na kama hajawa tayari anijibu tu na wala hakuna tatizo swali hili nimpe muda, ili aweze kuja kunijibu vizuri, maana yake hayo majibu alikuwa akiandika hivi sasa. Kwa hivyo, hayuko tayari na wala hakuyo *serious* kunijibu.

Kutokana na hali hiyo, naomba kwa heshima kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, nimpe muda mpaka atakapokuwa tayari aje kunijibu na kama haliko upande wake pia tulirejeshe tena na mimi niko tayari kustahamili na wala sio majibu ya mkato kama hivi. Kwa sababu tunahangaika kutafuta maswali na baadae tunapata majibu kama hivi, hali hii inavunja moyo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, tulichokieleza ni kwamba swali lake anataka kwa chombo kimoja kinakusanya kiasi gani. Sasa tulichomjibu ni kwamba kwa kila chombo kina idadi yake. Kwa mfano, chombo kinapakia watu 200 kitakuwa kina idadi yake maalum na kama chombo kinapakia abiria 300 pia idadi yake itakuwa ni maalum.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutwambia kwamba tuweke *rate* kwa kila chombo na mapato ya serikali ni shilingi 100,000/= au shilingi 200,000/= na hivyo haiwezekani. Lakini tumemjibu kwamba kuna *rate* ambayo inayotokwa na serikali kwa kila abiria anatoa kima maalum cha fedha.

Kwa hiyo, jambo la msingi utagundua idadi hiyo ya fedha kutokana na kile chombo husika abiria wangapi wamepanda na tozo walizotozwa na wala hakuna majibu ya kusema kwamba vyombo vyote vinachangia shilingi 50,000/=. hakuna majibu hayo. Isipokuwa utaratibu ni kwamba kwa kila chombo kila abiria anatozwa yeye tozo yake, kwa maana hiyo hakuna idadi maalum.

Hivyo, kilichopo ni kwamba unachukua idadi ya abiria waliosafiri ndio utapata kujua hesabu ya mapato kwa siku ile tena kwa chombo kile na wala hakuna kiwango maalum kinachotozwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kama boti inapakia watu 1,500 unafanya ile hesabu na itajulikana na hesabu iko wazi Mhe. Naibu Spika na wala haitishi na kama hujawa tayari kuwa na data hakuna tatizo Mhe. Naibu Waziri na serikali kutupa sisi majibu ameagiza Mhe. Rais. Kama utakuwa hujawa na jawabu utaandika kwa maandishi na nitakupa muda kwani tatizo liko wapi Mhe. Naibu Waziri, na wala usikubali kushindwa, kwa sababu serikali ipo na katika mpira mambo matatu hutokea kama vile kushinda au kushindwa ama sare.

Sasa kama Mhe. Naibu Waziri hajawa tayari naomba anijibu kwa maandishi na wala hakuna ugomvi na tusibishane kitu kiko wazi, na wananchi wanatusikiliza na hiki ni chombo cha wananchi na ukenda *ZRB* utaipata hiyo *data*. Kwa mfano, abiria 1000 ni sawa na shilingi ngapi, yaani utaipata jawabu.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu aliyojibu Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, kwa kweli nimemfahamu sana Mhe. Mjumbe swali lake. Kwa hivyo, nataka niweke sawa tu anachokiuliza Mhe. Mjumbe na anachokijibu Mhe. Naibu Waziri, wanahitilafiana kidogo. Lakini kimsingi ni kama hivi ifuatavyo. *(Makofi)*

Vyombo vinavyoondoka katika Bandari ya Zanzibar kuelekea Dar-es-Salaam vina ada za aina mbili, ya kwanza ni ile ambayo inakwenda kwenye Serikali Kuu ndio ile kodi ya Bandari, ambayo kila abiria analipa shilingi 2,000/= na Mhe. Naibu Waziri ameeleza. Pili ni zile ada zinazolipwa za bandari yenyewe haziendi Serikali Kuu. Kwa mfano, kuna ada ya kuegesha meli na ada nyengine ambazo hizi haziendi kwenye Serikali Kuu, zinakwenda kwenye Shirika la Bandari. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa maelezo ya swali la Mhe. Mjumbe, kwa kuongezea majibu ya Mhe. Naibu Waziri ni kama ifuatavyo. Ada inayokwenda Serikali Kuu ambayo kila siku inaweza kupatikana kwa mujibu wa swali lake ni ile ada ya bandari (*Port Services Charge*), kutoka Zanzibar kwenda Dar-es-Salaam ni shilingi 2,000/= kwa kila abiria. Sasa kila chombo kina idadi yake ya abiria ambayo wanaweza kubebwa, yaani ile *maximum capacity* yake, idadi yake ya juu kabisa na kila chombo kina idadi yake.

Kwa hivyo, kama ingekuwa kila siku idadi ile inafikiwa swali la Mhe. Mjumbe lingepata majibu ya kila siku. Kwa mfano, kila chombo ingekuwa kinapakia abiria idadi fulani kama vile 200, chengine 400 na kila siku inafikiwa ile idadi. Swali la Mhe. Mjumbe lingepata majibu, kwamba 200 x 2000 na 400 x 4000. Lakini kwa sababu abiria wanategemeana na hali ya msimu kuna baadhi ya siku abiria wanakuwa wanapungua kwa kila chombo.

Kutokana na hali hiyo, ndipo pale aliposema Mhe. Naibu Waziri kwamba upatikanaji wake kwa usawia wa kila siku unakuwa kidogo mgumu, kwa sababu kuna siku chombo ambacho kina *capacity* ya abiria 1000 kinaweza kikapakia 800 na siku nyengine kikapakia 600 au 700, sasa kwa usawia wa kila siku unakuwa ni mgumu. Kwa maana hiyo, hata mimi ninapoziangalia zile takwimu za zile fedha ambazo ninazoziona kila mwezi, naona hata kila mwezi nazo zinatofautiana zile *Port Services Charge*.

Kwa hiyo, nataka nimueleze Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu kwa jumla Mhe. Naibu Spika, kwamba pamoja na majibu ambayo ametoa Mhe. Naibu Waziri na majibu ya nyongeza ni kweli kwamba tunakusanya hizi fedha, lakini kwa usawia wa kila siku hazitakuwa sawa, kwa sababu inategemea na idadi ya abiria wanaopanda siku ile kwa mujibu wa chombo chenyewe.

Mhe. Naibu Spika, hilo ndilo jibu ambalo nilitaka nimueleze Mhe. Mjumbe. Vile vile kwa upande wa swali lake la pili, utaratibu wa kuhakikisha kwamba mapato yote yanayokusanywa bandarini yanawasilishwa serikalini haitawezekana, kwa sababu kuna mapato mengine yanawasilishwa na Shirika la Bandari lenyewe, yaani Shirika la Bandari lenyewe ndilo linalokusanya na mapato ya Serikali Kuu ni yale ambayo tumemuachia wakala wetu *ZRB* ndio anayetukusanyia.

Kwa hivyo, ninadhani kwamba jibu alilolitoa Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu ya nyongeza ambayo nimeyatoa mimi, hivyo ninamuomba Mhe. Mjumbe aridhike. Lakini kama atahitaji maelezo ya ziada kuhusiana na hali ya upatikanaji wa fedha, mimi niko tayari kukaa naye na nitajaribu kuwafuata wataalamu wa *ZRB*, ili waweze kumfahamisha pia wataalamu wa Shirika la bandari wanaohusiana na masuala ya fedha, ili waweze kukaa naye wampe maelezo ya ziada, tuko tayari kufanya hivyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, tuone Waziri dhamana wa Fedha Zanzibar kama atahitaji maelezo nimfuate niko tayari nahitaji maelezo kutoka kwake.

Mhe. Mahamoud Thabid Kombo: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Juzi wakati wa bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano lilizungumziwa Shirika la Bandari ambalo linazalisha takriban bilioni 15 kwa mwaka, naamini hayo ni mapato ambayo yanatoka sehemu mbali mbali. Likazungumziwa pia Shirika la Meli ambalo linazalisha bilioni 1.28 kama mapato ya uwakala. Sasa naamini kuna na mapato mengine ambayo yanakwenda moja kwa moja ZRB na kwengineko.

Mimi swali langu dogo tu Mhe. Naibu Spika, lenye kifungu a na b.

a) *Passenger terminal* yetu ina uwezo wa kuwahudumia abiria wangapi; hii tuliyokuwa nayo hivi sasa na
b) Kwa siku hivi sasa tunahudumia wastani wa abiria wangapi kwa vyombo vinavyokuja pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, *passenger terminal* yetu ya bandarini kwa wakati mmoja inao uwezo wa kuchukua watu zaidi ya 300 kwa wakati mmoja na wastani wa wasafiri wetu Unguja/Dar es Salaam, Unguja/Pemba uko takriban 1000 mpaka 1200 kwa siku.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea tumepata wageni leo. Tunao wanafunzi kundi la pili kutoka Skuli ya Ben-bela jumla ni 51 na walimu wao ni 3, naomba muwatambue walimu na wanafunzi simameni (*Makofi*). Waheshimiwa hao ndio wageni wetu wa leo tunawashukuru kaeni.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Fedha na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 Wizara ya Habari, Utamaduni, Uwezeshaji na Utalii

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba niwaarifu kwamba mpaka sasa hivi tuna wachangiaji 24 wamechangia wachangiaji 6 kwa hivyo waliosalia tunataka tumalize kipindi hiki cha asubuhi ikifika saa 7.00 tuwe tumeshamaliza. Sasa nawaomba wale wanaotaka kuchangia wasitoke toke nje nikiita jina Mheshimiwa katoka sirudii waliokuwepo watachangiya na tusipende kurejea rejea, mtu kama ana mchango mdogo aseme huo huo ampe nafsi mwenziwe. Sio tena anakaziya, anafanya hivi na hivi itakuwa ni yale kwa yale.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia kukutana hapa asubuhi hii kujadili bajeti hii ya Wizara ya Habari kwa mwaka 2014/2015. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba lakini pia niwapongeze watendaji wake ambao wamemsaidia yeye kumuwezesha na kuwasilisha hotuba ile hapa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanzia nitaanza na maeneo ya kipaumbele ya kisekta kwa mwaka, malengo mazuri lakini pawe na nia ya udhati na uthabiti wa kutekeleza malengo haya ya vipaumbele hivi. Nasema hivi nimeangalia lengo namba 4 linasema kuwashajihisha wasanii, kuitumia Studio ya Rahaleo kurekodia kazi zao ili waweze kunufaika na sanaa zao. Nina wasi wasi na hili neno kunufaika na sanaa zao, kadri nitakavyoendelea kuchangia mbele wataona kwa nini nina wasi wasi na wasanii kunufaika na sanaa zao, ndio maana nikasema malengo mazuri, tunaandika vizuri lakini kuwe na niya na uthabiti wa kutekeleza malengo haya.

Mhe. Naibu Spika, nikimaliza hapo niingie Shirika la Utangazaji; hili nalo lina mipango mizuri kama lilivyojiwekea lakini kama nilivyosema pawe na nia na uthabiti wa kutekeleza malengo haya. Nikiangalia lengo namba 3 *page* ya 23 Mhe. Naibu Spika, inasema kutoa taarifa sahihi na kwa wakati pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa vitendea kazi vilivyo bora kwa ajili ya kuondoa matatizo ya upokeaji wa habari. Kumekuwa na matatizo mengi wajumbe wengine wataeleza mimi sitaki kwenda *in detail*, lakini niseme tu kwamba tatizo letu waswahili tunajua kuandika sana lakini utendaji unakuwa mdogo mno.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo Shirika la Utangazaji nina malalamiko yangu kidogo ambayo Mhe. Salma na yeye jana ameyagusia. Malalamiko hayo Mhe. Naibu Spika, ni kuhusiana na suala la wafanyakazi wanawake wa ZBC pamoja na wageni wanaokwenda pale kutakiwa kuvua mabui bui yao nje ya ofisi. Mheshimiwa haipendezi kwa mwanamke pale ni barabarani ukiingia tu pale kuna *reception* ya kuingilia kwenye jengo hili, lakini haipendezi sana kuwataka sio vizuri kukaa na mabui bui ofisini, lakini pia sio vyema kuyavua pale nje hadharani ni vyema wafike katika ofisi zao wavue mabui bui, wawe na chumba maalum wakifika wanavua wanabaki na nguo zao ambazo wanavaa au kama kuna tatizo la mavazi basi Mkurugenzi kama ana ubunifu zaidi, angewatafutia *uniform* wafanyakazi hawa ili kuona kwamba wafanyakazi wanakwenda na utaratibu ule ambao mwenyewe anataka.

Mhe. Naibu Spika, lakini la pili hebu hii ZBC iwaachie hawa wanawake wana *issues* nyingi ambazo ni *chronic* ambazo wanatakiwa wadili nazo kuliko ku- *deal* na *issues* ndogo ndogo kama kuvua mabui bui ofisini. Ni vyema wakafanya yale makubwa yanayowahusu kuliko hivi vidogo vidogo, najua kila sehemu Mhe. Saleh alisema ni vizuri kuiga jema, lakini kila sehemu kuna utaratibu wake. Pale sio CNN kama mtu ataingia na

kichwa wazi au vimini hairuhusiwi, lakini tuna taratibu zetu na silka zetu na tamaduni zetu, ni bora wakawatengea chumba maalum wanawake wale ili kuweza kuvua mabui bui yao badala ya kuvua hadharani haipendezi sio vizuri wala sio staha.

Mhe. Naibu Spika, nikimaliza hapo sasa naingia kwenye hizo *chronic issue* ambazo ZBC wanatakiwa wa-*deal* nazo badala ya ku- *deal* na mabui bui, kuna deni la ZBC linalodaiwa na Afisi ya Hatimiliki hili limeshakuwa donda ndugu maana yake halitibiki tena tangu mwaka 2010. Ofisi ya Hakimiliki inadai deni hili ZBC mpaka hivi leo hawajalipa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 98 (6)(b) nataka kuanza kuondoa shilingi mia moja ya Waziri kama sitopata maelezo mazuri ya Mhe. Waziri kuhusiana na deni hili la hatimiliki kila siku wamekuwa wakitupiga dana dana, hapa wanatoa majibu ya kisiasa tutalipa ikimaliza bajeti, kuanzia mwezi wa Oktoba tutafanya lakini hamna chochote kinachofanyika.

Mhe. Mwenyekiti nataka nieleze kwa mujibu wa vifungu vya sheria, Tanzania imeridhia mkataba BENWA 1886 ambao mkataba huu kuna kifungu unasema "hakuna kituo chenye wajibu wa kufanya *promotion* ya nyimbo ama filamu au aina yoyote ya sanaa bila ya malipo". Mimi nathubutu kusema kwamba ZBC inawakandamiza wasanii, hivi inakuwaje *Private sectors* hizi kina *cable* kina *Coconut* FM na wengine wanalipia zile kazi za wasanii wanazotumia, iweje leo ZBC ishindwe. Hivi inaonesha mfano gani kwa zile *Private Sectors* kama wewe mwenyewe unashindwa kulipia wale watafanya nini Mheshimiwa? Haipendezi ni vizuri ZBC ikajipanga ili kuona kwamba inalipa deni lile.

Mhe. Naibu Spika, nina kopi za barua 8 ambazo ikiwemo na ya Waziri ambazo hatimiliki inaiandikia Shirika la Utangazaji kuona kwamba angalau wanapata ile pesa ambayo wanaidai. Kuna barua moja ambayo imejibiwa na ZBC hii hapa, malalamiko mengi sijui wameongeza pesa, yaani deni haliko sawa na sababu tele lakini hiyo haimaanishi kwamba wasilipe.

Kwa sababu kwa mujibu wa kanuni za *Copy right Act* ya Na.14 ya 2003 ambayo imefanyiwa *amendment* mwaka 2010 na Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, ndie aliyekuwa *Signatory* kipindi kile, inasema kifungu cha 3(1) inasema kuna *cable* ambayo inaonesha malipo ambayo kila kituo inatakiwa kulipa *minimum fee for public radio and television fee* T.shs. 5,000,000/= *late payment* unalipa *double* kwa kile unachodaiwa.

Mhe. Naibu Spika, malalamiko ya ZBC wacha walalamike kwamba wamefanyiwa *double* deni lakini basi na walipe zile ambazo wanadaiwa waache ile *penalty*, walipe zile wanazodaiwa hizo *penalties* wote wanajenga nyumba moja, wote ni Serikali ya Mapinduzi, wanaweza wakakaa wakazungumza lakini angalau wawape kile wanachodai hiyo *penalty*. Wanaweza kukakaa wakapunguziana Mhe. Mwenyekiti, haipendezi msiwe samaki mkalana nyie kwa nyie wewe ukiwa hulipi lile deni la mwenzio unamzorotesha kazi zake yule. Sio kazi zake tu yule, lakini unakandamiza wasanii ambao wanatumia jasho lao na nguvu zao kufanya kazi, ili kuona wanapata chochote cha kwenda mdomoni.

Mhe. Naibu Spika, haipendezi ni vyema ZBC ikalipa deni la hatimiliki na sitaki kusema kwamba Waziri wa Katiba ameshindwa kusimamia idara yake kupata haki yake kwa sababu na yeye anachukua juhudi, lakini ni vyema hawa wanafanyakazi kwa *collective responsibilities* lakini msitupe majibu ya kisiasa hapa. Kwa sababu hata Waziri wa Katiba na Sheria alivyojibu alijibu kisiasa siasa, tukamuacha kwa sababu halimhusu tukajua tutakuja kwa Waziri wa Habari tutapata maelezo, tutajua wapi tutamshika.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, haipendezi ZBC mnadaiwa miaka mitano mara mbili si vyema mlisaini zile haki za wasanii na wao wafaidike na kazi zao, kama nilivyosema sisemi patachimbika si kawaida yangu kuchimba lakini nasema Mhe. Waziri ajipange aje na maelezo mazuri ili nimpitishie bajeti yake.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Salma alipochangia alisema hapa kwamba inaonekana kwamba kwenye hii Wizara kuna mfumo dume na mimi naema kuna mfumo dume kweli, kwa sababu wanakandamiza wanawake. Mhe. Naibu Spika, Mkurugenzi wa Hakimiliki ni mwanamke pengine ule mfumo dume ndio unapelekea kwamba kumtikisa tikisa lakini haipendezi ni vyema Waziri akachukua hatua kuona kwamba ZBC inalipa deni la hakimiliki.

Mhe. Naibu Spika, nikimaliza hapo niingie kidogo katika hoteli ya Bwawani; hoteli ya Bwawani napongeza jitihada za uongozi zinazochukuliwa na uongozi wa hoteli hii kuona kwamba hoteli ya Bwawani inakuwa na

mazingira mazuri, sambamba na hilo nipongeze kwa makusanyo mazuri ya asilimia 89 ambayo wamefikia lile lengo walilopangiwa kufika.

Nikiangalia katika malengo waliyojipangia mwaka huu wamesema kwamba hoteli wamejipangia kufanya ukarabati wa maeneo ya hoteli vikiwemo vyumba na kumbi. Kuna kipindi Mhe. Naibu Spika, hoteli ya Bwawani ilifanya ukarabati wa paa la Salama *hall*, lakini hivi karibuni nilikwenda pale Bwawani *hall* na nikakuta dari ya salama *hall* imepasuka kabisa, sio vizuri haipendezi ni vyema wakifanya ukarabati wakakarabati lile *hall* kwa sababu ni *hall* kubwa linalotumiwa na kila mtu na kwa kiasi fulani linaingiza fedha nyingi sana, kwa hivyo ni vyema tukalikarabati ili tulitunze lidumu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia nizungumzie michezo; kuna hawa watoto walemavu ambao huenda nje ya nchi kushindana katika mashindano ya michezo mbali mbali, hawa watoto ni walemavu wa akili, hapa hutoka watu wazima na akili zao na kwenda huko lakini hawarudi na chochote hapa, lakini juzi tumesikia watoto walemavu wa akili wamekwenda wamerudi na medali ishirini na dhahabu na nyengine za silva.

Mhe. Naibu Spika, wito wangu ni vizuri watoto hawa wanaitangaza nchi, ni vizuri wakienda huko wakirudi *angalau* Wizara au serikali yetu kwa ujumla iwe inawaangalia, lakini pamoja na watoto hao pia na walimu wao ni vyema wakawatizama. Kwa hivyo ni vyema Serikali kupitia Wizara ya habari ikawaangalia watu hao.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa nafasi lakini namuomba Mhe. Waziri aje anipe majibu mazuri kuhusu deni la ZBC kwa hatimiliki.(*Makofi*)

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi asubuhi hii kupata nafasi ya kusimama katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kuhusu Makadirio ya Matumizi ya mwaka 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama mbele ya baraza hili nikiwa bado nina pumzi na angalau mdomo unakwenda ukirudi. Pia nikushukuru wewe na nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kutuandalia hotuba hii mwanana.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mimi sitokuwa na mengi lakini nianze na Shirika la Utangazaji yaani sekta ya habari. Shirika hili au sekta hii ni muhimu sana hapa nchini kwa sababu lengo kubwa la habari kwanza ni kutoa habari, kuelimisha watu habari za kisiasa, za kiuchumi na maendeleo kupitia shirika hili ndio habari hizi zinawafika wananchi.

Sasa Mhe. Naibu Spika, katika hali hii shirika hili lione kuwa lina dhima na kazi kubwa ya kuelimisha jamii ingawaje kwa shirika ni muda mfupi, lakini kama redio ni kitu cha zamani sana na kwa kuwa redio na Televisheni ya Zanzibar ndio mdomo wa serikali, kwa hivyo linawajibika kufanya kazi, ili hizi radio za FM zilizochipuka ambazo ni haki yao kuwepo Shirika hili lisije likashindwa na vyombo hivi ambavyo vilikuja juzi. Lakini mwendo wake unaonekana kuwa huenda hizi Radio za FM zikawa mbele kuliko hili Shirika letu la serikali kutokana na huduma zake.

Sasa tukifika hapo Mhe. Naibu Spika, itakuwa serikali kwa upande wa utangazaji imepoteza kipaji chake. Shirika hili ni la zamani yaani Radio na Televisheni kwa Afrika Mashariki *coloured television* Zanzibar ni ya mwanzo lakini leo Zanzibar iko mkiani, kwa nini kwa huduma mbaya ambazo zinatolewa. Tunawafanya watazamaji wetu kukosa hamu za kutizama vipindi vyetu vya Radio na Televisheni zetu na hatimae watu wengi kuelekea kutizama *Star* TV, ITV, TBC na nyenginezo ambazo ingawaje za Tanzania lakini si za Zanzibar. Zanzibar ndio petu kwa hivyo hiki chetu tungelikienzi tukakitukuza, ili kikapata kwenda mbele zaidi.

Mhe. Naibu Spika, habari ni mojawapo ya njia ya mawasiliano baina ya mtu na mtu, taasisi na taasisi na nchi na nchi. Chombo hiki kitakapotumika vyema kitavutia wasilikilizaji na watazamaji. Kitakapotumika vibaya kitapoteza watazamaji na wasilikilizaji walio wengi. Katika kufanya kazi kwake, vipindi vinavyoandaliwa ni vile ambavyo vinaelimisha jamii maadili mema, iwe ni vile vinavyoelekeza mambo mazuri.

Mhe. Naibu Spika, vipindi vya ZBC havielimishi zaidi lakini maana hata kupotoa ni taaluma. Kuna kipindi ambacho Mtazamani anapata taaluma lakini na kupotosha ni taaluma utakuwa umemuelimisha je, umemuelimisha kulingana na maadili yalivyo? Utakutia kipindi ambacho una-*act* pengine sijakiona lakini viko vya aina hiyo katika Radio au vipindi mbali mbali kufanya mwizi anashinda katika mambo yake anayofanya.

Kwa hivyo kama kuna vijana wanaotazama pale unamuonesha namna gani aweze kutumia mbinu za kufikia kuweza kupora au kufanya ujambazi. Hiyo ni taaluma lakini je, matokeo yake taaluma hii ni nini?

Mhe. Naibu Spika, nigusie kidogo kwenye sekta ya utamaduni. Mimi ninataka Mhe. Waziri anisaidie maana halisi ya utamaduni hapa Zanzibar, aliposema utamaduni wetu, tunakusudia ni nini, ni upi utamaduni wa Mzanzibari kwa hivyo ningeomba nipate maana ya neno hili utamaduni. Kwa sababu neno hili linafuatana na maneno mengi sana. Kuna utamaduni, silka, desturi, mila; mambo haya yote unapoyakusanya maana yake ni nini kwa sababu utamaduni mimi sijui maana yake.

Je, tujaalie hivi nilivyovaa mimi ndio utamaduni wa Mzanzibari? Je, vile alivyovaa mwenzangu mwengine kavaa shati kama hii lakini yeye hana kofia je, ndio utamaduni wa Mzanzibari. Je, alivyovaa Mhe. Abdalla Juma ndio utamaduni wa Mzanzibari, je, yule anayetembea barabarani mwanamke kifua wazi ndio utamaduni wa Mzanzibari? Je, yule mwaname aliyetia *jeans* linambana na fulana mikono mifupi ndio utamaduni wa Mzanzibari? Wote hawa tunasema wanakwenda na utamaduni wetu. Kwa hivyo ni upi utamaduni wetu hasa. Ni ipi hasa mila yetu, ni zipi silka zetu, ni zipi desturi zetu, mpaka tuone kwamba hii ndio yetu sisi Wazanzibari?

Mhe. Naibu Spika, niseme kwa kuwa wote watakaovaa hivi serikali wote wanatukubalia niseme huu ndio utamaduni wa Mzanzibari. Lakini Mhe. Naibu Spika, siku chache zijazo waislamu tunaingia katika mwezi mtukufu wa Ramadhani na tunapigana vibega masokoni, barabarani, kwenye daladala kuna mtu kafunga, kuna mtu kaingia kwenye gari *half necked* na jicho halina pazia, sijui mambo haya Mhe. Naibu Spika, tutayakabili vipi ili waislamu saumu zao zisibatilike. Kwa sababu tumeruhusu kila mmoja anakwenda na utamaduni wa Mzanzibari.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu michezo Wizara hii kwa michezo labda uliopewa kipaumbele ni mpira wa miguu peke yake au zaidi. Lakini kuna michezo mengine ya ndani ambayo inaitwa indo *games* sijui wanaipa kipaumbele kiasi gani. Jana kuna mchangiaji mmoja aliona kuwa kutoka katika Kombe la Muungano hadhi ya mpira Zanzibar imeteremka, mimi nina mtizamo tofauti. Kwa sababu huko nyuma Zanzibar ilikuwa inashiriki katika mashindano ya Afrika Mashariki, ilikuwa tunaita *gossage cup*, ilikuwa inaingia kama Zanzibar inayojitegemea na ilikuwa inaleta kivumbi kikubwa sana kwa sababu ilikuwa inaingia kama nchi. Leo tumebakia katika kombe la Muungano Kitanzania sisi ni nchi. Kwa hivyo kwa hapa tulipojikwamisha ndio tumeshakwama tu. Mtu asiseme kama tungebakia kule wachezaji wangeendelea, wangezidi kudidimia. Kwa sababu wasingeingia kama Wazanzibari, wangeliingia kama Watanzania.

Mhe. Naibu Spika, kuna maeneo ya utalii na utalii kulingana na taarifa za serikali pengine tayari, lakini mimi sijaamini kuwa inaipita karafuu kwamba utaliii unaingiza zaidi. Kwa hivyo utalii ni sekta kubwa inayoongeza pato la taifa. Watalii wanaoingia zaidi ni hawa wageni wa Ulaya na nchi nyengine za mbali. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu inafuata sana haki za binadamu imemuachia uhuru kila mtu aende na afanye apendavyo. Wakati ambao wengine waliomo hawajazaliwa Sheikh Abeid Aman Karume Rais wa Kwanza wa Zanzibar, pamoja na mengi yaliyokuwepo, lakini hajatokea Rais mwengine yeyote ambae kaupa heshima mwezi mtukufu wa Ramadhani kuliko yeye, ilikuwa mtu hata kama si muislam hathubutu kula ovyo mchana mwezi wa Ramadhan akaonekana, na akionekana hivyo ilikuwa anahifadhiwa kuanzia siku ile alieonekana mpaka Ramadhani imalizike.

Mwezi mtukufu wa Ramadhan mwaka jana mimi nilikuwa hapa Unguja, kwa sababu tulikaa kwa hii kazi nikenda mjini nikakuta watu wanavuta sigara bila ya hofu yoyote kwa sababu tumesaini mkataba wa haki za binaadamu. Kwa hivyo kila mtu ana haki kufaya anvyotaka.

Haki nyengine kwa kweli Mhe. Naibu Spika, zina hatari zake, kwa sababu wakaazi walio wengi asilimia kubwa wakaazi sisi ni wa dini ya kiislam, kwa hivyo hawa walio wachache si lazima watufuate, wakitufuata ni vyema lakini pia hii ibada yetu ya Ramadhani waiheshimu.

Mhe. Naibu Spika: Bado dakika tano.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Zinanitosha kwa sababu sina la kusema hata hivyo. Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ni hifadhi ya sehemu na mambo ya kale. Mhe. Naibu Spika, yapo maeneo kadhaa haya ambayo yanahitaji kuhifadhiwa, kutunzwa ili yatoe historia na kwa vizazi vinavyokuja. Kuna majengo ya zamani sana kule kwetu Kengeja sehemu ya Mtule, kuna kisima kilichojengwa miaka ya 18 na kimejengwa kwa mawe na chokaa. Lakini mpaka leo umadhubuti wake unakishinda kisima ambacho kimetiwa makalbi ya saruji ya leo. Sina hakika kwamba eneo lile Wizara hii inalijua kuwa wamelichukua au vipi. Lakini kama hawalijui lipo na ni

sehemu nzuri ingehifadhiwa kile kisima kikatunzwa na ikawa ni mojawapo ya kumbukumbu maalum. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, maeneo kama haya yakitunzwa vyema yanaweza kuwa pia ni kivutio cha hawa watalii ambao ndio tegemeo la uchumi wetu.

Mhe. Naibu Spika, hizo dakika tano mimi sitaki nizimalize nifanye *summary* ya maelezo yangu yote kuwa ZBC ijitahidi kufanya kazi ndio washashindwa na FM Radio zilizochimpuka, TV yetu ni ya mwanzo kuwa ya rangi wasiisahau. Mhe. Naibu Spika, Wilaya ya Mkoani katika mwezi wa Februari/Machi vin'gamuzi vya ZBC vilikataa kufanya kazi na kuna watu walikuwa wameshalipia, walipokwenda kudai waliambiwa wacheni tutawalipa. Mimi ninajua kuwa hawatolipwa pesa lakini walikuwa wasilipie kwa mwenzi mmoja hadi limalizike deni. Mhe. Naibu Spika, mpaka leo wakienda wanaambiwa mtalipwa, mtalipwa, mtalipwa.

Kwa hivyo ningeliitaka ZBC Televisheni waliokuwa kule Pemba Mkoani mwezi wa Februari ving'amuzi vyao vilishindwa kufanya kazi na mliwaahidi watu mtawalipa na hamjawalipa. Ningemuomba Mhe. Waziri kama hajui habari hiyo afuatilie na hawa watu walipwe.

Baada ya kusema hayo ninashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu mfupi. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa kabla sijamwita Mhe. Jaku tumepata wageni wengine *groups* mbili tofauti. *Group* ya mwanzo ni wanamichezo walioshiriki mashindano ya *special Olympic* Kibaha ni walemavu 30 na wamepata medali 30 kwenye mashindano hayo. Medali 17 dhahabu, medali 5 fedha na medali 8 shaba. Kwa hivyo naomba wasimame ili tuwatambue. Tunawapongeza, ahsanteni sana, kaeni. *(Makofi)*

Group la pili ni wanafunzi 30 kutoka Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar wao wamevutiwa sana na hamu kubwa kusikia viongozi wao wanajadili bajeti ambao kiasi kikubwa inawagusa katika masomo yao. Nao wamekuja kusikiliza wenyewe *live* kwa hivyo naomba wasimame na wao. Ahsante sana karibuni, kaeni kitako. Tunaendelea Mhe. Jaku Hashim Ayoub, baadae Mhe. Viwe Khamis na baadae Rufai na Mhe. Panya Ali Abdalla ajiandae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuniruhusu kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Kwanza kabla ya yote nitoe utangulizi wangu kwa kuwapongeza watendaji wakuu wa vyombo vya habari kwa kazi nzuri tu wanayoifanya pamoja na changamoto zinazowakabili. Pia niwapongeze waandishi wote wa vyombo vya habari wakiwemo wa vyombo binafsi na vya serikali pamoja na changamoto wanazokutana nazo. Niwapongeze sana kabisa kwa jitihada wanazochukua na kuwaelimisha watu kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Nianze mchango wangu kwa haraka haraka Mhe. Naibu Spika, bila ya kupoteza muda ninafikiri sitomaliza muda dakika zangu 7 au 5, zitanitosha. Nilikuwa nataka kuzungumza suala la waandishi wa habari kutokupelekwa Dodoma kwa muda mrefu, tatizo hilo hawapelekwi na hawajui wabunge wao wanafanya kazi gani kwa maslahi ya Zanzibar kwa kipindi kirefu.

Nije jambo jengine tulipitisha sheria ya utangazaji ZBC na Shirika la Magazeti, nataka kujua fedha za matangazo bado zinakwenda katika Hazina au zinabakia katika Shirika kwa sababu chombo chochote cha habari kinatakiwa kuwa na msingi wake. Nataka kujua serikali inadaiwa kiasi gani katika chombo hiki cha magazeti.

Baada ya hapo eneo jengine napenda kujua utaratibu gani unaotumika katika utoaji wa ajira kwa waandishi wa habari na utangazaji, kwa vile kuna malalamiko hasa katika Shirika la Magazeti kwa muda mrefu watu wapo pale wamekuja watu juzi wameajiriwa. Hiki kilio cha muda mrefu, Mhe. Waziri hili nitahitaji maelezo.

Eneo jengine kuhusu uchumi wa vyombo vya habari katika sekta ya uchumi na huduma ya kijamii hasa kwa kuzingatia maendeleo yote nchini yanatokana na mchango wa vyombo vya habari hasa katika kujenga misingi wa utawala bora, ambayo ni nguzo ya maendeleo ya taifa. Hapa pana mtihani kidogo. ZBC ninafikiri *camera* zao hazitoshi, camera moja usafiri nayo unakuwa mtihani katika kufanya kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, maslahi ya wafanyakazi; wajumbe wengi tumekuwa tukipigia kelele. Kazi wanazofanya waandishi wa habari ni nzito na ni ngumu kuelimisha jamii, lakini maslahi yao bado serikali haijataka kuyazingatia. Kwa hivyo maslahi ya wafanyakazi yaboreshwe, kwa muda mrefu tumepiga kelele hayalingani na mwenendo wao na kazi wanazofanya. Kwa hili nitahitaji maelezo hapa Mheshimiwa Waziri maslahi habari yaboreshwe.

Eneo jengine Mhe. Waziri kwa muda mrefu tulikuwa tunalipigia kelele kuhusu utoaji wa *license* za upigaji ngoma na *license* za hoteli hasa katika eneo langu la Paje. Mheshimiwa wananchi kule karibu miaka mitatu hawalali, hawasomi hata idadi ya kufaulu watoto imepungua sasa hivi, kijiji cha Paje kutokana na watu kutoka Mjini kwenda kupiga ngoma zao kule na mambo mengine hayawezi kuzungumzika. Vile vile wagonjwa hawalali wanateseka, bangi zinakamatwa siku zote, wavuta unga wamezidi. Mheshimiwa suala hilo nakushukuru sana kwa jitihada uliyoifanya wizara yako kukutana na wananchi wa kijiji cha Paje na kukaa nao lakini bado una uwezo kwani wewe ndiye waziri mwenye dhamana ya suala hili. Ingawa nao kiasi fulani BASAZA tuseme sijui kama walichangia kiasi fulani au vipi lakini hizi ngoma miezi sita zilisimama kwa muda mfupi wakafanya mchezo wa kwenda Mahakamani kama mchezo wa kuigiza na sijui muda gani *court junction* hiyo, na hakuna kesi inayokwenda na wananchi wanateseka katika kijiji chao, hii ni dhulma ya mwisho.

Mhe. Naibu Spika, leo watu wanatoka Mjini kwenda kuwakera watu kule Paje, Mhe. Waziri nataka ufahamu utaratibu gani wa ruhusa uoiotoka pale wa ngoma na kama hivyo Mhe. Waziri lazima ifike wakati mjue, haiwezekani kuteseka watu kuna wagonjwa kule. Leo hospitali hakuna dawa watu wakateseke kwa kupigiwa ngoma kule katika kijiji chao. Mhe. Waziri hili nitahitaji maelezo ya kina, tena nitakuwa mkaidi sana kwa suala hili; nakujua utendaji wako uko makini kabisa na ufuatiliaji wako ni makini nakushukuru ulikwenda kule sijui saa tisa usiku au saa nane ukaacha majukumu yako ukaenda kule. Kwa hiyo, nikupongeze katika waziri wa kupongezwa, hivyo jambo hili nitahitaji maelezo sana.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nilikuwa na Mhe. Panya hapa tulikuwa tuna mchango wetu wa muda mrefu wakati wake umefika na ukizingatia Ramadhani keshokutwa kuhusu mswada wa nguo fupi kutuletea humu Barazani. Tunausubiri kwa hamu na hivyo nataka jawabu tulikuwa tunazungumza sana Mhe. Panya suala hili na hapa ndiyo tuliambiwa waziri mwenye dhamana Mhe. Abubakar alilitema suala hili likawa limeanguka kwako, Mhe. Fatma Fereji nae alisema nafikiri liko kwako, kwa hiyo tunahitaji msaada wako kwa suala hili na ukizingatia mwezi wa Ramadhani keshokutwa Mwenyezi Mungu akipenda.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ni kuhusu mahoteli ya Mji Mkongwe kuendelea kujengwa; tuliambiwa muda huu ni marufuku maeneo yale na majumba yote sasa hivi kuwa mahoteli, kwa bahati mbaya tunaendelea kuona yanajengwa maeneo yale. Kwa hiyo, maadili yetu yatazidi kuporomoka kwa suala hili kila anayekuja Mji Mkongwe kununua nyumba na kujenga hoteli, hili suala tunalipigia kelele na muda mrefu na Waziri wa Ardhi alisema tushapiga marufuku lakini bado suala hilo linaendelea.

Suala jengine kuhusu Ngome Kongwe kupigwa ngoma bado Mhe. Naibu Spika, waziri alitoa amri lakini bado watu wa Mji Mkongwe wanateseka kule na ngoma zile zinaendelea, sijui utaratibu kama kuna mtu mkubwa kuliko waziri aliyetoa amri ile na bado ikawa inapuuzwa na wananchi wanazidi kuteseka kule.

Jengine Mhe. Waziri nataka kujua katika kipindi cha maswali na majibu mtu anapoulizwa swali humu Waziri au Naibu Waziri yule anayeulizwa hatajwi kwa sababu gani? Sijui umenifahamu Mhe. Waziri suala hilo, waziri anayeulizwa suala hutajwa lakini yule anayeuliza hatajwi sijui kwa sababu gani wakati ndio msingi wa lile suala liloulizwa. Hapa napo kidogo patahitaji maelezo.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine la michezo; nianze na mchezo wa ng'ombe kule Pemba umepotea kwa muda mrefu, sijui serikali imeliona jambo hili na hakuna hatua zinazochuliwa kwani ni mchezo wa asili kabisa ule, ilikuwa ni burudani tosha.

Jengine nije kwenye suala la *TFF* imeitwa Tanzania kutokana na Zanzibar kama sikosei, nataka Mhe. Waziri utakapokuja hapa utufahamishe kuna dola 250,000 zilizotolewa na *FIFA*, Zanzibar inanufaika na nini kule. Na kuna dola 100,000 zinazotoka katika *CAF* Zanzibar tunafaidika nini. Ninachokijua mimi ni uwanja wa nyasi tu wa bandia wa Gombani Pemba ndio taarifa niliyokuwa nayo. Niliuliza suala hili Bungeni na jawabu niliyoipata haikuniridhisha, walichoniambia wanaandaa *programm* kupeleka kule timu za vijana wanawake na riadha. Nikawauliza mimi je, kama *programm* hii mwaka huu mnapeleka nyie mtakubali kuachia mwaka mmoja Zanzibar nao wapeleke *programm* yao, jawabu halikupatikana. Kwa hiyo, nitahitaji maelezo tunanufaika nini *TFF* wakati kujiunga kwao *FIFA* inatokana na Tanzania wakiwemo Zanzibar, nahitaji maelezo suala hilo.

Nafikiri baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, atakapokuja kunieleza waziri hapa nitaunga hoja mkono wala sina matatizo yoyote. Ahsante sana.

Mhe. Viwe Khamis Abdallah: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii kwa kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Habari.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii nimpongeze Mhe. Waziri na Naibu Waziri kwa utendaji wao mzuri pamoja na watendaji wao wote.

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa jengo la judo lilofunguliwa hivi karibuni Pemba. Mhe. Naibu Spika, jambo hili ni zuri na limekuja wakati mzuri kwa vijana, vijana wetu sasa watapa sehemu nzuri yakuimarisha michezo yao hii ya judo.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho yake aje anipatie mahesabu yote yaliyotumika katika kujenga jengo hili. Ni kiasi gani cha fedha ambazo zilitumika katika kujenga jengo hili.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye Shirika la *ZBC* Pemba. Mhe. Naibu Spika, *ZBC* Pemba wanafanya kazi ngumu ya kujitolea wakati wowote ule, lakini mwaka jana kuna nyongeza ambayo iliongezwa kwa wafanyakazi, wafanyakazi hawa wa *ZBC* Pemba mpaka leo wao nyongeza hii hawajaipata; nyongeza ya shilingi 25,000 pamoja na *scheme of service*. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje aniambie ni kwa nini wafanyakazi hawa hawajapatiwa nyongeza hii ya mshahara.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende na mchango wangu kwenye mambo ya utalii. Mhe. Naibu Spika, kwenye kitabu cha Mhe. Waziri hatujaona usalama wa watalii, kutokana na matukio mbali mbali yanayotokea hapa nchini kwetu hivi karibuni kuna watalii ambao waliingizwa kwenye kisima na kupoteza maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, kuna watalii walimwagiwa tindikali na yote hii inasababishwa kwamba watalii hawana ulinzi wa kutosha. Sasa nimuombe Mhe. Waziri aje aniambie serikali wamejipanga vipi kuwalinda hawa watalii.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Haji Omar Kheir kwa kutaka kuleta mswada wa kuanzishwa Shirika la Ulinzi la Watalii. Mhe. Naibu Spika, jambo hili ni zuri na niipongeze serikali kwa kuona umuhimu huu wa watalii.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri aje anipe takwimu ya watalii ambao wameingia nchini kuanzia mwaka 2013 na 2014 kwa sababu tunapozitaka hizi takwimu mara huwa tunaambiwa sijui Wizara ya Fedha, mara sijui wapi kwa kweli namuomba Mhe. Waziri aje anipatie hizi takwimu. Kwa sababu watalii ndio wanaotuingizia mapato katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia nikipongeze Chuo cha Habari; naiomba serikali iamue kuwekeza katika chuo hiki cha habari kwani kinaonekana kinakusanya mapato yake vizuri ili chuo kiwezeshwe kwa kujenga majengo yake ya kudumu, kipatiwe vifaa vya kisasa pamoja na walimu wenye sifa za kusomesha chuo hicho. Naamini endapo serikali itaamua hasa kuwekeza katika chuo hiki basi chuo kitaweza kujitangaza na hatimae mapato zaidi yataweza kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, nikimaliza hapo niende kwenye udhalilishaji huu wa wafanyakazi wa *ZBC* hasa wanawake. Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo kwa sababu gani Mhe. Naibu Spika, wapo wanaume mbona wao hawajafanyiwa udhalilishaji huu. Ukimdhalilisha mwanamke mmoja huwa umewadhalilisha wanawake wote.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa wizara hii ina Naibu Waziri mwanamke na tatizo hili limetokea na Naibu Waziri yupo namuomba Mhe. Naibu Waziri aje anipatie ufafanuzi juu ya suala hili baada ya kulisikia alichukua hatua gani? Hili ni tatizo kwani maofisi mengi wanawake wanakwenda na mabaibui yao wakifika mabaibui wanavua wanabakia na nguo zao wanaendelea na kazi. Baada ya kutoka kazini wanavaa mabaibui yao wanarudi nyumbani.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu sio wafanyakazi wote wana magari; wafanyakazi wanaingia kwenye magari ya abiria na wengine hawawezi kuingia kwenye magari ya abiria na nguo za ofisini, lazima kwanza wavae mabaibui wakifika pale mabaibui yale wanavua halafu ndio wanaendelea na kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, tusiendelee kuwadhalilisha wanawake, tumechoka kila siku tunapiga kelele hapa wanawake, watoto Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Naibu Waziri aje anipatie majibu ya kina kuhusu suala hili.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri asilimia 80 asilimia 20 naziwacha mpaka nipate maelezo ya masuala yangu ambayo nimeyauliza.

Mhe. Rufaid Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi sina budi kwanza kutoa shukurani zangu za dhati asubuhi hii kupata nafasi hii. Lakini kwanza namshukuru Mewenyezi Mungu aliyetuwezesha na kuniwezesha na mimi kuwa mzima wa afya kuweza kuhudhuria kikao hiki na kuweza kutoa maoni yangu machache ndani ya hotuba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza ukurasa wa 20 katika shirika la utangazaji. Mhe. Naibu Spika, shirika hili linasema kwamba majukumu yake ya msingi ni kutoa habari, kuelimisha, kuburudisha na kuhamasisha jamii juu ya masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mheshimiwa haya ni majukumu muhimu sana katika nchi yoyote duniani kwa sababu kila mtu anahitaji kupata habari; kuna habari za mtu kwa mtu, kuna habari za kupitia kwenye mitandao kama hizo redio, televisheni na mambo mengine. Kwa sababu habari inamtoa mtu pale alipo kumpeleka eneo jengine kuweza kufahamu kwamba katika eneo fulani kuna mambo fulani yamejiri. Kwa hivyo, kuelimisha jamii ni suala muhimu mno, lakini ili jamii ielimike basi kwanza ni kuwaenzi hawa waandishi wa habari, ni kuwaboresha waandishi wa habari na ni kuwajali waandishi wa habari. Mhe. Naibu Spika, nilishukuru shirika hili limetuboreshea hapa Barazani, Taifa wanayaona yanayoendelea ndani ya hili Baraza, ni hatua moja nzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, lakini juu ya hayo wanayoyafanya lakini pia kuna kasoro ndogo ndogo sote ni mashahidi tunawashuhudia ndugu zetu hawa kuanzia saa tatu mpaka inafika saa saba wamesimama wanataka hizi taarifa zao zionekane vizuri na zifikishe maana. Mheshimiwa huo ni muda mrefu kwa mwanadamu kumsimamisha muda wote huo, kwa kweli umeitumia nguvu yake ya kusimama muda mkubwa. Lakini kuna taarifa kwamba hata lile posho lao la kazi hii halipatikani. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri aje atueleze habari hii ikoje, kwa sababu hii ni kazi moja kubwa na ni nzito. Kwa hivyo, naliomba sana hili tupate jawabu yake.

Mhe. Naibu Spika, tunashukuru wizara kwa kuwawekea wale wenzetu walio na ulemavu wakalimani wakawa na wao wanafaidi chombo hiki. Hili ni jambo moja zuri sana, kwani wanafahamu kinachoendelea ndani ya chombo hiki. Nikitaka kumuuliza Mhe. Waziri kuna uzito gani wa *ZBC* katika vipindi vyake vya taarifa za habari, taarifa ya Rais anapotoa ama mwisho wa mwaka au katika vipindi vyake mbali mbali Rais anavyotembelea na kutoa hotuba yake na matokeo mbali mbali yanayotokea nchini ikawa taarifa hizi hazina mkalimani, ili kuweza kufaidika wananchi wote wakiwemo ndugu zetu walemavu.

Mhe. Naibu Spika, tunawanyima haki yao kwani hawa ni wananchi kama wananchi wengine na kila siku tunasema na sisi kidogo tunaojiona kama tuko *fresh*, nasema ni walemavu watarajiwa. Kwa hivyo, ni lazima kila mtu tumjali na tumpe haki yake. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri nipate jawabu rasmi kwa suala hili kwenye *ZBC Television* ikawa hakuna mkalimani anayetoa taarifa hizi ili kuweza kufaidika wale ndugu zetu ambao wana ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, ndani ya vyombo hivi kiasi fulani kuna vipindi vinaleta uchochezi, vinaleta ubaguzi, hili ni tatizo. Sisi tunasema kwamba viongozi wetu wote wakuu ni viongozi wa nchi hii na ukishakuwa kiongozi wewe si kiongozi tena wa chama fulani, wewe ni kiongozi wa jamii nzima, pale ukimaliza muda wako wa uongozi wa kuitumikia serikali hapo uta-*base* katika kile chama chako au kundi lako, lakini wakati unapokuwa kiongozi wa nchi wewe si kiongozi tena wa taasisi wewe ni kiongozi wa nchi. Sasa vyombo kama hivi vikileta ubaguzi, vikileta matusi kwa viongozi hawa kwa kweli huko ni kuhatarisha amani ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri hivi yeye kama Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo hiki chombo hakiangalii? Kama anaangalia je, ameridhika na yale yanayooneshwa? Naomba nipate jawabu.

Mhe. Naibu Spika, ndani ya Shirika hili la Utangazaji inasadikika kwamba Mkurugenzi wa *ZBC* ni mtu ambae ameshamaliza muda wake wa utumishi wa shirika hili, lakini bado anaongezewa muda aendelee zaidi. Mimi mara nyingi huwa najiuliza sisi tunawaandaa vijana, tunawasomesha, baada ya kusoma wanahitaji kupata ajira.

Jana Mhe. Ali Salum Haji hapa amewataja wafanyakazi wa shirika hili ambao walikuwa ni watu mahiri lakini wote wamekikimbia chombo, hapa nchini hawapo wamekwenda kujiunga katika mashirika mengine, hivi ile ni bure bure? Inaelekea kwamba sio bure, inawezekana Mkurugenzi ana matatizo na kama kuna matatizo akaendelea tena muda wa kustaafu umefika mtu kama huyo unamuongezea tu muda, ina maana unasema na hao

waliobakia nao wamalizike kukikimbia chombo hicho. Mhe. Waziri nadhani Rais si mpumbavu ni mtu ana akili zake timamu hawezi kumuongezea mtu tena muda pale kama hakuna ushauri unaotoka kwa Mhe Waziri. Naomba kujua hilo.

Mhe. Naibu Spika, niingie ukurasa wa 54 na 55 tuna Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Idara hii ni hazina ya Zanzibar, kwa sababu Zanzibar ni visiwa ambavyo watu wake wamehamia kwa muda mrefu; historia yake ni refu sana kushinda maeneo mengine ya Bara. Zanzibar watu wamekuja karne nyingi sana na watu hawa waliishi maeneo mbali mbali ya Zanzibar, katika maeneo hayo historia yake imepotea hatukuyaenzi. Wananchi kutokupata elimu ya maeneo hayo wakaona ni njia moja ya urahisi kuendesha maisha yao na kujenga majumba wakabomoa magofu yale wakapata mawe wakaanzisha ujenzi katika maeneo hayo, ile haiba na historia ikaanza kupotea kidogo kidogo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hili ni suala la kufanyiwa kazi ya ziada ili kuhakikisha uhalisia wa nchi yetu tunajaribu kuurejesha kidogo kidogo. Kwa sababu mimi nahisi kwamba maeneo haya ni maeneo moja wapo ndugu zetu watalii wanayafanyia ziara na kujifunza katika mambo mbali mbali ya Zanzibar. Hapa niseme kwamba ndugu zetu hawa wa makumbusho wamejaribu kutuonesha kuna maeneo ya kihistoria kama kule Pete, Bungi, Unguja Ukuu, Chuini, Dunga, Shakani na maeneo mengine mbali mbali kwamba wamo katika kuyafanyia utafiti, ili yaweze kurudi katika historia ya Zanzibar. Niseme ni jambo moja la faraja niwaombe kwamba waendeleze suala hili ili iwe ni kivutio cha wageni wanaokuja kuitembelea Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa kule Pemba tunayo maeneo ya historia kama hayo. Mimi ndani ya jimbo langu nina eneo la Msikiti Chooko, hili ni eneo la kihistoria la muda mrefu sana na wameshakuja watafiti mbali mbali kufanya utafiti wa eneo hili na wakajaribu kuweka mabango ya kuoneshea, lakini Mheshimiwa mabango hayo sasa utayatafuta hata moja hulikuti. Kwa hivyo, ili kuwajuilisha wageni wanaoingia cha kuwajuilishia sasa hakipo.

Mhe. Waziri nimemsikia katika kitabu chake hiki kwamba mpango huu anataka kuyarejesha yale mabango. Kwa hiyo, nimuombe tu kwamba ni jambo muhimu na litaisaidia serikali na wizara yake hasa kwa ndugu zetu watalii kuweza kufahamu kwamba Chwaka Msikiti Chooko kulikuwa kuna nini na maeneo mengine. Kwa hivyo, hili nimsisitize sana alifanyie kazi ili kitabu chake hiki kiweze kuwa kikweli kabla ya kufika bajeti ijayo.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae ametujaalia uhai tukaweza kukutana hapa na kuendelea na majukumu ya taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, pili nikushukuru wewe kwa kunipatia na mimi nafasi ili niweze kusema machache katika hotuba ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Tatu nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kazi zao nzuri ambazo wanazifanya.

Mhe Naibu Spika, nianze mchango wangu katika ukurasa wa 38 kwenye Kamisheni ya Utalii. Sekta hii ni muhimu katika kukuza pato la taifa letu lakini pia kupunguza changamoto za ajira kwa vijana wetu. Hata hivyo sekta hii inakumbana na changamoto kubwa ya kukosekana kwa usalama wa kutosha kwa watalii wanaoingia nchini petu ambao huhofia usalama wa maisha yao, kutokana na changamoto ambazo zinaonekana kwa miaka hii.

Mhe. Naibu Spika, naiomba sana serikali kuweka ulinzi wa kutosha ikiwemo *CCTV* katika maeneo ya utalii hata katika *junction* zetu, ili kuweza kuepuka wimbi hili kubwa ambalo sekta hii inakumbana nalo ya majambazi wanaovamia watalii mara kwa mara. Sekta hii itakapofanya kazi vizuri tutaweza kuwasaidia vijana wetu katika ajira na nikiri vijana wetu wengi wamestirika kupitia sekta hii ya utalii katika kufanya kazi katika mahoteli yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia niiombe tena serikali pamoja na vijana wetu hawa kufaidika kupata kazi, lakini na wao wanakumbana na vikwazo katika kazi zao. Kwa hiyo, niiombe serikali kuweka mkakati maalum juu ya mikataba ya wafanyakazi hawa, kwa sababu inaonekana wanaachishwa kazi kiholela, kwa hivyo lazima serikali tuwalinde vijana wetu waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 59 ambapo kuna Baraza la Kiswahili. Baraza hili lina jukumu la kukuza, kushajihisha na kufuatilia matumizi na maendeleo ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar. Mimi niseme katika mchango wangu wa kipindi kilichopita nilisema sana kuhusu Baraza hili la Kiswahili na Mhe. Waziri atakumbuka hata akiifuatilia *hansard* yake atakumbuka kwamba aliniahidi jambo hili ambalo nililizungumza.

Mimi nilizungumza kuhusu Zanzibar ambapo sisi ndio tunazungumza Kiswahili fasaha, Kiswahili laini ambacho kinaeleweka, kinafahamika, kina mvuto. Nikamuomba Mhe. Waziri alifanyie kazi jambo hili katika kukitafutia soko ili Kiswahili hiki kiweze kuwa na hadhi nzuri zaidi nje ya nchi, tuweze kufungua madarasa huko ili walimu wetu waweze kupata manufaa. Pia tuweza kuitangaza nchi yetu vizuri. Mhe Waziri alichukua ahadi kwamba jambo hili atalishughulikia kwa sababu anajua kama lina tija, mimi nataka kujua ushughulikiaji wake huo ulifikia wapi.

Jengine Mhe. Waziri matumizi ya Kiswahili; kwa kweli Kiswahili chetu hivi sasa tunakipindapinda, niombe sana Baraza hili kuweza kushughulikia Kiswahili kibaki katika hadhi yake ile ile na sio kuwa kinaingiliwa na maneno mengine ambayo sisi hata hatuyafahamu.

Mhe. Naibu Spika, mimi niendelee na mchango wangu katika Shirika la Utangazaji *ZBC Television* na *Radio*. Shirika hili ili liweze kufanya kazi zake na kufikia katika ufanisi mzuri basi kwanza lazima tuangalie kuna watu wanaoitwa mafundi mitambo. Mafundi mitambo ndio wanaosababisha chombo chetu kikaweza kufanya kazi katika ufanisi mkubwa, lakini bado mafundi wetu hawa maslahi yao ni madogo kulingana na uzito wa kazi zao. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri au nimuulize, serikali ina mpango gani wa kunyanyua maslahi yao ili waendelee kuzitumikia taasisi zao hizi.

Mhe. Naibu Spika, niendelee katika Shirika hili la Utangazaji la *ZBC*. Kwanza niseme mimi ni mdau mkubwa wa kusikiliza redio lakini pia wa kuangalia televisheni. Wewe mwenyewe waziri utakuwa shahidi kwa sababu ninapoona kunajitokeza matukio ambayo hayako katika hali ya kawaida humpigia simu hata usiku nikamuuliza kulikoni! Mbona kunaoneshwa hivi na hivi. Sasa ajue kama nafuatilia na ninafuatilia kwa sababu naipenda sana televisheni yangu, naipenda na redio maana ndio iliyopo nchini pangu na watu wanasema uthamini chako japo kuwa ni kibaya, na wala hakina ubaya. Kwa sababu televisheni yetu sisi ndio watu wa mwanzo katika Afrika hii, kuna ubaya gani!

Mhe. Naibu Spika, nikisema sisi ni wapenzi wa kuangalia basi pia katika uangaliaji wetu ningependa Mhe. Waziri ajue ikiwa hakuna maandalizi mazuri basi wanatuvunja moyo watizamaji wa *ZBC* na wasikilizaji wa redio. Kila kitu siku hizi kina mdau wake kwa hiyo lazima uwapendezeshe wadau kwa yale ambayo wanayapenda kuyasikiliza au wanapenda kuyaona.

Katika televisheni zetu inafikia wakati sasa unashindwa kuiangalia kama pana mtu ambae unamstahi; hayo ndio mambo ambayo yanatuvunja moyo. Sasa naomba sana wizara lazima ikae na taasisi zake iweze kupanga vipindi vizuri ambavyo vitakuwa na mvuto ili tuendelee Wazanzibari kupenda televisheni yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna tatizo la kurejewa vipindi hivyo kwa hivyo. Hili pia linaondosha mvuto kwa watizamaji. Katika hili niiombe sana wizara kwa sababu naelewa wafanyakazi tunao wazuri wenye uwezo na wana sifa za kuweza kutuletea habari zilizo moto moto. Lakini bado kuna ukosefu mkubwa wa vitendea kazi ambapo inarejesha nyuma juhudi za wafanyakazi wetu hawa. Ili wafanyakazi waweze kufanya kazi vizuri basi pia wanatakiwa wapatiwe usafiri ili waweze kuzitafuta hizo habari na waondokane na habari zile za viporo. Inatakiwa habari hasa kila inapopatikana mpya basi iweze kutoka kwa wakati ule.

Kwa hiyo, sasa ni vizuri wizara ikajipanga katika kuwatafutia usafiri lakini pia kuwa na *camera* za kutosha ili wafanyakazi hawa waweze kuzunguka kutafuta vipindi, ili wawe na mbadala katika kuonesha vipindi vyao.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 62 ambapo kuna Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho. Bodi hii kweli ina kazi ya kuzikagua sanaa zetu mbali mbali ambazo zinategemewa kusikilizwa au kuoneshwa katika *TV* zetu. Lakini mimi niulize huu ukaguzi unafanyika kweli. Kwa sababu utaona hivi sasa sanaa zinazooneshwa ni zile ambazo hazifikii katika lile lengo tunalolikusudia. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana bodi hii kuangalia sana michezo ambayo itaweza kudumisha maadili ya nchi yetu, lakini pia itaweza kuwafanya wasanii wetu waweze kuijengea heshima nchi yao kwa kulinda mila na utamaduni wao.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilitaka kuuliza tu, kuna wasanii wale wa zamani ambao walikuwa wakiigiza michezo mbali mbali na mizuri na ina hadhi mpaka leo, yaani ikioneshwa utafikiri labda umeigizwa jana. Basi angalau mkakaa na wasanii na hawa wakawa wanakupeni ushauri ni vipi wao waliweza kufanikiwa wakaweza kuigiza michezo bila ya kukiuka mila na utamaduni wa nchi yao. Mimi ningeomba muwatumie wale wangeweza pengine kutoa elimu fulani kwa wasanii wetu hawa wapya. Hata hivyo wanafanya kazi nzuri.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri kuweza kuwaangalia wasanii hawa kwani kazi wanafanya nzuri wanachotakiwa ni kuelimisha tu. Kazi zipo nzuri na zinaonekana na niseme wasanii wetu wana vipaji vikubwa. Lakini bado sanaa hatujaipa msukumo tukaweza kuona na wao wanafanya kazi zao zikafikia katika kiwango kile cha kimataifa na wao wakaweza kutajikana. Nikuombe Mhe. Waziri uwatafutie wafadhili hawa wasanii wetu ili na wao waweze kuendeleza sanaa hii kwa ajili ya kukuza sanaa zao, waweze kufikia katika kiwango cha kimataifa. Kufanya hivyo itakuwa wamejiwezesha wao lakini hata nchi yetu pia tutaipunguzia mzigo mkubwa wa ajira.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu waliochangia wamesema kuna deni ambalo wanadai hakimiliki kupitia kazi zao. Nimuombe sana Mhe. Waziri aweze kulilipa deni hili, ujanja wa deni ni kulilipa. Kwa hivyo, ili siku nyengine unaweza ukakwama na shida na wewe ukaweza kutumilia kazi zao na wakijua kama utaweza kuwafanikishia kwa siku nyengine.

Mhe. Naibu Spika, pia na mimi nichukue fursa hii kutoa pongezi kubwa sana kwa wale vijana wetu wa michezo walemavu kwa ushindi mkubwa walioupata. Pongezi hizi niwape wao wanafunzi ambao wamefanya vizuri, lakini na walimu wao ambao wamewafunza michezo hii mpaka wakaweza kufanikiwa. Naomba sana tuwatunze vijana wetu hawa, kwa kweli wamefanya kazi nzuri na kweli wanailetea heshima nchi yao. Lazima na sisi tuwajali, tuwawezeshe ili waweze kufanya vizuri na kuendelea mbele zaidi.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu walisema kuhusu kadhia ya wanawake na mavazi ambayo wanapata muadhara wa kuvuliwa nguo mlangoni. Mimi niseme jambo hili wanawake tuna mambo mengi lazima mengine mtuvumilie. Lakini niombe si kama nakataa wasivuliwe mabuibui, napenda ile stara tu ipatikane, wavuliwe pahala ambapo watajua tunavua mabuibui yetu hapa lakini wamestirika. Kwa sababu huwezi kujua mwanamke saa nyengine yupo katika hali gani, tuna mambo mengi, lazima mtuvumilie kwa mambo mengine. Lakini pia tunaelewa jinsi ya dunia na ulimwengu ulivyobadilika, hilo tunakiri. Tuvuliwe lakini kuvuliwa kwenyewe iwe katika stara ili mtu aweze kujihakikisha yeye mwenyewe nipo vizuri aweze kuendelea katika chumba chake cha kazi.

Mhe. Naibu Spika, naomba niendelee katika michezo; nimpongeze Waziri katika kuhakikisha michezo inakua na kutuwekea viwanja vile ambavyo vimepimwa katika wilaya zetu. Naomba mtupatie na sisi uwezo wa kuweza kupata ma-*grader* ya kuvisawazisha viwanja vile ili viweze kutumika kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naanza kwa kumshukuru muumba wetu Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kutujaalia kuwa hai na wazima tukiendelea na shughuli zetu hapa.

Pili Mhe. Naibu Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii. Naomba pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kuwasilisha bajeti yake hapa.

Mhe. Naibu Spika, katika mchango wangu la kwanza kabisa niseme tu ili liingie ndani ya rekodi za *hansard* kwamba kuna vifungu kadhaa vya matumizi ambavyo nimeviomba maelezo yake, lakini kwa sababu ya uchache wa muda mara hii katika mfumo wetu huu tuliojipangia nikivisoma nitapoteza dakika zangu zote 20. Kwa hivyo, nimemuorodheshea Mhe. Waziri na nimeshamkabidhi kwa maandishi. Nitaomba atakapokuja kufanya majumuisho anipe maelezo na nampa uhuru. Pengine tena itakuwa kwa wakati wake atafanya majumuisho anaweza akaja akayasoma, akiona ni muafaka zaidi kunipatia tu pia sawa, huo uhuru namuachia mwenyewe Mhe. Waziri ili nijiridhishe katika vifungu mbali mbali ambavyo nimeviorodhesha.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo kwanza nataka na mimi nitangaze maslahi kwa mujibu wa kanuni ya 59, kanuni ndogo ya 9. Mhe. Naibu Spika, mimi nilipata bahati ya kuteuliwa na Mhe. Waziri kuwa mmoja katika Wajumbe wa Bodi ya *ZBC*. Kwa hivyo, tunapozungumzia utendaji wa chombo hiki hata kama si maslahi binafsi lakini nahusika. Kwa hivyo, naomba lionekane pia katika kumbukumbu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nianze na hapo hapo nilipotangaza maslahi kwenye Shirika la Utangazaji la Zanzibar *(ZBC).* Mhe. Naibu Spika, mimi sitoingia katika mambo yale ya utendaji kwa sababu moja tu, haya kimaadili ya kazi inanipasa kama ninayo niyazungumze katika mikutano ya bodi. Kwa hivyo, tukijaaliwa nitafanya hivyo. Yale ambayo wameniletea watendaji mbali mbali wa chombo hiki tumeyachukua.

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba hili moja lipo nje ya uwezo, moja nalisema hapa, na ndio maana nimeanza kwa kutanguliza suala la maslahi. Mhe. Naibu Spika, ili *ZBC,* Televisheni na Redio na huduma zake nyengine ziweze kufanya kazi ipasavyo, ziweze kukabili changamoto zote ambazo zimetajwa hapa. Bahati nzuri Mhe. Waziri anazijua sana. Kwa sababu siku alipokuwa akiizindua bodi tarehe 4/10/2013 aliziorodhesha zote kwetu. Nataka nimwambie Mhe. Waziri na kuiambia Serikali kwa ujumla, na hasa katika hii naomba ujumbe huu umfike Mhe. Rais; kwamba ikiwa haya tuliyoyazungumza hapa yote Mhe. Naibu Spika, yanataka yafanyiwe kazi, maana yake shirika ni lazima lijiendeshe kibiashara. Kulipa malipo ya wasanii kazi zao zinazotumika, kurekebisha maslahi mbali mbali ya wafanyakazi na mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, mimi *nataasaf* kusema kwamba kwa Mkurugenzi aliyekuwepo shirika halitaweza maisha kujiendesha kibiashara. Hata ukaipata bodi nzuri kiasi gani. Kwa sababu kumejengeka dhana tu ya kudhani kwamba lile shirika ni mali yake binafsi. Kadhia ya *ZBC* Mhe. Naibu Spika, haitofautiani na kadhia ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, nilikutana na Bodi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Kuna tatizo kubwa sana Mhe. Naibu Spika, kwamba unapofika pahala mtu ukajiamini labda kwa sababu ya ukaribu wake na mtu fulani anaweza kufanya anavyotaka asipokee maelekezo na maagizo ya mtu yeyote, iwe Bodi, iwe Waziri, iwe mtu yeyote mwengine. Mhe. Naibu Spika, nasikitika kadhia kama hiyo itakuwa vile vile kwa *ZBC.*

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hili nalisema hapa lipo nje ya uwezo wa hata waziri, lakini namwambia waziri kwa sababu yeye ni msimamizi wa Serikali hapa ndani. Kwamba kama kweli Serikali ina nia ya dhati ya kuweka mabadiliko katika *ZBC* tusizungumze historia tu kila siku; hapa tulikuwa wa mwanzo televisheni ya rangi Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara. Basi Mhe. Rais kama mteuzi anapaswa atizame tena uteuzi wake wa mkuu wa chombo hiki.

Haya mengi yanayozungumzwa ya maslahi ya wafanyakazi, mengine kweli kuna matatizo pengine ya fedha na uendeshaji, lakini mengine yanahusu tabia tu na khulka ya yule mtu aliyepewa kukiongoza chombo kile. Haya nasema yapo katika vyombo vingi, hata ukazipanga bodi namna gani, ikiwa *Chief Executive Officer,* yaani mkuu wa chombo kile mtendaji kaamua kuwa mbogo basi huna njia ya kumbadilisha. Kwa sababu aliyemuweka pale ndio mwenye uwezo wa kumchukulia hatua. Sheria hizi zote bahati mbaya hazizipi mamlaka bodi kuwa na uwezo wa kuchukua hatua dhidi ya wale watendaji wakuu wa vyombo wanavyovisimamia. Halafu sikwambii yeye mwenyewe pia ni Mjumbe wa Bodi.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hilo nasema kwa jumla tu, kwamba tatizo la *ZBC* ni mtu anaitwa Hassan Mitawi. Kama tunataka mabadiliko aanze hapo Mhe. Rais halafu ndio mengine yatafuata.

La pili Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la Sekta ya Utalii. Mhe. Naibu Spika, Sekta ya Utalii ni sekta muhimu sana katika nchi yetu. Sasa hivi uchumi wetu kwa kiasi kikubwa unategemea huku. Sasa kama hali ni hivyo, ni lazima na nchi yetu ionekane kwamba inathamini mchango wa sekta hii. Wawekezaji wa sekta hii wa ndani na wa nje wana malalamiko yao mengi ya msingi, namuomba Mhe. Waziri na haya ayafanyie kazi. Kubwa kalisema hapa Mhe. Panya Ali Abdalla nataka nimuunge mkono.

Kuna *concern* ya kwanza ya uimarishaji wa Sekta ya Utalii, kwanza ni suala la usalama katika nchi. Mhe. Naibu Spika, utalii ni sekta ambayo ni *very sensitive,* likitokea tukio lolote athari ndogo ambayo inaashiria hatari ya usalama wa wageni, mgeni haji pahala hapo.

Sasa kuna matukio mengine bahati mbaya ni sehemu ya dunia hatuwezi kuyakwepa. Vyombo vya usalama vinafanyakazi mara nyengine tusivilaumu kwa sababu kuweza kugundua matukio yale mtu anakuja anafanya yake ikisha anaondoka si kazi nyepesi, hata katika nchi zilizoendelea inachukua muda mrefu sana. Lakini nikisema hivyo haina maana kwamba tunasema tuendelee kuwa hivi hivi.

Mhe. Naibu Spika, yapo mengine unaweza kuyafanya. Moja, naiambia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kulisimamia, lakini Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa jumla, tumelisema hapa suala la *CCTV camera.* Matukio mengi ya uhalifu yanafanyika kwa sababu mtu anahisi kwamba anaweza kufanya

chochote asikamatwe. Lakini kukiwa na vifaa ambavyo vinaweza kutoa kitisho; inaweza kupelekea kumfanya mtu aogope kufanya uhalifu kwa sababu anaweza akajulikana.

Mhe. Naibu Spika, katika hili nataka kusema hasa jimbo ninaloliwakilisha la Mji Mkongwe kwa sababu ndio eneo moja ambalo kwa mjini watalii wengi ndio wanapokusanyika, na ndio maana matukio mengi yanatokea katika Mji Mkongwe. Kuna tukio lililotokezea lile mwaka jana limetuletea athari kubwa sana; tukio la wasichana wale wawili wa Kiingereza ambao ni watu waliokuja kujitolea hapa, lakini namna walivyokuwa wameripotiwa katika vyombo vya habari vya nje kuwa ni watalii, lakini wageni wale. Walivyoshambuliwa kwa kumwagiwa *acid* habari zilizotoka zilikuwa mbaya mno dhidi ya Zanzibar. Sasa pengine kungekuwa kuna *CCTV camera* ingetusaidia. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hiyo waitizame.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni namna ya uendeshaji kwa sekta hii. Moja naomba walitizame sana wizara, washirikiane Serikali na Wizara ya Fedha, ni suala la mfumo mzima wa kodi katika Sekta ya Utalii, wawekezaji wanalalamika sana. Zanzibar ni katika nchi ambazo zilipofanyiwa utafiti katika zile zinazoitwa *Bring Business in the World*, kuna *Bring Business in Zanzibar* ilikuwepo mwaka 2010. Zanzibar imetajwa kama nchi ya 155 duniani kwa ugumu wa kufanya biashara na uwekezaji. Kuna vikwazo vingi, moja ni mifumo ya kodi; kodi zinakuwa nyingi, zinakuwa hazina mpangilio, kila chombo kinatoza kodi. Inaonekana kila sisi tukipata tatizo tunadhani kwamba pahala pa kukamua ni Sekta ya Utalii.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi kuna ushindani mkubwa hata katika ukanda huu wa Afrika Mashariki kila nchi inavutia kwake. Itakapofanywa uwekezaji ukawa mgumu itapelekea kuwakimbiza wawekezaji katika sekta hii. Naomba hili pia Mhe. Waziri waliangalie katika wizara yao kama ndio wenye dhamana kwenye sekta hii.

Mhe. Naibu Spika, jengine hata kama halipo kwao wao ndio wasimamizi ni suala zima la mazingira ya nchi yetu. Mtalii hawezi kwenda pahala ambapo kuna uchafu na uvundo. Tumelisema sana hili Mhe. Naibu Spika, mji wetu mchafu, makaro yanapasuka kila pahala yakimwaga maji machafu, mataka hayazolewi, uvundo kila pahala. Ukenda sokoni watalii wanapiga picha usidhani panawavutia pale, wanapiga picha kuona mambo ya ajabu kwamba samaki anavuja damu anakokotwa barabarani ambapo tunatupa kila aina ya uchafu. Ule si utalii wa daraja la juu, hawezi kuja mtalii wa daraja la juu katika hali kama ile.

Mhe. Naibu Spika, Sychelles wameweka kikomo wanasema kila mwaka wanahitajia watalii laki mbili tu, lakini wameweka daraja ya watalii wanaowahitaji wanaoendesha uchumi wao. Sisi kama tunataka kwenda daraja hiyo ni ngumu kwa sababu mtalii wa daraja ile ili aje hapa kuna vivutio vyake viwepo, hapa havipo. Kwa hivyo, nasema suala la usafi vile vile Mhe. Waziri ni muhimu sana kulitizama.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuna suala zima la kero. Kama Serikali kwa jumla na hasa wizara haijashughulikia suala la kuwa na polisi, ikiwa kikosi chochote cha kusimamia utalii basi hatari. Hawa wanaitwa mapapasi Mhe. Naibu Spika, wanawasumbua watalii sana. Mtalii katoka alikotoka kaja hapa kupumzika, lakini kila anapokwenda kuna watu wanamfuata, anaweza kumfuata mtu kuanzia pengine lilipo jengo la Mahakama Kuu anakwenda nae mpaka atafika nae Malindi. Sasa hakuna askari nchi hii, hakuna vyombo vya kusukuma mambo haya yakachukuliwa hatua. Naomba Mhe. Waziri pia akija atusaidie maelezo haya.

Mhe. Naibu Spika, yapo mengi lakini kwa sababu ya muda naomba hili la utalii niliachie hapa. Labda kidogo hapo hapo niunganishe kwa ufupi sana suala la maeneo ya kihistoria. Mimi nimekuwa mmoja ambaye nimesema sana katika Baraza hili, kwamba mimi mwenyewe naipenda historia, napenda kujifunza, napenda kutembelea maeneo haya, Mhe. Waziri ayatizame. Nimeona katika hotuba yake maeneo ambayo aliyapa kipaumbele mwaka jana na mwaka huu anaendelea. Namuomba tena mwaka juzi na mwaka jana nilimwambia ayaangalie tena magofu ya Maruhubi, kati ya yale ambayo yameorodheshwa humu sikuyaona.

Moja nashukuru na nasikia Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ilisaidia angalau kuuhifadhi ule ukuta wa Maruhubi. Nawashukuru sana kwa kazi hiyo waliyoifanya. Lakini yale magofu yenyewe yatizamwe yakija yakianguka ile historia inazidi kuondoka. Mengine anajua.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo nipige debe katika maeneo ya Mji Mkongwe jimbo langu ninaloliwakilisha. Moja, tumelizungumza sana jumba la Beit el Ajaib. Hebu Waziri atwambie mpaka sasa hivi kinaendelea nini. Pia jirani pale kuna Makumbusho ya Kasri sehemu inatumiwa na Baraza la Mapinduzi. Ile sehemu ya Baraza la Mapinduzi ilitengewa fedha itatengenezwa. Sasa mgeni akija hajui kama mle ndani kuna makumbusho, lakini pia muna Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, ataona watu wa ajabu jengo limetengenezwa nusu linang'ara limepakwa rangi nusu limejaa… yaani umande ule wa baridi mpaka umefanya weusi mule ndani.

Mhe.Naibu Spika, hivi vitu vyengine ni vidogo vidogo lakini vinatuonesha watu hawa ni wa aina gani. Kwa hivyo hili alitizame pia.

Mhe. Naibu Spika, kuna jumba la *Tiptip* ambalo serikali ilitaka kuwahamisha wale waliomo mule ndani linakaliwa na watu. Lile ni jumba la kihistoria lile, kama halikufanyiwa kazi linaweza likaporomoka wakati wowote. Nilikuwa namuomba Mhe. Naibu Spika, haya na mengine wayatizame.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa sekta ya utalii kwa dakika moja tu kumwambia tena suala la kuangalia ajira kwenye sekta hii. Kiasi gani vijana wetu wa Kizanzibari wananufaika. Kuna siku baadhi yetu tulitoka humu katika kupitisha mswada wa Sheria ya Utalii. Kwa sababu tulisema kipaumbele kiwekwe kwa Wazanzibari tukaambiwa itakakuwa hivyo hata kama imeandikwa Mtanzania lakini hali haipo hivyo Mhe. Naibu Spika. Naomba tena na hili vile vile alitizame.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kwa muda mchache uliobakia naomba nimalizie katika suala la sekta ya utamaduni na michezo hasa katika michezo. Hapa kwa sababu ya muda, nimuombe Mhe. Waziri akija atwambie. Wizara kwa ujumla inafanya nini kukuza sekta ya michezo. Mimi sitaki kudanganywa, si mtu mwenye utaalamu sana wa mambo ya michezo lakini ukishakuwa unawawakilisha wananchi katika chombo hiki, kila unachopewa ni lazima ukilete humu ndani.

Mhe. Naibu Spika, kuna barua hii tulipewa baadhi ya Wawakilishi; sijui kama ni wote imeandikwa na mtu anayeitwa Mtumwa Said Haji kamuandikia Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, na kaandika tarehe 28/05/2014 mpaka lini Zanzibar kwenye mpira wa miguu tutakuwa kichwa cha mwenda wa wazimu, ndio kichwa cha habari cha barua yako.

Kawanukuu na kamuandika mwakilishi, sijui kama tumepata sote lakini humu anachosema cha msingi ni kwamba kuna tatizo la msingi katika *ZFA* ndio inayokwamisha ukuaji sio kwa Zanzibar. Sitaki kuisoma kwa sababu ya muda aje atwambie barua hii baada ya kuipata na haya yaliyokuwemo humu ndani anafikiria nini. (*Makofi*)

Jengine Mhe. Naibu Spika, vyama vyengine mbali mbali vya michezo vinalalamika. Hapa nina kadhia moja hatuwezi kuyasema yote na muda wangu ninaona unamalizika. Kuna kadhia moja nimeletewa ningeomba Mhe. Waziri aje anipe maelezo, hichi ni Chama cha *Zanzibar Weighting Association*. Hawa Mhe. Naibu Spika, ndio katika chama pekee cha michezo Zanzibar ambacho kinatambulika kimataifa kama chama cha Zanzibar, katika Jumuiya ile ya kimataifa ya dunia lakini pia katika Jumuiya ya Bara la Afrika.

Kinachosikitisha kulipa ada ya wananchi serikali inashindwa kuwasaidia, tena sio pesa kubwa ya hivyo. Unakuta unadaiwa dola elfu mbili mia nne, wanazuiliwa mpaka kushiriki katika mikutano ya kimataifa. Sasa walimuandikia ninafikiri kuna barua hapa walimuandikia mpaka Spika, waliiandikia wizara, wamefika pahala mpaka wamemuandikia Rais kwa jambo dogo kama hili. Hebu Waziri akija aniambie wanafanya nini kusaidia chama hichi ambacho angalau chama hichi Zanzibar imetambuliwa kimataifa, ili hizi kadhia zao za kila siku kuadhiriwa katika mikutano; mmoja alikuwa ananieleza mpaka anakaribia kutoka machozi Ndugu Jamal Adi maarufu nyote munamju katika mji huu.

Alifika pahala pa kuadhiriwa katika mikutano ya kimataifa ikabidi achangiwe na wenzake, wizara ilimwambia aende itamtumia, imepeleka pesa baada ya kushaondoka kishaadhiriwa mpaka hoteli kaondolewa. Mambo kama haya pia yamejitokeza katika timu yetu tulipoipeleka mashindano ya *challenge* ya mwaka jana Uganda, ikaleta kadhia kubwa.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hebu pia Mhe. Waziri akija aje atwambie katika suala hili la michezo kwa ujumla anafanya nini, ili kuona kwamba, ninajua anajitahidi sana, ninajua alifanya vikao na wana michezo mbali mbali lakini bado kuna malalamiko mengi sana. Ningeomba Mhe. Waziri anisaidie.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nitaiunga mkono bajeti baada ya kupata maelezo katika hoja hizi na zile za matumizi ambazo nimemuandikia katika mchango wangu.

Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana mheshimiwa. Sasa nafasi ninampa Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa baadae Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Hassan Hamad Omar na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu ajiandae.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia mchana huu nikawa na afya njema nikaweza kuchangia hotuba hii. Pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kutuwasilishia hotuba yake ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Pia niwapongeze watendaji wote kwa kazi zao wanazozifanya kila siku. Mhe. Naibu Spika, pia niwapongeze watoto wetu walemavu kwa kushiriki mashindano na kushinda na kupata medali.

Mhe. Naibu Spika, nianze na Hoteli ya Bwawani. Kwanza niupongeze uongozi wa Hoteli ya Bwawani kama tulivyopata taarifa kwamba wanajitahidi kuifanyia ukarabati hoteli hiyo. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri azidi kusimamia kuona hoteli hiyo inarudi katika hadhi yake.

Pia alivyosema kwamba hoteli hiyo inapendwa sana na watalii. Kwa hivyo basi namuomba kama alivyotuwasilishia hotuba yake, basi iwe kweli watalii wanaipenda kweli.

Pia nilikuwa ninataka nimuulize kuhusu hoteli za Pemba zile za serikali. Ninataka nijue taarifa zake zikoje. Atakapokuja kutoa majibu anieleze basi na hoteli hizi za serikali za Pemba zikoje.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye michezo. Mimi pia niipongeze Idara hii ya Michezo kwa kazi zake inazofanya lakini naomba kumuuliza Mhe. Waziri, kwa nini hapa kwetu Zanzibar michezo inarudi nyuma? Pia ninataka nimuulize ana mikakati gani kuona na sisi Zanzibar tunakuwa mbele katika michezo, hatuwi nyuma katika ulimwengu wa michezo. Namuomba Mhe. Waziri na hili anipatie jibu ili niweze kujua.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Chuo cha Waandishi wa Habari. Pia niipongeze wizara hii kwa kazi nzuri inazofanya kila siku. Idara hii haina jengo. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri basi awatafutie jengo ili na wao waweze kufanya kazi zao kwa uhakika, wasiwe katika afisi za kujibana na jengo walililokuwa wanalofanyia kazi haliridhishi. Kwa hivyo naomba awatafutie jengo ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Pia niipongeze idara hii kwa kutekeleza majukumu yao kwa kuenzi, kuhifadhi na kuendeleza historia ya Zanzibar. Lakini naomba idara hii katika kazi zao wanazozifanya za makumbusho naomba kwamba wazidishe juhudi kuona kuwa makumbusho yale wanayafanyia ukarabati. Kwa sababu makumbusho haya ni historia ya Zanzibar na makumbusho haya kusema kweli wageni wanapokuja wanatembelea ili kujua historia yetu ya Zanzibar. Kwa hivyo ninaiomba wizara hii ijitahidi kuona makumbusho wanayafanyia ukarabati kwa nguvu zote.

Pia nimuombe Mhe. Waziri kuona kwamba watalii wanakwenda kutembelea makumbusho hayo, kwa sababu makumbusho ni vivutio vikubwa kwa watalii na pia wanaongeza pato kubwa la nchi yetu. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Shirika la Utangazaji. Niipongeze idara hii kwa kufanya kazi zao vizuri. Idara hii kuna wafanyakazi wanaodai posho zao. Kusema kweli tatizo hili kila inapofika bajeti linakuwa linazungumzwa na bado maposho yao hawayapati vizuri, wanakaa siku nyingi ndio wanafikiriwa kupewa posho zao. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri awalipe maposho yao kwa utaratibu, kwani wafanyakazi tutawavunja moyo.

Mhe. Naibu Spika, pia nizungumzie kuhusu tatizo la chumba kilichoekwa mitambo. Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa tulizokuwa tunazo sijui kama na yeye anazo kama chumba kilichoekwa mitambo katika *ZBC* pale *Karume House*; kwamba chumba kile chenye mitambo wapo pamoja na wafanyakazi wanafanyakazi katika mitambo hiyo na chumba hicho kinasemekana kina baridi kali sana. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri aje kunipa maelezo kama taarifa hii yeye anayo. Kama taarifa hii yeye anayo kachukua hatua gani kuona wafanyakazi hawa anawaondosha katika chumbo hicho cha baridi na wao kufanya kazi katika maeneo yaliyokuwa salama. Pia ninamuomba Mhe. Waziri basi wafanyakazi hao awafikirie suala la posho la maziwa, kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Mhe. Naibu Spika, mwisho na mimi niungane mkono na Waheshimiwa wote waliochangia kuhusu wanawake ambao waliokuwa wamedhalilishwa pale Karume *House* kwa tatizo la kuvuliwa buibui. Ninataka na mimi nijue tatizo hilo litachukuliwa hatua gani. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mwisho kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjjni/Magharibi ninaunga mkono bajeti hii asilimia mia juu ya mia. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa. Sasa nafasi tunampa Mhe. Ashura Sharif Ali, baadae Mhe.Hamza Hassan Juma, atafuatiwa na Mhe. Hassan Hamad Omar na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetujaalia uhai lakini pia akatupa na uzima, akatuwezesha kuwemo humu kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Pia nikushukuru na wewe Mhe. Naibu Spika, kunipatia na mimi nafasi hii ya kuweza kutoa walau mchango wangu mdogo katika hotuba ya Waziri huyu iliyopo mezani wakati huu.

Mhe. Naibu Spika, nianze na kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake. Ameiwasilisha kwa mtindo wa aina yake ambao ametumia dakika kama 45 hivi.

Mhe. Naibu Spika, nianze na mchango wangu katika Shirika la Magazeti. Mimi nimwambie Mhe.Waziri kwa kweli wenzangu walizungumza jana, mimi niseme wakati sasa umefika haipendezi, hainogi kwa kweli magazeti yetu kwamba yakachapishwe huko. Hili jambo kwa kweli halipendezi.

Niiombe sana serikali kwa kuwa sasa tuna Kiwanda cha Uchapaji, serikali iboreshe hapo ili tuweze kufanya shughuli yetu kwa ufanisi. Naiomba sana serikali ifanye hivyo, iboreshe katika kiwanda chake cha uchapishaji ili tuweze kuona na sisi magazeti yeti basi yanapatikana kupitia hapa, tusisubiri ndege itoke Dar es Salaam na kutuletea magazeti.

Hichi kitu wakati huu hakipendezi tena, serikali yetu imekua ni miaka 50 tunaingia 51, ni vyema tukaliona hilo kwamba tunawweza kulifanya na nina imani kwmaba tukijiekea mipango madhubuti inawezekana.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu huu, nizungumzie Baraza la Kiswahili la Taifa la Zanzibar. Mhe. Waziri ameseka kwamba nia yake kuu ni kukuza na kuendeleza matumizi ya Kiswahili fasaha kitaifa na kimtaifa.

Napo ningependa kumwambia Mhe. Waziri wakati huu ninadhani kwamba unaamini kwamba Zanzibar ni kweli kabisa Mhe. Panya Ali Abdalla hapa alilisema nisingependa nilizungumzie sana, lakini alisema kwamba Wazanzibari katika mwambao huu tunasifiwa mno kwa Kiswahili chetu kizuri kinachopendeza, kilicho fasaha kabisa.

Ni dhahiri kwamba sote ni mashahidi tumeona jinsi wakati huu vijana wetu wanavyokitumia Kiswahili hichi kwa kuongeza maneno ambayo yamekuwa ya ajabu sana ambayo wazee wetu hawakuwahi kuyasikia. Wazanzibari wakitumia assalama aleykum na shikamoo, siku hizi kuna mambo, poa, mpango, mshikaji na vitu vyengine. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, tuangalie mambo haya kuwa yanaondoa na kuweka dosari kubwa ya ufasaha wa lugha yetu ya taifa ya Kiswahili. Sisi ndio Waswahili na wengi wanakipenda Kiswahili, lakini sisi wenyewe tunaanza kuondoa na kuweka vionjo vipya. Tuhakikishe kwamba ile dhana ya lugha ya taifa ambayo sisi ndio urithi ambao tunautumia isipotee na kuingia maneno ambayo hayakupaswa kuingia.

Mhe. Waziri uniambie una utaratibu gani wa kuona kwamba utalilinda hili kuona kwamba haivamiwi lugha yetu hii nzuri kuingizwa maneno mapya mapya ambayo hayakuwa na uasilia wetu. Ninadhani ingekuwa raha kama ingekuwa watu wanaingiza lahaja labda za Kimakunduchi, Kipemba na za Kitumbatu. Hii ndio asili yetu na ndio mambo yetu. Hiyo ni ladha na inakubalika kabisa, lakini yanakuja mambo ya ajabu ajabu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikiliacha hilo sasa labda niizungumze Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Idara hii ni muhimu sana katika sekta ambayo unayo ya utalii. Wengi wa wageni wetu huwa wanakuja hapa na huhitaji kwenda kuona mambo yetu ya kale kabisa. Mimi labda niseme kwamba labda uniambie kwamba, umesema kuwa utaimarisha maeneo ya kihistoria ili yawe na hadhi ya kitaifa na kimataifa. Kwanza nikiulize Mhe. Waziri, je, maeneo hayo umeyahakiki? Unayajua yote yalipo katika maeneo hayo kihistoria? Kwa sababu ni lazima uwe

unayajua kwanza halafu ndio unaweza kuyawekea hifadhi na kuanza shughuli zake ya kuweza kuyaboresha. Mimi ningependa kupata jibu.

Jengine Mhe. Naibu Spika, pembezoni mwa fukwe zetu, sisi tukiwa kama kisiwa; hizi ni sehemu za kihistoria ambazo wazee wetu mbali mbali waliokuwa wavuvi wakizitumia. Mhe. Waziri uniambie kwa kuwa na utalii nao umehamia katika sehemu hizo hizo za kanda za fukwe za bahari, je, kutokana na hali hiyo iliopo umeeka utaratibu gani ambao utaendana na yale mazingira yaliopo baina ya uwekezaji wa utalii na wewe unataka kuweka kumbukumbu ya mambo ya kale ya kihistoria ya Zanzibar yabakie vile vile?

Mhe. Naibu Spika, sasa niingie kwenye sekta yenyewe kabisa ambayo ni sekta ya utalii. Sekta hii ni kweli kabisa kwamba ni sekta muhimu sana kabisa sasa hivi kwa pato la taifa au kwa uchumi wa Zanzibar yetu. Ni sekta ambayo inaingiza pato la taifa ukiachia pale mwanzo tulipokuwa tukitumia sekta ya kilimo kwa kupitia zao la karafuu. Lakini sekta hii inakuwa tabu kufikika kwa sababu inahitaji miundombinu ya kutosha kabisa. Mwekezaji hawezi kuja katika sekta hii kama eneo analolihitaji halina miundombinu ya maji, umeme na barabara.

Mhe. Naibu Spika, wewe kama sekta hii inakugusa una utaratibu gani kuona kuwa unataka uboreshe ili watalii hao tunaowahitaji waje kuona unawafikishia huduma hizo kwanza, ili na wao wavutike kuja kuwekeza katika maeneo husika.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala ambalo wajumbe wenzangu waliligusia kwamba kwa wakati huu kumetokea mambo mbali mbali ambayo yanajenga hisia za wageni wetu kama mshtuko; usalama kwa wageni wetu wanaoingia ni suala la msingi sana kabisa.

Je, Mhe. Waziri umejipangaje ili kuona kwamba wageni hawa watatumia ile tamaduni yetu ya "Zanzibar ni njema atakaye aje" na watakapokuja wakaweza kupata ile hifadhi iliyokuwa ikitumika zamani hapa kwetu, kwamba akidondosha hata pesa yake ile dola basi anaipata. Anaambiwa mgeni wetu umedondosha kitu hiki. Lakini hivi sasa hali imekuwa ni nyengine. Wewe una utaratibu gani wa kuona kuwa unaweza kuweka hizo *camera* ambazo zinaweza kuona kwa ajili ya usalama.

Mhe. Naibu Spika, nimuambie Mhe. Waziri ni kweli kabisa tuna utalii hapa kwetu, lakini je, tutaendelea na utalii wa aina hii tu, ukizingatia kwamba nchi yetu ni kisiwa kidogo na ardhi yetu ni ndogo. Nadhni umefika wakati ujipange ili uone sasa tunaandaa miundombinu mbadala tunawaleta wataali wa daraja la juu ambao watatuingizia fedha za kutosha kabisa na ambazo zitakata kiu na makali ya uchumi wa taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, ukikiangalia kisiwa chetu ni kidogo na kanda zote sasa hivi zimeanza kuzungukwa na mahoteli, lakini bado fedha tunayoipata sio kidogo, tuseme tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu tumepiga hatua kidogo. Lakini maeneo tayari yamezungukwa na eneo letu ni dogo. Je, una utaratibu gani wa kuona kwamba tunafikia hatua ya kuweka utalii wa daraja la juu?

Mhe. Naibu Spika, ninamuuliza tena Mhe. Waziri kwamba dhana ya utalii kwa wote aliisema Dkt. Shein wakati akilifungua Baraza hili, kuona kwamba utalii utaweza kuwanufaisha wananchi wote wa Zanzibar. Namuomba Mhe. Waziri aniambie, je, anautaratibu gani juu ya wale wanyonge wanaolima mboga mboga, kwa sababu mahotelini kunahitajika bidhaa mbali mbali. Kuna wakulima wa mboga mboga, naona kwamba wakati huu zile bidhaa zote hutoka kwa wenzetu Tanganyika. Una utaratibu gani wa kuona kwamba dhana hii ya utalii kwa wote inafanikiwa hapa kwa wajasiriamali na wakulima wetu wadogo wadogo wa mboga mboga ambao wanaweza kupata soko humu ndani kwa kupitia sekta hii ya utalii?

Mhe. Naibu Spika, sio hawa tu, wanaagizia vitanda na *furniture* mbali mbali nje ya hapa, je, wewe una utaratibu gani wa kuwaboresha hawa vijana wetu wachongaji, kuona kwamba na wao sasa watapata soko katika sekta hii ya utalii.

Mhe. Naibu Spika, pia wavuvi wa samaki kuweza kupata soko katika sekta hii ya utalii, umewaandaliaje ili dhana hii aliyoisema Mhe. Rais ya utalii kwa wote tuweze kupata manufaa sote kwa kila mmoja na kwa namna anavyojiendeleza.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hayo ambayo nimeyasema pia kuna matatizo ambayo yanawakuta vijana wetu ambao wameajiriwa katika haya mahoteli. Vijana wetu wakati mwengine hawafungishwi mikataba, wakati mwengine hao wakuu wa hizo hoteli wanawafukuza kiholela bila ya utaratibu, lakini hata mishahara yao kazi ile

ile moja, yule analipwa hiki na yule mwengine analipwa chengine. Mhe. Waziri ningeomba nayo unipatie ufafanuzi wewe unautaratibu gani kuhusu hili.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika sekta ya utamaduni. Mhe. Naibu Spika, utamaduni wa Wazanzibari ni moja kati ya kivutio kizuri kabisa kwa wageni wetu wanaoingia nchini. Leo watu wanakwenda mahotelini haijawahi kuonekana kwamba vile vyakula vyetu vya asili hasa ambavyo tulikuwa navyo zamani. Tuna mseto sisi tunakula kwa mchuzi wa nazi, wageni wanapenda ndio mila zetu na tamaduni zetu kwetu, pamoja na ugali wa muhogo kwa mchuzi wa pweza; hizo ni tamaduni na hivi ni vivutio vya wageni vyakula vya mila na silka zetu.

Mhe. Naibu Spika, pia mavazi yetu ya kanzu na kofia, nguo zetu na mabuibui yetu ya asili ya kamba na vizoro. Haya yamepotea na yameondoka. Leo mishono na mavazi yanayovaliwa yako tofauti kabisa na mila, silka na tamaduni za Wazanzibari.

Mhe. Waziri kwa kuwa wewe umepewa sekta hii na utalii unao wewe pia je, unawaambia nini Wazanzibari kuhusu utamaduni wetu, kuna mambo mbali mbali yanayofanyika ambayo yanakwenda kinyume kabisa na taratibu za mila na silka zetu.

Mhe. Naibu Spika, tulizowea kuona wanawake na wanaume kwa miaka ya nyuma kulikuwa na gari za siti zile zinatengenezwa, wanawake wanakaa mbele na wamejificha na vizoro vyao na hawagusani na wanaume, na wanaume wanakaa sehemu yao. Hizo ndio tamaduni za Kizanzibari mimi nazikumbuka kabisa. Nakumbuka miaka hiyo nilipanda gari na mama yangu, basi tumewekwa pamoja kule mbele na huku nyuma wanaume wamekaa mbali, ndio tamaduni zetu. Leo unasemaje kuhusu hili Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu nakwenda katika Hoteli ya Bwawani. Hapa Mhe. Waziri nakupongeza sana kwa kuweza kuifanyia ukarabati mkubwa Hoteli ya Bwawani, kuona sasa ianze kazi na kuweza kufikia hadhi inayotakiwa.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe bado dakika tano.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, namalizia. Niseme kwamba mzarau chake huwa mtumwa, niziambie taasisi za serikali hizo shughuli zenu mlizonazo sasa, semina na mambo yenu muende kwenye ukumbi wa Bwawani hii ni sekta ya serikali muitumie, muache kwenda kwenye sehemu nyengine ili kuchangia basi nendeni huko Bwawani mkafanye shughuli zenu kwa kuongeza pato la taifa.

Mhe. Naibu Spika, namalizia mchango wangu kwa kuzungumzia Shirika la Utangazaji. Mhe. Naibu Spika, upatikanaji wa habari ni suala moja zuri sana na ili taifa liwe na muelekeo wa kujua wapi lipo na wapi linaelekea, ni wananchi wake kuwa na taarifa na mambo mbali mbali yanayoligusa taifa lao.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niulize kwamba haya mafao ya hawa watu wetu wa televisheni wamelipwa? Maana yake tusije tukawa tunawagida mambo yao wao wanatumia nguvu na jasho lao, na sisi tunajisifu tuna televisheni, tuna redio na kadhalika, lakini ikawa wao hawapati maposho yao. Naomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa unieleze je, hawakudai hawa, kama wanakudai basi fungu mimi nitazuia, ili mpaka pale utakaponiambia watapata lini haki yao.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni kwamba mambo yote husemwa kweli, lakini kuna mambo yana taratibu zake. Niliombe sana Shirika la Utangazaji, wajuwe kwamba vyombo hivi viwili televisheni na redio kwa Zanzibar ndio vyombo vya serikali. Je, inakuwaje yatokee matukio na mambo mbali mbali, halafu sisi tupate taarifa kupitia vyombo vyengine kabla ya hii redio yetu au televishini yetu, tuna nini? Tunalazimika tubadilike tuendane na wakati wa sasa. Tumesema tumeingia kwenye digitali, kwa nini leo sisi tunabaki nyuma hivi? Hata hivyo vipindi viendane na wakati, lakini sio wakati wa kubadilisha mila na silka za tamaduni za Zanzibar, *la hasha!* Lakini upataji wa habari kulingana na matukio na wakati muafaka kabisa ni muhimu.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa ni hili la utaratibu wa ukaguzi wa wanawake kuvuliwa mabaibui yao hadharani. Tamaduni ya Wazanzibari hairuhusu. Watayarishe chumba au eneo wakajivuwe wenyewe ili waweze kupita humo katika hali hiyo ya usalama ambayo inahofiwa. Ni kweli hali sio nzuri, lakini sio kumvua nguo mwanamke hadharani, mila na tamaduni za Wazanzibari tunazipoteza wenyewe kwa kufanyakazi katika mazingira hayo, ikiwa kama hali ni hiyo kama hakuna mashine basi wakawekewe mashine ili wapekuliwe katika misingi hiyo, ndio utaratibu. Sio tena kuvuana nguo hadharani.

Hata anayekwenda kupeleka tangazo la kifo basi nasikia avuwe baibui pale, mbona na wanaume hawavuliwi shati, wanafanyiwa wanawake tu? Kwa kweli hili jambo halipendezi kwa utamaduni wetu na ninasema kwamba sio jambo zuri, andaeni utaratibu ambao unaweza kufikika kwa urahisi na kutokuwapa matatizo wanawake hawa wakajisikia wanyonge hadi wakajutia kwa nini wakaajiriwa katika sekta hiyo au sisi tushindwe kufika hapo kwa ajili ya kufuata huduma.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, mimi naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia 95 na asilimia 5 zangu nazibakisha, ili atakaponipa jibu langu Mhe. Waziri basi *Inshaallah* nitamalizia 5 zangu na nitamgaia akatumie. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Nafasi sasa tunampa Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Hassan Hamad Omar afuatie, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu atafuatia na muda ukiwepo Mhe. Salim Abdalla Hamad.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia machache katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo; Mhe. Al Haji Sheikh Said Ali Mbarouk, rafiki yangu wa zamani ambaye kwa kweli namkubali sana katika utendaji wake.

Mhe. Naibu Spika, nataka niwapongeze Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri mama yetu Bi Hindi Hamad Khamis kwa usimamizi wa wizara hii muhimu kabisa kwa nchi yetu, wamepewa mdomo wa serikali. Vile vile wamekabidhiwa nguzo kuu ya uchumi wetu ya utalii kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa na mambo mengi lakini nitazungumza machache ili kuokoa muda. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naanza moja kwa moja katika eneo ambalo limekuwa likizungumziwa sana, *ZBC*. Nikisema *ZBC* nakusudia redio na televisheni.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza namuomba sana Mhe. Waziri ajaribu sana kutupia macho vyombo vyetu hivi viwili, sasa hivi ni shirika na shirika letu hili kwanza ilikuwa ni idara tu ya serikali, tukapiga kelele sana hapa tunamshukuru Mhe. Rais kwa kusikia kilio chetu na kwa kuona vyombo vyetu hivi vinadumaa siku hadi siku. Ndipo tulipopendekeza kwamba liwe shirika angalau waweze kupanga mipango ya kuweza kujitegemea na kuweza kutafuta fedha nje na hata zile za bajeti ya serikali. Lakini bado naona taasisi zetu hizi zinaendelea kusua sua.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba sana wenzetu tuliowakabidhi chombo hiki naomba waache kusokotana. Sasa hivi hakuna maelewano baina ya Mkurugenzi na Naibu wake, sasa kama wana tofauti zao basi wafanye tofauti zao katika mambo yao binafsi. Lakini katika majukumu ambayo tumewakabidhi kama serikali na sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ndio tunaowasimamia, basi tunawataka mara moja waache tofauti zao na wafanyekazi iliyowapeleka pale. Kama wameshindwa kazi basi waseme kwa Mhe. Waziri, ili Mhe. Waziri amuombe Mhe. Rais awatafutie shughuli nyengine ya kufanya.

Mhe. Naibu Spika, tunasikitika sana tunaposikia kwamba kila siku kunaendelea kuwa na manung'uniko katika chombo chetu hasa cha televisheni, lakini vile vile na redio. Mhe. Naibu Spika, bado maslahi ya watumishi wetu hayajawa mazuri. Kwa kweli wenzao ambao wanaitwa mashirika, maslahi yao yanakuwa ni mazuri. Nilikuwa nimeanza kwa upande wa televisheni.

Mhe. Waziri, naomba kaa na watendaji wako hasa hao wakuu. Kuna *hearsay,* na suala hili naomba uzungumze nao binafsi. Tunasikia pale panafanyika mambo ambayo hayapaswi kufanyika katika ofisi za serikali. Sitaki niyazungumze hapa Mhe. Waziri, naomba hiyo kazi ukaifanye wewe mwenyewe na huyo mfanyaji ajirekebishe mara moja. Sisi tunategemea watumishi wetu wanapokuwa serikalini, kama wameruhusiwa na waume zao kwenda ofisini, basi waendelee kuheshimiwa, watu wasitumie mamlaka yao kwa kuwadhalilisha kina mama wetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika eneo hili kwa kweli juzi kulitokezea tukio sio zuri sana, tulipokuwa tuko hapa Barazani. Hiki ni chombo cha wananchi na ndio mdomo wa wananchi na ni mdomo wa serikali, lakini ghafla tukaambiwa kuna *transmitter* ilichomolewa ili matangazo ya Baraza la Wawakilishi yasisikike. Sisi hapa tunayoyasema yote, mtu halali akaota nyumbani kwake. Tunaambiwa na wananchi wetu na ndio maana tunayazungumzia hapa.

Vile vile nilikuwa nataka nizungumzie suala la fedha za matangazo. Mhe. Waziri naomba sana watendaji wako wa *ZBC* wajaribu kuchunga sana hizi fedha za matangazo. Kwa taarifa tulizokuwanazo haya mapato wakati mwengine hayafiki ndani ya mfuko wa taasisi. Sasa je, kama mapato yanaanza kuvuja mapema, hili shirika kwa kweli litakuwa na uhai hili?

Jengine Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kuna jambo nilikuwa nataka ukija ututolee maelezo, kwamba hizi fedha ambazo zilitoka mfuko mkuu wa serikali shilingi karibu zilitakiwa bilioni 8 nafikiri zilitoka bilioni 6, na nadhani mwaka huu mtatuomba tuwaruhusu nyengine. Tutaomba tujuwe yale matumizi yaliyokusudiwa yamefanyika vizuri. Je, na lile tatizo la kuondoka kwenye *analogy* kwenda kwenye *digital* tumefikia hatua gani? Kwa sababu sasa hivi tumekuwa na malalamiko mengi hasa kwa upande wa ving'amuzi vyetu vya *ZBC*, wananchi wanalalamika havifanyi kazi vizuri kama vile ambavyo walivyokuwa wanatarajia. Sasa labda kuna tatizo gani la kiufundi ambalo mpaka hivi sasa matangazo haya yanasuasua.

Kwa kweli tulitegemea mtambo huu baada ya kutengenezwa wananchi wetu wangeweza kupata matangazo bila ya wasi wasi kwa Unguja na Pemba. Kwa hivyo, nitakuja kuomba matumizi ya hizi fedha zilizotoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali, kwa sababu katika ile bajeti ya mwaka uliopita hazikupangwa, lakini kama wanataka nyengine nadhani watueleze hizi za mwanzo zimetumika vipi.

Vile vile, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho aje anipatie maelezo kuhusu suala la mnara wetu wa Bungi, kwa sababu mpaka hivi sasa tunaambiwa bado kuna nyumba hazina umeme, inaonesha hata ule mradi wenyewe haujakamilika, kwa sababu kule zimetumika fedha nyingi kuhusu ule mnara.

Hata hivyo, kwa mara nyengine tena ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, atakapokuja kutoa majumuisho, aje anipe ufafanuzi kwa nini tumetumia fedha nyingi sana kwa mtambo wa *Medium Wave*, lakini hivi sasa umekuwa kama una homa ya vipindi, wakati mwengine unapatikana na baadhi ya wakati haupatikani. Sasa kama nilivyosema kwamba televisheni na redio ndio mdomo wa serikali, na vyombo hivi inatakiwa watendaji wake wawe makini, pia vyombo hivi vinatakiwa viwe vinafanya kazi masaa 24 bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli tunasikitika sana tunapoona vyombo vya habari binafsi vinafanya kazi vizuri kwa muda wote, lakini vyombo vyetu hivi vya serikali wakati mwengine vinakuwa vinasuasua. Kwa hivyo, suala hili ninamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba ajaribu kuliangalia vizuri.

Kwa mfano, nimejaribu kuangalia wenzetu Iraq walikuwa na vita kwa muda mrefu, lakini televisheni yao ilikuwa inafanya kazi na wakati mwengine mitambo inashambuliwa ndani ya nusu saa au masaa mawili matangazo yanatoka. Sasa chombo chetu hichi tuko katika hali ya amani na utulivu, lakini bado kuna ukataji wa matangazo.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na muda naomba niende haraka haraka, vile vile katika *programs* za vipindi na wenzangu sana wamezungumza masuala ya utamaduni pamoja na mambo mengine. Kwa mfano, Mhe. Panya Ali Abdalla amesema wakati mwengine usiku anampigia simu Mhe. Waziri anapoona Shirika la *ZBC* inaonesha matukio ya ajabu.

Sasa kuna kipindi nilikuwa nikikifuatilia sana ambacho ni kipindi cha watoto kuna vijana wamejitolea kuna kipindi kinaitwa USEWAZA. Kwa kweli kipindi kile kilikuwa kinawakusanya vijana wetu ambao ni wanafunzi na kipindi kile kilikuwa na *program* ambayo inatoa uelewa pamoja na elimu, watoto wengi kipindi kile walikuwa wanakifuatilia na hata na sisi wazee wao tunakuwa tunavutiwa tunakaa nao kwenye televisheni na kuangalia kwa pamoja.

Kwa hivyo, kipindi hichi hapa katikati nilipokuwa sikioni nikajaribu kumtafuta yule muhusika nikamwambia vipi mbona hichi kipindi mumekikatisha, akaniambia tumeambiwa kipindi hichi tukilipie karibu shilingi milioni 2,800,000/= kwa mwezi.

Mhe. Naibu Spika, kweli tumeanzisha shirika, lakini kipindi hichi sio cha biashara, isipokuwa ni kipindi cha kutoa elimu, na chombo chetu hichi kilipoanzishwa mwanzo kulikuwa na matangazo na siku zile sisi wadogo, inaimbwa nyimbo uhuru ni wetu; wanakuja watoto wawili na wakati huo sisi wenyewe tulikuwa ni watoto wadogo na tulikuwa tunafurahia, kwamba kipindi cha watoto kimemaliza na tunakwenda kulala na ilikuwa ikiandikwa Elimu kwa Televisheni.

Kwa maana hiyo, televisheni yetu ilikuwa ni elimu na hivi sasa imekuwa na burudani kubwa zaidi pamoja na biashara, lakini bado ninaomba ule msingi wa kuanzishwa vyombo hivi vya elimu ninaomba uendelee.

Kutokana na hali hiyo, ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kipindi hichi sio cha kibiashara ninaomba wale vijana waruhusiwe na labda wasaidiwe kutafuta wadhamini, ili kipindi kile kiweze kuendelea, lakini kwa kuondoka kipindi kile sisi wazazi tunasikitika sana.

Vile vile naliomba Shirika la *ZBC* (redio na televisheni), kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hivi sasa ni shirika wamtafute mtaalamu wa *Marketing*, ili aweze kufuatilia. Kwa kweli vyombo vyetu hivi wasisubiri kupelekewa matangazo wapelekewe pale ofisini, isipokuwa wahangaike.

Kwa hivyo, *Marketing Manager*, anatakiwa kuondoka na kwenda wizara tofauti, na kila wizara wanayo mambo yao mengi wanayotaka kutangaziwa, wanaweza kwenda kupatana na kuweza kutoa *advance* pengine ndani ya mwaka mzima wakakupeni *advance* mukaanza kuwatangazia matangazo yao, lakini kwa kukaa tu ofisini na kusubiri matangazo, nadhani vyombo binafsi vitawashinda. Sasa suala hili ninaomba sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wananisikia kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wajaribu kubadilika, hii *ZBC* kwa kweli iwe na hadhi.

Jambo jengine mwaka jana nilizungumzia kuhusu kadhia ya uajiri, ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwamba alilisimamia ingawa ajira bado, lakini Mhe. Naibu Spika, naendelea kusisitiza kwamba itakapotokezea ajira muangalie wale vijana wanaojitolea pale kwa muda mrefu sana na wala musije mukawaacha.

Kwa upande wa watangazaji sisi kwa bahati huwa tunafanya mazungumzo na waandishi tofauti. Kwa mfano, kuna mwandishi mmoja alikuja Dodoma kule ambaye ni mashuhuri sana na wala sitaki nimtaje jina, lakini alikuja Dodoma na kutuhoji kuhusu Bunge la Katiba na mambo mengine, na mimi nikajaribu kumuuliza mbona wewe unakuwa mtundu sana unatufuata mpaka huku, alisema kwamba mimi ndio *professional* yangu hii, kwamba nimekuja huku na kujaribu kusikiliza maoni, kwa sababu Zanzibar watu wanasikia mambo mengi, kwa hiyo ametuhoji sana.

Vile vile hapa anaandaa vipindi tofauti pamoja na mazungumzo baada ya habari, kwa mfano siku za Jumamosi anaandaa vipindi asubuhi pia anawaita Wakurugenzi pamoja na watendaji mbali mbali wa serikali.
Kwa hiyo, watu wengi wenye akili zao timamu kile kipindi cha asubuhi siku ya Jumamosi wanakisikiliza kwa sababu wanapata kujua utendaji wa serikali pamoja na matatizo mbali mbali na wananchi huwa wanapiga simu.

Mhe. Naibu Spika, hata na mimi mwenyewe pamoja kwamba si mtendaji wa serikali, lakini nimeshawahi kuitwa karibu mara tatu pale na ninakwenda pale ninahojiwa na wananchi wanapiga simu, kwa kweli ni kipindi kizuri sana.

Hata hivyo, mtangazaji huyu hata zile taarifa za habari za kiingereza kwa muda mrefu alikuwa akisoma yeye na hivi sasa wapo wengine wameongezwa, lakini ni mbunifu sana. Sasa mambo mengine inakuwa siri, kwa kuwa sisi ni wasemaji wa wananchi nilijaribu kumuuliza hebu tuambie maslahi yako yako vipi? Kwa kweli Mhe. Naibu Spika ni aibu hata kusema, mtu ambaye amefanya kazi zaidi ya miaka 31 hivi sasa mshahara wake ni wa kima cha chini kabisa pamoja na jitihada zote.

Hivi karibuni nilisikia kuna vijana wanasifiwa sana kwa mfano, yule kijana wetu ambaye yuko Dar-es-Salaam Juma Mmanga na alizungumzwa sana, lakini kijana mdogo wa juzi na anafanya kazi vizuri, yeye kazi yake kubwa ni kututangazia magazeti na mambo mengine, sasa kuna hawa wengine ambao wameshafanya kazi muda mrefu, tena ni wabunifu na vipindi vyao vinakubalika sana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ninaomba sana, tunajua mnayo *scheme of service* na tunaomba sana mjaribu kuangalia na hawa wenzetu, ili wasije wakatukimbia na wao.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende haraka haraka na wizara hii ina mambo mengine. Sasa naomba nizungumzie suala la Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari. Kwa kweli tamasha hili tumeanza kulikosa, kwa sababu ule mwezi wake unakuwa unaingiliana na mwezi wa Ramadhani, lakini tamasha lile Mhe. Naibu Spika linaitangaza Zanzibar sana, na hata sekta yetu ya utalii na wananchi wanapata nafasi ya kuonesha utamaduni wao. Kwa hiyo, hivi sasa ni zaidi ya miaka mitatu tamasha hili limekatika kwa sababu linaingiliana na mwezi wa Ramadhani.

Sasa ninaomba tamasha hili liangaliwe lazima liwe katika mwezi fulani, kama mwezi wa Ramadhani tulisogeze nyuma au kulipeleka mbele, ili wale wananchi wetu wenye kazi au mambo ya utamaduni yaweze kuendelea. Mhe. Naibu Spika, tunasikitika sana tamasha hili kwamba limesita kwa muda mrefu, hivyo tunaomba Mhe. Waziri, ambaye ni msikivu naamini ataweza kulifanyia kazi suala hili.

Vile vile ninamuomba Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba awasiliane na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, zamani sisi tulipokuwa tukisoma skuli kuna maneno ya hekima ya viongozi wetu unakuta katika *Notice Board*. Kwa mfano, "*Bora kuwa na kitu kidogo tukagawana, kuliko kuwa na kingi tukaanza kugombana*". Kwa hiyo, misamiati kama hiyo ya viongozi wetu hivi sasa imeanza kupotea.

Mhe. Naibu Spika, naomba ile misamiati naamini walimu wakongwe Mhe. Waziri kwa sababu wewe ndio unayelinda utamaduni, ni vyema kushirikiana na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, ili kuyarejesha hayo.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la utalii. Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nianze kwenye Hoteli ya Bwawani, mimi hivi sasa ile *interest* ya kusema Hoteli ya Bwawani iboreshwe, na vitu vyengine kwa kweli naona ndani ya akili yangu imeshaanza kunitoka, kwa sababu kila ninavyoangalia uchumi wa Zanzibar hapo mbele tunategemea utafunguka kwa kasi sana, na tatizo Zanzibar hivi sasa tumeshajenga sana.

Sasa mimi kwa fikira zangu lile eneo la Bwawani pengine baadaye wataalamu wanaweza kuja kuliona kwa mbali, eneo lile kuwepo Hoteli ya Bwawani naona limeshapitwa na wakati, isipokuwa fikra zangu zaidi kutokana na udogo wa bandari yetu juzi nilipendekeza kwamba yale mabanda ya kule ndani ya bandari yavunjwe, ili yawekwe makontena, lakini lile eneo la Bwawani hapa mbele ya barabara pakajengwa ukuta, ili yale makontena yasionekane wazi wazi, na lile eneo lote likafukiwa na ikawa Yadi ya Makontena.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni tumesikia serikali inataka kutafuta eneo Fumba kwa ajili ya kuwekea makontena kama nilivyosema juzi. Kwa kweli meli inapoteremsha makontena, na makontena yale yakawa yako mbali masafa marefu. Kwanza serikali itakula hasara kwa mafuta kutoa makontena bandarini mpaka Kisauni, lakini pale ni pahala karibu sana, kwa hiyo hata meli kama imekuja, inachukua muda mfupi kuweza kurejesha pale makontena matupu, na pia yale makontena yakaweza kutolewa pale.

Kwa hiyo, pamoja na Mhe. Waziri anayo mipango yake ya wizara yake, lakini mimi kwa mtazamo wangu na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yupo hapa, kwa kweli ninaona lile eneo la Hoteli ya Bwawani sehemu ile tukaifanya Kontena *Yard*, ili kwa kutegemea uchumi wetu hapa Zanzibar utafunguka. *(Makofi)*

Jengine Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wizara hii inashughulikia mambo ya utamaduni, bado kuna suala la mgao au mrahaba wa wasanii wetu. Kwa kweli ninaomba sana, kwa sababu wasanii wetu kwa kweli wanafanya kazi kubwa na redio bila ya burudani inafika pahala unaweza ukasinzia. Kwa hivyo, ninaomba sana na wenzangu wamezungumza suala la mrahaba na mimi nataka kulitilia nguvu, ili wasanii wetu zile kazi ambazo wanazozifanya ziwe na tija.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, bado dakika tano.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, dakika tano sawa. Sasa juzi nilipokuwa nikizungumzia wizara inayohusiana na masuala ya kazi, nilizungumzia ajira na sio ajira rasmi, lakini ni zile ajira za upakaji wa hina watalii katika mahoteli. Mhe. Naibu Spika, eneo hili ni la utamaduni, na kama tunatangaza utamaduni wetu utiaji wa hina na wanja kwa wanawake wa Zanzibar ni sehemu ya utamaduni. *(Makofi)*

Kwa kweli wanja unaotiwa na Wazanzibari Mhe. Waziri wewe mwenyewe unaujua, yaani ukitizama tu lile jicho lazima litarudi. Mhe. Naibu Spika, ajira hii hivi sasa katika mahoteli yetu imekuwa inachukuliwa na wageni, katika kitu ambacho sikipendi, kwa sababu hizi ndizo ajira ambazo Wazanzibari wana utaalamu nazo, kwanza ni utamaduni na pia wanao utaalamu. *(Makofi)*

Sasa naomba sana Mhe. Naibu Spika, kwamba Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo awasiliane na Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Kazi na Utumishi wa Umma, ili washirikiane katika hoteli zote kila zile sehemu ambazo zinashughulika za kutia hina na wanja, maeneo yale kama kuna wageni waondoke, kwa sababu zile ajira ambazo Wazanzibari wenyewe wanaziweza. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka niende kwa haraka haraka, ili nimalizie. Sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la utalii. Juzi Mhe. Waziri alituita kwenye semina na tumeanza kuona mipango yake. Kwa hiyo, tunamuomba sana na ile *Think Tank* iwe ya kitaifa na wala isiwe Mhe. Waziri anaanzisha jambo na halafu baadaye yanakuja mabadiliko.

Kwa kweli utalii wetu tumeshauona kwamba hivi sasa wale watalii ambao waliokuja mwanzo wanakuwa hawavutiwi kuja tena, kwa sababu vile vitu vinavyowavutia Zanzibar ndio vile vile. Kwa mfano, juzi alituonesha mpango ambao anataka kutangaza kwa ajili ya kuongeza vivutio vya utalii, mpango ule sisi tunakuunga mkono sana, na tunaomba mpango ule uendelee.

Lakini kubwa zaidi katika suala la usalama, kwa sababu tunawaita watalii ili waje, na mwenzangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu amelizungumza vizuri sana, kwamba suala la *CCTV camera* na hapa wamesema wanao Mradi wa Kuanzisha Kituo cha Taarifa cha Usalama cha Utalii.

Sasa naomba katika mradi ule na zimetengwa karibu shilingi milioni 100 kama sikosei, fedha zile ni kidogo na kama tungekuwa tunaweza kutafuta fungu eneo jengine katika wizara nyengine, eneo lile tungeliomba likatiliwa fedha nyingi.

Katika yale maeneo muhimu ya utalii kama vile kwenye *junctions* zile tuweze kufunga *CCTV cameras,* kama juzi tulikuwa nao wenzetu wa *HUAWEI* kutoka China, ambao afisi yao ni Dar-es-Salaam na Mhe. Waziri ninamuomba awafuate kwa ajili ya kuzungumza nao na kukopa si aibu na hasa kuwakopa Wachina si aibu zaidi, nadhani tuwakope, ili watufungie hizi kwa ajili ya kuweza kupata usalama wa watalii wetu pamoja na sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hivi juzi limetokea tukio na ninaomba Wazanzibari sote tulilaani tukio lile, yaani tukio la mwanzo kabisa lililotokea Darajani la bomu. Na vibomu vya hapa vilikuwa ni vile vya chupa imetiwa utambi, lakini lile la juzi wataalamu wanasema ni bomu la kutengenezwa kiwandani. Kwa kweli suala hili ni la kusikitisha sana, na kila mmoja anatakiwa alilaani. *(Makofi)*

Vile vile ninamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wakati atakapokuja kufunga Baraza hili alaani kwa kauli kubwa sana tukio lile, pia tunaomba yeyote atakayekutwa na kadhia ile achukuliwe hatua kali za kisheria, kwa sababu wale ndio maadui wa uchumi wa Zanzibar. Sasa kama leo mabomu yanaanza kuruka pale, hivi wageni wetu watavutiwa kuja hapa? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, suala lile linasikitisha sana na ndio maana tukasema kwamba hizi *CCTV camera* zikifungwa zitaweza kusaidia wale wanaofanya matukio kwamba walitokea wapi na walipitia wapi, ili kuweza kupambana na vitendo kama hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, malizia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuniambia nimalizie. Pia katika masuala ya michezo ZFA kwa kweli hakuko salama.

Jambo la mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, ninaomba na Mhe. Waziri hili alisimamie, kwamba ufanyike Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa Wadau wa Michezo, kwa ajili ya kuiangalia Katiba ya *ZFA* iko vizuri? Na kama haiko vizuri irekebishwe, ili turejeshe Historia ya Michezo ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, na hapa nimekuja na kitabu Mhe. Naibu Spika, lakini muda sina ambacho kimeandikwa na ndugu yetu Ali Shaaban, imeandikwa historia ya Mzee Karume.

Kwa kweli kwenye kitabu hichi kimeonesha Mzee Karume jinsi gani alivyokuwa anashiriki katika kuhamasisha michezo kwa upande wa wanafunzi pamoja na Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, na mimi nilikuwa simjui Mzee Abrahman Makungu baba yake Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Kwa hivyo, kitabu hichi ninaomba Waheshimiwa Wajumbe tukitafute; cha Historia ya Mzee Karume mwaka 1905 mpaka 1772. Mhe. Naibu Spika, kitabu hichi kina historia kubwa na kuna mpaka wale watawala wa Zanzibar pamoja na wake zao, yaani mambo mengi ya Zanzibar, lakini muda sina ningelikisoma hapa na nyote mungevutiwa. *(Makofi)*

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, nitaunga mkono bajeti hii, lakini zaidi baada ya kupata maelezo ya kutosha katika yale maeneo matatu makubwa, na hasa yale matumizi ya fedha makubwa ambayo *impact* yake tunaona bado haifanyi kazi sana. Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, sawa. Sasa nafasi tunawapa watu watatu muda uliobakia, lakini tusirejee Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na mwisho Mhe. Salim Abdalla Hamad.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru sana kunipa nafasi hii kwa ajili kuchangia Hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba yake kwa muda mfupi sana na imeeleweka.

Vile vile nichukue nafasi hii kwa sababu tunazungumzia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, ninaomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Timu ya *Shaba Sports Club* kutoka Kojani kwa kupanda daraja mwaka huu 2014/2015. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wale vijana ni machachari, na katika michezo yao miwili ya kirafiki iliyochezwa hapa Zanzibar baada ya kutoka Kisiwani Pemba kwa kupanda daraja, walicheza mchezo wa kirafiki na Timu ya Taifa ya Jang'ombe na waliiadhibu kwa mabao matatu kwa moja (3-1). Hata hivyo, siku ya pili wakiwa vijana wamechoka wakaifunga Timu ya *Malindi Sports Club* mabao wawili kwa moja (2-1). Kwa hivyo, vijana hawa tunavyo vipaji vya kutosha katika Kisiwa cha Kojani, ambavyo tunapaswa kuvienzi. *(Makofi)*

Pia mashirikiano haya nimeyapata kwa Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo; kanipa mashirikiano makubwa mpaka timu yetu kupanda daraja kwa kushiriki vikao mbali mbali nilivyokuwa namualika, na kuweza kufika malengo na kutoa nasaha zake na michango yake mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, sasa niendelee katika mchango wangu niende katika sekta ya habari. Sekta hii ya habari ni sekta muhimu sana kwa jamii. Sekta ya habari inahabarisha watu kupata habari za matukio mbali mbali; pengine mazuri na mabaya lakini watu wanapata habari.

Vile vile sekta hii ya habari kama utaitumia vizuri italeta faida kubwa sana na kama utaitumia vibaya basi unaiangamiza jamii. Nikizungumzia mambo ya sekta ya habari Mhe. Naibu Spika, kwa mfano mauaji yaliyotokea Rwanda ukitia na vita vya ukabila basi na vyombo vya habari vilichangia. Kwa hivyo niseme habari katika vyombo vya habari ni silaha, ukiitumia vizuri utawajenga wananchi wako vizuri na ukiitumia vibaya basi ni maangamizo makubwa sana. Juzi tu hapa tumo ndani ya Baraza la Wawakilishi tulipata habari katika simu zetu kwamba kuna bomu limetumbuka saa 2:30 Darajani, lakini vyombo vya habari hivi vinalikuza mpaka unaona Zanzibar inatisha, tunalaani vikali kama alivyozungumza Mhe. Hamza, hatulipendelei, lakini na vyombo vya habari vizungumze kwa umakini, majanga yametokea sehemu mbali mbali lakini Zanzibar kikitokea kitu kinakuzwa vibaya mpaka watu wanakuwa woga kufika katika nchi yetu, hili ni tatizo. Kwa hivyo tunasema magazeti haya yanapotoa habari yaseme vizuri, wasipotoshe kabisa, watoe kutokana na jambo lilivyotokea, waliandikie kwa uhalisia wake.

Mhe. Naibu Spika, nikielekea katika sekta hiyo hiyo ya habari uchumi wa TV yetu ya Zanzibar ilikuwa na vipindi vizuri sana vya kuelimisha umma, lakini sasa ukiangalia vipindi vile vya kuelimisha umma vinapotea hasa utamaduni wetu wa Kizanzibari. Mimi nadhani hapa palikuwa na kipindi cha adhana ukifika wakati wa swala Televisheni Zanzibar ilikuwa inasomwa adhana na dua ya adhana, lakini sijui ni mimi tu siioni dua ile ya adhana kusomwa tena ndio dua yake sijui katika TV yangu tu au na TV nyengine imepotea kabisa. Mheshimiwa kulikoni jambo hili? Hebu nataka utakapokuja hapa ulitolee maelezo, kwa sababu gani kipindi kile kizuri kimeondolewa. Ikisomwa adhana katika kipindi kile cha swala basi inaoneshwa watu wanakuja msikitini, wanatia udhu; vitendo vyote vinaoneshwa pale, lakini sasa hivi imepotea kwa nini? Na kama kimeondolewa hapo hamtutendei haki katika utamaduni wetu wa Kizanzibari na maadili yetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na michango yangu sanaa na maigizo ndani ya Televisheni tumesema vyombo vya habari vinaelimisha jamii, lakini ukiangalia maigizo yetu ya kisasa hayaendi jambo jema katika uigizaji huo. Kulikuwa na waigizaji wazuri kama Halikuniki na Bi Njiwa, wale walikuwa wanaleta burudani safi ya maigizo na utamaduni wetu, lakini sasa hivi *wallahi* unakuta igizo basi linachochea, mimi nasema linachochea kabisa kwa sababu mtu anaingia, mtu anafukuzwa na kitu ni kuwajenga vijana katika tabia mbaya na kujenga ujasiri

mbaya, lakini wale waliigiza mambo yale wanaigiza kwa utamaduni na mavazi mazuri lakini sasa hivi ukiangalia utamaduni ule unapotea. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo tunakuamini sana, tunaomba uturudishie mambo yetu yaliyo mazuri na haya mabaya yapotee kabisa hatutaki kuyaona.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na sekta ya utamaduni katika ukurasa wa 7 kifungu cha 16 nizungumzie pale kidogo, kazungumzia Mhe. Hamza hapa muda si mrefu nami nalizungumzia kwa sababu katika kwenye *point* zangu limo huu utamaduni wa Wazanzibari kupaka hina ni utamaduni mzuri ni wachoraji wazuri, na tunawaona wanavyokwenda safari basi kama mtu anatoka Unguja anakwenda Pemba anachora hina ili apendezeshe kwa mume wake; ni jambo zuri. Sasa fikiria kama ni jambo zuri na wengine watakuja mambo mazuri, na tayari sasa hivi watu wanatolewa hapa Zanzibar kwenda kuchora hina hata Tanzania Bara, kwa sababu ni jambo zuri. Mheshimiwa lakini tulikuwa na utamaduni wetu, tulikuwa tunatengeneza viatu vya ngozi hapa; makubadhi haya yana heshima yake haya, ulikuwa ukivaa kanzu yako koti na kofia na bakora yako unatembea vizuri na makubadhi, hata ukiangalia kisa cha Nabii Yussuf naye kavaa makubadhi haya, wale waigizaji wanavaa makubadhi kwamba vazi hili lina heshima yake, kwa hivyo ndio utamaduni wetu.

Lakini haitoshi angalia katika kitabu chako hichi mbele na nyuma huku utaangalia nini vazi zuri la kanzu katika ufunguzi Chuo cha Maendeleo mambo ya utalii wamevaa vizuri hawa, huku tukitizama na Rais wetu na wewe mwenyewe mumevaa vizuri katika utamaduni wetu katika kitabu hichi. Sasa wewe ukija hapa watalii wakituvalia vimini unatuonesha nini? Naomba utaratibu wa mtu ufuatwe, na hayo ndio maendeleo, kama unafuata hivyo ukija kule mtu atajua tu ukienda Zanzibar tena mimi ninavyokwambia hao watalii wanapovaa kanga wanapendeza kuliko vimini vyao, sasa vyenginevyo utakuwa hutufanyii haki ni kutosimamia vizuri tu. Angalieni kikundi kile cha wanawake watupu kuna mzungu kule anaimba nyimbo za Kizanzibari tena kwa lugha ya Kiswahili; kikundi cha Tausi kile kimejijengea heshima, yule mwanamama wa kizungu anasimama anaimba pale nyimbo za Kiswahili kabisa, japo Kiswahili chake hakiendi sambamba na sisi lakini unamjua au sivyo bwana, huu ndio utamaduni wetu.

Mhe. Naibu Spika, itakumbukwa ni tarehe 23/5/2014 katika timu niliyoitaja mimi na wewe limefanyika tamasha kule kisiwani Kojani. Tamasha ambalo limetuletea hadhi sana, ni wewe mwenyewe uliyekuwa mgeni rasmi katika shughuli hiyo ulishuhudia vipaji vya vijana wetu wa Kojani jinsi wanavyoogolea.

Mwenyewe ulishuhudia na uvukaji wa mitumbwi jinsi wanavyofanya kazi, kama utawaendeleza vijana hawa basi wanatujengea heshima katika taifa letu hili kitaifa na kimataifa wanataka kuelekezwa tu. Umemkuta bi Mwanteta anafanya shughuli zake kuvuta kamba pale na aliwashinda wanaume, wewe ulikuwa shahidi. Nasema tamasha hili lipangwe na liendelezwe vizuri, kwa sababu ile hatua ilikuwa ni ya muda lakini ukiliendeleza mwaka hadi mwaka tunalifanya kwa Zanzibar nzima tunachagua muafaka wapi tunafanya.

Mhe. Naibu Spika, lakini ikumbukwe katika enzi hizo basi kulikuwa na michezo mbali mbali angalia nchi yetu hii ni ya kisiwa, haifai hata watoto wetu wakawa hawajui kuogolea, ni watu wa kufanyiwa mazoezi wanajifundisha kidogo mpaka wanaelewa Mwenyezi Mungu atuepushie mbali likitokea jambo mtu anajihami, lakini mtu wa kisiwa hajui kuogolea wewe ni mtu wa kisiwa, kweli tatizo, lakini yote yanataka kuelimishwa na kufanyiwa michezo. Maskuli kule kulikuwa na michezo mbali mbali ya ukakamavu, kulikuwa na michezo ya mbio na kadhalika lakini sasa hivi michezo yote imepotezwa.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika sekta ya utalii. Ni kweli inatupatia kipato kikubwa katika nchi yetu ya Zanzibar lakini pamoja na mabadiliko ya tabia ya nchi basi na mabadiliko ya tabia ya watu kuwaelimisha watalii wetu, bighairi ya hivyo basi tutakuta majanga mbali mbali hawa wanaotumia pembe za watalii kuna wengine si wema lazima wanapata muongozo mzuri katika kufuatanishwa.

Unakuta mtu mtalii anatembezwa saa 4:00 katika vichochoro hapa pana usalama? Lazima tujikite katika kuelimisha watalii, lakini kama kwamba haitoshi tumesema sehemu nyingi wamewekeza wawekezaji lakini wazalendo nao wana haki zao za msingi katika nchi yao. Kuna sehemu nyengine mzalendo hawezi kupita kwa sababu ya hawa hawa shughuli za kitalii. Ni maeneo waliyokuwa wakitumia sasa hivi yote yamewekezwa hawapati hata kupita kwenda kwenye sehemu zao. Kuna wavuvi, kuna wengine wanatembea sehemu mbali mbali kule lakini wao hawana haki ya kupita maeneo kama haya Mheshimiwa tuliangalie kwa kina kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu tumesema wapate angalau wenzangu wawili nao basi nitafupisha mambo yapo tele, naomba nielekee katika Baraza la Kiswahili la Zanzibar. Katika ukurasa wa 19 Mheshimiwa tunavyozungumzia Kiswahili ndio lugha yetu lakini katika kukienzi Kiswahili ili kitumike na watu wengi wakitumie, basi sisi wengine tuanze, lakini leo unaweza kwenda benki ikawa fomu yote imejazwa kwa

Kiingereza unampa mtu hata kuijaza haijazi, panapouzwa tiketi za meli basi yote ya Kiingereza, je hiki Kiswahili tunakifanyia haki yake hasa katika nchi yetu? Nakumbusha Mheshimiwa kama tunataka kutunza Kiswahili basi tutumie maneno ya Kiswahili kama tunavyozungumza hapa Barazani.

Mhe. Naibu Spika, kwa kujali muda wako na taa yako umeiwasha hujaizima, naomba kwa haya machache niishie hapo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa hali ya uzima na afya njema, pia nakushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Pia nimpongeze sana Mhe. Said Ali Mbarouk kwa kazi yake nzuri kabisa, pia napongeza watendaji wake wote wa Wizara kwa kazi yao kubwa inayogusa wananchi kwa maendeleo ya nchi yetu hapa Zanzibar, lakini pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati na watendaji wake wote.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianzie na sekta hii ya utamaduni na michezo imeundwa na Kamisheni ya Utamaduni na Michezo. Niipongeze sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuutengeneza uwanja wa Amaan kwa kutia *tartan* na kuutia nyasi bandia. Kazi hiyo nzuri na imefanyika vizuri sana, pia na uwanja wa Gombani kwa kazi nzuri iliyofanyika, lakini mimi niseme tuangalie sana kwenye viwanja vya ndani sasa naomba sana Serikali iangalie suala la kutengeneza viwanja vya ndani *in door* au uwanja wa Tennis pia nao muhimu katika kukuza vipaji vyetu vya michezo hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia vipaji hivi vinatoka maskulini, na kutokana na hali inavyokwenda sasa hivi maskulini vipaji vimeachwa haviangaliwi, hasa ukitizama mpira wa miguu kwani mpira wa miguu si kwa ajili ya burudani tu; ni kuunganisha watu mbali mbali kitaifa, kisiasa na kijamii kwani suala hili ni muhimu. Na tuangalie sana katika maisha yetu na mazingira yetu tuliyokuwa nayo hasa katika mpira wa miguu. Suala kubwa lililoshusha soka letu katika nchi yetu ya Zanzibar mimi niseme wanaochangia kushuka mpira wetu ni ZFA wanachangia sana kushusha soka letu, kwani kuwa wakati mwengine haki ipatikane kwa timu zetu inakuwa haipatikani. Kwa hivyo mimi naomba sana Mhe. Waziri, uangalie sana suala hili, kama juzi nilikuwa na mfano timu yangu ya jimbo langu Bububu imeshindwa katika kucheza mechi na kuingia katika daraja la pili lakini inatolewa inaingia timu nyengine ya kiwanda cha Bakhressa, naomba Mhe. Waziri ufuatilie suala hili, hapa kuna ubadhirifu umefanyika kwenye timu hizi mbili, kwa hivyo naomba sana liangaliwe suala hili.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika ukurasa wa 5 kifungu namba 12 uimarishaji wa studio za kurekodi kwa kuipatia vifaa. Kwanza niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuliona hili na umuhimu wake; suala la studio kurekodi muziki kwa ajili ya vijana wetu na wananchi wetu, lakini hapa nimeona kwenye kitabu Mhe. Waziri kuna milioni 80 Serikali imewekeza kwenye vifaa hivi, kwa kweli napongeza sana kwa juhudi hii nzuri na kubwa kabisa kwa vijana wetu hawa, na kwa serikali imeonesha nia njema kwa wasanii wetu wanaokabiliwa na changamoto nyingi sana katika kazi zao za kurekodi filamu na muziki, kwa kweli hili ni suala la kupigiwa mfano na hatua hii iendelee.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme katika wasanii wetu kuna changamoto nyingi sana hasa kwenye filamu na muziki. Ukiwa msanii kwa sasa hivi jamii inakuona kama wewe ni muhuni au huna maana katika jamii yetu, kwa kweli hichi kitu si cha ukweli na hizo dhana potofu kabisa, kwani wasanii wana mafanikio makubwa ukilinganisha na wafanyabiashara wengine mbali mbali.

Ukiangalia mfano mzuri tu tuna msanii wetu Diamond juzi alikuwa Marekani na alikuwa na Mhe. Rais Jakaya Kikwete walizungumza na kula chakula chao cha usiku na wakazungumza mambo mengi kuhusu kushughulika kwenda kule kufanya kazi zake kwa kuwakilisha Tanzania kwa ujumla pia kwa ajira yake kwa kupata kipato.

Pia na wasanii wetu hapa Unguja Berry Black na Baby J washakwenda nje lakini wana mazingira magumu sana ya kufanya kazi zao hasa hii kazi ya studio kurekodi miziki yao. Kwa kweli niipongeze sana Serikali kwa hatua iliyoichukua hapa na iendelee mpaka tufikie lengo la kuwapatia wasanii hawa kituo maalum cha kurekodi kazi zao kama vile Dar es Salaam wanayo; Mhe. Rais Jakaya Kikwete aliwaandalia kituo maalum au Studio maalum inayoitwa *THT* (*Tanzania House of Talents*) ambayo inatoa wasanii wazuri ni hao mfano wetu akina Diamond na Lina wanatoa nyimbo nzuri na wamefundishwa vizuri kwa kweli kufanya kazi zao, kwa hivyo naipongeza sana serikali kwa hatua hiyo.

Mhe. Naibu Spika, niseme wasanii wetu hasa hapa Zanzibar wanapata tabu sana, nichukue mfano mzuri kabisa wasanii wetu hawa wanaorikodi tamthilia katika Televisheni Mr. Muddy na wenzake kwa kweli hawa wasanii wanapata tabu Mhe. Naibu Spika. Mhe. Waziri hawa wasanii wanatoa filamu zao ZBC lakini unakuta hawana usafiri, hawana vifaa, hawana chakula, hawana hata udhamini hata zile pesa za kulipwa inakuwa hamna wanajitolea tu hawa vijana.

Kwa kweli Mhe. Waziri naomba uwasaidie sana hawa vijana wapate wadhamini wa kuwasaidia ili waweze kuendelea na kazi zao vizuri sana, pia na sisi hawa wasanii wakati wa kampeni zetu sisi binafsi tunawatumia hawa wasanii kwa kazi zao, nyimbo zao, ili sisi tupate ushindi katika Majimbo yetu, lakini inapomalizika kampeni zile tunawasahau na tunawatupa kabisa.

Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri wasanii naomba waangaliwe sana, ni muhimu sana katika maisha yetu na katika kazi zao wanavyozifanya kutusaidia hata sisi uongozi wetu tunaoupata kupitia kwao wao kutusaidia kutuimbia nyimbo nzuri na wananchi wakatukubali.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimshukuru sana Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete na Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuwathamini wasanii hawa. Mimi nampongeza sana Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano na Rais wa Zanzibar kwa kuona umuhimu wao na kuwaita na kuzungumza nao kila baada ya muda ukifika anakuwa anawasikiliza changamoto zao, lakini mimi niseme bodi ya sensa wale wasanii ambao watakuwa hawana adabu au wanatuvunjia mila na utamaduni wa nchi yetu ya Zanzibar naomba bodi hii ya sensa iangalie sana kazi zao, na kama kazi zao itakuwa inavunja mila na utamaduni wa Zanzibar naomba wafungiwe kazi zao, na wafungiwe hata kufanya kazi zao kama za filamu au kazi za nyimbo zilizokuwa hazina maadili mazuri ya kufundisha na kuelimisha. Kwa hivyo naomba hilo Mhe. Waziri kupitia bodi hii ya sensa iangalie sana.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba sana vipindi kama hivi vya wasanii wetu hawa wa ZBC Mr. Muddy naomba sana Mheshimiwa hii ni kama ajira kwao. Hawa vijana wetu na kwa kweli hawana udhamini, naomba sana wafanyabiashara binafsi; makampuni ya simu, mabenki wawadhamini hawa vijana wetu ni moja ya ajira, tunasema Serikali kuwapa vijana wetu ajira haiwezi, kwa hivyo naomba sana Serikali yetu kupitia wizara yetu hii nzuri kabisa na Waziri wetu makini, awatafutie wadhamini hawa vijana wetu ili waweze kufanya kazi zao nzuri na waletewe ujumbe katika jamii yetu waweze kutuelimisha.

Mimi naomba sana sana hasa wasanii wa kike, hawa wasanii wajitambue na wajijue nini lengo lao au mahitaji yao katika ndoto zao za kufikia malengo, kwani wasanii wa kike Mhe. Naibu Spika, wanakuwa kwa kweli ukitizama wanaonekana kama wahuni, watu ambao wamekosa muelekeo au wamekosa dira ya maisha yao.

Kwa hivyo naomba sana wasanii wa kike wanapofanya kazi zao za kisanii wawe makini na kuwa kwenye hali ya kutafuta rizki sio kwenye hali nyengine ya kuharibu maisha yao, mwisho wa siku ikawa ule usanii hauna maana yoyote, hauna tija yoyote kwao. Kwa hivyo naomba sana wasanii wa kike muwe makini katika kujitatua. Na pia Wizara Mhe. Waziri naomba iwasaidie sana hawa wasanii wa kike kwani wao jamii inawadhania wahuni, hawafai kufanya filamu au usanii wa muziki, kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri kuhusu suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, niingie kwa haraka haraka sasa kwenye ukurasa wa 44 kifungu cha 81 Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar; Maruhubi. Kina jukumu la kutoa taaluma itakayowezesha kujenga rasilimali watu, ujuzi na utaalamu kwa kuimarisha sekta ya utalii Zanzibar. Serikali imefanya Chuo hiki kwa nia njema kabisa na kwa nia ya dhati, kwani vijana wetu waweze kusoma hapa na kutoka katika taaluma nzuri kabisa iliyokuwa inaweza kuwapatia ajira. Hasa katika Chuo hiki mimi ninawapongeza sana hawa walimu wanaofanya kazi hii ya kusomesha vijana wetu kwa kazi yao kubwa a kuwapa taaluma hii ya utalii.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa wa 7 kifungu namba 17 Sekta ya Utalii. Sekta hii ya Utalii Mhe. Naibu Spika, ina changamoto nyingi na hasa katika hawa wenzetu ambao wanaovutia watalii hapa Zanzibar. Tizama ubunifu wa kazi zao katika kukuza utalii wa utamaduni, kusaidia kukuza mapato ya taifa na maendeleo kwa ujumla kwa kivutio cha utalii, lakini hawa vijana wetu au vikundi vyetu vina changamoto nyingi sana tukiangalia hasa vikundi vya ushirika, kwa kweli wanakosa elimu, ujasiri amali na vikundi vinategemea sana wafadhili, na mara nyingi vikundi hivi vinakuwa kwa kweli vinasaidia kuvuta utalii kwetu Zanzibar hapa lakini wanakosa ufadhili na wanakosa hata fedha za kufanyia kazi zao Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo naomba Wizara iangalie sana hawa wenzetu; hawa vikundi hivi viweze kutusaidia kupitia utalii. Ukiangalia sana suala la ngoma na muziki wa asili na ngoma zetu hapa Zanzibar, pia ukitizama hapa kuna *Bongo flavor*, kuna *Zenji flavor*, taarab, mziki wa dansi, ukitizama Mhe. Naibu Spika, yote ni ajira kwa vijana

wetu. Tusidharau kazi hizi tukaona hazina maana, lakini pia wakati mwengine ni kivutio kwa wageni wetu na pia kwa ajira kwa vijana wetu wa hapa Zanzibar.

Tukiangalia mfano mzuri sasa hivi kuna Tamasha hili la *ZIFF* Ngome Kongwe linaendelea ndani ya Mji Mkongwe, kwa kweli Tamasha hili linavutia sana Wageni wanatoka nchi mbali mbali kuja kuangalia Tamasha hili, na wanakuja kutizama utamaduni wetu pia wa nyimbo zetu na ngoma zetu za asili ili kuja kuona ufakhari mkubwa ukitizama vijana wetu wanatangaza pia nchi yetu kupitia kazi yao hii ya usanii, lakini Mhe. Waziri ukitizama ukumbi wenyewe wa Ngome Kongwe kwa sasa hivi hali yake mbaya, hauko hali nzuri, na ule ukumbi ni wa kimataifa na wa historia kubwa katika nchi yetu. Kwa hivyo naomba sana ukumbi ule Mhe. Waziri uangaliwe vizuri kwani una tija kubwa katika kuvutia watalii katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala la ulinzi hasa katika Mji Mkongwe. Kwanza ninawapongeza sana hawa wenzetu Polisi Jamii wanatufanyia kazi nzuri kwa kuulinda mji ule Mji Mkongwe na wageni wanapata kutembea kwa amani na utulivu, lakini nimpongeze sana Mwakilishi wa Mji Mkongwe Mhe. Jussa kwa kujitahidi sana, kwa kuona ule Mji Mkongwe uwe safi na uwe katika hali nzuri wakati wote ili tuweze kupata watalii wengi waweze kuja kuangalia Zanzibar na taifa kupata kipato kupitia utalii huo.

Kwa hivyo ninampongeza sana Mhe. Mwakilishi kwa juhudi zake kubwa hata leo hapa kaongelea hapa suala la usafi, bado tuko nyuma katika suala la usafi. Kwa hivyo mimi naomba sana juhudi tuchukue tumsikilize Mwakilishi ili tuweze kufikia lile lengo la utalii, na watalii wakaja wakaridhika kabisa.

Mhe. Naibu Spika, niingie kwenye suala hili la ulinzi. Kama tunavyojua sasa hivi ulinzi ni muhimu lakini nimshukuru sana Mhe. Waziri juzi kutoa semina ya Shirika la Ulinzi kuanzishwa. Hili wazo ni zuri na naomba lisifikie pale, liendelee na mswada ule upite Barazani hapa hawa wenzetu waweze kulinda na kuzidisha ulinzi katika nchi yetu ya Zanzibar.

Pia kuna haja ya *CCTV* mfano mzuri Mhe. Naibu Spika, juzi tu pale Darajani tulikuwepo Barazani hapa likaripuliwa bomu na bahati mtu mmoja kafariki, Mungu amlaze mahala pema na wengine wameumia, lakini tungekuwa na *CCTV* hapa tungejua aliyefanya tukio lile nani au gari gani iliyofanya vile. Kwa hivyo naomba sana suala la *CCTV* tulifanyie mipango kwa serikali yetu na iweze kufunga mitambo hii japo kwa fedha nyingi lakini kidogo kidogo tuanze kwanza kwa Jimbo la Mji Mkongwe ili tuweze kufikia malengo tuliyojipangia.

Mhe. Naibu Spika, niingie kwenye ukurasa 48 katika kifungu 86, kwanza nipongeze sana uongozi wa hoteli ya Bwawani. Kwanza Meneja na watendaji wote kwa kazi yao kubwa na kazi yao ngumu, kwani hoteli hii ni ya kihistoria kwa Zanzibar na tangu wazee wetu walijenga hoteli hii ili tupate wageni, na kwa historia kwa wazee wetu lengo lao kuona maendeleo katika Zanzibar na hoteli ile ni ya mwanzo Zanzibar hoteli kubwa.

Kwa hivyo mimi ninawapongeza sana hawa ndugu zetu kwa kazi yao kubwa. Katika mwaka wa fedha 2013/2014 hoteli ya Bwawani ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kupokea idadi kubwa ya wageni
- Kutoa huduma bora
- Huduma ya maji umeme vimeimarishwa
- Vyumba 32 vimefanyiwa ukarabati
- Hoteli imewalipia ada ya masomo vijana wetu 12. Hii ni kazi kubwa na hongereni sana Meneja wa Bwawani kazi mliyoifanya kuwasomesha vijana wetu.
- Kuuboresha ukumbi wa Salama Hall, ukumbi nao muhimu Mhe. Naibu Spika, kwa kazi yao kubwa hawa vijana wetu wanayofanya.

Lakini kubwa zaidi Mhe. Naibu Spika, mimi niwapongeze sana uongozi ule wa Bwawani kwa kazi yao kubwa, kwa kweli mimi mwenyewe nimeshangaa hapa kuona katika ripoti yao wameweza kukusanya 850,154,351 kwa kweli hii ni ya kupigiwa mfano na lengo la wazee wetu na azma yao imefikia kwa lengo hili. Kwa kweli uwezo upo wa kupata fedha hizi kwa mwaka ni fedha nyingi lakini naamini wana uwezo wa kuongeza pato hili la Taifa kwa mwaka unaokuja kwa juhudi zao kubwa hawa vijana wetu wa Bwawani.

Mhe. Naibu Spika, niingie kwenye ukurasa wa 20 kwa kuokoa muda wako.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia nimekupa robo saa na mwenzio anasubiri robo saa. Dakika 15 umeshamaliza.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa ZBC TV. Kituo hiki ni kituo muhimu sana katika nchi yetu hasa katika kurusha habari, kukidhi mahitaji ya habari ya wananchi, lakini Mheshimiwa kuna changamoto nyingi katika kituo hiki za wafanyakazi, kuvunjika moyo, motisha hawapati, fedha za likizo pia hawapati, hamna mazingira mazuri ya utendaji kazi, vitendea kazi havitoshi, usafiri unakuwa tatizo kwa hawa ndugu zetu kwenda kwenye maeneo husika. Kwa kweli Mheshimiwa hili ni tatizo kubwa, na inafaa Mhe. Waziri tuliangalie kutoka serikalini ili tuweze kuliweka kwenye hadhi nzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie haraka kwa takwimu nilizofanya haraka haraka niipongeze sana ZBC kwa uzalendo wao mkubwa wafanyakazi na kwa kazi yao nzuri. Niseme tu haraka haraka Wazanzibari wengi wanasikiliza ZBC hii Redio pia na TV, lakini nasema kwa sababu ya redio muda hamna asilimia karibu 42 wanasikiliza redio hii ZBC. Kwa kweli hii ni changamoto kubwa lakini wenzetu wanajitahidi juu ya kazi yao; uchakavu wa vitu lakini wanafikisha ujumbe kwa jamii kwa asilimia nzuri kabisa.

Lakini mimi Mhe. Naibu Spika, niwaombe sana wale wafanyakazi ambao wanasomeshwa na fedha za serikali. Kama tukiangalia hapa kuna wafanyakazi 10 wamesomeshwa nchini China lakini wanaporudi hapa baadae wanaondoka kwa ajili ya maslahi madogo wanayopata pale ZBC, lakini mimi ninawaomba sana wajitolee kwa ajili ya nchi yao wasiondoke, kwa sababu wanasoma kwa hizi fedha za wananchi na za walipa kodi. Kwa hivyo wamefika hapa watumikie, watuoneshe uzalendo wao kwa kujitahidi kabisa na kuonesha kama wamesoma kwa pesa za wananchi na walipa kodi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa suala moja la mwisho; ninamuomba Mhe. Waziri katika sherehe zetu za Muungano kwa nini hawa waandishi wetu wa ZBC hawafiki kule Tanzania Bara. Naomba suala hilo utakuja kunijibu utakapokuja, lakini nikupongeze kwa dhati kabisa kwa hotuba yako hii ya bajeti, mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kupata dakika hizi chache na moja kwa moja nianze kwa hoteli ya Bwawani. Hoteli ya Bwawani Mheshimiwa ni hoteli ya serikali, ni hoteli yenye historia ya Mapinduzi, ni hoteli ya aina yake iliyojengwa kwa makusudi na muasisi wa Mapinduzi haya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kwa lengo maalum iwe ni chombo cha serikali kinachotoa huduma inayofaa. Na kwa namna ilivyojengwa pamoja na mambo yaliyomo mpaka leo ni hoteli ambayo bado inaendelea na hadhi yake.

Nashukuru sana kwa mipango iliyomo ya kuimarisha hoteli ile, hoteli ambayo mwanzo wake ilikuwa na wafanyakazi wengi ambao walikuwa wakipata malipo ya kutwa, na marekebisho yakafanywa sasa hivi ni wafanyakazi wengi wa kudumu. Ile ni historia yetu lakini Mheshimiwa kwa masikitiko makubwa kutokana na wakati, kwa taarifa nilizonazo ni kwamba pamoja na mambo yote yaliyoekewa haya mpaka kuingiza wageni wengi kufanyiwa matengenezo vyumba vyake vipeperushi na kadhalika, ile hoteli ninasikia inataka kuuzwa. Na mwenye kutaka kuinunua ni kwa kuivunja kabisa kabisa na kujenga hiyo anayoiona inafaa katika mazingira hayo anayoyajua mwenyewe.

Mimi Mhe. Naibu Spika, sitokuwa radhi wala sidhanii kwamba nitapitisha bajeti hii kama sijapata sababu za msingi kwa nini Serikali hii ya Mapinduzi Zanzibar inasahau vyanzo vilivyowekwa; ambavyo ni Mapinduzi ya Zanzibar ikawa sisi tunafanya kazi kubwa ya kuuza tu. Sasa kila kitu kinauzwa mpaka hoteli kama hii inauzwa iangalie ilivyo, kwa hivyo mimi kama sijapata jibu sahihi kwa nini iuzwe, na nikaridhika bajeti hii haipiti. Hilo ni moja.

La pili kwa sababu ya wakati niende katika Shirika la Utangazaji. Taarifa ni kitu muhimu sana na alikuwepo mwanasayansi mmoja akiitwa Lamack alisema naomba kunukuu kwa Kiingereza. *"A change in condition create new needs"* Yaani panapotokea mabadiliko kunakuwa na mahitaji mapya. Usoni siendelei, tujue tumekwenda na wakati sasa tumetokewa na mabadiliko ya kisiasa tumo katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Sasa Mheshimiwa na Katiba tunayotumia ni hii Katiba ya Zanzibar kabla sijaleta hoja yangu naomba nisome vifungu vya kuunganisha hoja yangu na kwa ruhusa yako ni kama ifuatavyo:-

Tukiangalia kifungu nambari 11(1) cha Katiba kinasema kuwa:-

"Binaadamu wote ni sawa, binaadamu huzaliwa huru na wote ni sawa"

Kifungu cha 11(2) kinasema:-

“Kila mtu anastahiki heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake”

Kifungu cha 12(1) kinasema hivi:-

“Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ubaguzi wowote kulinda na kupata haki sawa mbele ya sheria”.

Tukiongezea kifungu cha 12(2) kinasema:-

“sheria itakayokuwa na kifungu chochote ambacho ni cha ubaguzi wa moja kwa moja au kwa taathira yake”.

Kifungu cha (4) kidogo kinasema:-

“Hakuna mtu atakayebaguliwa na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya sheria yoyote, au katika utekelezaji wa kazi Afisi yoyote ya serikali au uongozi mwengine wa chombo chochote na vyombo vyake’.

Na kifungu cha mwisho kinasema neno kubagua maana yake:-

“Ni kutimiza haja kwa watu mbali mbali kwa kutegemea utaifa wao, kabila, jinsia, ulemavu, mahala wanapotokea, muelekeo wao kisiasa, rangi au dini; ambapo watu wa aina fulani wanaonekana kuwa ni dhaifu na duni na wawekewe vikwazo na pingamizi ambavyo wale watu wa aina nyengine hawawekeani na wanapewa fursa au faida ambayo hawapewi watu wa aina nyengine”.

Mhe. Naibu Spika, ninasema hivi kwa sababu gani, chombo hiki kwa mujibu wa taarifa tulizozipata na Mhe. Salma Mohammed Ali jana kinafanya ubaguzi wa dhahiri wa kisiasa. Na inasikitisha ikiwa chombo ni chetu sote na Katiba inaeleza hivyo ni kwa nini Mkurugenzi wakati ana akili zake timamu ni msomi, kawekwa kwa kuaminiwa kwa maslahi ya wananchi wote akaruhusu kuleta wanasiasa waliopitwa na wakati wakaweza kuwakashifu viongozi wakuu wa kisiasa, kutoka Chama ambacho si Chama cha Mapinduzi, hili ni kosa kubwa sana kweli kweli.

Kwa hivyo kama kuna haja ya kufanya hivyo, kila chama chenye uwezo wa kuweka vyombo vya habari viweke si chombo cha CCM, watu wafanye wanavyotaka lakini kwa Mkurugenzi kutumia chombo hiki kisiasa hivi ni kutudhalilisha na ninamuomba Mhe. Waziri, kwa sababu suala hili lilitokea kwa muda mrefu analijua, na linasitishwa eti kwa sababu tunapitia bajeti aeleze kwa nini akakiruhusu kikatokea kitendo hicho kwa muda mrefu bila ya kufanya vyovyote. Vyenginevyo itakuwa ni vigumu kupitisha Wizara hii, kwa sababu sasa tunakwenda na vifungu vya ubaguzi wa dhahiri ambalo ni jambo linalopingwa kweli kweli.

Jengine Mhe. kwa sababu ya wakati umekwisha kuna vikundi vyetu vya utamaduni au vya sanaa vilikuwa vikifanya vizuri vinaburudisha, vinaelimisha, lakini kwa sababu ya umaskini na kutoangaliwa hivi sasa vimenyamaza kimya. Mfano ni kikundi cha Wazera kilioko Kiungoni, tunacho kikundi cha Mwangaza Tumbe, tulikuwa naye profesa Gogo Kangagani. Vikundi kama hivi vimeachwa kabisa.

Kwa hivyo kwa sababu Wizara inaeleza kuwa itakuza utamaduni wetu, kwa hivyo ni sababu zipi zilizowekwa mpaka leo ikawa Mheshimiwa hajaona vyovyote muhimu wa kuvisaidia vikundi ili vikafanya kazi ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kwa sababu ya wakati wafanyakazi wetu wa Wizara ya Habari hii wanafanya kazi katika mazingira magumu, na katika utafiti tumeona hawapewi posho zinazostahiki kutokana na likizo, muda wa kazi hata kazi wanayoifanya humu pamoja na mambo mengine.

Kwa hivyo kwa sababu wakati umemaliza, ninamuomba Mhe. Waziri atupe kauli ni vipi atawashughulikia watu hawa ili wasiweze kufanya kazi katika mazingira haya magumu yaliyokuwa hayastahamiliki na badala yake wafanyakazi sawa sawa na watu wengine. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamaliza pana tangazo moja hapa limeletwa na Mnadhimu wa CUF. Mnatangaziwa kwamba tukimaliza kikao hiki wanachama wa CUF kutakuwa na mkutano kwenye ukumbi wa juu. Mkutano ni muhimu sana mnasisitizwa mfike nyote kwa pamoja.

Baada ya hayo ninaakhirisha kikao hiki mpaka saa kumi na moja za jioni ya leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa na Waheshimiwa watatu waliobaki kuchangia lakini yupo mmoja, nampa aliyekuwepo baadae tumwite Mhe. Naibu Waziri na baadae Mhe. Waziri.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiye aliyetuwezesha kwa jumla sote kufika humu katika hali ya uzima.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote jinsi walivyowasilisha hasa Mhe. Waziri alivyowasilisha kitabu hiki kwa *speed* na kwa aina yake.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Utalii kwa Wote. Mhe. Naibu Spika, Rais aliita taasisi mbali mbali kutoka Unguja na Pemba na akaelezea habari ya utalii kwa wote. Hii natoa pongezi kwa sababu kila mwananchi utalii huu umemgusa kwa namna moja au nyengine.

Pia Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba nimuombe sana Mhe. Waziri nimeona kitabu chake hiki Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Muhtasari wa Programu ya Pamoja ya Kuimarisha na Kuendeleza Sekta ya Utalii 2014/2015 – 2017/2018.

Sasa najua kitabu hiki hayumo peke yake, kitabu hiki kimeorodhesha mawizara mengi ambayo kila mmoja atahusika kwa upande wake, lakini ninaloliomba, naiomba sana wizara husika na zile wizara ambazo zitapewa majukumu lakini fedha hizi zinaingia Wizara ya Habari basi kwa kweli watoe mashirikiano ya hali ya juu ili utalii wetu uweze kuwa wa kisayansi na teknolojia.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa niingie katika mambo ya michezo. Mhe. Naibu Spika, mimi kila bajeti nikisimama nasimama hapa nazungumza kuhusu habari ya michezo na hasa upande wa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mimi nasikitishwa sana na ZFA ya Pemba, niseme ukweli. Kwa sababu watu wanajitahidi wao wenyewe kutafuta timu wakajitolea, wakafanya mambo yao, wakahangaika hawana msaada wa aina yoyote ili kuhakikisha kwamba suala la michezo lisipotee hasa mpira wa miguu, lakini huu ni mwaka wa tatu Mhe. Naibu Spika, kila nikisimama nasema hapa lakini leo nitamuomba Mhe. Waziri anipe tamko kuhusu timu ya *Hard Rock* na timu ya Mwenge ilikuwaje?
Kwa sababu hapa nina *documents* zote tena kutoka ZFA sisemi feki nina *documents* zote hizi. Ni kwamba Mwenge walipewa ushindi lakini baadae ushindi ule wamenyang'anywa, sasa nataka Mhe. Waziri aje anieleze tukae tukubaliane, hili ni suala ambalo linarejesha nyuma michezo Mhe. Naibu Spika, na sisi kule Pemba hatuna baba wala hatuna mama tujipigepige sisi wenyewe tuchangishane, tuchangishwe na akina sisi ndio timu za Pemba ziweze kufanya vizuri.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri hapa nitakuwa mgumu pamoja na kwamba hii ni wizara yangu, hapa nitakuwa mgumu mpaka anipe sababu kwa nini timu ya Mwenge imenyang'anywa ushindi wakati barua ya ZFA ipo hii hapa.

Mimi nitakupa wewe Mhe. Naibu Spika, apelekewe Mhe. Waziri asome hizi *documents,* ushindi ameshapewa Mwenge halafu *Hard Rock* wamekata tena rufaa kwa jambo jengine Mwenge amenyang'anywa ushindi wake. Kwa hivyo, hili namuomba sana Mhe. Waziri. Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, niseme mbio mbio kwa sababu ya wakati.

Mhe. Naibu Spika, kwanza wale wanawake wenzangu mimi ni mwanamke Mhe. Naibu Spika, najua umuhimu wa mwanamke ni kitu gani, hivyo nawaomba sana tusiyakuze mambo yakawa makubwa ili kuonekana kwamba siku hiyo ya hao waliovuliwa mabuibui yakawa makubwa sana.

Kwanza mimi Mhe. Naibu Spika, sikubaliani kwa sababu ofisi zina taratibu zake hapa tunaleana tu, lakini ofisi zina taratibu zake na hatuwezi kumuacha mtu akapita na buibui moja kwa moja, huu ni utandawazi, mambo yamebadilika Mheshimiwa lazima tukubali, wewe umeshamruhusu mtu Marehemu Karume kauliwa hivi hivi kwa masihara tu kwa kuaminiana.

Wewe unampisha mtu anavaa buibui hujui amebeba nini, mimi hili kwa kweli isipokuwa kama kuna sehemu maalum mtu anaingia anavua buibui lake halafu anakwenda ofisini kwake, lakini kwa kusema kwamba wanawake wamedhalilisha, ameroa chapachapa, tusikuze mambo Mheshimiwa, lazima tukubali kwamba mimi hizo enzi tokea mimi sijazaliwa watu wanafanya kazi na hayo mabuibui ya asili ya kamba mtu hajaendapo na buibui ofisini, hivyo tunaleleana tu, lazima tufuate taratibu na sheria za kazi Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo, wasinifikirie vibaya wanawake wenzangu, nayasema haya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunafuata taratibu za kazi.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niseme kwamba niungane mkono na wale wenzangu waliosema kuhusu habari ya Hoteli ya Bwawani. Mimi bado Mhe. Naibu Spika, Hoteli ya Bwawani mimi sikubaliani kwamba iuzwe, labda ikodishwe lakini ile ni *asset* ambayo ni *asset* kubwa kwa Zanzibar, *assets* nyingi tumeshaziharibu haribu. Kwa hivyo, ile ni *asset* kubwa, naomba sana kama hoteli ile itakodishwa atapewa mtu ubia mimi sina matatizo, lakini kwa kweli Hoteli ya Bwawani isiuzwe!

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nitamuomba Mhe. Waziri ni mara ngapi vyombo vyake vyote amefanya *scheme of service* kwa sababu wafanyakazi na wao wananung'unika. Kwa hivyo, na hasa hizi sheria mpya mpya tulizozipitsha, hivyo nataka aje anieleze hapa na hasa hii Kamisheni ya Utalii.

Nikitoka hapo Mheshimiwa naomba sana mambo ya riadha ni mazuri kwa sababu yanatoa taaluma, kwa hivyo na hili namuomba ili liweze kuingia katika haya.

La mwisho Mheshimiwa leo mimi sasa hivi natoka huko kwenye mambo ya habari habari hayo maana yake nimetoka hapa saa saba, saa saba na nusu mimi niko *Fisherman's Resort* kulikuwa na mambo ya uandishi wa habari.

Namuomba sana Mhe. Waziri chonde chonde na Idara ya Nyaraka na Makumbusho, kwa kweli itapotea, namuomba sana Mhe. Waziri Idara ya Makumbusho kwa kweli tuihifadhi na tukaangalie kama kuna mambo ya kuweza kuyafanya basi tuyafanye, si hivyo itatupotea *history* kubwa sana kwa kweli, ni *history* kubwa sana kwa Zanzibar tuliyonayo.

Baada ya kusema hayo Mhe. Waziri uje unijibu vizuri suala langu la Mwenge na *Hard Rock*, si hivyo nakupa asilimia 80 tu asilimia 20 naziacha mpaka nije nipate jawabu nzito. Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 80 asilimia 20 nazitenga.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kupata nafasi jioni hii kuweza kuzungumzia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Hii ni wizara ya mkwe wangu siku zote nasema ni lazima niipongeze kwa nguvu zote.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nakwenda kwenye michezo. Mhe. Naibu Spika, nchi nyingi duniani kumekuwa na utaratibu wa kuanzisha vyuo vingi vya michezo, lengo kuu la vyuo hivyo ni kukuza michezo na kuwakilisha nchi zao kwa ngazi mbali mbali za kitaifa au za kimataifa, lakini cha kusikitisha Mhe. Naibu Spika, sijasikia hata siku moja serikali yetu kuanzisha au kuzungumzia kitu hiki.
Je, Mhe. Waziri hatuoni sisi ipo haja ya kuanzisha kitu kama hicho ili na sisi kupata vijana wenye sifa na kutuwakilisha kwenye ngazi za Kitaifa na Kimataifa, hata kama ikitokezea suala la kujiunga na FIFA basi na sisi vijana tukawa wazuri na wenye hadhi ya FIFA ili waweze kutuletea sifa katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika sekta ya utalii. Sekta hii ni moja kati ya nyenzo za uchumi lakini kwa kiasi kikubwa sekta hii imetawaliwa sana na wafanyakazi wageni. Sijui tuseme watu wetu kwamba hawana elimu ya kutosha au sijui vipi, basi kwa hilo nimuombe Mhe. Waziri anieleze kwamba watu hawa ni kuwa hawana elimu au sijui kwa nini huingiliwa na wageni wengi.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, katika sekta hiyo hiyo niseme kwamba kisiwa chetu cha Unguja na Pemba hupata watalii wengi wenye daraja la chini, na watalii hao hasa kipato chao ukiangalia Mhe. Naibu Spika huwa ni

kidogo sana.Kwa hiyo, pamoja na udogo wake nimuulize Mhe. Waziri watalii hawa kwa mwaka tunapata kiasi gani kwa watalii wetu hao.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni niseme kwamba kumetokea tukio la kusikitisha sana hapa Zanzibar ambalo limetutia wasi wasi sisi sote Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, huu uchomaji wa magari moto ni tatizo kubwa sana au urushaji wa mabomu yasiyojulikana ni tatizo kubwa sana, na sisi hapa katika nchi yetu Mhe. Naibu Spika tunatembelewa sana na watalii. Je, nimuulize Mhe. Waziri wizara yake imejipanga vipi na suala hili kama likitokezea tena.

Vile vile huoni kutokea kwa matukio haya ni kukosa kuingia kwa watalii nchini na kukosa serikali yetu mapato.

Mhe. Naibu Spika, nije katika sekta ya utamaduni. Sekta hii kwanza ni sekta nzito sana, kwani tukiangalia mila, silka na utamaduni wetu wa Kizanzibari hivi sasa Mhe. Naibu Spika umekuwa ni tatizo, kwani kuna ongezeko kubwa la kuporomoka mila na silka zetu za Kizanzibari kuingiwa na tamaduni za kigeni ambazo hivi sasa tunaziiga.

Pili, mambo ya utandawazi ambayo kwa wakati huu imekuwa hatuwezi kuyaepuka, mitandao imekuwa mingi na wigo umezidi lakini serikali imeweka mkakati gani kuweza kudhibiti suala kama hili. Kwa sababu hapo zamani Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na masuala kama haya ya wigo, lakini viongozi wetu waliweza kuyadhibiti. Sasa kwa hiyo naomba serikali pamoja na viongozi waweze kuyadhibiti masuala kama haya ili tusiendelee kuharibikiwa na utamaduni wetu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika ZBC. Ni chombo cha mwanzo katika ukanda huu wa Afrika, lakini hapo zamani kilikuwa kikiitwa TVZ, lakini cha kusikitisha chombo hiki kimeshindwa kuwavutia watazamaji wake kutokana na mipangilio ya vipindi vyake ambavyo wananchi wengi huwa hawavitazami au hawaangalii.

Kwa hiyo, naiomba serikali au wizara itoe elimu kwa watendaji wake ili waendane na wakati, laa kama si hivyo mashirika mengi Mhe. Naibu Spika yatajitokeza hapa Zanzibar yaweze kufunguliwa, na *ZBC* yetu iweze kukaa pale pale na kupendwa na wananchi.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho niseme na mimi watu wengi wamewatetea hawa watu wa Wizara ya Habari, watu hawa Mhe. Naibu Spika na mimi niseme kwamba ni watu wanaofanya kazi kubwa sana na wana kazi nzito.

Mhe. Naibu Spika kutwa nzima kukaa wakasimama watu kama hawa mimi siwezi Mhe. Naibu Spika, lakini ukiwaangalia wao hawakai kitako kutwa nzima wanatuangalia sisi na kuandika habari zetu sisi.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, na mimi nasema kama walivyosema wenzangu Mhe. Waziri awaangalie watu hawa kwa jicho la huruma sana, ili na wao waweze kuendelea na kazi zao. Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nakushukuru, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia leo hii tukawa tuko kwenye Baraza hili Tukufu tukiwa tuko salama na wazima.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mashirikiano anayonipa ya wizara hii kwenye majukumu yetu ya kila siku. Pia nimpongeze Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kunipa mashirikiano ya pamoja tunapofanya kazi zetu za kila siku.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kujibu kwa upande wa Shirika la *ZBC*, nianze kujibu kwa Waheshimiwa saba waliozungumzia kuhusu kadhia iliyotokea *ZBC TV* ambalo ni shirika.

Mhe. Naibu Spika, nataka niwataje Waheshimiwa waliochangia kuhusu kadhia hiyo.

Mhe. Salma Mohammed Ali, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Viwe Khamis Abdalla, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Mhe Hamza Hassan Juma na Mhe. Ashura Sharif Ali.

Mhe. Naibu Spika, nataka wanisikilize wanawake wenzangu akiwemo na mwanamme mmoja, wanisikilize kwa kina ili nipate niwaeleze tatizo lililotokea *ZBC* ikiwa ni Shirika. Waheshimiwa wameeleza kuwa niwajibu majibu ya kina. Nataka niwaambie kwamba ikiwa ni Naibu Waziri mwanamke ambaye naongoza Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo niwahakikishie wanawake wenzangu suala hili nimelifuatilia kwa kina, na nimepewa majibu mazuri na nyinyi nitawapa majibu mazuri.

Waheshimiwa Wawakilishi nataka niwaambie kwenye wizara zote sisi wanawake ni upendeleo tu wa kuvaa mabaibui mpaka tukaingia kwenye ofisi zetu, lakini tunatakiwa tukifika tuvue mabaibui yetu tuyaweke sehemu tuendelee na shughuli zetu za kazi. Kama ni kadhia hizo zilizotokea nakanusha kwenye Baraza hili la Wawakilishi halikutokea suala hilo. Kwa sababu mimi mwenyewe binafsi nilipozipata fununu hizi nikasema akili za kuchangiwa uchanganye na zako, mimi nilitoka nikaenda *ZBC* saa moja kamili nishafika, na nikaenda nikakaa maeneo ambayo wafanyakazi, walinzi na askari wasinione. Pale alipita mwanamke wa mwanzo na baibui lake, akapita mwanamke wa pili na baibui lake, akapita wa tatu ikawa mlinzi keshakuja pale nikajitokeza, lakini yule kijana mwanamke hakuwahi kuvua baibui. Nasema hivyo kwa sababu mimi nilikwenda na yule kijana aliingia ndani, akavua baibui, sio kama mnavyosema nyinyi Waheshimiwa kuwa wanapambazuliwa mabaibui nje.

Siku ya pili siku ya Jumanne nikaenda Redio nako kulitokea tatizo kama hilo wanavyosema Waheshimiwa na watu wengine. Nilikwenda nikahakikisha kama muda niliokwenda *ZBC* Televisheni, nikakaa sehemu ambayo sionekani na wakapita wafanyakazi na mabaibui yao wakaenda ndani wakavua ndio baadae wakaenda kwenye vituo vyao vya kazi, lakini nataka niwaambie Waheshimiwa wajue kwamba kituo chetu kile cha Televisheni ni kituo muhimu sana, sasa nawaomba wafanyakazi wetu wa Wizara ya Habari wanapowaambia mambo Waheshimiwa wasikilize vizuri, na wafuatilie watufuate sisi viongozi ili tuwape majibu ya kina na waweze kufuatilia wao wenyewe.

Waheshimiwa Wawakilishi nataka waniamini nikiwa ni mwanamke mwenzao, najua hali ya wanawake walivyo, wanawake wana mila na desturi zao za Kizanzibari na desturi nyengine ambazo tunazo, kwa kweli wamesema mambo mengi wanawake wenzangu, lakini nataka niwahakikishie nikiwa Naibu Waziri suala hili nimelifuatilia kwa kina na nimelipatia ufumbuzi. Nataka watoke hata kesho asubuhi, Waheshimiwa waende wakahakikishe, kwa sababu nimechukua hatua za kutosha, na wale wafanyakazi wamewekewa sehemu yao kwenye chumba kubadilisha mabaibui yao waweke, wakitoka kwenye shughuli zao za kazi wavae mabaibui yao, sio hivyo walivyosema kuwa wanadhalilishwa hilo si kweli Waheshimiwa wenzangu. Nawaomba sana bajeti yetu muipitishe na wala msiwe na ukakasi wowote, chonde chonde!

Mhe. Naibu Spika, niende kwa upande wa Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali. Kwa kweli jana Mheshimiwa alichangia vya kutosha ridhaa nafsi yake, akaonesha na picha, lakini nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza hili ile picha aliyokuja nayo ni ya mwaka 2013, kombe lililoanza mwaka 2013 la miaka 49. Sababu ya kuwaambia hivyo nina ushahidi tosha, Mhe. Waziri Ikulu alikuwa hayuko, nilikwenda mimi na watendaji wangu akiwemo na Mhe. Mohammedraza Hassanali na wale wafadhili wengine waliokuwa wakichangia Kombe la *Mapinduzi Cup*.

Tulikaa na Mhe. Rais nikamkaribisha, tukazungumza wakapewa vyeti vyao, Mhe. Mohammedraza Hassanali akasema yeye mwenyewe kwamba, Mhe. Rais mimi nitajenga uwanja nitie nyasi bandia, lakini Mhe. Mohammedraza Hassanali aliingia mitaani, lilipofika Kombe la *Mapinduzi Cup* la mwaka 2014 hatukumuona tena. Sasa nataka niwaambie Waheshimiwa tunaposema vitu tuseme kwa uhakika, Mhe. Nassor Salim Ali japo unaniangalia, na wewe ulikuweko kwenye hafla hiyo, nataka Waheshimiwa wawe na umakini wa kufuatilia mambo.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye maeneo ambayo amechangia Mhe. Panya Ali Abdalla, yeye amezungumzia kuhusu mila na desturi ya Kizanzibari na Mhe Ashura Sharif Ali.

Mhe. Panya Ali Abdalla amezungumzia kuhusu viwanja vya wilaya vya michezo vitiwe *bulldozer*. Nataka nimwambie Mwenyekiti wangu wa Baraza la Michezo, Bi Sheri amefanya ziara Unguja na Pemba, ametembelea maeneo yaliyokuwa na viwanja vile vitakavyojengwa vya wilaya vikiwa vimo kwenye maeneo ya skuli, wamekaa na Maafisa wa Wilaya wa Elimu na ma-*DC* ili kuona kwamba vile viwanja tunaviongeza ili vijana wetu waweze kutengezewa mazingira mazuri na waweze kufaidika na matunda ya serikali yao ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea pia niende kwa Mhe. Salum Abdalla Hamad amezungumzia kuhusu kikundi cha Taarab cha Tumbe na kikundi cha Chake Chake. Mheshimiwa kikundi cha Tumbe kila siku tunasimama hapa tunasema kwamba kikundi hiki kiliingiliwa na mambo ya dini na kikundi hicho kiko kwenye wilaya yangu ya Micheweni. Kwa kweli kama wewe Mhe. Mwakilishi tukishirikiana na Mwakilishi wa viti maalum Mhe. Bikame Yussuf Hamad, kama tutakwenda kukaa nao wanakikundi wale tuweze kuwaelimisha ili kikundi kile kifufuke hakuna tatizo, tutakwenda ili tukae nao tuwape mawaidha hayo hayo ya dini mpaka wakubali ili kikundi kile kiendelee.

Kikundi cha Wazera pia Mhe Mwakilishi amekizungumzia. Ni kweli kikundi chetu kile ni kizuri na kinatoa faraja kubwa sana. Namuomba Mhe. Mjumbe tukimaliza bajeti twende tukakitembelee pamoja na yeye, najua jimbo lake ni la Mtambwe lakini naona anamtetea Mheshimiwa wa Jimbo la Chake Chake. Si vibaya pia na yeye tukawa pamoja tukaenda kuwatembelea na kuweza kuzungumza nao tukajua tatizo lao ni nini.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa sababu mchango wangu huu ni mdogo, na nishatoa ufafanuzi basi pamoja na wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kupata nafasi hii ya kujumuisha kuhusiana na michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi inayohusiana na Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa michango yao, kwa kweli niwashukuru kwa sababu michango ambayo wamenipa na namna ambavyo wameijadili hotuba yangu ni michango ya kujenga sana, wameielekeza sana wizara, wameishauri; na ninachowahakikishia ni kwamba ushauri wao na maelekezo yao tutayatumia mimi na wenzangu katika wizara kuhakikisha kwamba ni chachu ya kupata mafanikio zaidi katika shughuli zetu za kila siku.

Mhe. Naibu Spika, wizara imepata wachangiaji 29, nianze kwa ruhusa yako kuwatambua kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Asaa Othman Hamad
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali
4. Mhe. Nassor Salim Ali
5. Mhe. Salma Mohammed Ali
6. Mhe. Ali Salum Haji
7. Mhe. Saleh Nassor Juma
8. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
9. Mhe. Mohammed Haji Khalid
10. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
11. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
12. Mhe. Rufai Said Rufai
13. Mhe. Panya Ali Abdalla
14. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
15. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
16. Mhe. Hamza Hassan Juma
17. Mhe. Marina Joel Thomas
18. Mhe. Ashura Sharif Ali
19. Mhe. Hassan Hamad Omar
20. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
21. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo
22. Mhe. Salim Abdalla Hamad
23. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
24. Mhe. Omar Ali Shehe
25. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
26. Mhe. Asha Bakari Makame
27. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
28. Mhe. Fatma Mbarouk Said
29. Mhe. Hija Hassan Hija wa mwisho wakati naondoka kwenye kiti hata mchango wake sijautizama; na
30. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu imenisaidia sana na imenishauri vizuri, ninachoahidi kwamba ushauri wao na maelekezo yao yote tumeyachukua tutayafanyia kazi vizuri sana, naamini kwamba itakuwa ni moja katika dira za kufuata katika bajeti inayokuja.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nianze na michango ya jumla nianze na Shirika la Magazeti ambapo Mhe. Asaa Othman Hamad, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe Ashura Sharif Ali, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo hawa walipata nafasi ya kuchangia Shirika la Magazeti. Kwanza nawashukuru sana kama nilivyosema kwa ushauri wao na wengi walizungumzia suala la kushindwa kununua mtambo wa gazeti.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba mipango yetu ya kununua mtambo wa kuchapishia gazeti bado haijazaa matunda. Azma hii tunayo kwa muda mrefu, tumejaribu kutafuta fedha serikalini bado kidogo na tumejaribu kuomba kwa Washirika wa Maendeleo.

Mimi mwenyewe nimemuomba Balozi mdogo wa China, kimsingi amekubali kutusaidia lakini bado si *priority* kwa hivi sasa katika misaada ambayo wanatupa. Kwa hivyo, bado tunaendelea kuzungumza na serikali kuangalia kuiweka *priority* kwa mtambo wa gazeti katika bajeti ya mwakani. Tumekubaliana na Tume ya Mipango basi tukijaaliwa serikali itanunua mtambo wake wenyewe.

Wazo la kuwa kwa vile tuna Idara ya Uchapaji tayari kwamba tushirikiane na Idara ya Uchapaji tuchapishe gazeti pale. Tumelichukua lakini ni kwamba mitambo ya uchapaji wa vitabu hivi na magazeti ni mambo mawili tofauti. Kwa hivyo, ili tufanye hivyo itabidi tuweke uwekezaji mwengine, hilo ndilo jambo ambalo tunalizungumza baina ya Tume ya Mipango, sisi na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tuangalie namna gani suala hili litaweza kuchukuliwa, lakini kimsingi ni kweli kwamba imefika wakati sasa kwa nchi yetu kumiliki mtambo wa gazeti kwa ajili ya kuchapisha magazeti yake.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo limezungumzwa ni usiri au kutokuwepo na uwazi katika uajiri, hili amezungumza Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Tunajitahidi kwamba shughuli za ajira ambazo siku hizi zimepelekwa serikalini zaidi hasa Utumishi ndiko mambo ya ajira yanakoanzia na Tume ya Utumishi kuhakikisha kwamba shughuli za uajiri zinakuwa wazi, zinatangazwa na yeyote ambaye anataka kupata kazi apeleke ombi lake.

Sasa ninachomwambia Mhe. Jaku Hashim Ayoub ni kwamba kwa hivi karibuni uajiri wowote ambao umefanywa basi umezingatia taratibu hizi ambazo Idara ya Utumishi Serikalini umeelekeza.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo tunakushukuru kwa mchango wako, umezungumzia suala la Zanzibar Leo kwamba linachapishwa wapi. Hivi sasa linachapishwa katika Kampuni ya *Tanzania Standard Newspaper*, Dar es Salaam kwa kiasi cha shilingi 30 milioni kwa mwezi. Kunakochapishwa Gazeti la Ikulu ni Kampuni ya *Digital Printing* ya Dar es Salaam kwa gharama ambazo wanazijua wenyewe watu ambao wanamiliki. Mimi kama mwenye Idara ya Habari Maelezo jukumu langu ni kujua wapi gazeti linachapishwa kwa gharama gani ni juu ya mchapishaji au mmiliki wa gazeti.

Kuhusiana na mapato ya shilingi milioni 504 ambazo gazeti limepata, katika fedha hizo ambazo zimetumika kulichapisha gazeti ni shilingi 301 milioni na ambazo zimetumika kwa kusambazia gazeti ni shilingi milioni nane (8).

Mhe. Naibu Spika, katika Kamisheni ya Utalii waliochangia ni Mhe. Asaa Othman Hamad, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali, Mhe. Viwe Khamis Abdalla, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Husein Ibrahim Makungu, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe Mahmoud Thabit Kombo, Mhe. Suleiman Hemed Khamis, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Asha Bakari Makame.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wote waliochangia katika Kamisheni wametupa ushauri mzuri ambao utaelekeza serikali yetu kuwa na umakini mkubwa zaidi katika kuhakikisha kwamba sekta hii ambayo ndio mapato yetu yote ya Serikali tunayategemea basi iende vizuri zaidi. Kwa hivyo, tunawahakikishia kwamba ushauri wao tunauchukua.

Mhe. Asaa Othman Hamad kwa niaba ya Kamati ushauri wako tunauchukua. Na kuhusu kuisimamia Kamisheni ili ikutanishe Bodi ya Makamishna tumeanza hiyo kazi na matokeo yake yameonekana wameanza kukutana vizuri.

Na kuhusu takwimu za utalii za mwaka huu ni kwamba watalii walioingia ni 181,301. Na katika jibu hili basi namjibu Mhe. Fatma Mbarouk Said wa Jimbo la Amani, ndio ambao wametaka takwimu za utalii.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk suala la kwamba utalii haumnufaishi Mzanzibari nadhani sio sahihi sana, wananchi wengi wa Zanzibar wananufaika na sekta ya utalii kwa njia moja au nyengine. Na utalii wenyewe ni kwamba wakati wa ile *season* basi wananchi wengi wa Zanzibar huwa wanahangaika hangaika, lakini *high season* kwa kweli wanachangamkia hali na mzunguko wa fedha huwa mkubwa.

Wanaopewa vibali vya kutembeza wageni Kamisheni ya Utalii inahakikisha kwamba ni Wazanzibari. Sasa sisi kipimo cha kumjua Mzanzibari ni mtu mwenye *ZAN ID*, akituletea *ZAN ID* ni Mzanzibari. Sasa kama kuna watu wengine wanakipata hichi kinyemela itabidi Mhe. Makame Mshimba Mbarouk mimi na wewe tushirikiane. Masheha wetu waliopo huko mitaani kwetu majimboni wahakikishe kwamba hawawapi *ZAN ID* kwa watu wasiohusika, vyenginevyo tukiachia hivyo kazi watazichukua halafu tutakuja kulalamika katika Baraza.

Kwa hivyo, hili ni suala letu sote tuhakikishe kwamba anayekuja sifa moja lazima awe Mzanzibari. Na hatumuulizi vyenginevyo, isipokuwa tunamwambia lete *ZAN ID*, akitupa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi huyo ndie Mzanzibari tunayemtambua kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo, kama kuna utaratibu mwengine wanakwenda kinyemela nadhani tushirikiane kuhakikisha kwamba wasio Wazanzibari hawapati vitambulisho, kwa sababu wakipata itakuwa ni mtihani kwa maslahi ya Wazanzibari na shughuli zao za kazi.

Kuhusu kufanya ziara ya kutembelea mahoteli. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk nipo tayari wakati wowote, kama itabidi Kiwengwa vizuri tutakwenda. Na kama kuna masuala ya ajira tutashirikiana na Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma kulizungumza hilo, ama twende na watu wake wa *Labour* pengine, ili kuhakikisha kwamba suala hili limetatuliwa. Kwa sababu ni kweli kwamba hatuwezi kujaza mahoteli mengi hapa nchini halafu vijana wetu wakawa wanarandaranda kutafuta kazi, wasio Wazanzibari wanapata kazi. Kwa hivyo, hili ni suala la kulifuatilia Mheshimiwa na nipo tayari wakati wowote.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali kuhusu gari za punda ambazo zinawachukulia watalii. Jambo zuri, lakini ni vyema kwamba ulete mchanganuo wa mradi wako ama *ZIPA* au Kamisheni ya Utalii. Wakikubali hauna matatizo watachukuliwa. Kwa hivyo, la msingi lete mchanganuo wa mradi tu ndio utaratibu.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla pamoja na Waheshimiwa wengi walizungumzia suala la ulinzi katika Sekta ya Utalii. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba jambo muhimu katika Sekta ya Utalii ni suala la usalama. Na pahala ambapo hapana usalama basi wageni hawaendi hawafiki. Kwa hivyo, Serikali imeliona hilo, nafurahi juzi tumepata semina kuhusiana na azma ya Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Mhe. Haji Omar Kheri, kuona kwamba JKU sasa inaelekea huko, lakini kwa ufafanuzi zaidi ni kwamba Serikali suala hili imelizingatia kwa mapana, na katika maabara ya utalii ambayo imeundwa basi suala hili limepewa mkazo mkubwa.

Suala la kuweka *CCTV* limezungumzwa na Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na Mhe. Suleiman Hemed Khamis. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba hili suala ni muhimu sana na Serikali inaliangalia kwa mazingatio mapana. Katika kufanya hivyo kampuni mbili zimealikwa kufanya utafiti wa awali. Na tayari zimeshafanya utafiti chini ya uongozi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imetoa kibali, na tayari ripoti ipo Serikalini kwa mazingatio.

Na suala ambalo limepewa kipaumbele kwanza ni eneo la Mji Mkongwe wa Zanzibar ambako karibu watalii wengi wanapitia hapa Zanzibar. Kwa hivyo, suala hilo lipo tayari limeshafanyiwa utafiti na ripoti yake ipo Serikalini, lakini pia katika maabara ya utalii ni suala ambalo limewekewa utaratibu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu alizungumzia suala la kodi, uchafu na mazingira. Nadhani kile kitabu ambacho tumeambatanisha na kitabu kidogo katika hotuba yetu. Sasa ile ni maabara ya utalii, ukisoma pale utaona kuna mambo mengi ambayo yana matatizo katika Sekta ya Utalii hivi sasa. Serikali imewa-*commission* wataalamu wa Sekta ya Utalii na wataalamu wengine Serikalini imelizingatia hilo suala kwa mapana.

Kwa hivyo, hayo ni mambo ambayo tumeyaona na tumeanza kuyafanyia kazi katika mwaka huu wa fedha tukijaaliwa. Kwa hivyo, ni suala mtambuka, linaratibiwa tu na Wizara yangu kwa muda, lakini ni jambo ambalo tunahakikisha kwamba suala hilo limewasaidia nchi nyingi waliolisimamia kwa makini. Muhimu ni usimamizi

makini, na Serikali tumeamua suala hilo kuliendeleza ili kuona sasa tunakwenda katika *second generation* ya utalii katika nchi yetu. Hilo ndio lengo ambalo tumekusudia.

Kwa hivyo, matatizo mengi ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wameyazungumza hivi sasa ambayo wanayaona katika Sekta ya Utalii, basi kwa kweli jibu lake limo katika *tourism labo* ambayo imeandaliwa na matokeo yake tayari yametolewa na yameanza kufanya kazi.

Nadhani Mhe. Naibu Spika, kwa sababu suala hili ni geni bado, na kwa sababu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wengi hawajapata uelewa nalo, basi nimeshauriwa na Kamati yetu inayosimamia Wizara hii ya Habari, Utalii na Uwezeshaji kuona kwamba tunatafuta fedha kwa ajili ya kuwafanyia semina Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi ili wajue nini *second generation of tourism* na nini Serikali imepanga katika hilo.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naomba Waheshimiwa watukubalie kwa hilo. Na kwamba tunatafuta fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora ambao Tume ya Mipango ndio tume yao, kuangalia namna gani Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watapatiwa dozi nzuri ambayo wakishaielewa wao watatusaidia sisi Wizara ya Habari na Kamisheni katika kulisimamia hili.

Mhe. Naibu Spika, katika hili kuna suala la miundombinu katika Sekta ya Utalii, na hili nimelizungumza katika eneo hilo. Suala la kuendeleza utalii na utamaduni nalo limepewa mazingatio makubwa katika mpango huo mkubwa ambao umeandaliwa na Serikali.

Kuhusu *National Carrier* Mhe. Omar Ali Shehe alilizungumza hili. Mheshimiwa hili ni jambo ambalo la uwekezaji mkubwa na ambalo linahitaji kushirikiana baina ya Serikali na wawekezaji tofauti. Kwa hivyo, tumeanza kulizungumza hili kuwashajiisha baadhi ya wawekezaji wa ndani na nje, na bado mazungumzo yanaendelea katika kuona kwamba nchi yetu inakuwa na ndege ya ndani ambayo inaenda nchi mbali mbali kwa ajili ya kuchukua watalii na kuleta hapa. Hili tukifikia hapo tutakuwa tumefika hatua kubwa katika kustawisha utalii katika nchi yetu.

Pongezi kwa Bwana Said Salum Bakhressa kwa uwekezaji wa bandarini. Namwambia Mheshimiwa tutaufikisha kwa kupitia hasa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kama alivyosema Mhe. Mahmoud Thabit Kombo. Ni kweli kwamba amefanya kazi nzuri pale bandarini, amebadilisha taswira ya ile bandari, na kwa kweli ni jambo zuri sana kwa mwekezaji mzalendo kuisaidia nchi yake katika eneo hili. Anastahiki pongezi kama alivyosema Mhe. Mahmoud.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu *package tours;* kwa hivi sasa kwa hali ya utalii ulivyo mimi sina matatizo. La msingi ni kwamba linalohitajika hapa ni kuimarisha taratibu zetu za makusanyo ya mapato. Kwa hivyo, hali hiyo ikifanyika vizuri basi hilo jambo halina matatizo. Isipokuwa ni kweli kwamba hawa si watumiaji wakubwa katika nchi. Kwa hivyo, kinachofanywa sasa ni kuangalia utaratibu wa kuvutia wawekezaji ambao wanaweza kuja wachache lakini wakatumia katika kiwango kikubwa. Hilo ndio jambo ambalo linaweza kuchukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo nakubaliana na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo ni suala la *ZIFF*. Kweli sikulitaja suala la *ZIFF*, lakini *ZIFF* kwa ukubwa wake sasa linajitaja wenyewe halipaswi kila mara kutajwa na mtu mmoja mmoja, kwa sababu ni jambo ambalo kubwa katika nchi yetu linafanya kazi nzuri.

Kwa hivyo, nadhani mchango wake katika sekta ya utamaduni na katika sekta ya utalii ni mkubwa. Mhe. Naibu Spika, naomba labda nichukue nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wake Mhe. Mahmoud Thabit Kombo katika kuliendeleza na kulipanga hili na kuona kwamba kila mwaka linafanyika, na kwa kweli linatoa uchangamfu mkubwa katika nchi yetu. Kwa hivyo, Mhe. Mahmoud nakushukuru kwa hili, naomba utuendeleze zaidi ili tushirikiane pamoja kuliendeleza hili kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi katika suala la utalii ni kweli kwamba kunaonekana kuna wageni wengi walioshika nafasi kubwa katika mahoteli. Ni kweli kwa sababu bado mafunzo tunayoyatoa katika Chuo chetu cha Utalii ni yale ya ngazi za kati, lakini katika masuala ya meneja na upishi bado inahitaji mafunzo zaidi jambo ambalo tutalipanga huko baadae.

Kuhusu watalii fedha ya Kamisheni iliyopata mwaka huu ni kama shilingi bilioni 1.3.

Mhe. Asha Bakari Makame tunakushukuru kwa ushauri wako kuhusu *tourism labo* na nafurahi kwamba ni mmoja kati ya waliopata dozi ndogo katika suala hili. Umuhimu wake umeuona na tunakushukuru umetushauri

kwamba tushirikiane vizuri na wengine ambao watasimamia suala hili. Tunakuhakikishia kwamba suala hili tutalichukua.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Shirika la Utangazaji wachangiaji wengi ni eneo hili. Waliochangia ni Mhe. Asaa Othman Hamad, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Nassor Salim Ali, Mhe. Salma Mohammed Ali, Mhe. Ali Salum Haji, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Viwe Khamis Abdalla, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, Mhe. Suleiman Hemed Khamis, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Marina Joel Thomas, Mhe. Asha Bakari Makame na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa. Hawa ndio ambao kwa kweli walichangia Shirika la Utangazaji. Tunawashukuru sana kwa michango yao.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu uwezo wa bajeti ni kweli kwamba kwa mujibu wa shughuli za *ZBC* bajeti wanayopata ni ndogo na hili ni shirika.

Namshukuru sana Mhe. Asaa Othman Hamad kwa niaba ya Kamati kuzungumzia suala la matangazo ya kibunge kwa shirika hili. Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wengi walizungumzia namna ambavyo *ZBC* inadaiwa. Ni kweli inadaiwa sana, lakini isipokuwa Mhe. Asaa peke yake kwa niaba ya Kamati ndio angalau alizungumzia suala la malipo ya *ZBC* kutoka Baraza la Wawakilishi.

Sasa Mhe. Naibu Sika, sote ni Wajumbe wa Bunge la Katiba. Bahati nzuri Katibu wa Baraza la Wawakilishi ndio Katibu wa Bunge la Katiba, lakini Katibu wa Bunge la Katiba ambaye ndiye huyo huyo Katibu wa Baraza la Wawakilishi anailipa *TBC* mamilioni ya shilingi ya kutangaza Bunge la Katiba, lakini hakumbuki kulipa hata shilingi kwa muda wote waliotumia Baraza la Wawakilishi. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kuonekana Jimbo la Kitope akileta mchango wake hapa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nadhani hapa pana mazingatio ya kuchukuliwa na Waheshimiwa Wajumbe. Ni vizuri sana kuilaumu *ZBC* kuwa haina *performance* nzuri, lakini isingekuwa vibaya hata kidogo kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuambiana wenyewe kwa wenyewe na hasa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi kwamba wanapotengeneza bajeti wasisahau kuweka fungu kwa ajili ya kulipia *airtime* hii. Sasa hilo ndio jambo la msingi.

Kwa hivyo ni kweli Mhe. Naibu Spika, *ZBC* imerithi madeni ya shilingi milioni 800 kutoka Sauti ya Tanzania Zanzibar na Idara ya Televisheni, Shirika lililoundwa mwaka jana. Katika milioni 800 hizo zimo pamoja na shilingi milioni 40 za mirabaha ambayo nilitakiwa niilipe.

Mhe. Naibu Spika, jengine hakimiliki ambayo Wajumbe wamezungumza kwa hamasa sana. Mwaka jana nilisema kwamba nitajitahidi sana kuisimamia *ZBC* ilipe. Na kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu wakati naizindua Bodi ya *ZBC* jukumu hili niliwapa. Kwamba nawapa chombo kusimamia lakini kuna deni hili, hili na hili. Lakini Wajumbe wa Bodi walipoona yale madeni wanayodaiwa *ZBC* wakasema hapana tusubiri kidogo. Wakanijia wakanambia Mhe. Waziri pamoja na agizo lako tunaomba muda kidogo. Tunadaiwa shilingi milioni 800 pamoja na deni la umeme ambapo *ZECO* wanasema tutakatisha umeme wetu kwa mitambo yetu yote ya *ZBC*.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana kwamba shirika hili linahitaji kwenda kibiashara. Na bila ya kulisaidia kwenda kibiashara kwa kweli haliwezi kufanya shughuli za kiuchumi pamoja na kupata ufanisi na kulipia madeni yake. Kwa hivyo, wale wote ambao wamesimama hapa kuniondolea shilingi mia kwa ajili ya kulipa hakimiliki na malipo mengine naomba wanistahamilie kidogo. Nikishirikiana na Bodi yangu ambayo najua ni bodi makini sana, kwamba baada ya muda madeni haya yote tutafanya utaratibu yaweze kulipwa.

Mimi wasanii ni watu ambao ninawasimamia, hali yao mbaya ni hali mbaya yangu kama msimamizi. Ningependa sio wapate hizi milioni 40 lakini wapate kiwango kikubwa zaidi, lakini Mhe. Naibu Spika, hali ya *ZBC* ndio hiyo. Kwa hivyo, tushauriane Baraza la Wawakilishi tuandae utaratibu na hasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais yupo mwenyewe hili linamhusu. Waziri wa Fedha mwenyewe yupo tukae kwa pamoja tuone namna gani Baraza la Wawakilishi litaweza kuwalipa *ZBC,* halafu ndio *ZBC* iweze kulipa madeni ambayo yanadaiwa.

Utaratibu

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Naibu Spika, nilitaka kuweka maelezo ya Mhe. kwenye *hansard* sawa ili Waheshimiwa Wajumbe wapate nafasi ya kufahamu juu ya suala la Baraza la Wawakilishi na kulipa matangazo ya *ZBC*.

Mhe. Mwenyekiti, ZBC walivyowasilisha *bill* yao kwa chombo hichi kwenye Kamati ya Uongozi, *bill* ambayo ilionekana ni kubwa. Sisi kama Baraza la Wawakilishi, Kamati ya Uongozi tukawasiliana na Wizara ya Fedha ili zile fedha ziingizwe huku kwa ajili ya kupeleka *ZBC*. Wizara ya Fedha wakaeleza kwamba wao kama serikali wanaipa ruzuku *ZBC* kwa ajili ya kuendesha shughuli zao.

Sasa kama wanahitaji Baraza la Wawakilishi liilipe *ZBC* basi zile fedha ambazo zinapewa *ZBC*, ziingizwe kwenye Baraza la Wawakilishi, halafu Baraza la Wawakilishi liipe *ZBC*. Kwa hivyo, suala la kulipa *ZBC* lilikuwa katika utaratibu huo na mpaka leo hawajajibu chochote juu ya rai ile iliyokuwa imetolewa.

Kwa hivyo ninataka kuweka *hansard* sawa kwamba Baraza la Wawakilishi halikushindwa kulipa, isipokuwa wao ndio walioshindwa yale masharti waliyopewa na serikali. Kwa sababu Baraza la Wawakilishi linapokea fedha kutoka serikalini.

Mhe. Naibu Spika, ni hivyo. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Salmin Awadh Salmin. Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru. Ninashukuru utaratibu wa Mhe. Mjumbe. Ninachosema umeletwa wakati mbaya angesubiri wakati wa vifungu tukazungumza.

Suala hili na *TBC* inapewa ruzuku na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, lakini mbona ruzuku yake inarusha vipindi vya Bunge, *TBC* inalipwa. Suala hili ni lazima tukae pamoja, na ndio nikasema hapa kwamba tukae pamoja Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, nikamtaka Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Waziri wa Fedha tulizungumze hili ikiwa *ZBC* inatakiwa kuisimamia ifanye kazi zake kwa ufanisi na kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, naomba niendelee. Mhe. Naibu Spika, kuhusu Mhe. Naibu Waziri amelizungumza vizuri suala la mabuibui na wafanyakazi wa kike. Mhe. Naibu Spika, sio lengo la wizara wala shirika kuwadhalilisha wafanyakazi wanawake. Kama limefanyika vibaya basi unajua wakati mwengine wizara, shirika linaweza kutoa maelekezo watendaji wakateleza katika kulifanyia.

Kinachofanyika ni kwamba pale pamewekwa chumba maalum, pale *reception*. Kipo wakati wowote munaweza mukaenda kukiangalia ambapo mfanyakazi anayekwenda na buibui lake, basi apite pale kwa stara kabisa avue buibui lake, ahifadhi anapotaka, halafu aingie katika utaratibu wa kazi katika maeneo ya kazi.

Ni jambo la kawaida Mhe. Naibu Spika, sote humu tunafanya kazi, mimi sekretari wangu kazini haji na buibui kabisa. Kuna chumba pale pale chini wanavua wenyewe, pale ukishapita mapokezi wanavua wenyewe wala hawasimamiwi.

Kwa hivyo, hili jambo halihitaji kutiwa chumvi kiasi hicho. Inaonekana kwamba mumelifahamu vibaya na siwalaumu, hata kama mimi ningeambiwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ningelifahamu vibaya, lakini nia ya shirika, na wizara ni kuhakikisha kwamba utaratibu wa utumishi serikalini ndio ambao unaofanyika. Kwa hivyo, naomba tushirikiane katika hili eneo la salama, la stara, la kuvua buibui upo na ninadhani tukubaliane.

Kuhusu wanaopeleka matangazo ya vifo. Yale matangazo ya vifo hayapelekwi kule ndani, yanawekwa hapa hapa kwenye *reception*, kuna ofisi pale pale. Kwa hivyo, hana sababu ya kuvuliwa kwa sababu ni pale pale *reception* yanafanyiwa kazi yake. Ama yule ambaye ana mgeni basi tumekubaliana kwamba kama hapa Baraza la Wawakilishi wanavyofanya kwamba asubiri mgeni aitwe aonane na mgeni wake kule katika maeneo maalum. Kuna mitambo, kuna maeneo mengine nyeti, si vizuri kila mgeni kumuingiza jikoni kwa kweli Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, pale ni *sensitive* kwa nchi, kwa hivyo ni vizuri taratibu za kiusalama tumekubaliana kuzichukua, na katika hili hatukusudii kumnyanyasa au kumdhalilisha mtu yeyote, ni katika utaratibu. (*Makofi*).

Kwa hivyo, kama mumelipokea vibaya tunaliombea radhi hilo lakini utaratibu ni huo, na tunaufanya kwa nia njema sana kabisa. Hivyo Wajumbe wote ninafurahi kwamba Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wameungana na hili na wana sababu ya kufanya hivyo, kwa sababu ukipewa suala kama hili kwa kweli unaweza ukapata hisia ambazo zinaweza kukujengea vibaya.

Hivyo, kama limefanyika vibaya basi maelekezo tuliyoyatoa ni hayo, na kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, yeye mwenyewe kwa sababu na yeye alipata akahamaki sana lakini alipokwenda alikuja chini, akaona kwamba kwa kweli hakufanyiki baya. Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumze hilo.

Mhe. Naibu Spika, limezungumzwa suala la kumkejeli Makamu wa Kwanza wa Rais. Limezungumzwa suala hili kwa hamasa kubwa. Ninaambiwa kwamba tumesitisha kwa sababu tunapitisha bajeti. Mhe. Naibu Spika, lililotokea ni kwamba kulikuwa kuna kipindi kinaendeshwa. Wenzetu wa Chama cha Mapinduzi waliomba kwa utaratibu ambao unaokubalika wa kurusha kipindi chao. (*Makofi*).

Na vyama vyengine wakati huo navyo vilikuwa na nafasi. Kama wangekuwa na vipindi vyao kwa kupeleka kwa utaratibu ambao wamekubaliana na uongozi vikarushwa, Hatukufunga milango. Sasa kikawa kinarushwa kinakwenda vizuri mwanzoni. Mimi mwenyewe ni mtizamaji sana wa *ZBC*. Kikaenda vizuri kinaburudisha, mimi nilikuwa ninakitizama chote, lakini baadae kikawa kinakwenda vibaya kidogo. Mimi nikawashauri Mkurugenzi hebu fanya *editing* nzuri. Hiyo *editing policy* yetu idhibitini vizuri.

Wakaniambia Mheshimiwa sawa. Baadae nikavitazama tena nilipokuwa katika Bunge la Katiba, niliporudi ikasadifu, tulikuja kwa Baraza la Mapinduzi Jumamosi moja na Jumapili ikasadifu nikakiona bado inaachiwa jazba jazba inaanza kupanda. Nikamwambia Katibu Mkuu hebu kaa na hawa vijana ili suala hili, huu mche unaweza ukapanda vibaya. Unajua jambo ukiliachilia kama hulisimamii vizuri basi linaweza likaleta matatizo.

Kwa hivyo, Katibu akajitahidi kidogo kama kawaida yake. Siku mbili kikawa vizuri lakini baadae kidogo likachomoza tena ooh! vibaya sana. Sasa mimi bahati njema nikaja tena Baraza la Mapinduzi, nikakikuta kile kipindi kimekwenda vibaya sana. Sasa mimi mwenyewe nikawaambia hichi kipindi hebu kisitisheni kidogo. Kwa sababu nchi yetu ni nchi ambayo kama walivyosema Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tujenga utamaduni wa kuvumiliana kwenye utaratibu mzuri katika kila jambo, lakini sasa kama tunakwenda *that extreme* basi loo! haitakuwa vizuri.

Kwa hivyo, ni mambo ya kawaida katika *editing* ya vipindi. Unaweza ukamuweka mtu ukadhania ni mtu mzuri katika *editing*, lakini kidogo akatelezateleza. Kwa hivyo, yamekwenda hivyo lakini Mhe. Naibu Spika, mambo tumeyadhibiti hayana matatizo na Waheshimiwa Wajumbe ninaomba hatukukizuia kwa sababu ya upitishaji wa bajeti aah! tumezuia kwa sababu ya kufanya mambo yawe mazuri zaidi ili. Ile ni televisheni ya umma, lazima tuhakikishe kwamba wananchi wote wanapata nafasi, na viongozi wetu wote wanapata nafasi ya kuweza kutangazwa bila ya kunyanyaswa au kudhalilishwa au vyenginevyo. Mhe. Naibu Spika, naomba wale wote waliozungumza hilo waelewe hivyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ali Salum Haji nimekusikia mchango wako, ninakushukuru sana. Kawaida Mhe. Ali Salum Haji michango yake huwa ni michango yenye kutujenga sana, tunamshukuru sana. Mara nyingi anapozungumza huko *cafeteria* ni tofauti na akikaa hapa katika Baraza, huwa anazungumza michango ambayo mizuri sana.

Suala hili la mafao ya wafanyakazi. Nimewaachia Bodi hili wanalisimamia na Mwenyekiti wa Bodi, mama mmoja ninamuheshimu sana, mtu mzima, amewahi kuwa Mbunge lakini bahati nzuri amewahi kuwa Mkurugenzi wa chombo hichi na halafu alikuwa mtangazaji mwenyewe.

Kwa hivyo zile *hardship* za watangazaji anaelewa vizuri sana. Mtu akishakuwa mtangazaji wa chombo kile, yeye mwenyewe keshakuwa Mkurugenzi wa chombo hichi, halafu akapanda mpaka kuwa mwanasiasa kuwa Mbunge. Kwa hivyo, ana maarifa mazuri. Tumeshauriana mimi na yeye kama ni kweli maslahi ya wafanyakazi wake ni madogo, wamekaa wao na Bodi wameanza kuyafanyia *scheme of service* ya suala hili.

Kwa hivyo, Mhe. Asha Bakari Makame suala hili tumelianza, umeliliuliza suala la *scheme of service* ya *ZBC*. Hivyo tumelianza, nimemuachia Mhe. Bi. Tatu kama Mwenyekiti wa Bodi, ninamuamini katika hili. Nawaomba tuwape nafasi kidogo lakini hali ya *ZBC* ndio hiyo, lakini yeye mwenyewe amesema kwamba tutashirikiana kuona kwamba maslahi ya wafanyakazi wa *ZBC* yanaboreshwa, na Wajumbe wenyewe ndio Mhe. Ismail Jussa Ladhu, naamini kwamba hili watalisimamia wenyewe. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, makundi ndani ya *ZBC*. Mhe. Ali Salum Haji amenishauri kwamba tukae pamoja na uongozi. Ushauri wake tumeuchukua, tutaufanyia kazi na ninaamini kwamba tutafika pahala kwamba tutapata uongozi ambao utakwenda vizuri sana. Hasa wenyewe wanasema kwamba wafanyakazi pale ni wengi pale. Na ni kweli wafanyakazi kwamba wafanyakazi mia tatu na zaidi. Naamini kwamba watafika pahala kuona kwamba suala hili la makundi linamalizika. Watapunguzwa wale watakaopunguzwa, watanileta wizarani, nitaangalia wapi niwapeleke, lakini tuwe na wafanyakazi wachache ambao wenye uwezo bila ya makundi waweze kufanya kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Saleh Nassor Juma amezungumza suala la *ZBC*. Suala la kumsema vibaya Makamu wa Kwanza, nimeshalizungumza. Kuiachia *ZBC* kuwa *interahamwe*, hatufikii huko tukijaaliwa. Tutaisimamia vizuri kuhakikisha kwamba inakwenda vizuri.

Kuhusu malipo ya swahibu wako Bi. Tatu Khamis wa Pemba. Tayari ameshalipwa Bi. Tatu na hana tatizo. Kwa hivyo, pesa zake za likizo alizokuwa anadai, tayari anasubiri pesa zake za kustaafu, na kwa sababu kama amestaafu karibuni taratibu za kumlipa zinafuata kwa utaratibu wa utumishi serikalini.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, ninakushukuru sana kwa mchango wako. Suala lako la hatimiliki tumelizungumza. Ni kweli kama nilivyosema, deni tunalikubali lakini sijapata uwezo kulilipa. Nitajitahidi sana kwa kushirikiana na wenzangu na ikabidi nikamkamate miguu Mhe. Waziri wa Fedha kuona namna gani tutasaidiana katika kuondoa deni hili.

Kwa hivyo, naomba ile shilingi yangu mimi uniachie ili niweze kupata nafasi na nguvu ya kusimamia zaidi mambo ili hali hii iweze kwenda zaidi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammed Haji Khalid ushauri wako tunauchukua na hii ndio mageuzi ambayo Bodi ya ZBC wanayafanya, wanataka kuona kwamba *ZBC* sasa inakuwa mbele kuliko mashirika mengine ya habari hapa ndani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub alisema kuhusu *camera*. Mwanzoni mwa mwaka huu *ZBC* ilipewa shilingi milioni mia mbili thalathini (230,000,000) kwa ajili ya kununua vifaa vya dharura, ikiwemo *camera* sita. Nilipoambiwa kama *camera* zimeshaletwa, nilimuagiza Mkuu wa Manunuzi wa Wizara akahakikishe *store*, akaniambia kwamba *camera* ameziona na zimeingizwa katika *store* ya *ZBC*.

Kwa hivyo, kuniambia kama ana ukosefu wa *camera* hivi sasa itakuwa labda zimeharibika katika kipindi cha muda wa miezi mitatu, na siamini kwa sababu zilikuwa *camera* mpya. Kwa hivyo kama kuna tatizo jengine sijaarifiwa bado.

Mhe. Viwe Abdalla Khamis kuhusu nyongeza ya wafanyakazi Pemba shilingi ishirini na tano elfu(25,000). Ni kweli hawajalipwa na hawa ni watu wa ruzuku, wafanyakazi wa ruzuku kidogo nyongeza hizi zilichelewa. Hapa kwa Unguja wamelipwa kwa mwezi huu wa Mei na taarifa nimeambiwa kwamba tukijaaliwa mwisho wa mwezi huu, basi kwa Pemba nao watamalizwa.

Kuhusu Mhe. Rufai Said Rufai ameleta mchango mzuri na ushauri mkubwa. Kuhusu kuweka wakalimani, tumejaribu hapa Baraza la Wawakilishi. Tunashukuru kwamba Baraza la Wawakilishi wanatusaidia kwa hili. Na tutajitahidi tuweke wengine pale katika taarifa ya habari na maeneo mengine kuona kwamba wanaona. Ni jambo zuri. Tutafanya mageuzi katika hilo.

Kuhusu Mkurugenzi kwamba ameshamaliza muda wake wa utumishi. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Mkurugenzi Mkuu wa *ZBC* amefikia umri wa kustaafu na Ofisi ya Katibu Mkuu wa wizara imeshaiarifu Wizara ya Utumishi Serikalini kwamba Mkurugenzi Mkuu amefika umri wa kustaafu. Sasa tunasubiri maelekezo kutoka kwao na utaratibu mwengine wa kustaafu.

Mimi sijaarifiwa kwamba ameongezewa muda wala sijapewa ushauri kwamba aongezwe muda au laa, lakini utaratibu ni kwamba mstaafu akishamaliza muda wake wa utumishi basi wizara inaziarifu taasisi zinazohusika na utumishi kwa ajili ya shughuli za kustaafu.

Mhe. Panya Ali Abdalla ninakushukuru sana kwa mchango wako na ni kweli kwamba miongoni wa wafuatiliaji wazuri wa vipindi vya *ZBC*, na ukiona dosari husubiri Baraza, hunipigia ukaniambia Mheshimiwa kweli hapa tuwe na tahadhari.

Ninakushuru sana kwa hili, naomba tuendelee kwa sababu suala hili ni la usimamizi wa pamoja baina ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na sisi ndio wenyewe, wakimsukuma Waziri katika ufuatiliaji wa shughuli hizi. Kwa hivyo, ninakushukuru sana katika hili. (*Makofi*).

Suala la maslahi ya mafundi. Ni kweli kwamba kuna mafundi wa aina mbili. Kuna mafundi ambao wana vyeti ambao wamemaliza Mbweni ama amemaliza *diploma* ya juu ama amemaliza digrii. Hawa maslahi yao yamepangwa vizuri na serikali kwa mujibu wa vyeti vyao, lakini wale mafundi ambao wana uzoefu, serikali mwaka huu imeelekeza kwamba mafundi na waandishi wa habari waangaliwe maslahi maalum katika kutekeleza shughuli zao. Kwa hivyo, suala hili limeshapitishwa na serikali, na Wizara ya Utumishi inalifanyia kazi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu ambaye ni Mjumbe wa Bodi. Ninamshukuru kwa mchango wake. Ushauri wake kwamba tatizo la ufanisi wa *ZBC* ni la Mkurugenzi Mkuu mwenyewe. Ninamshukuru kwa maelezo hayo na kwa sababu yeye ni miongoni mwa Wajumbe wa Bodi, basi ninadhani kwamba ikiwa hiyo ndio mawazo ya Bodi yangu. Basi tutashauriana na serikali kuhusu la kufanya katika hali kama hiyo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri zimebakia dakika 15 jitahidi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: *Inshaallah*. Kuhusu chumba cha baridi *ZBC*, ni kweli kwamba mitambo ile inahitaji *temperature* ndogo kidogo. Kwa hivyo naomba Waheshimiwa Wajumbe wajue hilo, kwamba hata humu Barazani kidogo wakati mwengine huwa tupo baridi zaidi kuliko nje. Kwa hivyo na mitambo ile inahitaji baridi ni jambo la kawaida Waheshimiwa. Kwa hivyo, hatuwezi kuiondosha. Tukiondoa *AC* pale itaharibika ile mitambo. Kwa hivyo, ninaomba tukubaliane na hilo.

Mhe. Ashura Sharif Ali nimeshazungumza kuhusiana na mabuibui. Mhe. Hamza Hassan Juma ninakushukuru sana kwa ushauri wako. Umezungumza mambo mengi, umenishauri vizuri na mara nyingi ushauri wako huwa ni wenye kujenga. Ushauri wako tunauchukua.

Mtambo ya *medium wave* unafanya kazi, kwamba nyumba hazijakamilika. Si kweli, mimi mwenyewe juzi moja nilikwenda usiku saa mbili pale Bungi na nikakuta nyumba zinafanya kazi na taa zinawaka. Kwa hivyo, zimekamilika Mheshimiwa wamo wanakaa.

Suala la *analogue* kwenda *digital* nitatoa maelezo baadae. Mhe. Naibu Spika, wale wote waliochangia kuhusu Hoteli ya Bwawani, ninawashukuru. Mhe. Asaa Othman Hamad, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, Mhe. Salim Abdalla Hamad, na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo.

Tunawashukuru wote kwa mchango wao na namna ambavyo wamepongeza, wamepongeza sana Hoteli ya Bwawani na Mhe. Marina Joel Thomas pia amelizungumzia suala hilo, tunakushukuru.

Ni kweli kwamba Hoteli ya Bwawani uongozi wake unafanya kazi vizuri. Na kuhusu uwekezaji ni kweli kwamba serikali ina mpango wa uwekezaji mkubwa pale, uwekezaji ambao utabadilisha sura ya eneo la Bwawani, ile *trial angle* ya Bwawani itabadilika sana, lakini suala hili bado liko kwenye utaratibu wa mazungumzo na *ZIPA* na serikalini, kwa hivyo haujafika wakati wa kutolea maelezo, kimsingi ni kwamba kuna wawekezaji wengi wamekuja bado wanazingatiwa na serikali, ikiwa tayari serikali itatoa maelezo.

Maelekezo yenu kwamba serikali isilibinafsishe basi tumelipokea na tutashauriana na Waziri wa Fedha pamoja na serikali kwa ujumla kuhusu masuala haya.

Mhe. Hamza Hassan Juma, kuhusu haki miliki nimeshalizungumza.

Mhe. Hassan Hamad Omar ulizungumza mambo mengi na ushauri umetupa tunakushukuru, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu tunakushukuru kwa mchango wako na hasa maslahi ya wafanyakazi uliyotushauri.

Mhe. Salim Abdalla Hamad tunakushukuru kwa suala lako la kuhusu Mkurugenzi Mkuu nimeshajibu, pia posho la wafanyakazi nimeshajibu.

Mhe. Omar Ali Shehe kuhusu kusimamia vyombo vya habari visitumike vibaya. Ushauri huo tunauchukua na tutausimamia. Pia kuhusu nyimbo ile ya Bi Mwanahawa bint Ali, ile nyimbo bado iko hewani haijapigwa marufuku.

Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo, kuhusu waigizaji mbali mbali ni kwamba hakuna mikataba maalum. Taarifa niliyonayo ni kwamba hakuna mikataba maalum ambayo wametiliana na *ZBC* na waigizaji.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tusitoke tunataka kupitisha vifungu, naona Waheshimiwa wanatoka tu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: La msingi ni kwamba suala hili huwa linafanyika kwa makubaliano maalum, na hali ikiwa nzuri wasanii huwa wanalipwa.

Mhe. Marina Joel Thomas na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi tunawashukuru kwa michango yenu. Mhe. Asha Bakari Makame, tunakushukuru kwa suala lako la baibui.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, kuhusu kipindi cha michezo, kinaendelea lakini kinahitaji kufanyiwa maboresho zaidi, *ZBC* wanaifanya kazi hiyo. Pia kuhusu Idara ya Makumbusho, Mhe. Naibu Spika, tumepata ushauri mwingi ambao tunaufanyia kazi. Kuhusu kisima kiliopo Kengeja, Mhe. Mohammed Haji Khalid nitakuja tukakiangalie.

Mhe. Rufai Said Rufai kuhusu Tumbe na Msikiti Chooko. Kazi nzuri wamefanya wananchi wa Tumbe tunawashukuru kwa hili, tuendelee kusaidiana. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa tunakushukuru kwa ushauri wako. Kuhusu uhakiki wa maeneo yote ya kihistoria, kazi hii imefanywa na tunaielewa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Beit El Ajaib na Kasri. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba mradi huu bado serikali unao, Mhe. Ismail Jussa Ladhu amelizungumza hili, tunashirikiana na Serikali ya Oman. *Feasibility* ya kwanza imeshafanywa na hivi karibuni wahandisi wa Mji Mkongwe wamekwenda Oman na wamerudi, wametupa ripoti kwamba wahandisi kutoka Oman watakuja tena kama baada ya mwezi hivi kuja kukamilisha na kuanza kazi. Lengo ni kufanya matengenezo makubwa sana na ya kudumu ya jengo la Beit el Ajaib, utakuwa ni mradi mkubwa na ambao kwa kweli utaleta sura nzuri, lakini utajengwa kwa haiba ile ile.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Ngome Kongwe. Taratibu za kuitengeneza tunaendelea nayo. Mhe. Naibu Spika, kuhusu Kamisheni ya Utamaduni, tunashukuru michango ya Waheshimiwa Wajumbe. Kuhusu nini maana ya utamaduni wa hapa kwetu. Utamaduni ni mila, ustaarabu na silka ya Zanzibar ambayo sote tunazifahamu.

Vile vile kuhusu ujenzi wa Judo. Mhe. Viwe Khamis Abdalla alilizungumzia suala hili, umejengwa na nchi ya Japan kwa shilingi milioni 230 na vifaa vilivyowekwa mule ni shilingi milioni 270, kwa hivyo mradi mzima umegharimu shilingi milioni 500.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu barua ya Mtumwa Said Haji ambayo inazungumzia *ZFA* na wale wote waliozungumzia *ZFA*. *ZFA* ni chama cha kijamii kina katiba yake, kina utaratibu wake na ni kweli kina matatizo mengi wananchi wanalalamikia, lakini msingi wa suala hilo ni mabadiliko ya katiba yake ambayo tumewaambia kwamba Baraza la Michezo, lihakikishe kwamba kabla ya mwisho wa mwaka huu katiba ya *ZFA* imerekebishwa kabla hawajafanya uchaguzi mwengine.

Kwa hivyo, hayo ndio maagizo ya Wizara kwa Baraza la Michezo, na Mrajis anasimamia hilo ili kuona kwamba *ZFA* iwe na katiba mpya na uongozi ambao utachaguliwa kidemokrasia.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu *Weight Lifting Association* Mhe. Ismail Jussa na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo. Ni kweli kwamba suala hili tunalo wizarani, chama hiki ni chama ambacho kinafanya kazi vizuri, lakini masuala ya kuwalipia ada Mhe. Naibu Spika, ni juu yao. Wizara ikiwa na uwezo tunawasaidia, mwaka jana tuliwasaidia lakini hali ya bajeti ikiwa mbaya basi hilo huwa haliwezekani.

Mhe. Hassan Hamad Omar kuhusu suala la shamba, hongera kwa suala hilo. Kuhusu picha za viongozi Mhe. Mahmoud Thabit Kombo zinachapishwa na Idara ya Habari Maelezo, lakini bendera zinachapishwa na Bohari Kuu.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa ni Chuo cha Uandishi wa Habari, wajumbe waliozungumza tunawashukuru. Ni kweli hawana majengo, serikali tumeamua kwamba tuwape eneo la Kilimani pale palipokuwa Kilimani Bar kwa ajili ya kujenga majengo yao ya kudumu.

Vile vile kuhusu Baraza la Kiswahili linajitahidi kufanya kazi zake na tutajitahidi ili kuhakikisha kwamba suala hili linakamilika. Hivi karibuni tunategemea kuanzishwa hapa Kamisheni ya Kiswahili ya Nchi za Afrika ya Mashariki.

Pia Baraza la Michezo Mhe. Naibu Spika, lilizungumzwa na Wajumbe wengi. Mjumbe mmoja ambaye alilizungumza hili ni Mhe. Raza, bahati mbaya hayupo.

Mhe. Naibu Spika, suala hili lisingepaswa kuzungumzwa tena katika kikao hiki, kwa sababu Mhe. Raza aliyezungumza suala hili, kama nilivyozungumza na leo narudia, kwamba Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na serikali hazidaiwi na Mhe. Raza. Bahati nzuri sana katika Baraza hili la Wawakilishi kuna kiongozi wetu, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Sio vizuri katika ndani ya muda wa wiki mbili Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kama keshalitolea jambo kauli, halafu Mwakilishi yule yule anazungumza tena suala hili, sio jambo la kawaida Mhe. Naibu Spika, na halipaswi kwa kweli.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ningewaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi tufuate utaratibu. Suala hili alilizungumza na kamati, nikalitolea utaratibu. Yeye anazungumza siku ile nilizungumza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hata sikumtaja, na bahati mbaya asizungumze maneno ya kutia chumvi katika chombo kikubwa kama hiki, haina sababu ya kutoleana taarifa na utaratibu, kwa sababu sote ni watu wazima, lakini siku ambayo nilizungumza suala hili kwenye kamati, sikumtaja hata kidogo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Lilizungumzwa suala hili wizara haina habari, tumelisikia Mhe. Raza katika vyombo vya habari. Sasa kama una uthibitisho umekopesha serikali, lete vielelezo serikali hii haiwezi kushindwa kutoa shilingi milioni 70 kama imekopa hata siku moja. Baya zaidi kukopa serikali ina utaratibu wake, Waziri wa Fedha ni lazima ahusishwe. Sasa mimi nitachukua tu pesa kwa Mhe. Raza, haiwezekani!

Mhe. Naibu Spika, mimi nilishakwenda kwa Mhe. Omar Yussuf Mzee, Waziri wa Fedha nikataja shilingi bilioni 2, akaniambia subiri baada ya wiki mbili akanipa shilingi bilioni 2, iwe shilingi milioni 70.

Lakini kama alivyosema Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, naomba kurudia na iwe jibu kwa Mhe. Raza katika suala hili, kwa sababu baada ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuzungumza katika Baraza au katika Bunge, yeye ni kiongozi wa serikali katika Bunge, haiwezekani Waziri awe na maneno mengine kinyume ya yale Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameyazungumza, itakuwa ni jambo la ajabu, na itakuwa ni utovu wa nidhamu ambao mimi siwezi.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais amezungumza hivi, Mhe. Naibu Spika, naomba unipe nafasi ya kulizungumza. Mhe. Naibu Spika, nanukuu.

"Kuhusu mkopo wa Mapinduzi Cup, kwanza niipongeze Kamati ya Mapinduzi Cup, kamati hii imefanya kazi nzuri na wamefanya kazi vizuri na hasa kwa kupitia wizara husika ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na wakafanya kazi nzuri ya kuhamasisha michezo mbali mbali, hasa mchezo wa mpira wa miguu. Kwa hivyo, nawapongeza sana kwa kazi hiyo.

Pia Nimpongeze Mhe. Mohamedraza Mohamedali kwa kuamua kuwakopesha Mapinduzi Cup fedha ambazo walitaka kutoka kwa Mhe. Mohammedraza. Mhe. Spika, lakini napenda niseme hivi, Mapinduzi Cup ni taasisi isiyo ya kiserikali, Mapinduzi Cup ni taasisi isiyo ya serikali".

Haya ni maneno ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika Baraza hili.

"Kwa hivyo, sio vyema kuipaka matope serikali kwa jambo lisilokuwa sio lake. Mapinduzi Cup wamekwenda kukopa kwa Mhe. Mohammedraza na mimi nashukuru kwa kuwakopesha,lakini kidogo limetokezea tatizo, tatizo la msingi lilikuwa hapa alipoona amecheleweshwa kulipwa fedha zake, basi alikuwa awasiliane na Kamati ya Mpinduzi Cup wajue kinachodaiwa na wao wangekubaliana, walipoona kwamba

jambo hili limewashinda basi wangewasiliana na wizara husika, na wizara husika watakapoona jambo hili limewashinda basi sisi milango yetu iko wazi, nakuhakikishia hili jambo halitushindi".

"Mhe. Spika, tatizo lililokuwepo hapa ambalo nafikiri hata Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo limemkera ni Mhe. Mohammedraza kujikurukupia kwenda kwenye vyombo vya habari kabla ya kupitia kwenye kamati husika, kabla ya kwenda kwenye uongozi wao mkakaa mkazungumza. Nataka nikuhakikishie kwamba hakuna litakalotushinda, hili ni jambo dogo sana kwetu".

"Mhe. Spika, kwa hivyo ninachokuombeni kwamba madhali sasa mmelileta kwetu tutachunguza tulimalize na tutaona tutalimaliza vipi, maana uwezo wa kulimaza tunao, lakini sio vyema kuipaka matope serikali kwenye mambo ambayo yanatokea kwa nia njema. Kwa hivyo, Mhe. Mohammedraza milango yetu iko wazi, na madhali sasa umeleta malalamiko yako rasmi kwetu, basi nakuhakikishia utaona majibu yetu". Huo ndio mwisho wa kunukuu.

Mhe. Naibu Spika, hayo ndio majibu ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ndani ya Baraza. Sasa mimi nizungumze nini baada ya majibu hayo. Yeye aliikopesha NGO kama alivyosema, sasa anataka serikali ishughulikie malipo. Sasa kama anataka kulipwa, na kama ana vielelezo hilo ndio la msingi, serikali haiwezi kutoa pesa kama njugu. Kama hana vielelezo serikali haiwezi kutoa pesa kama njugu. Basi kama alivyosema bosi wangu ambaye namuheshimu sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Ilivyokuwa milango ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais iko wazi, basi alete vielelezo vyake hazina matatizo ni pesa ndogo sana hizo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya Saba. Mhe. Naibu Spika, nilitaka nijibu hilo.

Mhe. Nassor Salim Ali nakushukuru. Namalizia Mhe. Naibu Spika, naona unaniangalia sana, nakushukuru kwa michango yako. Wewe ni mwanamichezo mzuri sana nakushukuru sana, timu yako ya Ujamaa nasikia mara hii imefanya mambo mazuri na hongera kwa hilo, najua ni jitihada zako hizo.

Vile vile ulionishauri kuhusu kutafuta fedha zaidi kwa timu unazokwenda, najua una jambo umeliwekeza hapa. Ushauri huo umenipa nitaufanyia kazi na tutashirikiana na wewe kulitafutia ufumbuzi. Migogoro ya *ZFA* nimeshazungumza ni kweli imepungua kidogo, lakini tunahitaji kushirikiana katika hili.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu *league* ya Muungano, nimekusikia tutalifanyia kazi Mhe. Mjumbe.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie katika suala hili kwa kuzungumzia hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuhusu mchezo wa ng'ombe, tumechukua hili.

Mhe. bi Panya Ali Abdalla tunakushukuru kwa mchango wako. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu tunawashukuru kwa michango yenu mizuri mliyotupa.

Vile vile Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kuhusu chama cha *Weight Lifting Association,* tumeshalizungumza hili tutaangalia hali yetu ikiwa nzuri tutawalipa. Hivi sasa wako *Athens* kwa timu ya Tanzania Bara naambiwa.

Kuhusu Mwenge, Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwa kuna tatizo kati ya watu wa *ZFA* na mambo yao ya rufaa. Tumekubaliana serikali kwamba sisi wanasiasa tujitoe katika mambo ya michezo. Sheria zimezungumza hivyo na sera zinazungumza hivyo. Kwa hivyo, masuala haya yamezungumzwa ndani ya kanuni na ndani ya taratibu za *ZFA*. Kwa hivyo, mimi nasikitika kwa yale ambayo Mhe. Mama Asha Bakari amenipa na kabla ya hapo alizungumzia Mhe. Nassor Salim Ali katika suala hili. Kamati ya rufaa imeshatoa uamuzi wake, sasa kwa mujibu wa Katiba ya *ZFA*, kamati ya usuluhishi na rufaa ikishatoa uamuzi wake basi inakuwa vigumu sana kwa sisi wanasiasa kuingilia kati, lakini hata hivyo naomba baadaye Mhe. bi Asha Bakari ambaye amelizungumza tupate ushauri wa Mhe. Nassor Salim Ali ambaye amelizungumza, ana uzoefu mkubwa kidogo katika masuala haya basi tushauriane na wizara, tuwaite Baraza la Michezo na *ZFA* Taifa tukae pamoja tuone tutakwendaje katika suala hili.

Mhe. Naibu Spika, waliozungumza suala la *ZMUX* tunashukuru sana, kuna Wajumbe wengi walilizungumza suala hili, imeanza vizuri. Kampuni ya AZAM TV Mhe. Nassor Salim Ali, haijazuiwa kufanya matangazo yake hapa Zanzibar, imepewa leseni na imeanza kuuza ving'amuzi vyake viko vimesambaa nchi nzima na wanatumia *satellite*. Kwa hivyo, na sisi hata *ZBC* tayari nayo iko katika *AZAM TV*, kwa hivyo wanapoirusha Afrika nzima na *ZBC* nayo wamechukua inaonekana. Kwa hivyo, popote ulipo Afrika kama una king'amuzi cha *AZAM TV* basi utaweza kuiona *ZBC* haina matatizo, kwa hivyo tuna mashirikiano nao mazuri sana.

Mhe. Naibu Spika, Mhe.Salma Mohammed Ali kuhusu kukatika kwa matangazo Pemba. Ni kweli kwamba bado tunalifanyia kazi hili, na nimeambiwa suala hili ni vipi. Kwa ufupi Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nikilizungumza hili naomba nizungumze tena kwamba tulipo-*design* tulitegemea kwamba tutumie mkonga wa taifa ndio wa kupeperusha matangazo. Kwa bahati mbaya haukuwa tayari kwa matumizi, hivyo tukatumia yale makawa ambayo yanatusaidia. Sasa kwa bahati mbaya baina ya Unguja na Pemba kuna mikondo ya bahari ambayo yanasababisha kitu kinaitwa *passage* ambayo inatusumbua kidogo. Kwa hivyo tumekubaliana serikalini, Wizara ya Fedha na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwamba tutumie mkonga wa taifa katika hilo, Kwahani wameshafika pahala pazuri, tunategemea kwamba baada ya muda mfupi suala hili litakamilika.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kuhusu kampuni ya *ZMUX,* imeanzishwa chini ya sheria ya makampuni na imesajiliwa rasmi. Kampuni ya *ZMUX* inaendeshwa na bodi ya kampuni ambayo kwa hivi sasa Afisa Mtendaji wake ni ndugu Hiji Shajak.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, ushauri kuhusu Bodi ya Sanaa tumeuchukua na hasa kuhusu maadili yanachukuliwa katika kuangalia mambo yanayooneshwa katika vyombo vya habari.

Kuhusu Baraza la Sanaa. Ushauri wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuhusu ghasia mbali mbali katika eneo lake la Paje. Mhe. Naibu Spika, ni kweli Mhe. Jaku Hashim anaghasiwa sana na suala hili, lakini anajua jitihada ambazo sisi wizara tumezichukua katika hili, tumeshirikiana na Baraza la Sanaa na Bodi ya Sensa na wizara kwa jumla, tulikwenda mara tatu Paje usiku na tumefikia pahala pazuri, lakini bahati mbaya baada ya kuchukua hatua za kuhakikisha kama ngoma na ghasia nyingi hazipigwi kule, basi wenye mahoteli kule wakaenda mahakamani wakapata *injunction order*. Kwa hivyo, sisi hatuwezi, mahakama ndio *supreme* katika mambo haya. Kwa hivyo bado kesi iko mahakamani, wakati wowote ikimalizika suala hili litakuwa limekamilika.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu fedha zilizotumika katika kuweka mtambo wa *digital*. Mhe. Naibu Spika, mwaka jana nilisema na naomba niseme kwamba Kampuni ya *AGAPE* ndio iliyopewa kazi ya ujenzi wa Miundombinu ya *digital* kwa thamani ya dola za Kimarekani milioni 3,921,925 kwa kutupa *channel* 36 na Kampuni ya *Sony* ndio iliyokubaliana itujengee mitambo mipya ya studio ya Karume House na Mkoroshoni kwa thamani ya dola za Kimarekani milioni 1,062,138. Kazi hizo zote zimekwenda vizuri na zinaendelea katika hali nzuri sana. Kazi ya kuweka miundombinu takriban imefika asilimia 100, kazi inayofanywa sasa ni kuhakiki mitambo iliyowekwa na kazi ya kuweka studio hizi mbili zimefikia hatua nzuri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo ambayo nimeyazungumza, nashukuru kwamba nimepata nafasi ya kulizungumza hili. Kuna maelezo ya vifungu mbali mbali ambavyo vimeombwa maelezo na Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Ali Salum Haji. Mhe. Naibu Spika, kwa pamoja Waheshimiwa Wajumbe hawa walitaka kuzungumza gharama za vilainisho Pemba na ujenzi wa majengo mapya.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba gharama za mafuta Pemba mara hii zimeongezeka kidogo, kwa sababu mbili. Sababu ya kwanza tumejenga Studio mpya ya *ZBC,* na katika hili tunahitaji kupata taarifa nyingi kutoka vijijini kuja pale, vyenginevyo itakuwa ile *studio* ni *white elephant;* itakaa haina kazi.

Kwa hivyo, Idara ya Habari Maelezo na wizara kwa jumla tumekubaliana kwamba hili ni suala muhimu kwenda kutafuta habari, yaani twende vijijini kwa wananchi kwa ajili ya kuangalia maendeleo yao pamoja na shughuli zao mbali mbali, ili *studio* ile iweze kufanya kazi vizuri. Hilo ni jambo moja muhimu.

Jambo jengine ni kwamba mara nyingi ziara mbali mbali za viongozi hasa Makamu wa Pili na Makamu wa Kwanza pamoja na Mhe. Rais wa Zanzibar, hulazimika kuwa na *crew* ya waandishi wa habari mbali mbali, ili kuhakikisha kwamba wanakwenda kule kwa ajili ya kuja kuleta taarifa.

Kuhusu gharama za majengo mapya kufika shilingi milioni 643,400,000/=. Ni kwamba tunakusudia kuweka ujenzi wa mpira wa kukimbilia na mwaka jana tuliweka *other charges* zetu zote katika ujenzi wa nyasi bandia, badala ya kutumia *other charges* zetu kwa mambo mengine, na sisi huzikusanya na tukazitia kwenye fungu moja na tukaliweka jambo lionekane.

Kwa hivyo, mwaka jana *other charges* zote tulizikusanya na tukajenga nyasi bandia, jambo ambalo tulidhani haliwezekani, lakini tunashukuru kwa mashirikiano ya idara zote tulikubaliana hilo na tuliweka nyasi bandia badala ya kutumia kwa mambo mengine.

Vile vile na mara hii tumezikusanya *other charges* zetu na kujibanabana tukapata fedha kwa ajili ya kuweka mpira au njia ya kukimbilia Pemba. Kwa maana hiyo, ndio mkaliona hili fungu limeongezeka kiasi hicho.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie katika hili, kwa sababu kuna vifungu vingi ambavyo nimetakiwa maelezo. Kwa hiyo, naomba nitoe maelezo hayo.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu Kamisheni ya Utalii, gharama za safari; uhaba wa fedha. Imepunguza kuhudhuria matamasha kutoka 10 hadi 7, kwa sababu ya kuanzishwa *Tourism Lab*, kule nako kuna uwezekano wa kupata *component* ndogo kwa kufanya *promotion* kwa njia moja au nyengine. Kwa hivyo, tukaona tupunguze katika suala hili.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu vifaa na huduma *sub vote* ile iliyokuwa na shilingi 98,000,000/=. Kwa kweli kifungu hichi kimeongezeka, kwa sababu tunakusudia kushirikiana na nchi ya Singapore kufanya mapitio Mpango Mkuu wa Utalii na Mpango Mkakati wa Utalii. Hivyo, tumekubaliana tuweke fedha kidogo, ili watakapokuja wenzetu kushirikiana nao katika hili, tuwe na uwezo wa kulifanya hili suala.

Kuhusu ruzuku na uimarishaji wa utalii na masoko. Mhe. Naibu Spika, tatizo la uhaba wa fedha ndio limepunguza na hali tunaiona.

Pia kifungu cha Idara ya Habari na Utamaduni na Idara ya Mipango na Sera, vifungu vilivyowekwa hapo ni shilingi 22,000,000/= ni vifungu vya *computer*, kuanzisha tovuti, *server* na *database*. Mhe. Naibu Spika, jambo hili tumelipanga kulitekeleza mwaka huu.

Afisi Kuu Pemba gharama za safari shilingi 36,000,000/= kwa ajili ya safari za ndani kusaidia mambo mbali mbali kama nilivyozungumza.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu vifungu vya posho maalum Idara ya Utumishi na Uendeshaji, kwa sababu linatokana na ongezeko la mishahara suala hili.

Gharama ya mafunzo ongezeko la ada ya vyuo vikuu kuendelea kuwasomesha wafanyakazi 6 na kuwapeleka wengine 3 nje ya nchi.

Idara ya Habari Maelezo samani za afisi, ununuzi wa mapazia ya *electronic* kama tulivyosema kwenye maelezo yetu, kwamba tunakusudia kidogo tubadilike badala ya kuweka yale matangazo ya kwenye maeneo mbali mbali, tuweke angalau kama wenzetu wanavyoweka mapazia ya *electronic*, ambayo tutaweza kwa kutumia mitambo kuonesha maendeleo mbali mbali ya nchi yetu.

Baada ya hayo, sasa naomba Mhe. Naibu Spika, nieleze Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwamba nimejitahidi kujibu hoja zao, na kama kuna Mhe. Mjumbe yeyote ambaye sikujibu hoja yake, hiyo haikuwa kwa makusudi na niko tayari kutoa ufafanuzi juu ya tatizo kama hilo. Ninachokusudia kusema ni kwamba Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inagusa maisha ya wananchi wote wa Zanzibar kwa pamoja.

Kwa kweli wizara hii ni ya wananchi wetu popote walipo; kwa wale wanaoshughulikia na habari na hata wale wanaosikiliza nao pia ni wadau wa hili. Wale wanaoshugulikia masuala ya utamaduni ni wizara yao, wanaoshughulika na michezo ndio wenyewe hasa wizara yao hii na utalii ndio zaidi.

Ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba baada ya maelezo hayo watupitishie bajeti yetu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hotuba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza lako Tukufu limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Sasa naliomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 31 - KAMISHENI YA UTALII

Kifungu 0201	Utawala Unguja	1,340,000,000/=
Kifungu 0301	Afisi Kuu Pemba	47,658,000/=
Jumla ya Fungu		**1,387,658,000/=**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 42 - WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Kifungu 0701	Idara ya Habari Maelezo	19,000,000/=
Kifungu 0702	Tume ya Utangazaji	52,000,000/=
Kifungu 1101	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Unguja	210,000,000/=
Kifungu 1208	Kamisheni ya Utamaduni na Michezo	50,000,000/=
Jumla ya Fungu		**331,000,000/=**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 31 - KAMISHENI YA UTALII

Kifungu 0201

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa sifanyi haki kama sikumpongeza Mhe. Waziri kwa umakini wake katika kujibu hoja zetu mbali mbali, lakini ndio dasturi na ada ya *backbenchers* kwamba kupata maelezo ya kina zaidi, nadhani hata yeye atasikitika akija kutoka mtupu hapa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu vifungu vingi vile ambavyo nilivitolea hoja ninashukuru amejibu vizuri, lakini kama alivyokiri mwenyewe kwamba kulikuwa na vifungu ambavyo niliomba maelezo kuhusu matumizi, ninashukuru amejitahidi.

Sasa swali langu Mhe. Mwenyekiti ningeomba anisaidie Mhe. Waziri, kwenye Kamisheni ya Utalii nilihoji kwenye gharama za safari, utayarishaji wa mpango wa bajeti, lakini zaidi katika uimarishaji wa utalii na masoko kuna shilingi milioni 198,000,000/=.

Vile vile katika mchango wangu niliomba maelezo ambapo kwa bahati nzuri katika majibu yake amenisaidia kuhusu zile fedha za maendeleo ambazo kuna shilingi bilioni 5,595,375,000/=.

Mhe. Waziri ametueleza kwamba kupata maelezo ya mpango ule tusome kitabu cha bajeti. Mhe. Mwenyekiti, swali langu limekuja hapa kwamba nikisoma kitabu hichi Mhe. Mwenyekiti, ambacho kina ufafanuzi wa mpango wa maendeleo, na nitafahamika tu hoja yangu ninakusudia nini. Kwa kweli huku kuna nyanja mbali mbali zikiwemo masoko, utangazaji na mambo mengine kama hayo.

Sasa ninajiuliza Mhe. Mwenyekiti, ikiwa fedha hizi za maendeleo ni bilioni 5 na kidogo zinakwenda kufanya kazi hizo, kwa nini hazikupunguza fungu katika shughuli za Utawala wa Kamisheni katika mambo ambayo sasa yamepatikana au yatakidhiwa haja zake kupitia fedha zile za maendeleo.

Mategemeo yangu ni kwamba ikiwa kuna fungu linakwenda kutangaza kwa maana ya masoko, ikiwa kuna fungu linakwenda kushughulikia mambo ya matamasha tayari lipo, kwa nini tena fedha za utawala katika Kamisheni bado kuna mafungu kama haya ya safari shilingi milioni 148,000,000/= au fungu hili la uimarishaji wa utalii lenye shilingi milioni 198,000,000/=. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anisaidie.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru na nimemfahamu sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Kwa kweli nilidhani kwamba angesema fungu la Utawala lizidi sasa badala ya kupungua, kwa sababu kuna kazi ambayo imepangwa na *Tourism Lab*, ambapo huku kuna kazi Kamisheni ya Utalii itabidi izifanye pia. Kwa hiyo, kuna kazi ambazo zimepangwa na utaratibu wa kawaida wa Kamisheni, lakini sasa kuna kazi za ziada ambazo zimepangwa katika *Tourism Lab*.

Vile vile kuna ***score card*** ambayo Katibu Mtendaji wa Kamisheni ameekewa lazima aikamilishe na fedha za uendeshaji na utawala ndio hizo ambazo zimewekwa huku. Kwa maana hiyo, huku kuna malengo ambayo yamewekwa na lazima ayakamilishe.

Kutokana na hiyo, nilidhani kama wewe umeongezewa kazi, lakini mbona *resources* za kazi zimepungua, hapo ingelikuwa sawa, lakini huku wameongezewa kazi na halafu nipunguze *resources* zao za kazi ah! nadhani hiyo si sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Mjumbe angewatetea kwa sababu huku kuna kazi wanataka kufanya, ndio kwa fedha zipi, watajibana kwa fedha hizo hizo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwa maelezo hayo ningeweza kukubali tuendelee nikaja nikamsubiri tena kwenye fungu la maendeleo, lakini nataka hili suala tulimalize kabisa hapa. Kwa kweli mantiki ya hoja yake nimeifahamu, lakini nataka tuekane sawa tu, kwa sababu zote ni fedha za walipa kodi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, labda niulize swali *specific* katika hiyo *Tourism Lab*, ambayo bahati mbaya Mhe. Waziri amewapa semina baadhi ya watu na sisi wengine hatujaipata ndio maana inabidi tujitosheleze humu kwenye kitabu, lakini hilo kwangu mimi sio suala muhimu.

Kwa mfano, mradi wa ukuzaji wa masoko katika ukurasa wa 7 kwenye kitabu chake kina shilingi milioni 173,345,000/= katika mambo hayo kuna kuanzisha Kitengo cha Masoko na Uhamasishaji, Kuimarisha Masoko kwa Njia ya Mtandao, Kuimarisha Masoko kwa Njia Shirikishi na mambo mengine.

Sasa ndio maana nikajiuliza ikiwa fedha hizi zinafanya suala hili, hizi fedha ambazo zimeekwa kuhusu uimarishaji wa utalii na masoko kwenye *sub vote* 263100 iko kwenye ukurasa wa 11, ambapo ni shilingi milioni 198,400,000/= hizi zitafanya shughuli gani ambayo ni tofauti na hii, ndipo nilipotaka anisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, labda niende *very specific*, ili aweze kunisaidia na akinionesha hii tofauti yake hii Mhe. Mwenyekiti, sina matatizo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Aaa! Mhe. Mwenyekiti, nimeomba anisaidie tofauti. Kwa mfano, hizi shilingi milioni 173,345,000/= ambazo ziko kwenye ukurasa wa 7 wa kitabu chake hichi, ambazo ni Mradi wa Ukuzaji wa Masoko, na miongoni mwa shughuli zake kama nilivyozisoma ni kuanzisha Kitengo cha Masoko na Uhamasishaji, Kuimarisha Masoko kwa Njia ya Mtandao, Kuimarisha Masoko kwa Njia ya Shirikishi na haya ni mambo ya masoko.

Lakini huku katika ruzuku kwenye Kamisheni sasa ninapozungumzia kwenye utawala kuna uimarishaji wa utalii na masoko shilingi milioni 198,400,000/= ndipo pale niliposema kwamba masoko haya, kwa sababu yote yanahudumia utalii, ambayo tayari kuna fedha kwenye fungu la maendeleo. Sasa ni shughuli zipi na zinatafautiana vipi, na akiniridhisha kwa hilo nitasema mafungu yote yaendelee, lakini hivi sasa kidogo bado sijaridhika.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kama alivyosema na kama nilivyotoa ahadi pale kutafuta namna ikiwezekana, kama hali itaturuhusu na kupata mashirikiano mazuri ya wadau wengine *Tourism Lab*, tufanye semina, ili Waheshimiwa Wajumbe wajue nini *Tourism Lab* hilo ni jambo muhimu sana.

Lakini suala hili la mradi wa ukuzaji wa masoko. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niseme kwamba hii *Tourism Lab* inao wadau wengi sana, yaani kuna wizara nyingi sana, na imeandikwa huku kama vile Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inahusika, Wizara ya Fedha, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Sasa *component* hii ya masoko tunaweza kuwa na kifungu kidogo sana ambacho sisi Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo au Kamisheni ya Utalii itakishughulikia, lakini vifungu vyengine kwa mfano, pale kuna suala la *branding* na hilo utaona lipo hapo, lakini litakwenda kwenye wizara inayohusiana na mambo ya *branding;* Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kwa hivyo, naomba utukubalie hili, lakini naomba ukubali kwamba suala hili ni suala ambalo limepangwa kwa uangalifu mkubwa sana na Kamisheni na Tume ya Mipango, sisi tumeshirikishwa, lakini wametafuta watu ambao wenye maarifa mazuri na naamini kwamba wakati wa semina ikija, basi kama ambavyo walipata wenzetu na sisi kwa jumla tutapata kufahamu nini serikali imepanga katika suala hili. Naomba tukubaliane hivyo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, uzuri wake katika hili na wenzake wasimuonee wivu, ni kwamba namuamini sana Mhe. Said Ali Mbarouk katika usimamizi wa kazi. Kwa hivyo, ninachomuomba tu mimi ni kwamba kwa sababu nasema hapa nitakuja kusema kwenye mafungu mengine, ni kwamba yale mafungu ambayo nilimuandikia, sababu nina hakika anayo baadae ayasimamie mwenyewe ajiridhishe, kwa sababu hofu yetu tumeshaiona hapa katika Wizara mbali mbali, ni kwamba mara nyengine fedha hizi zinatengwa kwa wingi, lakini haziendi katika lile lililokusudiwa. Kwa hivyo, mimi namuamini kwamba ni Mhe. Waziri makini. Kwa hivyo, nimuombe tu kwamba katika hili asimamie nitakuja kumuomba katika mafungu mengine tukifika.

Mhe. Jabu Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nimpongeze sana tena sana Mhe. Waziri kwa umakini wake alipokuwa akijibu hoja moja baada ya moja, nimpongeze kwa dhati kabisa. Hoja yangu moja nafikiri Mhe. Waziri, itakuwa kwa muda hakupata kunijibu majumba ya Mji Mkongwe kuna hatari ya kumalizika kuwa mahoteli na chombo hichi hichi kupitia kwa Mhe. Waziri wa Ardhi, alisema majengo yale yatakuwa ya mwisho, tunaendelea kuziona nyumba bado kuendelea kuwa hoteli Mji Mkongwe, kauli ile ya serikali iko je?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Jaku, amelizungumza suala hilo na bahati mbaya sikupata muda wa kulitolea majibu, sera ya serikali na mtazamo wake kwanza Ofisi zote zihame kutoka Mji Mkongwe na tayari kuna mpango maalum wa kuhakikisha kwamba majenzi yanajengwa nje ya Mji Mkongwe hasa Ofisi za Serikali, kwa sababu ni kwamba yale majengo ni mabovu ya siku nyingi, juzi moja sijui ilikuwa nini, likaporomoka ikawa mtihani mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa lazima tukubaliane kwamba haya majengi yameshakuwa ya siku nyingi, kwanza Ofisi za Serikali, serikali imeamua kuzihamishia nje, ndio maamuzi ya serikali, ndio maana ukaona Mheshimiwa anajenga vile, yake kubwa sana pale Mazizini. Mhe. Mwanasheria Mkuu tayari ameshahamia na wengine wanakuja kidogo kidogo, Wizara ya Elimu ndio amefika, ndio wa mwanzo mwanzo. Kwa hivyo, wengine wote watakuja.

Mhe. Mwenyekiti, sio lazima pale Mazizini, lakini maeneo mbali mbali ya nje ya mji, sasa suala la wananchi nalo ni suala ambalo tutaendelea kulishughulikia kwamba ni muhimu wananchi wetu wakae maeneo ambayo yanausalama. Kwa hivyo, muhimu ni matengenezo ya nyumba zenyewe. Kwa hivyo, nyumba zile ambazo serikali imehama kwa ajili ya Maofisi wanakuja wawekezaji kuomba kuekeza na wengi wao kwa sababu ya mandhari ya Mji Mkongwe na ulivyo wanapendelea kuekeza katika masuala ya hoteli. Kwa hivyo, Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango hapa ndiyo mambo wanayoshughulikia, hayo sisi wengine huwa tunaambiwa ni hoteli, basi kazi yetu ni kushirikiana nao katika suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kimsingi ni kweli kwamba Hoteli nyingi zinazojengwa baadae pale huwekwa mahoteli ni kivutio kikubwa na wananchi ninachowaomba ni kwamba waendelee kujenga zile nyumba zao ambazo wanaishi ili waweze kukaa katika majengo ambayo yana usalama, Serikali haiwalazimishi wananchi wahame, lakini la msingi ni kwamba waendelee kuyatengeneza ili usalama wao uwepo,hatupendelei kusikia kesho na keshokutwa wananchi wetu wameporomokewa na jengo hilo ni jambo muhimu. Kwa hivyo, Wawakilishi tushirikiane hilo na hasa Mwakilishi wa Mji Mkongwe tushirikiane kuona kwamba wapiga kura wake wapo katika salama kwa sababu kesho mwakani *Inshaallah* anawahitaji hawa. Kwa hivyo, lazima wakae katika maeneo salama.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hoja yangu Mhe. Waziri, hakusikia vizuri, labda nizungumze kidogo kidogo, hoja yangu nyumba za Mji Mkongwe zinamalizika kufanywa mahoteli, kwa kuwa mahoteli yanakuwa mengi hivi sasa na chombo hichi kimepiga marufuku, sasa kuna mvutano kati ya Kamisheni na Mji Mkongwe ya utalii kutoa vibali, marufuku yale yameondoshwa, watu waendelee kujenga yale mahoteli. Chombo hichi hichi kilipiga marufuku na suala hili niliuliza mimi katika masuala na majibu, sasa naona hii hali na kasi inazidi kuendelea na mmong'onyoko wa maadili unapungua Mji Mkongwe. Kwa hivyo, nataka kujua marufuku yale yapo au bado wanaendelea kutoa vibali kutoka Kamisheni ya Utalii, mahoteli yaendelee, ndiyo hoja yangu, sio majumba mabovu Mji Mkongwe, majumba yapo mabovu na wengine wakidai hawayapati mpaka leo.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani labda nikusaidie nilivyomfahamu kwamba majumba yanayohamwa na Mawizara hayawezi kuachwa kukaa shetani, wanakuja watalii wanayatengeneza yanafanywa mahoteli na wengine watalii ndio wanapenda kukaa katika Mji Mkongwe, ni mji wa Historia, kakujibu hivyo, tatizo nini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, tatizo vibali, zile nyumba wengine wananunua, majumba yanaendelea kufanywa mahoteli. Kwa hivyo, ule mji wetu Mji Mkongwe utakuwa haupo itakuwa ni mahoteli matupu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naomba tushirikiane na Mhe. Jaku, katika mambo mawili; la kwanza, nipe muda wa kushirikiana na wewe tuitafute hii *reference* ya katazo la kuendelea kujenga hoteli katika Mji Mkongwe, naona hili wacha nimfanyie kazi kidogo, nikishalipata hilo, namhakikishia kwamba nitaisimamia Kamisheni ya utalii isite kutoa vibali kama kuna hilo toleo hilo, ndio muhimu. Kwa hivyo, namuomba kidogo anipe nafasi kupekua pekua nikishirikiana na yeye kama ana *reference,*baadae namhakikishia kama nitafanya usimamizi wa Kamisheni ya utalii, kama ndio inayotoa vibali kuhakikisha kwamba vibali hivyo vinasita.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa sina mashaka naye hata saa tisa za usiku ukiniamsha nipo kumfuata moja kwa moja, kwa kauli hiyo, nitakuhakikishia tu Mhe. Waziri, Mhe. Waziri mwenzio alitoa katika chombo hiki na mimi nitajaribu kutafuta *reference* ya masuala yenyewe. Kwa hivyo, naomba tuendelee, sina mashaka naye hata kidogo, hata saa sita za usiku ukinambia kutoka kidole chake cha gumba mpaka uchogo unaweza kukuta mweupe, tuendelee.

Mhe. Mahmoud Thabid Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, mimi sina nia ya kumzuilia kifungu Mhe. Waziri, wala shilingi ila kwanza nampongeza sana sana kwa majibu yake mazuri yaliyokuwa na mpangilio mzuri aliokuwa akimtaja Mjumbe kila mmoja aliyekuwa anachangia, pamoja na kuinukuu *Hansard* ya Makamu wa Rais ndani ya hili Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, suali langu mimi lipo zaidi kwenye muundo wa Wizara na bahati nzuri, nilimuandikia Mhe. Waziri, lakini nafikiri kwa sababu mambo yalikuwa mengi kidogo, hili hakuliangalia. Kwa hivyo, nilikuwa naomba tu ufafanuzi wake katika muundo wa Wizara ambao mara nyingi huingia katika Idara hii ya Mipango, Sera na Utafiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mahmoud Thabid Kombo, hapa tupo kwenye Kamisheni ya Utalii, subiri Idara.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, si tupo Idara ya Mipango?

Kifungu 0201	Utawala Unguja-	1,179,684,000
Kifungu 0301	Afisi Kuu Pemba-	209,716,000
Jumla ya Fungu-		1,389,200,000

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 42 WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Kifungu 0201

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii, leo nimekukubali kweli una chaguo, lakini wakati nachangia, nilichangia kuhusu deni la *ZBC* inayosaiwa na Hatimiliki na nilitangaza nia ya kuzuia shilingi mia moja ya Mhe. Waziri, wakati Mhe.Waziri, ananijibu nilimsikiliza sana hoja zake na yeye alisema

kuwa yeye mwenyewe anadai Taasisi za Serikali kama Baraza la Wawakilishi na taasisi nyengine, lakini mimi nilikuwa nataka niseme tu kama unadai, haimaanishi kuwa na wewe usilipe deni unalodaiwa.

Mhe. Mwenyekiti, *contract* inam-*bind successor* kurithi deni, hakumvui mrithi kulipa, wanaokudai hao wengine Mhe. Waziri, *is none of my business*, lakini *issue* hapa ni deni la mirahaba ya vijana wasanii, vijana ambao nawawakilisha hapa, wavuja jasho kwa nguvu zao wenyewe na hii ni haki yao.

Mhe. Mwenyekiti: Wajumbe, mkigonga mabao, hoja hatuzisikii, kwanza mwacheni atoe hoja, halafu ndio mtashangiria, mkipiga mabao na yeye anasema hatufahamiani Mhe. Wanu Hafidh Ameir, anza tena.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, hamna tatizo wakati nachangia Mhe. Waziri, alijibu kwamba yeye mwenyewe anadai Taasisi za Serikali ikiwemo na Baraza la Wawakilishi, lakini mimi namwambia kama unadai haimaanishi kuwa na wewe usilipe lile deni ambalo unadaiwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili, *contract* inam-*bind successor* kuridhi deni hakumvui mridhi kulipa deni, wanaomdai Mhe. Waziri, hayanihusu, lakini linalonihusu ni *issue* ya deni la mirahaba ya vijana wasanii ambao mimi ndio nawawakilisha hapa, wavuja jasho kwa nguvu yao wenyewe na hii ni haki yao, lakini Mhe. Waziri. Pia, amejibu kwamba anachukua jitihada hizi tokea mwaka jana, ameniambia nachukua jitihada bajeti ikipita ataanza kulipa, sasa Mhe. Waziri, amenipuuza, sasa hivi sikubali tena, anifanye mjinga.

Mhe. Mwenyekiti: Lugha si nzuri hiyo, tumia lugha fasaha.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, alinidanganya, sijui kama vizuri Mhe. Waziri, amenidanganya mara moja, sasa mara hii sikubali anidanganye tena, mimi nitaamini vipi kwamba mara hii amesema anakwenda kushauriana na bodi ambayo ndiyo iliyomshauri mara ile kwamba asilipe kwa sababu *ZBC* inadaiwa madeni mengi, mimi nitaamini vipi kwamba ananiambia nistahamili, nivumilie, wakitoka hapa wanakwenda kukaa na bodi ile ile iliyomwambia asilipe mwaka jana ili wazungumze waone vipi itakuwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri, anipe maelezo ya kina ambayo yatanifanya niamini kwamba lile deni atakwenda kulipa ili wasanii wale waweze kupata haki yao ambayo wanaitafuta kwa jasho lao.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Wanu na watu wake ambao anawawakilisha katika Baraza lako tukufu, yeye ni kijana na vijana wengi wanashughulika na wasanii hapa nchini, sasa kuwateteya ni haki yake. Ninalomwambia kwamba mimi sijakataa kwamba sidaiwi nakubali sana Mhe. Wanu, kwamba *ZBC* inadaiwa na wasanii mbali mbali na hukunisikiliza vizuri, sijasema mimi kama *ZBC* inadai aa, *ZBC* inadaiwa milioni 700, nilivyozungumza milioni 700 ya wadai mbali mbali, deni hili mimi nimelirithi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa wanaonidai wote wakiwemo vijana wa fani hii, ninachoahidi kwamba nitajitahidi sana, mwaka jana nilipokuahidi nilikuwa sijawa na bodi bado. Kwa hivyo, baada ya kupata bodi, Mhe. Jussa, ni shahidi yule pale Mjumbe wa bodi, jambo la mwanzo nililowapa ni deni hili, la pili, maslahi ya wafanyakazi kuna mambo matano niliwapa kwa maandishi na wakaniahidi kwamba watalisimamia.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wanajitayarisha kulilipa wakapata kadhia moja mbaya sana, sasa naomba tuwape tena muda kama ninavyokwambia kwamba bodi ina watu ninaowaamini sana, mimi jukumu langu ni kuwasimamia tu, katika utendaji wa siku wa shirika, lakini kama nilivyomwambia nina Mwenyekiti wa Bodi mzuri sana yule mama na hili ameniahidi kwamba nimpe muda. Kwa hivyo, Mhe. Wanu, naomba uniamini sikusudii kufanya usanii hata kidogo, hawa wasanii wako chini yangu na wajibu wangu kuwaendeleza na ndio maana tukawajengea kumbi za kisasa iliyotugharimu shilingi milioni sita kwa kurekodia muziki pale Rahaleo, Serikali tumefanya hivyo na Wizara. Kwa hivyo, hatuna nia mbaya hiyo. Tutawalipa.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia sana Mhe. Waziri, lakini wakati Mhe.Waziri mwaka jana anatoa ahadi hapa hakujua kama yeye hana bodi, lakini pia, suala hili sio la leo, ni la siku nyingi linapigiwa kelele, mimi angalau Mhe. Waziri, angepunguza angalau milioni tano kulipa Ofisi ya Haki Miliki, ningefahamu kwamba nia ipo, lakini Mhe. Waziri, katoa kauli hapa kipindi kama hichi cha bajeti, halafu baada ya bajeti yake kupita kapuuziya, lakini mbali ya hilo, mwaka 2009 Dkt. Shajak akiwa Katibu Mkuu wa Wizara hii alilipa mirahaba na wasanii wakapata haki yao na hakuhitaji bodi wala hakuhitaji Mhe. Waziri wa Fedha kukaa nae ili kulipa na kipindi hicho wakati analipa yeye hakuwa na fungu la kulipa mirahaba hii, lakini sasa hivi *ZBC* ina fungu la kulipa mirahaba hii na hawalipi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi bado sijaridhika na majibu ya Mhe. Waziri na nataka kauli ya serikali, ama Mhe. Waziri mwenyewe aji-*commit*, ni lini *exactly date* deni litalipwa?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana lilipokuja suala hili katika Baraza lako tukufu kipindi kama hiki, ilikuwa tayari tushaanzisha Shirika la *ZBC*, tulikuwa tunasubiri Mhe. Rais amtangaze Mwenyekiti na mimi niteue bodi ishughulikie mambo tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2009 wakati huo ilikuwa ni Idara fedha yake ilikuwa inapita kwa Katibu Mkuu, sasa fedha yake haipiti tena kwa Katibu, ruzuku hii inakwenda moja kwa moja katika uongozi. Sasa mimi ku-*impose* moja kwa moja lipeni, itakuwa ni kuingilia *administrative*, kazi yangu mimi kuikamata bodi na kama walivyokwisha kunambia Wajumbe wa bodi baada ya ile kadhia waliyokuwa nayo, jambo jengine ambalo watalipa kwa haraka sana ni suala hili la Haki miliki. Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Mjumbe, aniamini sana baada ya kumaliza suala gumu tuliokuwa tunalo, suala hili tutalilipa katika kipindi kifupi kijacho. Naomba nitoe agizo mbele ya Baraza lako tukufu kwa Mwenyekiti wa Bodi na Bodi yake ihakikishe kwamba kabla ya mwezi wa kumi, angalau walipe milioni kumi katika tunachodaiwa.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, unasema?

Mhe. Mwenyekiti: Kauli Mhe. Waziri, keshatoa, umesikia?

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Kwamba.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, atalipa kabla ya mwezi wa kumi milioni kumi kwa awamu ya kwanza.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, kauli hii hii ilitoka mwaka jana kwamba atalipa kiwango kidogo ili kila hali itakapomruhusu aendelee kulipa, lakini mimi niseme nakubali na maelezo yake kwamba ilikuwa Idara wakati wa Dkt. Shajak sasa imekuwa *ZBC* na yote aliyoelezea, lakini niseme kwamba kuendelea kutumia kazi za wasanii hawa bila kuwalipa haki zao ni kosa kwa mujibu wa sheria ambayo imepitishwa hapa Baraza la Wawakilishi mwaka 2003. Wasanii wanisikilize vizuri, wana haki ya kushtaki kwa kutumia kazi zao ambazo hawapati malipo kwa kazi ambayo wanayoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mbali ya kushtaki Mhe. Mshimba ana *loby*, mbali ya kushtaki, hata wakishtaki, lakini bado ile haki yao ya msingi ambayo wanatakiwa kupata, bado watakuwa hawajaipata. Tatizo Mhe.Waziri alitoa ahadi kuwa atafanya na mwaka huu anatoa ahadi kuwa watafanya, mnawaambia nini wananchi kwamba hii ni serikali ya kutoa kauli kauli tu za ovyo ovyo. Mimi bado sikubali, nataka serikali iji-*commit exactly*, lini deni litalipwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ni serikali vile vile.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, hayo ndio maelezo ambayo ningeweza kuyatoa katika suala hili sina zaidi ya suala hili kwa mujibu wa Wizara ya Habari Utamaduni Utalii na Michezo. Nimeshaiagiza bodi mbele yako wahakikishe kwamba ifikapo Oktoba, wawe angalau washalipa milioni kumi na kila baada ya miezi 3, walipe milioni 10 mpaka limalize. Sasa baada ya *commitment* hiyo, mimi siwezi kutoa tena *commitment* nyengine ya serikali.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nimesikia Mhe.Waziri, alivyosema kwamba yeye hana majibu ya nyongeza, sasa naomba muongozo wako Mhe. Mwenyekiti. Kwa mujibu wa Kanuni 98(1) na Kanuni (6) inasema hoja ya kupunguza fungu lolote katika makadirio ya matumizi ya mwaka itatolewa wakati kifungu kinachohusika cha fungu hilo kitakapokuwa kinajadiliwa na Kamati kwa namna ifuatavyo, lakini kifungu 6(e), ikiwa baada ya hatua iliyoelezwa hizo hatua mbali mbali ambazo zimeelezwa katika hicho kifungu katika aya ya (f) ambayo kinasema maamrisho ya aya ya (e), yatatumika pia endapo Mjumbe ametoa hoja ya kupunguza fungu kwenye Kamati ya Matumizi na ambapo Mhe.Waziri, anayehusika au kiongozi wa shughuli za serikali kwenye Baraza anaweza kutoa ahadi ya kuondoa na kutekeleza jambo ambalo ni msingi wa hoja, lakini hoja yangu ikiwa baada ya hatua iliyoelezwa katika aya ya (f), haikukubaliwa na Mjumbe akashikilia hoja yake, basi itapigwa kura. Naomba muongozo wako.

Mhe. Mwenyekiti: Uamuzi nilionao ni kupiga kura Mhe. Hamza, kaa kitako kwa sababu tayari uamuzi keshazungumza mara 4 na hakukubali, sasa Baraza liamue kwa pamoja.

Utaratibu

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Wanu, hajaridhika na maelezo ya Mhe. Waziri na sasa hivi tunaelekea kwenye kupiga kura. Sasa suala hili lilikuwa linaonesha Mhe. Wanu, kidogo hakumpata vizuri Mhe. Waziri, kwa sababu hoja ya Mhe. Wanu, anasema kwamba alau walipwe japo kidogo. Mhe. Waziri, kakubali kwamba ndani ya miezi 3, kamuagiza Mwenyekiti wa Bodi walipe alau milioni kumi. Sasa ina maana sisi tukipiga kura tutakuwa tunapiga kura kitu, kwa sababu Mhe. Waziri, kakubali, maana yake sisi huku tunatakiwa vile vile tumsaidie Mhe. Wanu na yeye katika hoja yake, lakini hoja ya Mheshimiwa ili wale wasanii walipwe, kwa sababu katika suala hili hata na sisi wengine tulilizungumza. Mhe. Waziri, keshasema alau ndani ya miezi, yaani kabla ya mwezi wa Oktoba, alau waanze kulipwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa labda hili Mhe. Wanu, yeye hataki kwamba hizi milioni kumi zilipwe ndani ya hii miezi mitatu, pengine labda hakufahamu vizuri, maana yake pale walikuwa wanamsemesha semesha kidogo. Sasa labda Mhe. Wanu, angelijaribu kufahamu hii hoja, kwa sababu tusije tukapiga kura tukaharibu kila kitu. Hii ndio hoja yangu, maana yake tunataka tunapopiga kura tunapiga kura kwa kuwaokoa wasanii. Mhe. Waziri, keshakubali kuwaokoa wasanii, sasa sisi tunapiga, maana yake kura yangu mimi sitaki iharibike. Sasa kidogo labda kabla ya kwenda kwenye kura, tungelipata maelezo ya ziada kwa Mhe. Wanu, kwamba hii kabla ya Oktoba kulipwa milioni kumi, yeye hajaridhika nayo au vipi, ili tunapopiga kura, tujue tunapiga kura ya kitu gani. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Wanu Hafidh Ameir, hoja umeifahamu sasa kwa msaada wa Mhe. Hamza?

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru, lakini sikujua kama *backbenchers* pia wanajibia serikali. Inaonekana Mhe. Hamza, ule Uwaziri bado unamfukuta.
Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana kwa hoja aliyoitoa Mhe. Hamza mimi niseme kwamba hivi ndio ndivyo tulivyozoea kwamba Wawakilishi tunasema, serikali inatoa majibu wanayotaka wao wanatuondosha njiani. Kwa hivyo, ninakubali Mhe. Waziri, lipa milioni kumi huku akitafuta namna kumalizia zile nyengine zilizobaki.Tuendelee.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, nashukuru sana, naomba niwapongeze pia watendaji wa Baraza la Wawakilishi, maana *internet speed* ilikuwa kali kidogo, ndio maana nimefika huku Idara ya Mipango. Niliuliza swali moja tu dogo kwa kuomba ufafanuzi kutoka kwa Mhe. Waziri, katika muundo wa Wizara kwamba kuna hii Kamisheni ya Utamaduni na Michezo. Nadhani Mhe. Waziri, atakumbuka katika mchango wangu niliulizia kuhusu uteuzi wa Kamishna na pia niliulizia kuhusu ukubwa katika utendaji, maana hapo awali kulikuwa na Idara ya Michezo mbali na Idara ya Utamaduni. Sasa nimeuliza kwamba ukubwa wa hii inawezekana ufanisi wa utendaji usiweze kupatikana sasa ningeomba ufafanuzi juu ya hilo na uteuzi wa Kamishna mpya.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, katika mchango wake amelizungumza hili kwa maandishi na sikupata nafasi ya kulijibu, namuomba radhi kwa hilo. Kamisheni ya Utamaduni na Michezo inaongoza vyombo vifuatavyo:-

Kwanza, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale.

Pili, Baraza la Michezo.

Tatu, Bodi ya Sensa na Filamu Maonesho, na

Nne, Baraza la Sanaa.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa aliyekuwa Kamishna wake Mzee Mshindo amestaafu na Kamisheni inaongozwa na Kaimu Kamishna ambaye ni Mkurugenzi wa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, Dkt. Amina ndie anayengoza hadi hapo Mhe. Rais atakapotuteulia Kamishna mwengine.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru sana tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena nataka nimpongeze Mhe. Waziri, kwa ufafanuzi aloutoa kwa hoja zetu mbali mbali, lakini kuna baadhi ya hoja kutokana na muda tuliouweka sisi

wenyewe, inaonesha hakuwahi kupata muda wa kuweza kutoa ufafanuzi. Hoja yangu nilizungumzia kuhusu suala la bilioni 6 za mradi wa *digital* kutoka kwenye *analogue* kwenda kwenye digital. Sasa hili Mhe. Waziri naona kidogo pengine unajua mambo yalikuwa mengi na simlaumu kwa sababu sisi wenyewe ndio tulijipangia safari hii kupunguza muda.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba maelezo kwa sababu nilieleza kwamba sikuridhika kwanza nilikuwa nataka hizi bilioni sita kwa sababu katika bajeti iliyopita hatukuziidhinisha, lakini tulipata tu taarifa kwenye vyombo vya habari kwamba walimuomba Mhe. Rais, kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali alikubali, lakini bila shaka kuna utaratibu, fedha zinapotoka Mfuko Mkuu wa Serikali ninafikiri kuna taarifa ya Baraza ili tuweze kujua. Sasa utaratibu huu naona haukutumika na kwa kuwa Mhe. Waziri wa Fedha, yupo anaweze vile vile akatusaidia maelezo, lakini pamoja na hayo, lakini ile kazi iliyokusudiwa, sisi sasa hivi wananchi wengi tunaona kwamba mbona bilioni sita zimetoka, lakini mbona *impact* yake haionekani.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ndio hili ambalo nilikuwa ninaliuliza.Ving'amuzi vimesifiwa sana, lakini sasa hivi utendaji wake haviridhishi, labda Mhe. Waziri, akitoa maelezo anaweza kunisaidia.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa, kwa kuwa kazi yetu bado sehemu ndogo kumaliza na muda unataka kutukimbia ninamuomba Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, atoe hoja ile tumalize kazi iliyobakia.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu ya Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kumaliza shughuli iliyopo kwa mujibu wa Kanuni. Hivyo, naliomba Baraza lako tukufu liweke Kanuni ya muda kando ili tuweze kuendelea kumaliza shughuli mpaka hapo ambapo tutaweza kumaliza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa, niwahoji waliokubaliana na hoja wanyooshe mikono. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nilijitahidi kujibu labda Mhe. Hamza, hakuridhika na ufanunuzi wenyewe.Tulipokuwa tunapitisha bajeti ya Wizara ya Habari Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka 2012/2013, Wajumbe wa Baraza lako tukufu wengi waliielekeza Wizara kuhakikisha kwamba ifikapo tarehe 31 Disemba, wakati nchi za Afrika Mashariki zitakapokuwa zinahama kutoka *analogue* kwende *digital*, basi na Zanziar nayo ihame. Hayo ndio iliyokuwa maelekezo ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, akiwemo mwenyewe Mhe. Hamza. *Hansard* zipo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa kuitikia agizo hilo la Wizara, Serikali na hasa kwa usimamizi wa Mhe. Rais mwenyewe, iliona lazima nayo Zanzibar isikae nyuma katika hili. Kwa hivyo, akatuagiza mimi na Mhe. Waziri wa Fedha, kuhakikisha kwamba nayo Zanzibar inaingia katika zama za *digital*, kwa sababu nchi zote za Afrika Mashariki ndio zilizokuwa zinahama kwa mujibu wa utaratibu walivyokubaliana. Kwa hivyo, tulikuwa tunatafuta *means* nyingi na moja ilikuwa nipate mkopo kutoka serikali ya China, bahati mbaya tukapata maagizo na maelekezo ya watendaji kwamba mradi wa *digital* ungegharimu karibu shilingi bilioni arubaini.

Mhe. Mwenyekiti, sasa katika hali hiyo, mimi na Mhe. Waziri wa Fedha, tukaka tena chini tukaangalia kwa umakini mkubwa, tukatafuta utaratibu mwengine bahati nzuri sana, sana nasema Mhe. Mahmoud Thabit Kombo na wenzake walipokuwa katika Wizara ya Habari katika awamu ya sita, walifanya utafiti wa namna gani Zanzibar itaingia katika *digital n*a waliita Kampuni ya *Agape* mwaka 2008, wakafanya utafiti mkubwa na ripoti tunazo. Ripoti hiyo ndio iliyokuwa kigezo cha nchi yetu namna itakavyoingia katika *digital* na kwa gharama ipi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, baadae tukazialika Kampuni mbali mbali na Kampuni nne zikataka kuingia katika *digital.* Moja *Huawei* iliyotaka bilioni 40, *Star Times* iliyotaka iwe ubia isiyo tupitishe ki-*channel* tu pale, lakini miundombinu yake, *AGAPE* ikataka bilioni 4 na Kampuni moja ya Kichina ikataka bilioni 4 na kidogo. Sasa katika vigezo ambavyo viliwekwa na serikali wakati huo ni kwamba kwanza miundombinu hii iwe ni mali ya serikali, huwezi ukaiacha miundombinu hii ya *digital* ambayo ni ya muhimu sana katika *information power* ukaiachia Kampuni binafsi, lazima serikali imiliki *infrastructure* mapendekezo ya serikali haya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya kupitisha tenda hizi, Kampuni ya *AGAPE* ikapata tenda hiyo kwa sababu wao mwaka 2008 walifanya *Feasibility study* na wakatupa ripoti ambayo tunayo. Sasa tukakubaliana kwamba Kampuni ya *AGAPE* gharama ambazo wangehitaji ni dola 3,921,625, ilikuwa ndio ndogo kuliko Makampuni mengine, lakini pia, yeye ana *advantage* kama ameshafanya *Feasibility study*.

Mhe. Mwenyekiti, Kampuni ya *SONNY* ikataka dola bilioni 1,062,138 kwa kuweka mitambo, *studio* mbili Unguja na Pemba. Kwa hivyo, mradi huu wa *digital* una *component* mbili; *Component* ya kwanza, ni kujenga miundombinu (*infrastructure*) na *component* ya pili, ni ujenzi wa *Studio* mbili. Sasa Kampuni mbili tofauti ndio zikapata. Kwa hivyo, *AGAPE* yeye alikuwa na ushirika na Kampuni moja inaitwa *Electronic* ya Afrika ya Kusini ya kujenga miundombinu. Miundombinu iliyokuwa inataka kujengwa imejengwa katika eneo la Rahaleo, Muyuni Unguja imewekwa miundombinu, Masingini imewekwa miundombinu, Nungwi, Kichunjuu Mkoani, Mkoroshoni Chake Chake na Bungala.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, *infrastructure* tayari ipo imejengwa, lakini *construction* ni mwengine na ku-*operate* hii mitambo ni suala la pili. Sasa bahati mbaya *digital technology* ni jambo jipya sana, mafundi wetu wengi walikuwa hawana maarifa nalo. Sasa tukafikia pahali kwamba huenda tukishajenga, lakini tukawa hatuna uzoefu wa kuiendesha. Kwa hivyo, tutakubaliana tena na mjenzi kwamba tumpe mkataba wa uendeshaji kwa muda wa miaka miwili.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hicho yeye mwenyewe ndiye ataleta ving'amuzi kwa gharama zake na atatufunzia watu wetu wakiondoka miaka miwili watakwenda. Kwa hivyo, tukakubaliana mikataba yote hii miwili ule wa kuweka mitambo na ule wa uendeshaji imetiwa sahihi kwa msaada wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, mitambo imewekwa na *operation* imeanza, kama nilivyosema mwanzo kwamba mitambo hii ilikuwa *designed* kwamba mawimbi yasafirishe kwa mkongo wa Taifa, ndio hasa tulivyokubaliana mwanzo lakini ulipochelewa uanzishwaji wa matumizi ujenzi ulikamilika, lakini na wao uwazishwaji wa mkongo wa Taifa tukaona lazima tuingie katika matumizi na tukatumia hizi *microwave* ambazo zipo zinafanya kazi na kusafirisha mawimbi. Kwa hivyo, mitambo inafanya kazi vizuri na iko makini na ni kwamba mujibu wa taratibu tulizojiwekea.

Mhe. Mwenyekiti, ili kutukabidhi kuna kitu kinaitwa *acceptance certificate* mpaka sisi wenyewe tujiridhishe kwamba *every thing is okay*. Jambo hili linafanyika hivi sasa wahandisi wetu na wahandisi wao wanapita kituo baada ya kituo kuangalia baada ya kufanyiwa majaribio yote haya muda wa mwaka mmoja kuangalia vipi inavyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba jambo hili ni jambo geni kidogo linahitaji ujuzi mkubwa, teknolojia hii ya *digital*, ni mpya kidogo inahitaji ujuzi mkubwa na kwa hivyo, tunaamini kwamba baada ya muda *contact* ikishamaliza hiyo *operation*, basi miundombinu ipo na vijana wetu watakuwa wameshakuwa tayari vyakutosha kuweza kuiendesha mitambo hii kwa ujuzi kabisa na tunaweza tukafanya lolote baada ya hapo yeye akiondoka kwa mujibu wa mikataba hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo niliyotaka kusema ni hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu pesa tumepata wapi, serikali kwa sababu ya umuhimu huo ikaamua kutoa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na kwa sababu sisi katika bajeti yetu tuliadhimia kwamba suala hilo tutalitekeleza kama ambavyo Waheshimiwa Wawakilishi, wametuagiza. Kwa hivyo, utaratibu sidhani kama upo kwamba pesa zimetoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali Baraza liarifiwe, nadhani tukishapitisha kama fungu hili, ndio fungu la Mfuko la Mkuu wa Serikali, basi serikali inayo utaratibu mzuri wa kutumia fedha zile kwa sababu tayari itakuwa zishapitishwa na Baraza lako tukufu.

TAARIFA

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo kuweka *record* sawa alizosema Mhe. Waziri, kwa sababu na mimi kanitaja kwa jina ingawa Mhe. Waziri wangu yuko pembeni yake karibu zaidi Mhe. Ali Juma Shamuhuna, aliyekuwa Mhe. Waziri wakati huo. Alisema utafiti umefanywa na *AGAPE*, utafiti wakati huo haukufanywa na *AGAPE*, utafiti ulifanywa na *Zanzibar Broadcasting Commission* (Tume hii ya Utangazaji ya Zanzibar) ikishirikiana na *TCRA* (Tume ya Mawasiliano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) ambapo utafiti huo ulifadhiliwa na *ITU* (Shirikisho la Mawasiliano Ulimwenguni) pamoja na *UNESCO* na utafiti huo bahati nzuri ripoti yake ipo. Haikuhusishwa Kampuni yoyote binafsi katika utafiti huo, ila hivyo ni vyombo vya kiserikali na ni mashirika ambayo mengine yako katika Umoja wa Mataifa, yaani Mashirika ya Kimataifa hayo.

Mhe. Mwenyekiti, pili, baada yakufanyika utafiti huo walialikwa watu ambao ni *interested parties (expression of interest*) na mmoja wapo miongoni walioalikwa, ndio walikuwa *AGAPE*, akaja na *Star Times* na wengineo ambao Mhe. Waziri, amewataja na katika utafiti huo ilionekana kwamba *AGAPE* ndio alikuwa rahisi kuliko wote, lakini sio kwamba kwa urahisi ule ndio anaweza kufanya mambo yote.Kwa hiyo, utafiti ulifanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikishirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu na wao wakati huo walikuwa wakifanya pamoja na kufadhiliwa na Mashirika hayo ya Umoja wa Mataifa. Naomba niweke sawa hapo tu, maana jina langu limetajwa kwenye *AGAPE*.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, chombo hiki kwa kweli ni chombo kikubwa sana na mimi nawaomba tu wenzangu Waheshimiwa Mawaziri, tunapokuwa tunahoji masuala kama haya, basi vizuri kama wale *Stakeholders* wapo ambao walioshiriki katika mambo mbali mbali wakashirikiana nao moja kwa moja ili hizi taarifa zisiwe zinagongana gongana, lakini pamoja na hayo, mimi hoja yangu Mhe. Waziri, hii moja kwa kuwa amesema hawa *AGAPE* ndio waliopewa hiyo kazi na bado hawajaikabidhi serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, ile hofu yangu sasa hivi nimejaribu kuanza kuipunguza kwa sababu najua ndio bado wanaendelea na hizo *processes*. Kwa hiyo, tunaendelea kufuatilia Mhe. Waziri, labda anaweza akatwambia tu katika mkataba wao ni muda gani ambao wamekubaliana, watakuja kukabidhi hiyo kazi, lakini hoja yangu zaidi iko hapa kwamba fedha zilitoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambazo katika bajeti ambayo Mhe. Waziri, alikuja kuisoma hapa zilikuwa hazimo katika bajeti ile na sisi kutokana na kuumwa na vyombo vyetu vya habari na tukaona kwamba sisi kuja kuachwa nyuma watu wanaondoka kwenye *analogue* wanakwenda kwenye *digital,* sisi tuko kule kule, ndio maana tukajaribu kumshawishi Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa namshukuru Mhe. Rais, alikubali kutoa fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali, lakini hoja yangu baada ya kutoa fedha zile kwa sababu hapa chombo hiki kinaendeshwa kwa mujibu wa Katiba, lakini vile vile na Kanuni. Ukiangalia Katiba ya Zanzibar kifungu 106, naomba kidogo nikinukuu ili twende sawa.
Kifungu 106 kinasema kwamba;

> "Ruhusa ya matumizi ya Mfuko Mkuu wa Hazina kwa sheria ya matumizi ya fedha".

Kifungu 106 (1) kinasema kwamba;

> "Waziri anayehusika na mambo ya fedha atapeleka Baraza la Wawakilishi mapema iwezekanavyo, kila mwaka wa fedha unapoanza mswada kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya serikali ukiwa na kasma zinazohusika katika shughuli mbali mbali zinazohitajika pamoja na jumla ya fedha zote zinazoombewa kwa matumizi hayo mbali na matumizi yanayohitajika kisheria kwa mwaka huu wa fedha".

Kifungu 106 (2) kinasema;

> "Inapotokea kwamba fedha zilizotumika au zinazotaka kutumika katika mwaka wowote wa fedha kwa madhumuni fulani ni zaidi ya fedha zilizoruhusiwa kisheria na matumizi ya mwaka ule; na

(b) "Kwamba fedha zilizotumika au zitakazotaka kutumika (mbali ya matumizi yanayohitajika kisheria) kwa mwaka wowote ule wa fedha kwa madhumuni yoyote yale na ambayo fedha hazikuidhinishwa katika sheria ya matumizi ya mwaka ule.Maelezo ya matumizi ya ziada au kadiri itakavyokuwa makadirioya matumizi ya nyongeza yatawasilishwa kwenye Baraza la Wawakilishi kuyakubali hayo makadirio ya matumizi ya nyongeza na maelezo ya matumizi ya ziada kutawasilishwa kwenye Baraza la Wawakilishi Mswada wa Sheria ya

Matumizi ya Fedha ya Serikali kwa ajili ya kuidhinishwa matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali na fedha hizo zitatumiwa kulipia gharama za shughuli zinazohusika katika makadirio ya maelezo hayo".

Mhe. Mwenyekiti, sitaki niende mbali kwa sababu hii Katiba tayari inajieleza na huku kwenye Kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi kifungu 101, sitaki nikinukuu kwa sababu kinarejea haya haya kwamba fedha zozote ambazo za ziada ambazo hazikupangwa kwenye bajeti ya wizara husika, basi Mhe. Waziri wa Fedha, ataleta mswada ili kuidhinisha matumizi hayo. Sio kama tunakataa fedha hizi kutumika, lakini zile taratibu za kikatiba tunasema kwamba zilikiukwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nadhani Mhe. Waziri kama walipitikiwa, basi aseme tu walipitikiwa ili sasa tukubali kwamba fedha hizi matumizi yake katika utaratibu uliokuwa halali au kama labda pengine mimi nimeisoma, vyengine hii Katiba kwa sababu najua mnaweza mkawa darasa moja, lakini kila mmoja akawa na tafsiri yake na hata wana sheria Mahakamani, Jaji huyu anaweza akaamua kesi hivi, Jaji wa Mahakama ya Rufaa akaja akatengua. Kwa hiyo, labda angenisaidia Mhe. Waziri, ili yale matumizi tukahakikisha kwamba yalikuwa ni halali kabisa. Nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Hamza, ameisoma Katiba vizuri sana na nataka nianzie na pale alipomalizia kila mmoja anaweza akaisoma na akatoa tafsiri ya kwake.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nataka niseme mwaka jana Baraza lako tukufu limepitisha bajeti na likapitisha fedha katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa mujibu wa taratibu zetu Mhe. Waziri wa Fedha, kama atatumia zaidi ya ile bajeti ambayo mmeipitisha, bajeti kuu sio bajeti ya wizara au bajeti ya kifungu ile bajeti kuu tuliyoipitisha hapa ambao mmeipitisha mwanzoni wakati nasoma bajeti yangu. Ningetumia zaidi ya ile kweli anayosema Mhe. Hamza, ningepaswa kuleta mswada hapa wa kutaka Baraza lako tukufu liidhinishe nyongeza ile, lakini kilichofanyika ni kwamba hata ile muliyoidhinisha sijaifikia, nilichofanya mimi ni kwamba nimefanya uhaulisho tu badala ya Mfuko Mkuu kutumia chini ya mfuko mkuu tumezitumia chini ya Wizara ya Habari.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ndani ya vifungu vyetu vile vile na ndani ya fedha zile zile ambazo nyinyi katika Baraza lako tukufu mmeidhinisha. Kwa hivyo, anachosema Mhe. Hamza, ningekuwa nimetumia zaidi ya kile serikali nzima haizungumzii Katiba, haizungumzii wizara, haizungumzii kifungu inazungumzia bajeti ya serikali nzima ningelazimika kuleta mswada hapa na kuomba *supplementary* bajeti, kwa vile ambavyo inavyotaka serikali. Sisi hatujafikia nimeeleza hapa wakati nasoma ile bajeti yangu kwamba mpaka itakapofika tarehe 30 June, nadhani tutafikia kama asilimia 88 tu ya ile bajeti ambayo tumeidhinishiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, Kikatiba hatujakosea kama kifungu alichokisema Mhe. Hamza, hatujakosea na kisheria ya fedha vile vile, *The Finance Bill Act* hatujakosea. Nimempa Mhe. Waziri wa Fedha, nguvu kufanya *appropriation,* ndio hiyo mnayoipitisha baadae *appropriation bill* kwamba mnanipa mimi nguvu yakuweza ku-*appropriate* kuweka katika maeneo mengine na fedha hizo kutumika katika maeneo mengine. Kwa hivyo, Mhe. Hamza, nataka nisaidie tu kwamba laiti ningeliizidisha ile bajeti siku zote, huwa sisahau ningelileta mswada hapa wakuomba idhini ya Baraza lako tukufu, lakini sijazidisha na tukaona tuwape wenzetu wa Wizara ya Habari waweze kutekeleza ule mradi wetu wa *digital*. Kwa hivyo, tuko katika *line* Mhe. Hamza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nadhani tutakapofanya marekebisho ya Katiba hii *marginal note* labda tuifanyie marekebisho na kwa sababu Mhe. Waziri, jinsi alivyosema yeye ingelikuwa kwamba tunahitaji matumizi ya ziada zaidi ya hata yale matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali, lakini hayo mimi nafikiri sijui tungeliyapata wapi kwa sababu tunapopitisha bajeti ya serikali *lump-sum* pamoja na Mfuko Mkuu wa Serikali, lakini hii *marginal note* inasemaje? Inasema ruhusa ya matumizi ya Mfuko Mkuu wa Hazina kwa sheria ya matumizi ya fedha. Kwa hiyo, ina maana hapo kwa tafsiri inaonesha kwamba fedha zinapotoka Mfuko Mkuu wa Serikali ndio kifungu hiki kinachotoa ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, ndio maana nikasema labda pengine katika suala zima la tafsiri, lakini unaposema ruhusa ya matumizi ya fedha, ina maana sisi tunavyojua kwamba zile fedha za Mfuko Mkuu wa Hazina zinapotaka kutumika, ina maana kuwe kuna taarifa inakuja Barazani au mswada unakuja Barazani kwa ajili ya taarifa ya ziada. Sasa mimi nadhani kama nilivyosema sina wasi wasi kwa sababu kama alivyosema Mhe. Waziri, kwamba mpaka sasa hivi kwamba zile fedha zinaendelea kutumika vizuri na kwa kuwa ule mradi haujakabidhiwa, lakini hoja yangu ilikuwa katika eneo hili. Sasa labda Mhe. Waziri, anisaidie tu hii *marginal note* iko sawa sawa, kwa sababu hii *marginal note* ndio niliyotafsiri mimi na ndio nikaona kwamba kuna fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali kwa matumizi ya ziada.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi ndio hoja yangu iko hapo, kama anahisi kwa yeye iko sawa, basi nitakuwa sina matatizo, lakini kama itakuwa haiko sawa, basi tutakapofanya marekebisho ya Katiba, mimi nafikiri kwenye *marginal note* labda tuje tuelezane vizuri, lakini pamoja na hayo Mhe. Mwanasheria Mkuu, nadhani ipo haja yakufanya semina ya kuchambua hizi Katiba ili hizi tafsiri tuweze kuzipata vizuri. Sasa Mhe. Waziri wa Fedha, nadhani nilikuwa naomba anisaidia hii *marginal note* na tafsiri yangu mimi iko sahihi au ina matatizo kidogo. Ahsante na tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza, maelezo yalitolewa, lakini sasa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na yeye ataongezea.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwanza katika utaratibu wa sheria *marginal note,* siku zote huwa hazitumiki, *marginal note* zimewekwa kusaidia tu kujua kifungu kile kinazungumzia nini. Kwa hivyo, huwezi kutafsiri *marginal note* katika misingi hiyo. Hili ni msaada tu katika *marginal note* yoyote ile katika sheria na katika Katiba. Kwa hivyo, *marginal note* hii haina maana yoyote kisheria, hii ni kisaidizi cha kuona kwamba kifungu hiki kinazungumzia mambo haya. Hiyo ni ya mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, pili, ni kwamba katika tafsiri ya *supplementary budget* inakuja ikiwa utatumia ziada ya fedha ambazo zimeombwa. Kama tumeomba shilingi X, tumeshazitumia X na tunataka kuongeza Y ambazo zile hazikuidhinishwa na Baraza. Kwa hivyo, pale lazima ulete *supplementary budget* ili kuruhusu pesa zile zitumike, lakini katika matumizi haya fedha hizi zilizotumika zilikuwa zimeshakuwa *approved* na Baraza wenyewe. Kwa hivyo, ilikuwa haina haja ya kupeleka *supplementary budget* kwa misingi hiyo. Nakushukuru Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani sitaki tupoteze muda, lakini hili suala iko haja tuje tuliangalie upya.Kwa sababu fedha zimeshatumika sasa hivi tunaangalia *value for money,* lakini zaidi katika matumizi haya ya Mfumo wa Mkuu wa Serikali, nadhani tuje tukae tuelezane vizuri, fedha hizi zinavyotoka na kwa utaratibu gani? Kwa sababu hapa mimi hujiuliza uletwe Mswada Baraza la Wawakilishi, hapa ingelikuwa angalau ile bajeti kuu ya serikali labda tumeimaliza, lakini kama nilivyosema tuendelee nitakuja kutaka ushauri wa pamoja Mhe. Waziri wa Fedha, Mhe. Mwanasheria Mkuu na Waziri wa Katiba na Sheria waje watuelimishe vizuri namna gani ya fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali zinavyotumika na ile idhini ya Baraza la Wawakilishi inatakiwa iwe vipi.

Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0201 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti- 120,305,000
Kifungu 0201 Afisi Kuu Pemba-

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na vifungu vingi niliviombea maelezo, lakini naviachia kwa hoja ya kwamba naamini atavisimamia kama nilivyomwambia mapema Mhe. Waziri, lakini kuna kifungu kimoja nilikuwa naomba hiki anipe maelezo kidogo katika Ofisi Kuu Pemba, nacho ni kifungu kilichoko katika ukurasa wa 346 katika eneo lililopewa namba 311100, Mali isiyohamishika chini ya kijifungu kidogo cha 311101, Ujenzi wa Majengo Mapya, pana jumla ya shilingi 643,400,000.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri, ikiwa yeye, ikiwa Mhe. Waziri wa Fedha, anisaidia kwamba ninavyofahamu mimi kwa ugeni wangu katika chombo hiki na masuala haya ya bajeti ni kwamba hii ingepaswa kuwa ni *capital budget*. Sasa kuiona katika fungu la matumizi ya *recurrent,* ujenzi wa majengo mapya kidogo imenipa tabu. Isipokuwa kama imekusudiwa vyenginevyo kuliko vile ambavyo imeandikwa hapa na bahati mbaya kile kitabu cha Mhe. Waziri, sikuliona hili likifafanuliwa vizuri. Hebu anisaidie kwamba huu ujenzi wa majengo mapya kwa sababu kama ni jengo jipya nilitegemea ningekuta katika bajeti ya maendeleo, kwa nini imeingizwa katika fungu la *recurrent,* nisaidiwe maelezo kidogo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, nilijaribu kumjibu Mhe. Ismail Jussa Ladhu, wakati natoa majumuisho, kwamba tumeamua kuweka kifungu hiki hapa kama ambavyo mwaka jana katika kifungu chengine, tuliweka kifungu kama hiki kwa ajili ya uwekaji wa Mpango wa Uwekaji wa Nyasi Bandia hapa Unguja. Sasa shughuli inaweza ikaweko katika mradi wa maendeleo au pesa hizi za kawaida. Kwa hivyo, sisi tumeamua kuziweka pesa hizi hapa ili tuweze kuzitumia kwa ajili ya uwekaji wa *darning a track* katika kiwanja cha Gombani Pemba. Kiwanja kile kina tatizo hilo kwa muda wa siku nyingi

tulipata ushauri wa kutia lami, tukaona zama hizi kutoa lami tena haipendezi lami inatiwa barabarani, lakini kuweka kwenye viwanja itakuwa haiwezekani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, tukaweka pesa hizi hapa na tunaamini kwamba tutalikamilisha kama vile tulivyokamilisha suala la nyasi bandia, basi na hili *Inshaallah* tutalikamilisha katika fedha hizi ambazo tumeziweka. Tumeamua kuweka fedha zetu *other charges* katika eneo moja ambalo unaweza ukaziona vipi zimetumika kwa manufaa zaidi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru, lakini niombe tu, kwa sababu hili mara nyengine linaweza likatuletea matatizo kwamba uandishi wa hivi vijifungu, nafikiri umefika pahala Wizara ya Fedha kwa jumla uviangalie. Kwa sababu ni kweli pengine zinarefushwa muda mrefu bila ya sababu hapa, kwa sababu tu ya maelezo ya kifungu namna yalivyokaa, maana ukinambia mimi *construction of view building* na *other structures* au ujenzi wa majengo mapya, maana yake ni kuweka nyasi bandia kidogo, napata tabu, pamoja na kwamba nilipasi Kiswahili na Kiengereza nilipokuwa *Form IV* na *Form VI*. Kwa hivyo, nashukuru Mhe. Waziri, kanisaidia maelezo haya na nikiamini kwamba zitatumika kufanyia shughuli hizo ningesema tuendele, lakini niiombe Wizara ya Fedha ivipitie tena vifungu vikae vizuri. Ahsante sana.

Kifungu 0301 Afisi Kuu Pemba- Kifungu 0401 1,278,161,000

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, niseme namshukuru sana Mhe. Waziri, katika masuala yangu haya aliyonijibu, lakini nilikuwa nataka kupata tarehe ya hiyo ziara yetu tunayotaka kwenda. Mhe. Waziri, amenijibu yuko tayari kutekeleza shauri langu nililolitoa tufanye ziara na amesema kuwa yuko tayari atawaalika na vitengo vyengine akaviainisha, Idara ya Kazi na vyenginevyo. Kwa hivyo, ningemuomba ili kuondoa tofauti ya kuambiwa asilimia zile za kutaka kumchangia kuziweka sawa. Naomba hapa kidogo aniweke sawa, nirudishe ile 20 iwe asilimia mia moja.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kama nimemfahamu vizuri, anataka niweke tarehe ya kwenda katika matembezi yetu ya hoteli maeneo ya Kiwengwa. Kama hivyo ndivyo, basi tufanye labda siku ya Kuvunja Jungu, tutembelee vizuri. *(Kicheko)*

Mhe Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo na yeye na kwa kuwa muda huo siku hiyo utakuwa ni muda muwafaka, kwa kuwa na yeye ili kuwasaidia wananchi wetu kuona kupata zile ajira zinazokusudiwa, hakuna tatizo. Kwa hilo naomba tuendelee na mimi namsubiri tarehe hiyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilisema tuangalie maslahi ya wafanyakazi hasa *ZBC*, tumuangalie yule kijana muda gani kasimama pale, tumuangalie huyu mama kasimama muda gani kutufanyia kazi nzuri Waheshimiwa humu ndani maslahi yao angalau kwa hawa wanaokuja hapa tu katika Baraza la Wawakilishi, wachangiwe posho angalau kwa kile Mjumbe shilingi 20,000. Naiomba serikali itoe kauli kwa suala hili.

Mhe Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nafahamu hisia za Mhe. Mwakilishi na kwamba Mheshimiwa ni mtu mwenye huruma sana. Kwa hiyo, naomba atuachie kidogo kwa sababu mara mbili nishakwenda kwa Katibu wa Baraza kumuomba kwamba sawa suala la Baraza kulipa *ZBC* halijawa tayari, lakini angalau unaonaje Katibu hawa wafanyakazi wanaofanya kazi hapa *ZBC* wakaingia katika *roster* ya maposho ya Baraza. Sasa Katibu ananambia linazungumzika. Kwa hivyo, linatughasi na Mhe. Mjumbe ndio ukaona tunalishughulikia na pia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Dodoma alituita Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, akatupa agizo kwamba lazima tukae tuangalie namna gani ambapo Baraza la Wawakilishi na *ZBC* litafanya masuala ya malipo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, tuna agizo la Mheshimiwa yakikamilika haya, ama mambo mawili hili linaweza likaanza mwanzo au hili, lakini kwa vyovyote vile tutajaribu kuhangaika katika njia hizo tatu, ama suala la kukubaliana na uongozi wa Baraza, hawa vijana kulipwa katika *roster* ya Baraza, kama hilo halikuwezekana, basi mpango huo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ametupa kazi, kama haujawa, basi tutaendelea kujibanabana zile tunazopata *ZBC* kuwapa chochote, lakini ilimradi wapate chochote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, niendelee tena kumshukuru Mhe. Waziri kwa umakini wake, lakini uzuri wenyewe serikali yote nzima ipo hapa na ikitoka hapa, ndio ishatoka. Mimi nataka kauli watalipwa

lini hawa watu wanateseka sana, Mhe. Waziri wa Fedha yupo, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yupo, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais yupo, hawa walipwe ikitoka hapa, imetoka, tujue hapa hapa tunawasaidia vipi, kazi nziti wanayoifanya. Mhe. Waziri, nafikiri kazi itatoka mbele huku kwa Mhe. Waziri wa Fedha au Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, acha kwanza tuisikilize serikali kuhusu vijana hawa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, naomba pia nitoe maelezo ya ziada kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Ni kweli waandishi wetu wa habari ambao wanakuja hapa kutuchukulia taarifa na wanaziwasilisha vizuri, wanafanya kazi nzuri, kwanza napenda tuwapongeze kwa kazi kubwa wanayoifanya.Vile vile, nimpongeze Mhe. Jaku Hashim na Waheshimiwa wengine ambao wamekuwa akiwazungumzia sana, vijana hawa kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Jaku Hashim Ayoub, atustahamilie kwa sababu kama alivyosema Mhe. Waziri, tumepewa agizo la kulifanyia kazi jambo hili na naamini tutalipatia ufumbuzi mzuri na kadiri ya ufumbuzi tutakaoupata itakua ni jambo ambalo litawapa nafuu kubwa watangazaji wetu hawa. Kwa hivyo, naomba atukubalie tuendelee na bajeti yetu hii, huku tukilitafakari kwa kina jambo hili ili tatizo hili liweze kuondoka na tuliondoe lisirudie tena hapa katika Baraza letu tukufu.

Mhe Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, tusiwe na huruma ya mdomo, tuwe na huruma ya vitendo, serikali kumlipa shilingi 20 elfu kijana yule na redio kweli tukashindwe! Tusiwe na huruma ya mdomo, tuwe na huruma ya vitendo, tukose shilingi 20 elfu, basi japo shilingi 15,000, Mnadhimu wangu ananambia, basi japo shilingi 10,000, natii amri ya Mnadhimu wangu wa chama shilingi 10,000. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, umejibiwa na serikali inalifanyia kazi, hilo suala hawezi mtu akatoa pesa sasa hivi. Baraza barua imeletwa, Kamati ya Uongozi itakaa itaamua, serikali itaamua, lazima jambo lifuate utaratibu.

Mhe.. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, itabidi na mimi nitumie Kanuni ya 98, tupige kura humu kama kweli serikali inashindwa na shilingi 10,000, hilo tuone haya, hawa watu wanateseka sana.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Kamati ombi wanalo, hawajaamua bado, tena Kanuni ya nini au huelewi? Mhe. Jaku Hashim Ayoub, hebu nisikilize vizuri, tunasema hilo suala limeletwa, makisio yapo katika Baraza la Wawakilishi na serikali wanayo, Kamati ya Uongozi itakaa itaamua na wewe utashirikishwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hayo ndio majibu ya Mawaziri, siku zote tukitoka hapa tushatoka, hatuna pakuwatetea hawa watu, kwa kweli shilingi 10,000 inashindwa serikali kulipa, tuone haya. Haiwezekani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo ya ziada, naomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub, aelewe kwamba serikali hii haijawahi hata siku moja kuwanyima haki zao wafanyakazi. Imekuwa ikichukua kila jitihada kuhakikisha tunaboresha mishahara ya wafanyakazi wetu na tunafanya kila namna kuweka posho mbali mbali ili kuwapa moyo watendaji wetu. Nataka Mhe. Jaku Hashim, aelewe kwamba hakuna umuhimu wa kuchangishana sisi wenyewe na hatujawahi kuchangishana katika kulipa posho mbali mbali, kwa sababu dhamira njema ya serikali ya kufanya mambo hayo, tushafanya mambo mengi na tunaona wazi wazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, aelewe imani aliyonayo yeye, ndio imani hiyo hiyo inayo serikali, si vyema wakati mwengine kusema maneno ambayo hata kama tuna nia njema kiasi gani, ukawa unavunja moyo ile dhamira yetu, ni vizuri aelewe dhamira yetu ni kufanya mambo mengi kama alivyokuwa na dhamira yeye, si vizuri unapokuwa na dhamira njema ya kufanya mambo mema, halafu Mhe. Mwamkilishi kama Mhe. Jaku Hashim, anatuvunja moyo katika kufanya wema huu, ni vizuri akubaliane kwamba nia yetu ni njema na jambo hili litafanywa na ndio maamuzi ya serikali. Naomba avute subira kwa sababu jambo lolote lina utaratibu katika kukamilishwa kwake.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, aniombe radhi, mimi siwavunji moyo, hawa nawatetea kama kuvunja moyo, anavunja moyo yeye sasa. Sasa kama sikuwatetea humu nikawatetee wapi, yeye ajibu tu kama nishafanya haki, washanisikia wenyewe kama serikali haina uwezo wa kulipa, basi mimi nitakuwa nishatetea na wenyewe washasikia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, masuala yamesemwa, sasa hivi serikali imesema inao uwezo, inafanya utaratibu wa kulipa, wewe unasema haina uwezo vipi na serikali imesema inatayarisha utaratibu walipwe, wewe unasema kama haina uwezo!

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, kanambia mimi navunja moyo, wakati si kitu cha kweli kwamba nawavunja moyo, mimi nawatetea. Tuendelee.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kuzuia fungu, lakini nilikuwa nataka kuongezea hapo hapo. Wakati nachangia hotuba hii nilizungumza hawa ambao wako ndani na wale ambao wako katika chumba cha mitambo, ambao huwa wanapigwa na baridi na wanalalamika kwamba hata ile pesa ya maziwa hawapati. Sasa namshukuru sana Mhe. Waziri, kwa kauli yake nina imani kwamba serikali itawafikiria na watapewa posho, lakini na wale ambao wako katika chumba cha mitambo, nashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante serikali imesikia tunaendelea.

Kifungu 0401 Idara ya Utumishi na Uendeshaji-	1,127,035,000
Kifungu 0402 Chuo cha Habari-	254,810,000
Kifungu 0403 Kifungu hiki kinarekebishwa na kisomeke	
Shirika la Magazeti ya Serikali-	592,726,000
Kifungu 0404 Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar-	419,029,000
Kifungu 0701 Idara ya Habari Maelezo-	

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, mimi niliuliza swali dogo tu hapa baada ya tukio la hivi karibuni katika timu moja wapo iliyokuwa ikisafiri kwenda nje, mimi nilishiriki katika kuwatafutia bendera, ninajua Idara hii ndiyo iliyokuwa inashughulikia masuala ya kuuza picha za viongozi na bendera. Sasa nilimuuliza Mhe. Waziri, kwamba je, bendera zinaendelea kuchapishwa ama kutengenezwa na Idara hii? Kama zinafanywa hivyo, urahisi wake wa kupatikana uko vipi? Kwa sababu bendera za nchi za nje zinapatikana kwa wingi zaidi hapa Zanzibar kuliko bendera yetu ya Zanzibar. Sasa niliuliza swali hilo na naona sikujibiwa katika majumuisho ya Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi umekuwa ukisema kwamba sisi tunapotoa majumuisho Waheshimiwa Wawakilishi, wawe wanasikiliza majumuisho yenyewe, sasa mimi nimejibu vizuri na naomba nimjibu tena kwamba Idara ya Habari Maelezo ina jukumu la kuchapisha picha za viongozi, lakini bendera zinachapishwa Bohari Kuu iliyopo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kwa hivyo, narudia kwamba si jukumu la Idara ya Habari Maelezo kuchapisha bendera.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, naamini Bohari Kuu na Wizara yao husika wamelisikia hilo kwa sababu bendera za nchi yetu ya Zanzibar hazipo na hazipatikani hivi sasa. Juzi tulihangaika sana aliyetusaidia ni Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis kwa kutuazima bendera yake ambayo ilikuwemo Ofisini kwake na timu hizi zote zinazokwenda nje kuwakilisha Zanzibar kama nchi huwa zinatakiwa kuwa na bendera zake. Nashukuru sana.

Kifungu 0701	-	Idara ya Habari Maelezo-	350,333,000
Kifungu 0702	-	Tume ya Utangazaji-	201,499,000
Kifungu 0703	-	Idara ya Habari Maelezo Pemba-	30,495,000
Kifungu 0704	-		

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa fursa. Nilipochangia kwa maandishi kwa Mhe. Waziri, niliomba kutaka kujua suala la kile kipindi cha michezo ambacho kilikuwa kinaoneshwa kila Jumamosi na ikawa kimekatika. Sasa Mhe. Waziri, alipokuwa akijibu alisema kwamba watakifanyia utaratibu. Kipindi kile kimo ndani ya *program,* toka mwanzo ilikuwa inaonesha kila wiki, ikawa wiki tatu, sasa hivi hakioneshwi kabisa. Je, kuna matatizo gani yaliyosababisha hilo litokezee. Mhe. Waziri, naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu vizuri Mhe. Mahmoud, mimi nilidhani labda kipindi cha michezo cha redio, maana redio kuna kipindi cha michezo pia ambacho kinatoka. Kwa hivyo, nilimjibu suala langu hilo. Sasa katika *ZBC* taarifa niliyonayo ambayo nimepewa ni kwamba wamejaribu kufanya mabadiliko ya mfumo wa vipindi. Sasa hilo ndio jambo ambalo

linaathiri. Wacha tuliangalie vizuri zaidi, lakini walikuwa wanaangalia wakati gani mzuri zaidi wa kukitoa kile kipindi. Kwa hivyo, bado wamo katika hiyo *format*, sasa wakiwa tayari watatoa vipindi vyengine na mabadiliko ya vipindi vingi ambavyo wanajaribu kuvitayarisha hivi sasa vipo pamoja na kipindi hichi cha michezo.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kipindi hichi kusema kweli vijana wengi wanakipenda sana hususan wanamichezo na vijana wengi walikuwa hawapendi kuangalia *TV*. lakini wamevutwa kutizama *TV*. Zanzibar kwa sababu ya kipindi hichi. Kipindi hichi kilikuwa kikisimamiwa na kutangazwa na ndugu yetu Farouk Karim, pamoja na kijana wetu Adam Natepe pale kwenye maeneo yetu. Sasa taarifa tulizonazo ni kwamba kipindi hichi kimekatishwa kutokana na kwamba wao wenyewe *ZBC* hawana watu wa kuweza kuendeleza, lakini kuna watu ambao wao wamejitolea na wapo tayari kuendelea na kipindi hichi. Sasa sijui hii Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha hichi kipindi kitakuwa kinaendelea na watu wa Zanzibar wataendeleza kupata taarifa za kimichezo kupitia *ZBC* Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tunazungumza lugha moja na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa. Nimekubali kwamba hichi kipindi cha michezo ni muhimu kwa vijana wetu, lakini pia kuna umuhimu wa kukiendesha kwa vizuri zaidi, ndio kazi ambayo inafanywa *ZBC* hasa na Mkurugenzi mwenyewe. Kwa hivyo, kinataka kifanywe katika *format* zaidi ili kiwe na tija zaidi. Kwa hivyo, atupe muda Mheshimiwa si muda mrefu tutauelekeza uongozi kwamba katika mageuzi ambayo inafanya, basi hili waliharakishe ili watoe kipindi ambacho kwa mujibu wa mageuzi yenyewe, lakini kwa mujibu wa vijana wanavyohitaji. Hivi sasa bahati nzuri kuna hili Kombe la Dunia. Kwa hivyo, wachukue muda huu ambao vijana wameshughulikia Kombe la Dunia wamalize mageuzi yao ili baada ya kombe hilo kipindi kitoke vizuri katika *format* ambayo vijana wanahitaji. Hili tutalifanyia kazi.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, katika kazi ambayo walikuwa wakiifanya ndugu yetu kina Farouk Karim, pamoja na Adam Natepe ilikuwa moja ni kutoa tathmini ya michezo hususan kama hili Kombe la Dunia ambalo kwa sasa linaendelea. Sasa ni sababu zipi hasa zinasababisha wakati kombe linaoneshwa, wale vijana ambao walikuwa wakijitolea wakakatishwa, wakati haya mambo mazuri na matamu yanaweza kufanyika na watu ambao wapo katika nchi yetu hapa hapa Zanzibar au kuna tatizo la malipo? Watwambie tuweze kufahamu vizuri zaidi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, huu utamu ambao Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, anauona atauona vizuri zaidi baada ya hii kazi ambayo inafanyika. Kwa hivyo, atupe nafasi hiyo tumalize ataona raha zaidi.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa nikichangia katika Shirika hili la Utangazaji nilisema ili mafanikio yapatikane na tuweze kuwa hewani katika vyombo vyetu vya redio au *TV*, ni lazima kuwe na watu ambao wanaitwa mafundi mitambo. Nimshukuru Mhe. Waziri, kwa majibu yake mazuri ambayo alinijibu akasema wale mafundi wakuu ambao wataalamu wao tayari wameshaongezwa yale mafao ambayo tunayapigania, lakini wale mafundi wadogo wadogo akaniambia wao bado, lakini serikali nayo pia imejipanga ipo katika mpango wa kushughulikia katika mwaka huu. Nilitaka tu uthibitisho zaidi kwa sababu Mwenyezi Mungu anasema katika kitabu chake kitukufu *Wa aufu bil ahadi inna l ahada kana mas'ul"*, yaani na tekelezeni ahadi zenu, hakika kila ahadi mtakwenda kuulizwa. Nilitaka kujua tu na hawa mafundi wetu wadogo wadogo na wao serikali inawaangaliaje katika mtazamo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia, niishukuru *ZBC* katika hata zile kamera na wao sasa tushughulikie kuhusu usafiri ili waweze kutupatia habari moto moto. Nataka majibu kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba Mhe. Panya Ali Abdalla, ni mdau mzuri sana wa *ZBC*. Mimi nikikaa mwezi kama sijapata ushauri wa Mhe. Panya, katika suala la ku-*improve ZBC*, basi ni jambo la ajabu sana, lakini mwezi haufiki lazima ataniambia pale kidogo rekebisheni, pale rekebisheni na mara nyingi ninapopata ushauri wake, basi najaribu kuufanyia kazi na humwambia kwamba kwa kweli ushauri wako tumeuchukua tunaufanyia kazi. Kwa hivyo, hili suala la mafundi ni kweli kama nilivyokiri pale kwamba maslahi yao hawa ambao hawana vyeti, si mazuri, lakini kuna taratibu la kwanza bodi yenyewe katika kikao cha kwanza wameshughulikia masuala ya *scheme of service* na muundo wao wameupitisha na upo katika ngazi mbali mbali za serikali kwa ajili ya kuthibitishwa. Kwa hivyo, naamini baada ya kupitishwa muundo huu mafundi hali yao itakuwa nzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, siwezi kumuahidi kama alivyosema mwenyewe *"Inna l ahada kana mas'ul"*. Siwezi kuahidi, halafu ahadi ile ikanirudia mwenyewe, lakini namuahidi kwamba aendelee kila baada ya muda

kama utaratibu wake kuniuliza vipi umefika, namuahidi kwamba tutapata ufumbuzi wa suala hili. Yeye ni mdau mzuri anasaidia sana kulisimamia shirika na naomba tuendelee kusaidiana. Hili ni jambo muhimu sana tutapata fungu kwa Mwenyezi Mungu kutokana na hili. Kwa hivyo, ni jambo la maana sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, nimshukuru sana Mhe. Waziri, kwanza Mhe.Waziri, huyu ni msikivu na naamini ataweza kwa kadiri ya uwezo atakaomuwezesha Mwenyezi Mungu kuwashughulikia mafundi hawa, kwa sababu mafundi wetu hawa niseme hasa kwa ukweli ni mahodari sana. Hawa ndio waliofanikisha hizo *TV.* nyengine ambazo tunaziona huko zinaonekana vizuri. Watu wengi wamekuja kusoma *TV.* hapa kwetu Zanzibar. Kwa hivyo, lazima hawa mafundi wetu tuwapongeze na juhudi ya makusudi ichukuliwe. Nakushukuru na mimi kama unavyomwambia huwa sichelewi nitakuwa nakukumbusha ili tuone mafundi wetu hawa wanafikia katika ufanisi mzuri.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, asione tabu kuona tumepiga buti kwenye *ZBC,* ujue tunaiangalia sana na tunaipenda sana. Kwa hivyo, buti zetu hizi zimo katika kuboresha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nilikuwa nataka nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, kwa ufafanuzi wake nilimsikia na pia na Mhe. Waziri, lakini Mhe. Naibu Waziri, ule ufafanuzi alioutoa yeye wa udhalilishaji, mimi wala sikuwepo katika ile ya kuvua mabuibui. Hapa kuna kadhia nyengine ambayo ndio maana nikasema watendaji hawa wa *ZBC,* hasa wale wazito wajirekebishe. Kwa sababu kuna mtu walimzuia na panga, alikuwa anataka kwenda kule. Sasa hiyo hoja kwa kuwa ameisikia naomba wao wenyewe wajirekebishe.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi nilizungumza kile kipindi ambacho sisi watu wazima huwa tunapata nafasi ya kukaa na watoto wetu. Kuna kipindi kile wanachokiita Ukiweza sijui. Kipindi kile vijana wameamua kujitolea wamekwenda pale na wanawaita vijana mbali mbali, wanakuja wanatoa mafunzo mbali mbali ya kitaaluma kabisa. Sasa walikuja kukatishwa kwa kuambiwa kwamba wanatakiwa walipe shilingi milioni 2,800,000/= kwa mwezi. Sasa kile kipindi sio cha kibiashara, kile kipindi zaidi ni cha kutoa taaluma, lakini tumeona kuna vipindi vyengine vya muziki na wanamuziki wenyewe ndio kama hivyo, sasa hivi kila ukipigwa muziki wao wanazidi kudai, lakini hivi vyengine wao hawana malipo yoyote isipokuwa ni kuelimisha.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nilikuwa namuomba tu Mhe. Waziri, labda pengine ndio katika haya mabadiliko ya *program,* lakini kwa kweli kipindi kile bado tunakihitaji, watoto wetu wanapata elimu kubwa na tunapata nafasi ya kukaa na watoto wetu majumbani tukaangalia kwa pamoja. Sasa nilikuwa kidogo tu nataka maelezo, labda pengine walipokaa na watendaji wake walijadiliana vipi kuhusu kipindi hichi. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nimemfahamu sana Mhe. Hamza Hassan Juma. La kwanza, kuhusu ulezi tutalifanyia kazi, tutakaa nao kuangalia nini tatizo na turekebishe mambo. Kwa sababu kama imefika hali hiyo, lazima kuna jambo ambalo linahitaji kurekebishwa. Kwa hivyo, tutalifanyia kazi. Kuhusu kipindi hichi, naomba Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa heshima sana. Nimejaribu kupata maelezo ya watendaji mchana wa leo, lakini mwenyewe hayakunitosheleza. Kwa hivyo, sitaki nikudanganye kama hivi na hivi sana. Mimi na wewe tunaaminiana sana, naomba unipe niendelee kulifanyia kazi na naomba nikujibu kesho jioni kuhusu mustakbali wa kipindi hichi, lakini leo saa hizi sitaki nikupe majibu ya kupitisha bajeti. Naomba univumilie twende, lakini naamini kwamba nitalifuatilia kwa kina zaidi ili nikupe jibu ambalo litakuwa ni la kujenga, lakini nitakachokuahidi kwamba tutafanya maamuzi ambayo yatakuwa na maana zaidi kwa mustakbali wa vipindi vyetu na kwa maslahi ya watu wetu ambao wanaipenda *ZBC.* Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nadhani watendaji wa *ZBC* wanatusikia na wajue kwamba hivi vipindi vyao na sisi pia huwa tunapata nafasi ya kukaa na watoto wetu tofauti na vile vipindi vinapozungumza huwezi ukakaa na mtoto wako. Sasa vipindi kama hivi tunaweza kukaa na watoto wetu, lakini pia, vinaelimisha na vinawaelimisha wanafunzi wengine. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri, utakapokaa na watendaji wako, kubwa zaidi uangalie sisi wazazi tunaokaa na watoto wetu kuangalia hichi kipindi. Mhe. Waziri, nakushukuru na nakujua katika utendaji wako, kwa kweli sitaki kusema huna doa, lakini unajitahidi sana. Ahsante.

Kifungu 0704	-	Shirika la Utangazaji Zanzibar-	1,629,290,000
Kifungu 0705	-	Shirika la Utangazaji Zanzibar Pemba-	

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, una hoja Pemba.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Naam, kuna siku hili Baraza litahamia Pemba ninavyotegemea *Inshaallah*. Hoja nilitoa, lakini nafikiri Mhe. Waziri, kapitikiwa katika kujibu, pengine binadamu kasahau. Nilisema kuna sababu gani Mhe. Waziri, anapoulizwa ikawa anajibu swali, yule anayeuliza swali ikawa hatangaziwi. Ni sababu gani nataka kujua hilo tu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Jaku Hashim Ayoub, amelileta hili kwamba kwa nini kipindi cha asubuhi wakati wa kuuliza maswali *ZBC* haitaji muulizaji swali, lakini badala yake inataja Mhe. Waziri atajibu swali. Hilo tumeshalitolea maelekezo, kuanzia kesho waseme kwamba swali hili limeulizwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Tumeshawaambia vijana na kuanzia kesho maswali yaende katika utaratibu huo, ndio maelekezo niliyoyatoa leo mchana.

Kifungu 0705 Shirika la Utangazaji Zanzibar Pemba- 185,246,000
Kifungu 1101

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nina hoja mbili katika Idara hii ya Makumbusho na Mambo ya Kale; Ya kwanza, nilipokuwa nikichangia nilisisitiza suala la kuyatunza majumba ya kihistoria na magofu yetu. Sasa nikaja katika mchango wangu mahsusi suala la jumba la *Beit el Ajaib* na jumba la Makumbusho ya *Kasri*. Nashukuru katika jumba la *Beit el Ajaib* kwa hali ilivyo, Mhe. Waziri, kanipa maelezo ya kutosha kuhusu mradi ambao unategemewa kufanywa kwa pamoja kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Oman.

Mhe. Mwenyekiti, sasa labda anithibitishie tu katika hii hoja yangu ya kwanza kuhusu jumba la Makumbusho ya *Kasri.* Katika mchango wangu nilimwambia kwamba vile lilivyo, sasa hivi ile sehemu inayotumiwa na Baraza la Mapinduzi imefanyiwa matengenezo kidogo, lakini limefanywa jumba kama vile jumba moja nusu limefanyiwa marekebisho, nusu bado, sura yake haipendezi hata kidogo. Sasa hata kama limo katika huo mradi, kwa sababu mwaka huu katika fungu la matengenezo ya Ofisi lipo. Naomba anihakikishie kwamba angalau atalistiri lile jumba ambalo pia linatumika ninavyoamini mimi, sasa hivi kwamba hata Ofisi ya Mkurugenzi nilikuwa najua mfumo umebadilika, yumo mle mle ndani. Kwa hivyo, nasema ilikuwa kuna haja ya kulistiri ningeomba hilo anihakikishie.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili, nimuombe Mhe. Waziri, katika fungu ambalo nilimuomba anisaidie maelezo, lilikuwa ni fungu la gharama za safari katika Idara hii. Sasa kidogo nilipatwa na mashaka na katika ufafanuzi alionipa hili kidogo hakunitosheleza vizuri. Kwamba nikiangalia safari za nje zimetengewa shilingi 400,000/= katika gharama za safari za Idara hii, lakini malipo ya viza milioni 10. Katika jumla ya safari kidogo nilikuwa naomba aniweke sawa hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu gani.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kipo katika Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale kinapatikana ukurasa wa 356, kijifungu 220300, gharama za safari. Sasa jumla yake ni 19,800,000/=, lakini akiangalia Mhe. Waziri, ataona kwamba safari za ndani milioni tisa, safari za nje laki nne, lakini malipo ya visa milioni kumi. Nilikuwa naomba maelezo katika hili.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ni kweli kwamba Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alizungumzia suala la *Kasri.* Mapendekezo ya jengo la *Kasri* umepangwa katika utaratibu namna mbili.La kwanza, serikali yenyewe kuu wana majengo wameona ni jengo muhimu sana katika Historia. Kwa hivyo, baada ya kupata mwelekeo wa huu msaada wa Oman wa *Beit el Jaib*, serikali yenyewe ndio imeamua kulitengeneza jengo lile kwa awamu. Hivyo, wameshamaliza lile, tunatafuta utaratibu wa kuendelea sehemu ya pili. Kwa hivyo, huo ndio utaratibu wa serikali na hautosimamiwa na wizara yangu kama ambavyo ule umesimamiwa na Ofisi ya Rais Ikulu. Hivyo, *engineer* yule yule ambaye yupo pale *State House*, basi ndiye yule yule amesababisha matengenezo yale, ndio atakayepewa sehemu ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo, utaratibu wa kwanza ni huu, lakini utaratibu wa pili, tunaendelea pia na Serikali ya Oman kwamba majengo haya mawili wayachukue kama ni *component* moja na wana mwelekeo huo. Kwa hivyo, wakimaliza *Beit el Jaib*,basi kwa sababu nalo ni jengo ambalo lina Historia kubwa, nalo wanazungumza. Hivyo, ni jambo ambalo wanaweza kulichukua.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, katika yale mambo ya kuwahi angalau ya kujaribu kuchomolea hapa na pale, basi fedha hizi za matengenezo ya Ofisi tutahakikisha kwamba hatuachi mambo yakaharibika. Kwa hivyo, pale ambapo panataka matengenezo ya dharura, fedha hizi tumetumia tutaziweka huku. Hivyo, hiyo ni

katika jengo la *Kasri,* lakini tumeliona na tunaliwekea utaratibu mkubwa, tunalitizama sana. Kuna wakati tulipata taarifa maji ya chumvi yanaingia pale barazani, tukahamanika sana. Sote tulikwenda pale tukaangalia tufanye nini, lakini bahati nzuri hali haikuwa hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo, Mhe. Mwakilishi, tunaomba utaamini kwamba lile jengo nalo tunaliangalia kwa jicho kubwa serikali nzima.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kifungu hichi cha gharama za safari kifungu 220300. Pale pana matatizo kidogo ya *typing error*. Ile laki nne ilikuwa ije huku kwenye milioni kumi na hii milioni kumi ilikuwa iende kule. Kwa hivyo, badala ya laki nne, pale juu ni milioni kumi na huku chini ni laki nne.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze na hizo gharama za safari.Ninashukuru kwa ufafanuzi huo, ninaamini kwamba marekebisho yatafanywa ili tuelewane tumepitisha nini, lakini nimshukuru Mhe. Waziri, vile vile, kuhusu ufafanuzi wake juu ya suala la jumba hili la kumbusho ya *Kasri.* Kama nilivyosema pametengwa hapa hamsini na saba milioni na laki mbili kwa ajili ya matengenezo makubwa na madogo ya Ofisi. Sasa hili la mradi mkubwa linaweza likachukua muda mrefu la mashirikiano na Oman, pengine hata na Ofisi ya Mhe. Rais. Mimi niombe tu aisimamie Idara yake angalau afanye kile kitu ambacho Waingereza wanakiita "*First up listing"* ya lile jengo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kama nchi, mgeni yeyote akifika kuanzia pwani kwanza anapita pale Mheshimiwa na boti au meli yake. Sasa haiba haipendezi kwamba nchi jumba kama lile nusu limepakwa rangi, nusu limejaa ukungu, haipendezi na linatoa taswira mbali sana, kama jamii ya watu kama serikali na vitu vyengine. Hivyo, nilikuwa naomba kwamba angalau wawe wanaangalia na matatizo mengine, angalau walipe haiba ya sura yake, kwa kulipaka angalau rangi, ile sehemu inayotumiwa na Baraza la Mapinduzi ilingane na ile sehemu nyengine ambayo hivi sasa imejaa ukungu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru. Tuendelee, ahsante.

Kifungu 11001 Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Unguja- Shs.665,773,000.00
Kifungu 11002 Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Pemba- Shs.53,367,000.00
Kifungu 1201

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati nilipokuwa nachangia nilizungumzia suala zima la vilabu vyetu ambavyo vinashiriki katika mashindano ya Afrika, pamoja na kombe la shirikisho. Niishukuru serikali kwamba inakuwa inatoa kasma kidogo kwa vilabu vyetu takriban milioni kumi na tano kwa kila klabu ambayo inashiriki mashindano ya Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini mashindano ambayo yanachezwa Afrika ni mashindano makubwa sana, timu inayoshiriki katika mashindano hayo hutumia takriban milioni sitini au milioni sabini na hapo inakuwa inajibanabana kwa kubana matumizi. Sasa nilimuomba Mhe. Waziri, kwamba angalau, basi serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015, angalau iongeze, basi kutoka milioni kumi na tano mpaka ishirini na tano.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile, nimuombe Mhe. Waziri, angalau kuweza kujitahidi kutafuta mfadhili kuweza kusaidia vilabu hivi. Kwa sababu vilabu vyetu sasa imekuwa ikifika wakati wa kutafuta ubingwa, wanajitoa katika kutafuta ubingwa, kwa sababu hawana uwezo wa kushiriki katika mashindano makubwa. Ingawa mara hii ni vilabu vya vikosi ikiwemo Kikosi cha KMKM ambayo ni klabu bingwa kwa Zanzibar ambayo inashiriki katika mashindano ya klabu bingwa ya Afrika, pamoja na timu ya Polisi, lakini vilabu hivyo pia wapo katika hali ngumu katika kushiriki mashindano hayo kutokana na gharama ya mashindano hayo makubwa ya Afrika. Sasa nimuombe Mhe. Waziri, ana mipango gani ambayo wanaifanya wizara kwa sababu yeye ni kama mlezi wa vilabu hivyo, ili kuweza kusaidia vilabu vyetu katika kushiriki vyema katika mashindano, sio kushiriki tu, waende washiriki na washinde na kuendelea katika mashindano haya ya Afrika na kuleta komba hapa Zanzibar kwa mara ya kwanza.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Nassor Salim Ali, alilizungumza hili na mimi nilijaribu kumjibu. Sasa kwanza kuhusu hizi gharama, timu kupata shilingi milioni kumi na tano mpaka ishirini na tano.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunataka tuwape pesa nyingi sana klabu, lakini wakati mwengine hali yetu ya kifedha inatukwaza sana. Sasa sitaki nimuahidi moja kwa moja, maana yake Mhe. Panya Ali Abdalla, amenipa aya leo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niifanyie kazi, lakini zaidi ni kwamba Mhe. Nassor Salim Ali, ni mtu ambaye mara nyingi katika masuala ya michezo huwa ananishauri, si hapa Barazani, aah! Akiona jambo ambalo litakuwa na manufaa kwa nchi, kwa hilo bwana! Huwa anajitahidi sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, na hili ni namna gani ya kutafuta fedha zaidi. Namuomba aje Ofisini kama kawaida yake, tukae tuumize vichwa kidogo, tuangalia nani au utaratibu gani tufanye ili tupate fedha zaidi kama mdhamini au mtu mwengine yeyote ambaye atatuwezesha kuongeza kutoka kile ambacho serikali imeji-*commit*, lakini zaidi ninamuahidi kwamba hali yetu ya kibajeti ikiruhusu, basi suala la kuongeza halina shida tutalifanyia kazi, lakini mimi na yeye tunalizungumza sana na katika haya sina siri na yeye anajua kiasi gani nimepata, hajui basi tutapanga, haya ni mambo madogo madogo ambayo kwa mujibu wa kupelekea mbele sekta ya michezo na yeye ni mdau mzuri wa michezo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, baada ya maneno matamu ya Mhe. Waziri na mimi ninakubali kuweza kukaa naye pamoja kuweza kushauriana, lakini kufanikisha michezo Zanzibar, lakini niiombe serikali katika mwaka wa fedha 2015/2016, basi ile kasma ya milioni ishirini na tano iongezwe na hilo la kushauriana *Inshaallah* hakuna tatizo, tutasaidiana katika kuhakikisha vilabu vyetu hivi ambavyo vinashiriki mashindano ya Afrika, vinafanya vizuri na vinaleta kombe Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru sana. Tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilitaka kujua mgao tunaopata kutoka *FIFA* kwa *TFF* dola laki mbili na nusu na dola moja kwa *CAF*, Zanzibar tunafaidika na kitu gani.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, suala hili la mgao wa fedha kutoka *FIFA* kuja kwa *ZFA* kwa mujibu wa taratibu na kwa mujibu wa uamuzi wenyewe wa *FIFA*, suala hili halilikubalika, maana ili tupate fedha hizo kutoka *FIFA* lazima Zanzibar iwe ni mwanachama wa *FIFA* yenyewe. Bahati mbaya kwa barua yao ambayo ninayo hapa hatukukubaliwa kujiunga na hili, lakini hata hivyo, wametwambia kwamba misaada ya *FIFA* kuja kwa Zanzibar, basi itapitia *TFF*. *TFF* ndio mwanachama, sisi sio mwanachama. Kwa hivyo, kile ambacho wanakipata tunaendelea kufanya mazungumzo.

Mhe. Mwenyekiti, nishawatuma *ZFA* mara mbili. Katika uongozi uliopita hatujapata mafanikio, lakini kwa huyu Mhe. Rais mpya ambaye *TFF* aliyeopo anaonekana yupo makini kidogo. Kwa hivyo, nimemuagiza Mhe. Rais wa *ZFA* waendelee kukamilisha huu utaratibu kuona namna gani *ZFA* inaweza ikapata gawio au mchango chochote kutokana kile ambacho wanapata.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana, tunaendelea Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Katika majibu ambayo Mhe. Waziri, ametoa kuna eneo moja vile vile hakunisaidia ufafanuzi. Ningeomba anisaidie jawabu ili tuweze kuendelea. Katika mchango ambao nilimpatia, niliomba kutaka kujua. Je, serikali ina mpango gani katika kuwasaidia hawa vijana ambao wanafanya kazi ya huu uchambuzi iwe ndani ya wizara au nje ya wizara, hususan katika mafunzo ya *football and administration*. Naomba maelezo ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, umemfahamu?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, bado sijamfahamu.

Mhe. Mwenyekiti: Hajafahamu.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi ambao nilimpelekea Mhe. Waziri, nilimuomba anisaidie kunielekeza au kunifahamisha, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wale watu ambao wanaofanya kazi ya uchambuzi kama vile kutoa tathmini ya mpira wa miguu ambao kwa sasa unakuwa unaendelea. Je, wizara yake ina mpango gani wa kuwasaidia vijana katika masuala ya kuwaendeleza kwenye masomo ya *football and administration*. Naomba kupata maelezo ya Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, masuala yale namna gani vijana wale watapata maarifa katika kufanya *analysis* ya michezo mbali mbali. Sisi utaratibu ambao tunaufanya ni kuwaalika makocha mbali mbali kutoka nje ili kuja kuwafundisha makocha wetu uwezo wa kufundisha.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tunachoamini ni kwamba hata mtu ukishakuwa na *Class B* au *C* ya ukocha, uwezo wa kufanya tathmini ya namna gani mchezo unachezwa atakuwa nao. Kwa hivyo, *current* hatujakuwa na utaratibu wa kuweka masuala ya *football and administration*, lakini ushauri wake tunauchukua, basi nitakaa na wataalamu wangu wa michezo tuangalie namna kada hiyo ya utawala wa mpira tutatoe mafunzo ya aina hiyo.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Tuendelee.

Kifungu 1201 Kamisheni ya Utamaduni na Michezo- Shs.863,412,000.00
Kifungu 1202 Baraza la Kiswahili- Shs.40,800,000.00
Kifungu 1204 Baraza la Michezo la Zanzibar-

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kuna suala ambalo nilimwambia Mheshimiwa wangu kwa ushauri bure ambao niliutoa kuhusiana na suala la kuwa Mwenyekiti wa Baraza lazima kutungwe sheria badala ya kuteuliwa na Mhe. Rais, awe anateuliwa na vilabu vyote.

Mhe. Mwenyekiti, suala hilo Mhe. Waziri, wangu hakunijibu, si kwa jeuri, naamini hiyo kapitikiwa binadamu kuwa ana mambo mengi. Kwa nini nikasema hivyo kuna matatizo yanaweza yakatokezea kwa mujibu wa sheria, kwa mfano kama hili suala kuwa fedha zimetolewa, lakini sisi Riadha tumefutwa, kumbe katika fedha zile tulikuwemo na sisi Chama cha Riadha kishiriki, lakini hatimaye hakikushiriki. Sasa kungekuwa na sheria tungesema kuwa vyama kapigiwa kura kwenye vyama tungeweza kumuondoa, lakini kwa kuwa ana uteuzi mkubwa tumeshindwa kuweza kumuondoa. Sasa ningeomba Mhe. Waziri, kuwa sheria wanasheria wapo, naomba sana hili suala aweke na yeye kumbukumbu katika Historia ya wizara hiyo atakapokuwa ame-*shift* kwenda wizara yake, sio aukose Uwaziri moja kwa moja, a-*shift* kwenda katika wizara nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, naomba anisaidie kwa hilo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nafahamu mazingatio ya Mhe. Makamu wa Zanzibar wa Chama cha Riadha, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Mwenyekiti, tangu apate dhamana hii, ameanza kufanya mageuzi muhimu katika chama chake na naamini kwamba mageuzi haya yatafanya Mapinduzi makubwa katika sekta ya riadha. Kwa hivyo, suala ambalo amenishauri wacha tuzingatie katika kikao cha Kamati ya Uongozi ya wizara, kwa sababu sheria ambayo tumeipitisha Baraza la Wawakilishi, hapa ni kwamba anateuliwa na Mhe. Rais. Hiyo ndio sheria ambayo tuliyoipitisha. Sasa kwa vile mdau muhimu wa michezo Makamu wa Rais wa Zanzibar wa Chama cha Riadha, ana maelekezo haya, basi wacha tuyachukue tuyafanyie kazi, halafu kama tukiona ni mjaribu, basi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu hapa ipo itatuelekeza namna ya kuja mabadiliko haya katika Baraza lako la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kama hatujaona ni mjaribu, yeye ni mdau wa michezo tutakaa katika vyama vya michezo kwa jumla na yeye mwenyewe akiwa ni mdau, basi tutapeana maelekezo ambayo bila shaka tutafanya maamuzi ambayo yatamfurahisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ni mjaribu. Sheria sasa hivi zinakuja na *time*. Sasa imekuwa *time,* sasa hivi kutokana na hali ilivyo, hata katika dunia inakuwepo wanafanya vitu kama hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni suala la mjaribu na ni zuri sana. Mwanasheria kama ulivyom-*quote* ipo, lakini wewe ndiye wa kupeleka suala kama hilo. Naamini kama tutalipeleka suala hilo, basi vyama vyote vitaku-*supporter* asilimia mia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee kwa kuwa Mhe. Waziri, wangu ni msikivu yupo pamoja na mimi kama nilivyosema jana tofauti yetu ni vyama tu, mimi na yeye, lakini ni mtu hodari, shupavu, tupo pamoja ninamuomba anifuate mimi. (*Makofi*)

Mhe Mwenyekiti: Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali,

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, ili kuweka *Hansard* sawa. Mimi nimshukuru Mhe. Waziri, kwa *wind up* yake aliyetoa kwamba...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali, kaa kitako kwanza. Mhe. Mohamedraza, Baraza lina utaratibu, wizara tangu inasoma nipo mimi, mpaka inafanya majumuisho nipo mimi na tunasema mtu akishachangia asiondoke angoje majumuisho. Hukuwepo, ninakuheshimu na unaniheshimu, ukiwa na dharura unaniaga. Leo hukuniaga. Kwa hivyo, hukuwemo ndani ya Baraza. Hivyo, siwezi kukupa nafasi ukatoa hoja. Ungekuwemo ndani, ningekupa, lakini ulikuwa nje ya Baraza. Kwa hivyo, ninakuomba samahani sana. Serikali ilikwambia kwamba hoja yako kwamba Mhe. Balozi Seif Iddi mlango wake uko wazi, Mhe. Waziri, mlango wake uko wazi, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, mlango wake uko wazi, Mhe. Waziri wa Fedha, mlango uko wazi, umeshasema na umeshajibiwa. Kwa hivyo, tunakuomba sana fuata taratibu. Tunaendelea Mhe. Nassor Salim Ali.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Taarifa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kanuni ya ngapi hiyo taarifa. Mhe. Nassor Salim Ali.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nachangia.

Mhe. Mwenyekiti: Muongozo Kanuni ya ngapi, Mhe. Raza.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeuguliwa na mama yangu...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, Baraza lina utaratibu. Unatoa muongozo kwa Kanuni.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, mimi nauguliwa, ndio maana nikachelewa, mama yangu yuko kwenye *wheelchair*. Sasa naomba nipewe haki yangu, mimi humu ndani. Silizungumzi hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi hukuniaga. Mimi ndio Mwenyekiti, kaa kitako Mhe. Mjumbe, ndio utaratibu, mimi ndio Mwenyekiti, kaa kitako na ufuate taratibu. Mhe. Nassor Salim Ali.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, wakati nilipokuwa nachangia jana kuhusu Baraza la Michezo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tusikilizane.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, nilizungumzia suala zima la Kanuni ya *ZFA* ambayo nategemea kwamba katika mwaka huu wa 2014, *ZFA* itafanya uchaguzi wake mkuu wa kuweza kupata viongozi wake.

Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Waziri, ananijibu kuwa analifanyia kazi suala hili la Katiba, lakini Mheshimiwa ZFA inakuwa inapata ruzuku yake kutoka Baraza la Michezo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunyamaze hatumsikii Mhe. Mjumbe, tunyamaze kidogo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Baraza la Michezo ruzuku yake ambayo inapata kutoka serikali kutoka mwaka wa fedha 2013/2014 ilikuwa milioni 141, lakini fedha ambazo waliingizwa katika mwaka wa fedha huo ni milioni 11, ni sawa sawa na asilimia 8. Sasa wanashindwa hata kusaidia *ZFA* kufanya mkutano mkuu kwa ajili ya kutengeneza katiba mpya. Je, Mhe. Waziri, atawasaidia vipi *ZFA* kwa sababu huku Baraza la Michezo fedha ambazo zimeingizwa kwa mwaka huu ni milioni 11 kutoka milioni 141 ambayo ni sawa sawa na asilimia 8. Kwa hivyo, hawana fedha za kuweza kuwasaidia *ZFA* kufanya mkutano mkuu wa kutengeneza Katiba mpya na kufanya uchaguzi mkuu katika mwaka huu wa 2014 kwa ajili ya kupata viongozi wapya.

Mhe. Mwenyekiti, sasa sijui Mhe. Waziri, ataisaidia vipi *ZFA* na Mhe. Waziri wa Fedha, atujibu kwa nini fedha hizi ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya Baraza la Michezo, shilingi milioni 141,699,000 wakaingiziwa milioni 11,646,000. Naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Haja ya kufanya uchaguzi mkuu wa *ZFA* mwishoni mwa mwaka huu, ni jambo la lazima, kutokana na kilio cha wapenzi wengi

wa mchezo wa mpira wa miguu hapa nchini. Wote wamekuwa wakisema kwamba *ZFA* ina matatizo makubwa na kwamba inahitaji kufanya uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunawaambia kwamba hatuwezi ku-*impose* mpaka pale ratiba yake ya uchaguzi itakapofika. Kwa bahati nzuri Disemba kwa mujibu wa kalenda yao ndio unafikia mwisho wa uongozi. Kwa hivyo, sisi tumewaambia kwamba ili mufanye uchaguzi na kwa sababu ya manung'uniko yaliopo, tumemuagiza Mrajis wa Michezo ahakikishe kwamba anashauriana nao ili kubadilisha Katiba yao iende sambamba na matakwa ya wadau wa michezo. Kazi hiyo inaendelea na inakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kama wana matatizo ya fedha ya kuendesha mkutano mkuu, basi wapeleke bajeti yao halisi Baraza la Michezo, kama ambavyo mwaka jana tuliwasaidia chama cha riadha kufanya uchaguzi, basi na wao tutaiangalia bajeti yao na tutauangalia uwezo wetu, kile ambacho tunaweza tutawapa na kile ambacho hatuwezi, basi wadau wa michezo wa mpira wa miguu wapo wataangalia namna gani ya kufidia lile pengo ambalo lipo. Kwa hivyo, tunamuahidi kwamba hilo ni jukumu letu la kuhakikisha kwamba tunalisimamia hilo. Pia, naamini kwamba hata Mhe. Rais mwenyewe ni mdau wa michezo kwa hilo, Mhe. Waziri wa Fedha, japokuwa hachezi, lakini anapenda sana kuwaangalia watu wanaocheza. Kwa hivyo, naamini kwamba katika hilo, atatusaidia chochote ili kuhakikisha kwamba mambo haya yamewezekana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Waziri, kwa majibu yake. *ZFA* mikutano yake miwili ambayo ni mikutano ya Kamati tendaji na mkutano mkuu, huo unagharimu takriban kama shilingi milioni 10. Kitu ambacho kinanitia wasi wasi, kwa sababu mwaka jana kama nilivyozungumza kwamba Baraza la Michezo ililiingiziwa milioni 11, kutoka milioni 141. Sasa inanipa shaka kwamba hizo fedha zitatoka wapi. Kwa hivyo, ningeiomba serikali kwa kupitia kwa Mhe. Waziri wa Fedha, atowe uthibitisho kwamba fedha hizi milioni 90 ambazo wameidhinishiwa Baraza la Michezo kwamba zitapatikana na kuhakikisha kwamba *ZFA* wanasaidiwa ili kuweza kufanya uchaguzi mkuu na kuweza kuchagua viongozi wapya na kupata katiba mpya.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kama bajeti ni hiyo ambayo ameizungumza, basi wacha wailete ni jambo ambalo linazungumzika na naamini kwamba serikali kwa umuhimu wa michezo ya mpira wa miguu, basi fedha hiyo itapatikana na ikiwa watathibitisha bajeti yao halisi, itaangaliwa na Baraza la Michezo. Kwa hivyo, suala hilo linawezekana, sisi tunahitaji tu kwamba ikifika mwezi Januari mwakani tuwe hatuna tena vurugu la *ZFA*, Katiba wanayo mpya na uongozi mpya ambao umechaguliwa kihalali na umepatika. Kwa hivyo, suala hili tutashirikiana na yeye mwenyewe kuhakikisha kwamba suala hili limekamilika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, *ZFA* wamenisikia, wanamichezo Zanzibar wamenisikia na mwanamichezo nambari moja Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein amesikia. Kwa hivyo, tuendelee.

Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, kwa hili Mhe. Waziri, atanisamehe kidogo, kwa sababu naona maajabu makubwa sana tunaipigania *ZFA* kwa kupitia *TFF* ili ipate uwanachama wa *FIFA*, kama nchi au hata *observer*, lakini huku tuna chama chengine cha michezo *Zanzibar Weight Lifting Association*, yaani chama cha wabeba uzito ambacho tayari kina uanachama wa ulimwengu, kama Zanzibar wana uwanachama, wana kura na wana kiti chao pale kama Zanzibar, tunashindwa kulipa ada yao hiyo ya dola 2,400.

Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi tayari nimeshawachangia chama hiki. Hivi sasa chama hiki kina timu yake iko Uturuki ambayo inafanya mazoezi kwa ajili ya kwenda kwenye kombe la dunia la kubeba uzito ama vyuma. Mimi kidogo nashangazwa, huku tunagombania sisi bendera yetu kuipeleka *FIFA* na huku tayari tuna bendera yetu inataka kushushwa tunashindwa na dola 2,400.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri suala hili mimi nimebahatika kuongea na Mhe. Waziri sana, barua nimempelekea na amenijibu vizuri, lakini majibu yake mazuri aliyonipa bado hatujajua ni lini tutalipa kule na kuna hatari ya Zanzibar kuweza kufutwa uanachama wake katika zile ngazi za Kimataifa na tayari hawa wameshachangishana. Katika hizo dola 2,400, mimi kama mzalendo wa nchi hii kama walivyokuwa wazalendo wengine nitamchangia Mhe. Waziri, dola 200, yeye aseme ni lini atazitimiza hizo dola 2,200 ili zikalipwe. Kwa kweli inatia huruma sana, tunataka hii timu ije hapa nje ya Baraza la Wawakilishi, isimame na bakuli ili kila Mhe. Mwakilishi, akiingia atie chochote mule na wakati hawa wanabeba bendera ya Zanzibar katika shirikisho hilo la Kimataifa. Namuomba sana Mhe. Waziri, atowe kauli ya kwamba lini watalipiwa pesa zao hizi, maana kama hawajalipiwa watafutwa ndani ya kipindi cha mwezi mmoja ambapo mashindano yataanza.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo, walizungumzia suala hili. Suala hili lilipokuja na Mhe. Naibu Waziri

wa zamani wa michezo, niliwaita watendaji wangu. Jibu lao kwanza ni chama kina wajibu wenyewe wa kulipia ada, jukumu lake hilo, lakini wamelimbikiza mpaka mwaka jana 2013, kuanzia mwaka 2009/2010 ambapo Mhe. Naibu Waziri wa michezo wakati ule, angeweza kuwalipia kwa miaka hiyo miwili hakuwalipia. Sisi tukalipia 2011,2012 na 2013.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, hiyo ya nyuma ambayo wao hawakulipa sisi tulilipa na hii mitatu. Kwa hivyo, miaka mitano tumeshalipa. Sasa chama hiki kila siku kinadai ada ya kulipiwa ni mtihani, lakini jambo la pili watendaji wangu wananiambia hawana *supporting document*, kwamba wao uthibitisho huo uanachama wao. Waliponiambia hivyo, nikawaambia musiwalipe. Mimi tatizo langu ni hilo, huwezi kutoa fedha serikali kama njugu na mimi wananijua katika hilo ni mgumu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, waje na uthibitisho kwanza kwamba wao ni wanachama, wakishakuja na huo, basi suala hilo linazungumzika kwa sababu ni chama chetu, lakini nawaambia hivi sasa wako *njia panda* kwa mgongo wa timu ya Tanzania, ndio maelezo niliyopewa na mara nyingi wanaposhiriki wamekuja angalau Baraza la Michezo kueleza walichopata na walichokosa hawaendi. Sasa chama cha aina hiyo ni lazima kiwe na mahusiano mazuri na taasisi inayosimamia michezo hapa nchini, ndio iweze angalau kujenga utaratibu wa kusimamiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, ikiwa chama cha *Weight Lifting Association* atatusaidia, ni jambo zuri, lakini akielezea kwamba hapa ndani kuna taasisi inayosimamia michezo, wafanya utaratibu wa mashauriano vizuri, Wajuwe lini wanaondoka na walete bajeti yao mapema, sisi hapa tunatengeneza bajeti na bajeti hii inasaidia, huwaambia wote wenye vilabu kwamba leteni bajeti yenu mapema ili sisi tuweze kupanga, kwa sababu tunadai vile vile, lakini inakujia timu katikati ya msimu wanakuambia sisi tunataka milioni 30 tunakwenda kwenye michezo. Tunawaambia hatuna pesa, kwa sababu sisi tuna bajeti, mnatujia katikati mnataka pesa, sisi tutapata wapi, sisi ndio tunapitisha bajeti hapa, vyenginevyo tuta-*over expend* na ndio tatizo la Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, lazima vyama viwe na utaratibu wa kuwasiliana na Baraza la Michezo chombo ambacho kimewekwa pale kwa ajili ya kuongoza, sio wajiondokee tu watuambie habari za barua. Sasa utaratibu Mhe. Mwakilishi, naomba washaurini hivyo, wafanye mawasiliano mazuri na Baraza la Michezo, ili tujuwe kalenda zao wanakwendaje na halafu mambo ya kusaidiana ni mambo ya kawaida tu, lakini pia, wawe na *supporting document* ili kuonesha kwamba wao ni chama ambacho kina usajili huko nje, hilo limekosekana.

Mhe. Mwenyekiti, isijekuwa ni watu wajanja wajanja wanakwenda michezo, mara kwa mlango wa Tanzania Bara, mara kwa huku, halafu wanakuja kwetu kutaka msaada. Hawajawahi kuja na medali pale Baraza la Michezo kutuambia kwamba tumekuja au tumeshindwa. Kwa hivyo, kuna mambo ya kuweka mawasiliano mazuri baina ya Baraza la Michezo na chama hiki.

Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo: Mhe. Mwenyekiti, katika siku aliyonisikitisha sana Mhe. Waziri, Mhe. Said Ali Mbarouk, basi ni leo. Sasa nadhani tutachezeshana foliti humu ndani, ndio.

Mhe. Mwenyekiti: Wende kwa hoja.

Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo: Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda kwa hoja moja baada ya nyengine. Nilimmwagia sifa nyingi sana, sitaki kuzifuta kama za Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa sababu bado anazo, lakini leo nimesikitika sana. Katika barua niliyompa, ikiwa na hati zangu pia, niliambatanisha na *supporting document* inayotoka katika shirikisho la Kimataifa la *Weight Lifting Association*, nilimpa Mhe. Waziri, humu humu ndani ya Baraza. Mhe. Waziri, kidogo nimesikitika kwa kauli hiyo uliyotoa kwamba hawa hawakuwa na *supporting document*, nimesikitika sana na kama kuna njia ya kuondosha sikitiko langu, basi naomba uifanye njia hiyo, hilo la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, la pili, sheria ya Baraza la Michezo ambayo ilipitishwa humu ndani ilitamka wazi kwamba Baraza la Michezo litachukua jukumu la kulipia vyama vyote vya michezo katika kuweka Utaifa wetu au nafasi ya Taifa hili la Zanzibar ulimwenguni. Sasa leo tusingekuwa tunagombaniana *FIFA* kwa kupitia wizara, kama ingekuwa *ZFA* inashughulika yenyewe, wala Mhe. Waziri, asingetoa kauli ya *ZFA* hapa ndani, ingekuwa *ZFA* yenyewe ndio inashughulikia huko kwenye masuala ya *FIFA*, lakini Mhe.Waziri, katoa kauli sasa hivi ya *ZFA* kwamba *ZFA* waende wakaongee na *TFF* ili angalau wapate *status* hiyo inayotakiwa huko *FIFA.*Kwa hivyo, naweza kusema Mhe. Waziri, awa-*consult* tena watendaji wake ambao na mimi wakati huo alionitaja nilikuwa nafanyakazi na watendaji hao hao na arudi tena kwenye sheria ya Baraza la Michezo ya Zanzibar inayounda, ataona kipengele hicho.

Mhe. Mwenyekiti, tatu Mhe. Waziri, amesema kwamba hawawasilishi taarifa zote. Mhe. Waziri, taarifa zote zinawasilishwa, hawa wanawasilisha taarifa zote wizarani kila wanaposhinda, kila wanapopata medali wakirudi wanawasilisha taarifa. Mhe. Ismail Jussa Ladhu, katika mchango wake aliwataja leo hapa ndani kuhusu chama hicho na akamtaja ndugu Jamali, ndio ambaye alikuwa mfuatiliaji wa karibu sana na mambo haya na bahati nzuri Ofisi yao iko karibu pale pale katika viwanja vile vya Mnazi Mmoja wamejenga na mimi nilishiriki pia, mbali ya hayo madeni mengine nilishiriki katika ujenzi wa Ofisi hiyo. Mhe. Waziri, anaweza kuwauliza viongozi wa chama hiki ataambiwa.

Mhe. Mwenyekiti, la nne, ametaja Mheshimiwa kuhusu bajeti kwamba inakuja katikati, wakati sisi tuko wizara ile bi Sheri, nakumbuka Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Zanzibar, alikuwa anapanga bajeti za vyama vyote na malipo yao yanayotakiwa kwa mwaka mzima, anatuletea sisi wakati huo tunakaa na Mhe. Ali Juma Shamuhuna, yule pale yupo atathibitisha, tulikuwa tunakaa tunapitia katika vikao vyetu kabla ya kuwasilisha kwenye bajeti. Tulikuwa tunajua kila chama kitalipiwa bei gani kwa uwanachama wake wa kuwakilisha kama nchi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Waziri, akizungumza hivyo, kidogo mimi napata wasiwasi. Naomba kumbukumbu hizi zote aziweke sawa na kwa bahati nzuri hizi nyaraka zote zipo na zimewekwa vizuri. Naomba nirudi tena kwa Mhe. Waziri, kwamba hili sio deni la nyuma, asitamke kwamba deni la nyuma, hilo ni deni la hivi sasa hivi. Zanzibar itatolewa uwanachama wake mwaka huu itakuwa sio mwanachama tena, hili deni ni la sasa hivi sio la miaka nyuma, sio alipokuwa Mahmoud Thabiti Kombo (Naibu Waziri) au Mhe. Ali Juma Shamuhuna (Naibu Waziri Kiongozi), deni hili ni la mwaka huu vyenginevyo itatolewa Zanzibar. Kwa hivyo, naomba aseme Mhe. Waziri, hivi sasa, natamka rasmi naomba aseme lini atalipa deni hili. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, na mimi namuheshimu sana Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo, aliwahi kuwa Naibu Waziri wa wizara hii ninayoiongoza, mara nyingi alinishauri sana, lakini kwa hili nasemaje, mimi niko wizarani pale tangu mwaka 2012 sijawahi kuona wala sijawahi kualikwa *event* yoyote ya chama hiki baada ya kurudi mashindano yoyote. Naalikwa judo, riadha na vyama vyengine, lakini chama hiki bado. Kwa hivyo, huo ni ushahidi kwamba wanakwenda wanarudi kivyao vyao. Hilo la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, la pili, *Accounting officer* wa wizara hii ni katibu mkuu, yeye ndiye anahakikisha malipo yanayofanywa yanautaratibu mzuri. Sasa wapeleke *supporting document original* kwa katibu mkuu na kwa katibu mtendaji wa Baraza la Michezo, kuthibitisha uanachama wao huko nje, hatuna tatizo hilo. Wasipewe Waheshimiwa vi-*photocopy* wakatuletea na sisi, siwezi kuruhusu mambo hayo hata kidogo hii ni fedha ya serikali. Kwa hivyo, mimi sina tatizo nasema tena ya kuwasaidia vijana na tunawasaidia wengi, lakini kwa utaratibu ambao tumekubaliana. Sasa kama Bi Sheri alikuwa akifanya bajeti, nasema kila chama kiandae kalenda yake ipeleke Baraza la Michezo, Baraza la Michezo li-*budget* kwa kulingana. Sio kwamba katikati mwezi wa nne mnatujia wizarani mnataka kwenda mashindano, yametokea wapi mashindano hayo, pesa ngapi, tunataka milioni 50 hatuna, lazima msikurupuke vyama, tumeshawaambia mara moja mara mbili. Mimi mwenyewe nimeshakaa nao vikao mara mbili, nawaambia kila kikao fanya *activity* zake mapema za mwaka. Sio vyama vya mkobani, halafu mnafanya masihara hapana, hatuwezi kuletewa michezo katika hali hii.

Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mhe. Waziri, leo anazidi kujizonga. Mhe. Waziri, mwenye maana humu ndani tunayo kiapo kwamba amekiri kwa ki-*note* ambacho ameniandikia mimi, sasa ananifanya niseme hata ambayo sikutaka kuyasema.

Mhe. Mwenyekiti, amekiri ameniandikia kwa ki-*note* kwamba kweli hili deni lipo na tunalishughulikia, lakini kwa hivi sasa hali ya fedha yetu si nzuri Mhe. Said Ali Mbarouk, *Alhajj*, Sheikh ameniandikia ki-*note* tena ninacho hicho ki-*note*, kwamba hivi sasa Mhe. Mjumbe, tustahamilie hali ya fedha si nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, mimi nilimjibu kwamba hawa fedha zao kama hazijalipwa kwa wakati itakayofutwa ni Zanzibar kama nchi itafutwa kule uwanachama wake na wala sio wao tu wale, isipokuwa wao watarudi pale Kikwajuni na kuendelea vyuma vyao na watakuwa na kunywa supu, lakini Zanzibar itafutwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa leo naona ameibadilisha kauli yake na kutoa kauli nyengine kwamba hajawahi kualikwa na wala hayo hayahusu, kwa sababu wanayo hiari yao ya kualika na pengine wamealika watendaji au

Mwenyekiti wa Baraza la Michezo, lakini *correspondence* yao wanapeleka mpaka wizarani na kwa taarifa yako mpaka kwa Mhe. Rais wamepeleka barua hawa, kwa bahati nzuri na mimi nilipata hiyo nakla nililetewa.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani ingekuwa uungwana kwa Mhe. Waziri, kutoa tamko kwamba hizi fedha tutazitafuta na tarehe fulani tutazilipa na wala sio kukanusha kabisa wakati hatua zote hizo tumeshapita pamoja, tumefanya mawasiliano mazuri kirafiki, yaani tumefanya mawasiliano *official* na yeye na mimi pamoja na ki-*note* chake cha kunifahamisha vizuri, lakini leo watendaji wamemwambia hivi na vile na yeye yuko hivi, kwa kwali hapo anaanza kujitia madoa na wala mimi nisingependa aingie madoa kwa mwanzo mzuri ambao tayari ameshauanza na amefikia hapa. Kwa hivyo, ninakuomba sana kabla hatujafikia, hivyo vifungu vyengine, ninamuomba sana Mhe. Waziri, kupitia kwako atoe tamko kwamba hizi fedha zao hawa watalipiwa lini na tamko hilo tayari ameshawahi kunipa mimi Mhe. Waziri, tena kwa maandishi na kuniambia kwamba tuvumilie hivi, sasa bado hali yetu ya kifedha si nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hata kama baada ya bajeti, wale wangelipiwa au waambiwe wakope pahala, ili Zanzibar iwe inapeperushwa kule, yaani ikakopewe kama tunavyokopa hii mikopo mingine na ile bendera iendelee kupepea na Zanzibar ibakie na kama si hivyo, tukubaliane tuwaambie wale kwamba serikali haiwezi, tujitoeni na uwanachama wetu ufutwe na tutangaze rasmi Zanzibar kutolewa kule.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kushughulikiwa jambo ni pamoja na kuhakikisha kwamba kuna uhalali wa malipo yenyewe. Sasa wizara yetu ipo karibu sana na hiyo taasisi anayoizungumza na yeye mwenyewe anasema anayo mahusiano mazuri. Kwa hivyo, kesho asubuhi wapeleke vielelezo vyao halali kwa Baraza la Michezo na tutaangalia hali halisi, lakini kwanza lazima uthibitishwe uhalali wa suala lenyewe na wala hatuwezi watu wakatunga au wakaandika kwenye karatasi na kuunganisha kwa kutumia *computer* mambo na halafu wakatufanya sisi serikali tutoe malipo bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, ninachomuomba Mhe. Mjumbe, aende kwa vijana wake na wathibitishe ama kwa Baraza la Michezo au kwa Katibu Mkuu wa Wizara na baadae hayo masuala ya malipo ni mambo ambayo yanaweza kuzungumzika.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, umemfahamu Mhe. Waziri.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ninasikitika sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, sasa Mhe. Waziri, amekubali kesho upeleke vijana wako.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, hapana isipokuwa Mhe. Waziri, afute kauli yake kwamba watu wanatunga vikaratasi kwa kutumia *computer* na wala hiyo si kauli sahihi. Hali hiyo inaitwa ni *forgery* katika lugha ya kisheria inaitwa ni *forgery* na Mhe. Mwanasheria Mkuu yumo humu ndani. Kwa hivyo, akisema hivyo Mhe. Waziri, ni kwamba na mimi nimeshirikiana na hao watu kufanya *forgery,* si kweli na wala sijashirikiana nao kufanya *forgery*. Kwa kweli zile ni *genuine documents* kutoka *Weight Lifters Association* ya dunia, ambapo Zanzibar kama serikali au nchi inao uwanachama wake.

Mhe. Mwenyekiti, sasa akisema kwamba watu wanatunga kwa kutumia *computer* kauli hiyo, naomba Mhe. Waziri, aifute kupitia kwako na wala sitokuwa tayari na naiheshimu sana serikali na kauli hii inaidhalilisha serikali nzima, kwa sababu mimi kila mara ninaposimama ninasema kwamba ninawatetea wao zaidi, yaani ninaitetea Zanzibar au bendera ya Zanzibar ambayo inapepea Makao Makuu yao kule Uswizi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kauli hii ya kusema kwamba watu wanatunga kwa kutumia *computer,* sio sahihi na naomba afute kauli hiyo. Pia, naomba tena afute kauli ya kwamba hizi *documents* hazijafikishwa kwake au yeye hana taarifa yoyote.
Vile vile, naomba pia aunge mkono au aikubali kauli ya kwamba yeye alinipa jibu hilo kwanza kwamba atashughulikia suala hilo, isipokuwa hali ya fedha hivi sasa ni mbaya. Sasa kauli zote tatu na mbili za kufuta. Hivyo, naomba azifute kwanza ili tuweze kuekana sawa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, hapo sioni sababu ya kufuta kauli hata kauli moja. Kauli ya kwanza ninarudia kwamba aende kwa vijana hao, ili watuletee *authenticity documents* na wala hatutaki *photocopy*, kwa sababu *photocopy can be forge by anybody*. Sasa kukwepa hiyo *forgery,* atuletee *authenticity original documents* juu ya uwanachama wao. Kwa hivyo, hapa hakuna sababu ya kufuta, hivi nifute nini hapa, naona hakuna kitu cha kufuta.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya pili, ni kwamba katika kulishughulikia na hiyo ni kuhakikisha kwamba hizo taratibu ziko sahihi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, Mhe. Waziri, anahitaji *original* na wala sio *photocopy*.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, *document* iliyopelekwa kwake ni *original* na leo sijui Mhe. Waziri, amefikwa na nini hata anasema maneno hayo humu ndani, lakini *document* iliyopelekwa kwake ni *original*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jambo la pili, mimi si kazi yangu kupeleka au kuwachukua watu kwenda nao Ofisini kwake, sio kazi yangu, kwa sababu mimi ni Mwakilishi ambaye nimechaguliwa na wananchi na kazi yangu ni kuwatetea wananchi kupitia chombo hichi. Kwa hiyo, nitaendelea kuwatetea wananchi walionichagua kupitia jimbo langu na hao watu ambao wanadai kupitia chombo hichi na wala si kazi yangu kuwashika mikono kuwapeleka Ofisini kwa Mhe. Waziri, hapana, yeye ni jukumu lake kuhakikisha kwamba vyama vyote vya michezo vya Zanzibar vyenye nafasi ya Utaifa au vinavyowakilisha Taifa vinalipiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sitokuwa tayari kuwapeleka hawa Ofisini kwake na nilichokifanya mimi kulikuwa ni *genuine*, lakini leo amekikataa na amekikanusha ndani ya Baraza hili, ambapo tunakula kiapo na nimempelekea barua na kuambatanisha na hizo *documents* zote, pamoja na ki-*note* cha kwangu na yeye amenijibu ki-*note* kizuri kabisa. Sasa kidogo leo ninapata wasi wasi, ndio maana nimesema naomba kauli hizo zifutwe na wala sio *documents* za kutayarishwa tu kwa kutumia *computer* na hiyo ni *forgery*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, kama wao wamezoea *forgery* kwenye mikataba mengine wanayofanya mbali mbali, sisi tulipokaa pale na Mhe. Ali Juma Shamuhuna, miaka mitano hakuna *forgery* yoyote pale na kama leo itaundwa Kamati Teule itaonekana kwamba hakuna chochote cha *forgery* pale kilichofanyika katika miaka yetu, lakini wao wakiundiwa Kamati Teule leo nadhani *forgery* zitaonekana wazi wazi. Naomba kauli hiyo ifutwe kabla hatujaendelea mbele. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, tumalize suala hili.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nimemaliza hapo nasimamia msimamo huo. Kwa hiyo, kama anataka alete au awaambie vijana walete *original copy* na huo ndio msimamo wa serikali pamoja na wizara yangu na wala sina tena suala jengine. Sasa kama anawatetea awatetee na hilo. *(Makofi)*

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, nitaendelea kusimamia na kuitetea Katiba ya Zanzibar pamoja na watu wake. Naomba tena Mhe. Waziri, afute kauli ya *forgery*, kwa sababu hilo amelitamka kwamba nyaraka tulizopeleka zilikuwa za kughushi, hapana na wala haijafanyika hivyo, iliyopelekwa ni *invoice* rasmi kutoka huko na imefikishwa. Vile vile, naomba tena kwamba Mhe. Waziri, atoe tamko lini fedha hizi zitalipwa na si hivyo tufuate Kanuni ya kufanya uamuzi na Waheshimiwa Wajumbe, wote wamo humu na wamesikia hoja za upande wangu pamoja na hoja za Mhe. Waziri na serikali yote ipo mbele. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tunacho-*argue* hapa ni dola 2200, hivi sasa maana dola 200 tayari nimeshajitolea kama mchango, isipokuwa tunacho-*argue* ni 2200. Pia, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, akuliwa ana-*argue* shilingi 20,000/= ikawa *negotiated* mpaka ikafika shilingi 10,000/= na Mnadhimu hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, tumekusikia labda tusikilize Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kama anayo maelezo ama Mhe. Waziri, yeyote anayeweza kusaidia.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo mazuri ambayo Mhe. Waziri, ameyaeleza na vile vile, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, ametoa maelezo ambayo anayaamini yeye.

Mhe. Mwenyekiti, ukitizama Mhe. Waziri na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, wote wanazungumza lugha moja na wote wanayo imani ya kuwasaidia ndugu zetu hawa wa Umoja huu wa Wanyanyua Vyuma. Kwa hiyo, kwa kuwa wanazungumza lugha moja na kwa sababu Mhe. Waziri, ameshaonesha nia kwamba wanapofuata utaratibu fulani ambao Mhe. Waziri, angependelea zaidi kwamba jambo hili lingefanyika. Kutokana na hali

hiyo, hakuna haja ya kuvutana, kwa sababu hawa wote ni ndugu wamekaa pamoja kwa muda mrefu, wanafanya shughuli zao kwa pamoja na hoja zote zina usahihi ndani yake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mjumbe, kupitia kwako kwamba tukubaliane tuendelee na bajeti yetu hii na vijana naamini wamesikia jambo hilo. Vile vile, Mhe. Waziri, naamini atawaambia watendaji wake namna ya kuwatafuta vijana hawa na kupatikana, ili mazungumzo yafanyike kati ya watendaji na vijana hawa na matokeo yake ni kusaidia vijana wetu hawa pamoja na vijana wengine katika shughuli za michezo, kwa ajili ya kuliimarisha Taifa letu kimichezo pamoja na mambo mengine muhimu ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mjumbe, kwamba tukubaliane na tusongembele katika bajeti yetu hii na lolote litakalokuwa naamini litapata ufumbuzi uliosahihi kama ambavyo Mhe. Mwakilishi, ametueleza. Naomba tuendelee na nimuombe Mhe. Mjumbe, ambaye ni ndugu yangu tuendelee. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, namheshimu sana kaka yangu na kama alivyosema ni ndugu yake, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, lakini leo naomba kidogo niweke pembeni na yeye awe Mwakilishi wa kuteuliwa na Mhe. Rais na mimi niwe Mwakilishi wa Jimbo la Kiembesamaki. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kupitia kwako kwamba asiseme kuwa kauli zetu mimi na Mhe. Waziri, siko sawa na wala haziko sawa, kwa sababu mimi ninawatetea *Weight Lifters Association* ambao wapo ndani ya wizara yake, wanabeba bendera ya Taifa na siku wakirudi na medali hapa Zanzibar hawatosherehekea Jimbo la Kiembesamaki tu, bali wizara ndio itakayosema huu ndio ushindi wangu na *speech* ya Mhe. Waziri ndio itakayojisifu humu ndani na kusema kwamba hawa wamerudi na mafanikio haya na medali fulani za dhahabu na wala sio Jimbo la Kiembesamaki. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, nawatetea watu ambao wizara yake Mhe. Waziri, inahusika moja kwa moja na wala hatuzungumzi lugha moja.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la pili ambalo namuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kupitia kwako kama serikali tunadhalilika siku zote humu, yaani munadhalilika nyinyi huko mbele na sisi kwa mikopo hii inayotolewa, kwa sababu kila mara mnadaiwa na *issue* hiyo inarudia mara tatu mpaka nne humu ndani. Sasa kama serikali ninakuombeni mutoe kauli kwamba hawa vijana watalipiwa lini, ili uwanachama ule usifutwe, kwa sababu haina faida kwenda kugombania *FIFA*, sisi wakati hichi cha rahisi zaidi. *FIFA fees* zake ni *U$* 55,000 ya uwanachama hamtoweza. Kwa hiyo, msiende *FIFA* mtaingia aibu. *(Mako,fi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba wasiende *FIFA* kwa ajili ya *ZFA*, kwa sababu wataingia aibu itakuwa hawawezi kulipa *U$* 55,000 na ikiwa *U$* 2,200 zinashirikana hivi sasa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, kwa heshima hizo akitoa kauli hiyo nitakubali kama si hivyo, leo tutacheza foliti, kwa sababu masuala mengine nimesingiziwa ya *forgery included* na hayo sikuyapenda na sina sifa hiyo na wala *record* hiyo katika nchi hii. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, baada kumsikiliza zaidi Mhe. Mjumbe na maelezo yake yenye ufasaha sana na ni kweli sisi ni ndugu na wala udugu wetu hauwezi kuondoka hata kama yeye amechaguliwa na wananchi na mimi nimeteuliwa bado udugu wetu utabakia pale pale, lakini naomba kumueleza kwamba kwa kuwa kiwango alichokitaja cha dola *U$* 2200 jambo hilo serikali inao uwezo nalo na pale taratibu zitakapokamilika, tutawalipia vijana hawa, ili waendelee kupata hiyo fursa ambayo inatakiwa ipatikane. Namuomba Mhe. Mjumbe, atukubalie tuendelee na hilo litakamilika. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, sasa katika kauli yake hiyo ninaikubali, lakini naomba sana kwamba taratibu zote kurejea tena ile alisema na yeye alikubali, kwamba taratibu zote zimeshakamilika Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na *invoice* tayari imeshaletwa na hawa wanayo *deadline* ya kulipa kule.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, *deadline* maana yake kikomo cha kulipa na ikifika hiyo *deadline* Zanzibar inafutwa kama nchi na huko ndio kwenye uwanachama, sisi tunao, kwa sababu tunagombania sehemu nyingi sana tuwe na uwanachama na mambo mengine mbali mbali katika Katiba hiyo mpya itakayokuja Zanzibar iwe na uhuru wake kiasi fulani. Sasa ikiwa hivi vidogo vidogo tunashindwa, sijui hivyo vikubwa tutaviweza vipi. Nadhani hatutaviweza na ndio maana nikasema *FIFA* hatutaweza.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri, atoe kauli ya kwamba taratibu zote zimeshakamilika, wizara inajua pia suala hili wizarani lipo. Hivyo, ni vyema atoe kauli kwamba lini yeye atatusaidia kulikamilisha hili, ili kama ninavyosimama hapa ninaitetea nchi ambayo inawakilishwa na serikali, serikali ni sehemu ya Baraza la Wawakilishi, ndio maana nembo ipo pale.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, muda huo unakwisha lini.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, unakwisha mwisho wa mwezi wa saba.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kama taratibu zimekamilika kama inavyotakiwa kwa mujibu wa utaratibu serikali fedha hizo zitalipwa, lakini kama taratibu zinahitaji vielelezo vyengine vikamilike, ili utaratibu ukamilike na hatua ziweze kuchukuliwa za malipo. Kwa hivyo, tutafanya hayo yote, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba ule utaratibu uliowekwa wa kiserikali haukiukwi unafuatwa na vijana wetu hawa uwanachama wao unabakia na namhakikishia kwamba utafanyika kabla ya muda huo ambao Mhe. Mjumbe, ameutaja. *(Makofi)*

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, kama si ukaka leo Mhe. Waziri, angetoka kamasi humu ndani. Hivyo, naomba aseme tu Mhe. Waziri, kwa ufafanuzi utaratibu upi ukamilike.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, serikali imeshakubali yote na fedha zina utaratibu na kama kuna *voucher* zipeleke kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, hivi sasa na wala sio kule tena Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, wewe uko upande wa serikali au wetu sisi, kwa sababu wewe unatakiwa kuwa *neutral.* Naomba nimalizie tafadhali.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba ukae kitako tufahamiane. Kwa kweli wewe umetaka vijana wasaidiwe na serikali itoe kauli na Mhe. Waziri, amesimama mara mbili kwa niaba ya serikali, kwamba imesema taratibu zikikamilika, zitalipwa kabla ya huo mwezi wa saba na niliuliza mwezi gani. Sasa kama hakuna matatizo Mhe. Waziri, ameshakubali kesho mukakae muzungumze kwa ajili ya kuekwa sawa mambo, ili mambo yamalizike na kama kuna matatizo atakwambia hapa bado na pale tayari na ikiwa tayari utafanywa utaratibu wa kulipwa, ndivyo nilivyofahamu mimi.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, nakubali ulivyofahamu wewe na ninakuheshimu kwa heshima na taadhima pamoja na unyenyekevu mkubwa sawa, kifungu tunapitisha leo hapa na mimi nitakwenda wizarani kwake kesho. Sasa nilichokiomba ni kitu kidogo kwamba ninachokiomba ni utaratibu upi autaje au aufafanue tu na akeshakuutaja mimi nimeridhika.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Fedha, kuhusu utaratibu.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kidogo tufahamiane katika suala hili, fedha za serikali katika kulipa hata kiwango kidogo zina taratibu zake na lazima taratibu hizo zikamilike, ndio fedha hizo zilipe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ndugu yangu Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, ameelezea *certificate* ya ile timu ya wabeba vyuma, lazima ithibitishe kama kweli ndio waliyoipata kwa sababu Mhe. Waziri wa sekta, hivi sasa kwa maelezo aliyotoa yeye mwenyewe inaonekana kwamba hajakubaliana nae, hiyo kwanza lazima tuithibitishe.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili, vile vile, tuithibitishe hiyo *invoice* kama *it is the genuine invoice,* si kwa sababu watu wanafoji laa, sitaki niende huko anakokuzungumza Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, nia yetu *for the first time* kama tunataka kuanza kulipa lazima tuthibitishwe kwamba hiyo *invoice* ni *genuine* na imetoka katika ithibati *institution.* Mhe. Mahmoud Thabit Kombo ni kijana wetu mzuri sana katika masuala ya *IT* anaelewa, risiti nyingi sana watu wana-*scan* na wala sio *genuine,* wanachukua kichwa wanakuja wanavichana utaona risiti kama ni *genuine*, sisi tunataka kuthibitisha kwa sababu pesa za serikali siku moja tutakuja tutahojiana hapa, kuna Kamati nzito sana ya *PAC* inapitia mahesabu yote ya *Auditor*.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nataka nimwambie tu kwamba tarehe anazozizungumza yeye za mwezi wa Julai, muda tunao mzuri Wizara ya Habari wataalamu watawatafuta hawa vijana watakuja na *Document* zao zote

tutashirikiana Wizara ya Fedha na Wizara ya Habari tufanye uthibitisho wa hizo *Document* zote kulipa pesa siku hizi *PBZ* wanapeleka leo, kesho zimeshafika hazina matatizo yoyote siku mbili, mimi nataka nimhakikishie Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, tutalifanya suala hili kwa nguvu zetu zote ili bendera ya Zanzibar iendelee kupepea nje nchi. Dola 2400 kwa serikali hii sio pesa nyingi uwezo wa kuzilipa tunao, lakini tunataka tuwe tunamlipa mtu sahihi, tusiwe tunalipa watu ambao sio kesho na keshokutwa tutakuja kuulizana hapa hatukuwa makini katika suala hili. Kwa hivyo, nataka nimthibitishie Mhe. Mahmoud, kwamba tukithibitisha kesho *everything in genuine* kwesho kutwa tutafanya kazi ya ku-*clear* wala hakuna matatizo yoyote.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, natafakari kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Lakini muda unakwenda.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, najua Mheshimiwa, maana huyo mmoja ni kaka yangu na huyu mmoja shemeji yangu, lakini serikali haiendeshwi kwa ushemeji au ukaka hapa, serikali ni serikali na Baraza la Wawakilishi ni Baraza la Wawakilishi, hiyo ni mihimili mikuu ya dola, watu wengi wanafikiria Baraza la Wawakilishi ni serikali, hapana, ni mhimili mmoja wapo katika dola, sasa Mheshimiwa, kwa kuwa Mawaziri wote wawili hawa nawaheshimu, naamini na Mhe. Waziri wa Habari, atakaa tena na watendaji wake ili alitafakari hili, maana leo tuhuma zilizotolewa dhidi yangu pia ni nzito sana, kwa kweli sijawahi kupata tuhuma kama hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nawakubalia na hiki kifungu tutapitisha leo, lakiini naomba sana serikali isikubali kutiwa madowa kama haya madogo madogo, muhimu sana sana hasa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, la si hivyo, itaanza kuja kupanguka kwa mapande, kwa sababu hawa waliokuwa wanadai wameshahangaika na hiyo timu ninayokwambia leo ni Timu ya Taifa ya Zanzibar imeshawahi kupokelewa hapa Kitaifa na medali wameleta, wako Uturuki wanafadhiliwa na Shirikisho hilo hilo. kwa hivyo, kifedha zimesharudi kwetu kupitia ufadhili huo, lakini sisi ada inatushinda. Kwa hivyo, Waheshimiwa naomba niwakubalie Mhe. Waziri wa Fedha, Mhe. Mohammed Aboud na mimi nitawatafuta hao vijana ingawa si kazi yangu, nitawaelekeza waende wapi kwa upendo wa nchi yangu uzalendo wangu na nafasi ya nchi yangu ndani ya Shirikisho la Kimataifa. Naomba tuendelee nashukuru sana.

Kifungu 1204	Baraza la Michezo la Taifa-	90,000,000
Kifungu 1205	Baraza la Sanaa na Muziki-	

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka ufafanuzi tu kutoka kwa vibali vinavyoruhusiwa wananchi kupiga miziki katikati ya wananchi na ukiacha watu kulala na wengine wagonjwa, ni utaratibu gani unaotumika pale kuwabughuzi wananchi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii naMichezo: Mhe. Mwenyekiti, ili vibali vitoke, muombaji lazima afuate taratibu, moja ya taratibu ni kwamba kabla ya kuja Baraza la Sanaa, basi inapita kwa Sheha wake, Sasa Sheha ndio mwenye Shehiya, akiamua shughuli hii ifanyike hapa, sisi Baraza la Sanaa kwa mujibu wa sheria na utaratibu huwa hatuna tena pingamizi, lakini tukigundua kwamba kuna matatizo vibali vyetu huwa tunavizuia na mwenyewe anajua huyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini mimi ningemuomba sana akiwa makini kama alivyo katika utendaji wake wa kazi bado wananchi wanaendelea kuteseka na wengine ni wagonjwa wanaweza kufa siku zio zao kwa muziki unaopigwa. Hivyo, Baraza lake andeliangalia upya utaratibu huu tuendelee.

Kifungu 1205	Baraza la Sanaa na Muziki-	20,800,000
Kifungu 1206	Bodi ya Sensa na Senema-	21,500,000
Kifungu 1207	Kamisheni y Utamaduni na Michezo Pemba-	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe naomba msitoke, ndio kazi tuliyojia kwanza nimpe pole sana Mhe. Waziri, wetu leo kidogo hali ilikuwa sio nzuri, lakini mambo ya kawaida, lakini hoja yangu kwamba nazungumzia Kamisheni ya Utamaduni na Michezo na Mhe. Waziri, hili kidogo kutokana na muda hakuwahi kulitolea ufafanuzi, niliomba katika suala zima la utamaduni kuna ajira vile vile, inapatikana na nilizungumzia ingawa watu wengine waliona kama masihara, lakini nilizungumzia vijana wetu ambao wanaopaka hina ambao wanafanya kazi katika mahoteli mbali mbali. Hii ni ajira kubwa sana na ajira hii pato lake inamshinda mpaka Mkurugenzi katika Wizara, leo kazi hizi zinachukuliwa na wageni na mwanzo

walikuwa wakipaka hina hawa hawa Da Tatu, Da Mwajuma na Da Fatuma, lakini wenzetu leo wenye mahoteli wameanza kugeuka, wanawachukua wageni. Sasa nilimuomba tu Mhe. Waziri, katika hili ashirikiane na Mhe. Waziri wa Kazi, ili huu utamaduni wetu iwe badala ya kwamba utamamduni uwe ni sehemu ya ajira kwa vijana wetu. Sasa hili najua hakuwahi kulitolea ufafanuzi, lakini naamini ni suala jepesi sana, ataweza kutusaidia na sisi vile vile tutamsaidia ni hoteli gani na hoteli gani ambazo waliwaondoa wale vijana wetu wa Kizanzibari wanaotiya hina za Kizanzibari wakaletwa wageni wazungu kutoka nje, wakaja wakatia hina za wazungu wenzao. Wakati mzungu anataka kutiwa hina na mswahili, leo wanaletwa wazungu kuja kutia hina wazungu wenzao, kwa nini wasiwatie huko huko kwao.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ushauri wa Mwenyekiti wa Wenyeviti ni mzuri sana na namuahidi kwamba tutafanya kazi kwamba hapa Zanzibar utaratibu wa kutiwa hina upewe nafasi kubwa zaidi na kwamba kwenye mahoteli basi tushirikiane na Idara ya Kazi kutoa maelekezo ya Kiserikali kwenye hoteli kwamba zile piko za wazungu zipungue na badala yake kuwe na hina nzuri na wanja nzuri.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru kwa hilo Mhe. Waziri na kama nilivyomwambia tutamsaidia yale majina ya hoteli ambazo wanafanyakazi hizo ambazo taratibu zetu wanapaswa wapewe Waswahili. Sasa mwisho kabisa ili tuendelee nilikuwa naomba tu hili ni ombi maalum kwamba sasa hivi utaratibu wa kupitisha vifungu, sasa tuwe tunafanya wakati wa asubuhi kwa sababu tunapofanya wakati wa jioni, kwa kweli ndio kama hivi wengine wamefunga, siku hizi kombe la dunia na mambo mengine. Kwa hivyo, hili tu lilikuwa ushauri kwa kiti chako ili tusiwabughuzi na wengine. Ahsante.

Kifungu 1207 Kamisheni ya Utamaduni na Michezo Pemba- 38,119,000
Jumla ya Fungu- 7,982,000,000

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu Vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0401	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	-5,595,375,000
Kifungu 1101	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale	-150,000,000
Jumla ya Fungu		**-5,745,375,000**

(Vijifungu vilivyopitishwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko.Sasa naomba kutoa hoja kwamba baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Naibu Spika: Hoja imetolewa Waheshimiwa sasa niwahoji wale waliokubali hotuba ya Wizara Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 wanaokubali wanyoonge mkono, waliokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza niwashukuru sana kwa kazi nzito tuliyoifanya leo, lakini kwa ushirikiano mkubwa na nawaomba tushirikiane zaidi kwa sababu bado tunaendelea na kazi hii na nawatakia mapumziko mema, ili kesho tuwahi mapema.

Naahirisha kikao hichi hadi kesho Tarehe 19/06/2014 Saa . 3.00 asubuhi.

(Saa 3:55 usiku Baraza liliahirisha mpaka tarehe 19/06/2014 Saa 3.00 asubuhi)